# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA SITA

### Kikao cha Sita – Tarehe 6 Februari, 2017

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Katibu!

**NDG. CHARLES MLOKA - KATIBU MEZANI:**

### HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI:** Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2016 hadi Januari, 2017.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:** Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2016 hadi Januari, 2017.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Katibu tuendelee.

**NDG. CHARLES MLOKA - KATIBU MEZANI:**

### MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na maswali kama kawaida. Tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, tunaanza na Mheshimiwa Zainab Athman Katimba, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 56

**Mfuko wa Maendeleo ya Vijana**

**MHE.PETER J. SERUKAMBA (K.n.y MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** aliuliza:-

Mwaka 1993 Serikali ilianzisha Mfuko wa Maendeleo wa Vijana *(Youth Development Fund – YDF)* ili kutoa mikopo kwa vijana nchini. Mwaka 2013/2014 Serikali ilitenga jumla ya shilingi bilioni 6.1 na mpaka mwezi Machi, 2014 jumla ya shilingi bilioni mbili zilitolewa na Serikali.

(a) Je, Serikali itakuwa tayari kuwaeleza vijana nchi nzima kuwa ni vijana wangapi na wa maeneo gani ambao wamenufaika?

(b) Je, maisha ya vijana waliopewa fedha hizo yamebadilika kwa kiasi gani ili tuweze kupima haja ya mfumo huo na usimamizi wake?

(c) Je, Serikali haioni ni wakati muafaka sasa kuangalia upya mfumo uendeshaji wa mfuko huo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zainab Katimba, Mbunge wa Viti Maalum na kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ni kuwawezesha vijana wote nchini kupata mitaji kwa njia ya mikopo yenye masharti nafuu ili kuanzisha au kuendeleza miradi yao ya uzalishaji mali. Kupitia utaratibu huu, vijana huwezeshwa kujitegemea, kupunguza umaskini wa kipato na kujiajiri wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya vikundi vya vijana 309 kutoka Hamlashauri mbalimbali nchini vilifaidika kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kwa kupata mikopo yenye jumla ya shilingi 1,867,899,520 ambako mpaka sasa tayari *SACCOS* za vijana kutoka katika Halmashauri 94 zimepatiwa mkopo huu.

Vijana hawa pia hupatiwa mafunzo ya uendeshaji na usimamizi wa miradi, utunzaji wa fedha na utafutaji masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za mkopo zitokanazo na Mfuko wa Maendeleo ya Vijana umekuwa msingi mzuri katika kuandaa vijana kujiajiri na kuajiri vijana wengine. Kupitia fedha hizo, vikundi vingi vya vijana vimefanikiwa kukuza vipato vyao kwa kushiriki katika shughuli mbalimbali za kiuchumi kama vile kilimo, ufugaji, usindikaji wa mazao na uanzishwaji wa viwanda vidogo vidogo. Aidha, shughuli hizo zimefanya vijana waachane na utegemezi na badala yake kutumia muda wao mwingi katika uzalishaji na hivyo kuongeza tija katika uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipo vikundi vya mfano ambavyo kupitia mfuko huu vimekuwa kielelezo cha dhati katika kubadili mtazamo wa vijana wa kutegemea kuajiriwa hadi kujiajiri wenyewe na kukuza vipato vyao. Vikundi hivyo ni pamoja na *THYROID Group* kutoka Halmashauri ya Chunya kinachosambaza taa za *solar* vijijini, *MIRANACO Group* kinachomiliki duka kubwa la dawa za binadamu kutoka Halmashauri ya Mbozi, *Maswa family* kinachoshughulika kutengeneza chaki na *Meatu Milk* kinachotengeneza maziwa kutoka mkoani Simiyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuboresha uendeshaji wa shughuli za Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, Serikali imekuwa ikifanya ufuatiliaji na tathmini mbalimbali mara kwa mara kwa lengo la kuhakikisha ufanisi unakuwepo na kubaini changamoto za kiutendaji zinazojitokeza. Katika mwaka huu wa fedha, Serikali inapitia upya muongozo wa utoaji fedha kupitia mfuko wa maendeleo wa vijana wa mwaka 2013 ili kuwawezesha vijana wengi zaidi kuanzisha viwanda vidogo katika kuendana na sera ya nchi kwenda kwenye uchumi wa viwanda.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ambaye aliuliza swali kwa niaba ya Mheshimiwa Zainab Katimba. Samahani nilikuwa sijamuona ni nani.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majawabu mazuri ya Naibu Waziri anaweza sasa leo akawaelekeza Halmashauri zote nchini kwamba kila mwaka ni *mandatory* lazima kutenga fedha kwa ajili ya Mfuko wa Vijana?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utaratibu wa kuwasaidia vijana kupata mitaji na mikopo, tunayo mifuko mingi sana. Moja wa mfuko ambao nimeusema hapa ni Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ambao umekuwa ukishirikiana na Halmashauri kupitia *SACCOS* mbalimbali na vijana wengi wamekuwa wakipata mikopo kupitia katika *SACCOS* hizo.

Kwa hiyo, nimuondoe tu hofu Mheshimiwa Mbunge ya kwamba kupitia Mfuko huo wa Maendeleo ya Vijana, kila mwaka tumekuwa tukikopesha vijana na wengi wamefaidika kama nilivyosema hapa isipokuwa tu katika zile asilimia tano za kila Halmashauri ambazo ni utaratibu mwingine tofauti, nako tumekuwa tukitoa msisitizo mkubwa kuhakikisha kwamba Halmashauri zinatenga asilimia tano za mapato yao ya ndani kwa ajili ya vikundi vya vijana.

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Bobali.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti swali la msingi, Mheshimiwa Mbunge aliyeuliza alizungumzia fedha iliyotengwa mwaka 2013/2014 na kiwango ambacho Serikali walikuwa wamekitoa. Nataka kujua ni kiasi gani cha pesa kilitengwa na kimepelekwa katika mwaka huu wa fedha tulionao wa 2016/2017?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kabla sijaenda katika kujibu swali lake nisaidie kutoa ufafanuzi kidogo ili jambo hili lieleweke vyema.

Katika utaratibu wa kuwasaidia vijana nchini iko mifuko mingi ambayo inashughulika na shughuli hii ya kuwasaidia vijana, lakini ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira tunao Mfuko wa Maendeleo wa Vijana ambao pamoja na mfuko huu tunao pia utaratibu wa utengaji wa asilimia tano za mapato ya ndani ya kila Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ndani ya mfuko wetu mpaka hivi sasa ninavyosema tayari tumeshakopesha vikundi vya vijana takribani 309 na wamepatiwa takribani shilingi 1,700,000,000 kwa hiyo, katika utaratibu ulioko hivi sasa, mwaka huu wa fedha tumetengewa shilingi bilioni moja ambako hizo nazo tutazisambaza kwa ajili ya vikundi vya vijana ili waweze kunufaika Nchi nzima.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jaffo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuongeza tu hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala zima la Halmashauri mwaka huu katika Bajeti ya Halmashauri kwanza tulitoa maelekezo katika utengenezaji wa Bajeti ya mwaka 2016/2017 ni lazima kila Halmashauri itenge 10% ya tano kwa vijana na tano kwa akina mama ambapo jumla ya fedha zote shilingi bilioni 64.5. Katika fedha hizo sasa kwa hivi sasa katika upande wa Halmashauri tumeenda sasa hivi karibuni shilingi bilioni tano Halmashauri mbalimbali zimeshaanza kutoa hivi sasa niwaelekeze Halmashauri mbalimbali sasa suala lile siyo suala la hiari, ni suala la lazima kila Halmashauri lazima itoe asilimia tano kwa vijana na asilimia tano kwa akina mama na hata hivyo mchakato wa bajeti tunaoondoka nao hivi sasa Halmashauri yoyote tutaizuia bajeti yake mchakato wake mpaka ile *commitment* tuloiwekea iwe imetekelezeka katika mwaka huu wa fedha.

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea na Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Emanuel Adamson Mwakasaka Mbunge wa Tabora Mjini.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kabla ya kuuliza swali langu kwanza naomba nichukue fursa hii kwa wananchi wangu wa Tabora Mjini kwa maafa makubwa yaliyowapata kwa mvua zinazonyesha hasa kwa shule ya msingi ya Bomba Mzinga ambayo yote imeezuliwa paa na mvua hizo. Baada ya haya machache naomba swali langu namba 57 kwa niaba ya wananchi wa Tabora lipatiwe majibu.

Na. 57

**Tatizo la Maji Jimbo la Tabora Mjini**

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA** aliuliza:-

Jimbo la Tabora Mjini katika maeneo ya Kata za Uyui, Misha, Itetemia, Ntalikwa, Kabila, Mtendeni, Ifucha, Itonjanda na baadhi ya vijiji vya Kata ya Tumbi vina shida sana ya upatikanaji wa maji.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha wananchi wa maeneo hayo wanapata huduma ya maji?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Emanuel Adamson, Mbunge wa Tabora Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutatua tatizo la maji Tabora Mjini, Serikali inatekeleza mradi mkubwa wa maji kutoka Ziwa Victoria ambao utahudumia kata na vijiji vya Tabora Mjini. Mradi huo utahudumia vijiji na miji ya Nzega, Igunga, Isikizya yaani Uyui na vijiji vyote vilivyomo ndani ya kilometa 12 kila upande kutoka linapopita bomba kuu la kupeleka maji katika miji hiyo. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali imetenga shilingi bilioni 589.6 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mradi huu utahusisha ujenzi wa mifumo ya maji katika Kata za Uyui, Misha, Itetemia, Ntalikwa, Kabila, Mtendeni, Ifucha, Itonjanda na Tumbi. Utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kuanza kati ya mwezi Aprili na Mei 2017.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Emanuel Adamson swali la nyongeza.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, kwa kuwa huu mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria unaonekana unaendelea kusuasua na hauna uhakika *exactly* lini utaanza na wananchi wa Tabora wanaendelea kuteseka kwa shida ya maji na sisi pale Tabora Mjini tuna bwawa kubwa la Igombe ambalo lina-*access* ya maji kwa maana ya lita za ujazo ambazo Serikali kama itaweka mpango mkakati wa

kusambaza maji yale ya Igombe na kwa unafuu, Wananchi wa Tabora Mjini watapata nafuu ya tatizo la maji.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba yale maji ya Igombe yaweze kusambazwa kwa bei nafuu kuliko kusubiri huo mradi wa Ziwa victoria ambao haujulikani utaanza lini? Hilo la kwanza

Swali la pili, moja ya tatizo lingine linalosababisha ile Mamlaka ya Maji *(TUWASA)* Tabora inapata matatizo katika uendeshaji wake ni pamoja na kutolipa deni ambalo Mamlaka ya Uendeshaji ya Maji - *TUWASA* pale Tabora inaidai Serikali kwa muda mrefu zaidi ya shilingi bilioni 2.3 ambazo zinadaiwa hasa kwenye taasisi zetu za majeshi pamoja na taasisi zingine za Serikali.

Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha *TUWASA*wanalipwa pesa hizo ili Tabora iweze kupata maji ambayo yatakuwa ni ya uhakika? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka tuweke kumbukumbu sawa. Katika mradi huu wa Tabora-Sikonge ambao katika bajeti yetu mwaka huu nadhani tulipitisha pamoja hapa. Tulitenga takribani shilingi bilioni 29 ukiangalia kitabu cha maendeleo lakini kwa juhudi kubwa zilizofanywa na Serikali kupitia ufadhili kutoka India ndiyo maana nimesema ile *figure* zaidi ya shilingi bilioni 500 ambayo Serikali imeshaweka *commitment* hiyo. Hivi sasa mchakato wa manunuzi upo katika hatua mbalimbali na lengo la mradi huu kati ya mwezi Aprili mpaka mwezi Mei mradi huu utakuwa umeanza, kwa hiyo, ndugu yangu, mtani wangu, Mnyamwezi wa Tabora naomba ondoa hofu katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala zima la jinsi gani tutumie bwawa la Igombe, wataalam wetu wameshaanza kufanya tathmini pale. Takribani ule mradi utagharimu shilingi bilioni 1.5 na hili ndiyo maana tumeona kwamba jambo hili kama Ofisi ya Rais - TAMISEMI lakini na kushirikiana na wenzetu ambao ni Wizara mama wa Wizara hiyo tutaangalia jinsi gani tutafanya kwa pamoja katika mchakato wa pamoja wakati tunasubiri mradi mkubwa wa maji wa hizo shilingi bilioni 500, jinsi gani tutafanya hizo *back up strategy* ya mradi mwingine huu mdogo katika bwawa la Igombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwahiyo lengo letu kama Serikali ni kuweza kutatua shida ya maji katika Mkoa wa Tabora na ndiyo maana nimesema mradi huu siyo Tabora peke yake, kuna watu wa Tinde pale, kuna watu wa Kahama,

kuna watu wa Shinyanga mradi huu utakuja kujibu matatizo ya watu wote wa ukanda ule. Niseme, Wasukuma na Wanyamwezi wa eneo hilo mmepata bahati kubwa sana kwa Serikali kuwaona kwa jicho la karibu kuwatengea takribani shilingi bilioni 580.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hata hivyo, suala zima la bili ya maji; suala la bili ya maji ni kwamba tumetoa maelekezo mbalimbali hapa kwamba bili ya maji kupitia Waziri wa Maji ameshatoa maelezo mbalimbali, sasa naomba niziase taasisi mbalimbali; kila taasisi inayodaiwa deni la maji liweze kulipa deni la maji siyo Tabora peke yake lakini katika maeneo yote ya nchi hii, kama taasisi inayodaiwa na maji, miradi hii ya maji au hizi mamlaka za maji zitashindwa kutupatia maji kwasababu watu wanashindwa kulipa bili za maji.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Shabani Shekilindi

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa maji ni kilio cha muda mrefu sana hasa katika Jimbo la Lushoto na ukizingatia Jimbo la Lushoto lina mto mkubwa sana unaitwa Kibohelo, lakini unakuta Lushoto mto ule hautumiki unamwaga tu maji kuelekea bondeni Mombo bila kutumika maeneo yote.

Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuhakikisha maji yale yanaenda hasa katika vijiji vya Dochi, Ngulwi, Miegelo, Kwekanga pamoja na Gare?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi kabisa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Shekilindi anafahamu si muda mrefu sana nilitokea katika Jimbo lake na Jimbo la ndugu yangu Shangazi na kwa bahati nzuri hapa kuna mwalimu wangu hapa kutoka huko huko Lushoto amekuja hapa leo na hili naomba niwahakikishie ni kwamba ni *commitment* ya Serikali kuangalia jinsi gani tutatumia fursa zote zilizokuwepo kutatua tatizo la maji. Na katika Mpango wa Maji wa Awamu ya Pili, Waziri wa Maji amezungumza hapa mara kadhaa, lengo letu ni kwamba kutumia hizi fursa zilizokuwepo nikwambie ndugu yangu Shekilindi kwa sauti eneo lile nilivyofika kule Lushoto niwaagize wataalam wetu wa maji katika Halmashauri ile waanze michakato ya awali suala zima tufanyeje sasa matumizi halisi ya mto ule uweze kutumika vizuri kwa ajili ya wakazi wa Lushoto.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hapo.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa matatizo ya maji ya Tabora ni sawa sawa na matatizo ya maji ya Mkoa wa Kagera hasa Bukoba Mjini. Kwa sasa hivi ukame umechukua muda mrefu mito mingi imekauka. Je, ni lini Serikali itatuweka kwenye Mpango wa Ziwa Victoria angalau hizi kata zilizoko karibu na Bukoba Mjini zipate maji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa ufupi kabisa.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge anazungumza kuhusu maji ya Ziwa Victoria kupelekwa Kata za Mjini Bukoba. Hivi sasa Serikali imejenga mradi mkubwa sana wa kutoa maji Ziwa Victoria kusambaza katika Mji wa Bukoba. Tatizo lililopo tu ni kwamba baadhi ya maeneo yako juu. Kwa hiyo, Serikali itaweka *pump* za kuweza kupandisha maji zaidi kwenye yale maeneo ambayo yako juu kuliko yale ya chini ili tuweze kuona kwamba wananchi wetu wa Manispaa ya Bukoba watapata maji ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni kazi ambayo inaendelea na kila mwaka tumeweka fedha kila Halmashauri na tumetoa mwongozo kwamba kwa kulingana na fedha ambazo zipo tumetenga kwenye Bajeti yetu kila halmashauri ianze kufanya manunuzi ili kusudi maeneo yale ambayo hayakuwa yamefikiwa maji yaweze kufikiwa maji kulingana na malengo ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tunataka maeneo yote ya mijini tufikishe maji kwa 95% ikifika mwaka 2020; kwa hiyo Wabunge ni sehemu ya Baraza la Madiwani, tuwe karibu sana katika mipango ya maendeleo ya sekta maji kuhakikisha wananchi wetu wanapata maji.

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, tunaendelea Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, ni Mbunge wa Bunda sasa ulize swali lake.

Na. 58

**Suala la Mazingira na Tabia Nchi**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE** aliuliza:-

(a) Je, Serikali ina mpango mkakati gani wa kunusuru Taifa na janga la mabadiliko ya tabianchi?

(b) Je, ni lini Serikali itahakikisha kwamba Ofisi za Majiji, Manispaa, Miji na Halmashauri zinakuwa na Idara ya Usafi na Mazingira inayojitegemea kuliko kuitegemea Taasisi ya *NEMC* ambayo inaonekana kuzidiwa na majukumu ya kudhibiti na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi?

(c) Je, Serikali ilipata ushauri gani kuiondoa Idara ya Mazingira kutoka kwenye Kamati ya awali ya Mazingira, Ardhi, Maliasili na Utalii na badala yake kupelekwa kwa Viwanda na Mazingira?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi, Serikali iliandaa Mkakati wa Taifa wa Mabadiliko ya Tabianchi wa mwaka 2012. Mkakati huo umeainisha vipaumbele vya kisekta na hatua za kuchukua ili kunusuru Taifa na athari za mabadiliko ya tabianchi. Baadhi ya hatua hizo ni ambazo Wizara za sekta zimekuwa zikitekeleza ni pamoja na kuhimiza kilimo kinachozingatia mabadiliko ya misimu ya mvua, ufugaji endelevu, kuhifadhi vyanzo vya maji na misitu, ujenzi wa mabwawa ya maji, upandaji miti, matumizi ya nishati mbadala, ujenzi wa miundombinu imara ya barabara, madaraja na mifereji ili kuhimili mafuriko na matumizi ya teknolojia rafiki wa mazingira viwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati huu unazingatia Wizara zote za kisekta na Serikali za Mitaa kuhuisha suala la mabadiliko ya tabianchi katika mipango yao.

Aidha, Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya kuhimili na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kama vile ujenzi wa kuta kwenye kingo za bahari, upandaji wa mikoko na kujenga uwezo wa wataalam kuhusu mabadiliko ya tabianchi.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI ilishatoa mwongozo wa uanzishwaji wa Idara ya Usafi na Mazingira katika Halmashauri

zote nchini na Halmashauri nyingine zimeshaanzisha idara hiyo. Aidha, kutokana na changamoto za utekelezaji wa majukumu yake, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imeandaa mapendekezo ya kuboresha muundo huo.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la muundo wa Kamati za Kudumu za Bunge ni jukumu la Ofisi ya Spika wa Bunge na Wizara haihusiki katika uandaaji wa miundo ya Kamati.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Boniphace Mwita, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Sheria ya Mazingira namba 20 ya mwaka 2004, Kifungu cha 182 na 183 (1) (2) na (3) na kifungu cha 36(1) na (2) tunatambua uwepo wa Maafisa Usafi na Mazingira katika Halmashauri zetu nyingi na kwa kuwa wahitumu hao wanamaliza elimu yao ya vyuo vikuu kwa vyuo vyetu hapa kwa wingi sana toka mwaka 1987, je, ni lini Serikali sasa itatangaza ajira ya wataalam hao ili kukidhi mahitaji ya mkakati aliyotaja Waziri? Swali la kwanza hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa maeneo mengi ya Nchi yetu mazingira yake yameharibika sana na kupelekea kuwepo ukame mkubwa na kusababisha njaa au uhaba wa chakula na hasa katika Jimbo langu la Bunda na Wilaya nzima ya Bunda. Je, Waziri yuko tayari kuitisha kongamano la kimazingira la kushirikisha Wabunge ili kujua hali halisi ya mazingira katika nchi yetu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS-MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la Maafisa Mazingira; kama nilivyozungumza wakati nikijibu swali la msingi kwamba Maafisa Mazingira hawa tayari katika Halmashauri zetu wapo. Aidha, nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge katika zile Halmashauri ambazo hawajaweza kuajiri watu hawa basi pale nafasi zitakapoanza kutolewa, Serikali itakapoanza kuajiri tena waajiriwe hawa wa Serikali zile Halmashauri zote zihakikishe kwamba zina Maafisa Mazingira katika Halmashauri husika kama maelekezo ambavyo yamekwishakutolewa. Lakini vilevile na Wizara zote ambazo hazina sekta hii ya mazingira wahakikishe kwamba wana hao maafisa katika sekta hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kuhusiana na ukame ambao umepelekea uhaba wa chakula na Mheshimiwa Mbunge kupendekeza kwamba liwepo kongamano. Ninaloweza kusema kwamba wananchi wote na Wabunge wote ni lazima tukubali kwamba sasa tupo katika mabadiliko makubwa na tuko kwenye athari kubwa za mabadiliko ya tabianchi ambapo sasa inatupasa sisi sote kuhusiana na kilimo, kilimo chetu sasa hivi ambacho kimekuwa na mvua ya kusuasua kuhakikisha kwamba wananchi hawa wanaelezwa namna ya kutumia taarifa sahihi za wataalam wetu, tafiti zinazofanywa kulingana na mabadiliko ya tabianchi waweze kujua mbegu bora zinazohitajika kwa sasa hivi ili kupambana na huu uhimilivu wa tatizo la tabianchi, mbegu bora hizo zinazozungumzwa katika mazao hayo, lakini vilevile na mazao ambayo yanahimili ukame huo kulingana na mvua ambazo zinanyesha kwa kiwango cha chini sana sasa. Ipo mikoa iliyokuwa inapata mvua ambazo zinanyesha kwa kiasi kikubwa sana lakini leo hii mvua hizo zimekuwa za kusuasua, kwa hiyo, wananchi lazima wafundishwe hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu makongamano na taarifa mbalimbali za kuwahujisha wananchi; Hizo tutaendelea kuzitoa kwa wananchi ili waweze kuwa na tahadhari na hali hii ya sasa hivi ya mabadiliko ya tabianchi na suala la makongamano hilo litazungumzika kulingana na kwamba tumeshaamua kwamba shughuli yoyote ambayo tutaifanya tuhakikishe tunazidhibiti matumizi ya hovyo ya Serikali na hivyo tutahakikisha kwamba elimu hii tunaifikisha bila gharama kubwa sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gashaza swali la nyongeza.

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna asiyetambua kwamba mabadiliko ya tabianchi ni janga la kitaifa na kimataifa. Kwa kutambua hilo binafsi kama Mbunge wa Jimbo la Ngara kwa kushirikiana na wataalam wangu katika Halmashauri yangu ya Ngara tumejipanga kuanzisha programu ya kuwa na vikosi kazi vya kupambana na moto kama kisababishi kikuu cha uharibifu wa mazingira. Programu hiyo ambayo tutaiita *Community Fire Brigade* kuanzia kwenye ngazi ya vijiji na kata.

Sasa swali, Serikali kupitia Wizara ya Muungano na Mazingira wako tayari ku-*support* programu hii kwa kutoa fedha kwa sababu lengo ni kuanzisha vitalu, kupanda miti katika maeneo ambayo yameathirika na moto lakini pia

kuanzisha miradi ambayo ni rafiki wa mazingira kwa maana ufugaji wa nyuki kwa malengo matatu, moja, kulinda mazingira; lakini pili, kuinua kipato cha wananchi na tatu, kutoa ajira.

**MWENYEKITI:** Naomba swali kwa ufupi Mheshimiwa.

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Tayari nimeshauliza swali…Serikali ipo tayari…

**MWENYEKITI:** Basi naomba ukae upate majibu!

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Haya!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS-MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuanzisha mkakati huo katika Jimbo lake na Wabunge wengine waige mfano wa Wabunge kama mtazamo alionao Mheshimiwa Mbunge nimhakikishie kabisa kwamba ofisi yangu haina tatizo lolote, tunaomba huo mkakati wake atuandikie ili tuweze kuona jinsi ya kuuingiza katika mipango ya Serikali tuweze ku-*support* mpango huo ili kuweze kuhakikisha kwamba mazingira yanalindwa kwa gharama zote kuhakikisha kwamba mazingira yako salama lakini tunapambana nahii hali ya mabadiliko ya tabianchi ambayo kwa kweli inahitaji wadau mbalimbali wote wa Tanzania wote kwa ujumla kuunga mkono jitihada hizi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yussuf swali la nyongeza.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, katika majibu yake Mheshimiwa Waziri amesema ili kupambana na suala la mmomonyoko wa ardhi katika kingo za bahari Serikali imechukua au itachukua hatua ya kujenga kuta katika kingo za bahari pamoja na kupanda miti ya mikoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmomonyoko wa ardhi katika kingo za bahari sasa hivi unakuwa kwa kiasi cha mita mbili kwa mwaka. Kiasi ambacho ni kikubwa sana. Je, Serikali inauwezo gani wa kujenga kuta katika ukanda wote wa bahari ili kuzuia mmomonyoko huu na hiyo elimu ya upandaji hiyo mikoko inatolewa kwa kiasi gani ambayo tunaweza tukakabiliana na kasi hii ya ukuaji wa mmomonyoko katika ardhi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS-MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli ipo kasi kubwa ya kuongezeka kwa kina cha bahari kumesababisha bahari kwenda kwenye makazi ya watu, kumesababisha mmomonyoko mkubwa sana wa fukwe zetu, lakini imesababisha pia hasara kubwa kwa sababu kuna baadhi ya majengo ya biashara na makazi yako kwenye hatari kubwa ya kumezwa na bahari na miundombinu mingine ya kiuchumi mikubwa kama visima vya gesi ambavyo na vyenyewe viko kwenye hatari vilevile ya kumezwa na bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunachofanya kama Wizara ya Mazingira katika pande mbili zote tunayo Idara ya Mazingira ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano, lakini tuna Idara ya Mazingira pia ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Serikali hizi zote kwa pamoja zinaendelea kufanya kazi ya kufanya tathmini ya kuweza kubaini hizi athari kila mahali sasa baada ya kubaini zile athari ambazo zinasababishwa na haya mabadiliko ya tabianchi tunaangalia kwamba ipi tuipe kipaumbele leo ili kuweza kuzuia athari ambazo zinaweza kujitokeza kwa muda mfupi kama sasa hivi tutakubaliana Wabunge wote kwamba hapa na mlitupitishia kwenye bajeti na sasa hivi kuta hizo zimeshaanza kujengwa, ukuta wa Pangani, ukuta wa *Ocean Road*, ukuta wa Kilimani na ukuta wa Kisiwa Panza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, visiwa hivi vyote ndivyo vilikuwa vipaumbele vyetu kwasababu maeneo haya yalikuwa yamepata athari kubwa na hivyo sasa naona Mbunge wa Pangani hapa ana hofu ni kwamba mkandarasi yuko *site* sasa hivi amekwisha ku-*report* sasa hivi ameanzia na *Ocean Road* na ndiyo huyo huyo ambaye atajenga ukuta wa Pangani ndiyo huyo huyo atayejenga ukuta wa Kilimani pamoja na Kisiwa Panza na anauwezo wa kutosha kufanya kazi hizo kwa muda tuliompa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi sasa namkaribisha Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mbunge wa Konde aulize swali lake.

Na. 59

**Kuchelewa Kwa Upelelezi wa Makosa Mbalimbali**

**MHE. KHATIB SAID HAJI** aliuliza:-

Kumekuwa na ongezeko kubwa la mahabusu katika magereza hapa nchini kutokana na kuchelewa kwa upelelezi wa mashauri mengi.

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani za haraka ili kukabiliana na ucheleweshaji huo wa kesi zilizopo mahakamani?

(b) Je, ni muda gani umewekwa kisheria pale upande wa mashtaka unaposhindwa kupeleka ushahidi mahakamani ili mahakama iweze kumuachia huru mshitakiwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiri, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mbunge wa Konde, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali na za haraka ili kukabiliana na ucheleweshaji wa kesi mahakamani ikiwa ni pamoja na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa majalada ya kesi unaofanywa na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka (DPP) pamoja na Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai *(DCI),* kuundwa kwa Jukwaa la Haki Jinai na kutembelea mahabusu magerezani na kufanya mahojiano na mahabusu gerezani ili kushirikisha wadau wengine wa sheria katika kesi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wa kisheria wa kuondoa shauri mahakamani kama upelelezi haujakamilika ni siku 60 na mtuhumiwa kuachiwa huru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khatib Said swali la nyongeza.

**MHE. KHATIBU SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuijaalia nchi yetu kuwa miongoni mwa nchi ambayo haiko katika matishio ya kigaidi. Lakini cha kusikitisha sana katika mahabusu walioko magerezani miongoni mwao ni washitakiwa wa makosa ya kigaidi. Hivi nchi isiyo na tishio la kigaidi inawezaje kuwa na mrundikano wa mahabusu wanaotokana na makosa ya kigaidi? La kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Waziri wa Vikosi vya SMZ-Zanzibar na Makamu wa Rais wa Zanzibar wamewahi kunukuliwa wakisema kwamba wamewaleta Masheikh wa Uamsho kutoka Zanzibar ili wanyee kwenye ndoo katika magereza Tanzania Bara. Hapa katika jibu imeambiwa siku 60 inatosha

kutoa ushahidi na kama ushahidi haukupatikana watuhumiwa waachiwe huru. Masheikh wa Uamsho wana miaka minne sasa wako katika magereza na ushahidi umeshindwa kupatikana. *(Makofi)*

Nataka kujua, familia za watuhumiwa wale wanataka kujua, dunia inataka kujua, Wazanzibari wanataka kujua watuhumiwa wale wanawekwa kwa amri ya viongozi wa SMZ au wanawekwa kwa sababu wana kesi ya kujibu? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimejibu katika jibu langu la msingi kwenye jibu (b). Muda wa kisheria wa kuondoa shauri mahakamani kama upelelezi haujakamilika ni siku 60. Maswali yake mawili yote hayapingani na majibu yangu ya msingi kama ambavyo walitaka kueleweshwa Wabunge pamoja na wananchi ambao wanatusikiliza hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kimsingi ni kwamba kesi za hawa watuhumiwa zote ziko mahakamani na kwa mujibu wa sheria zetu hatupaswi kuzungumza mashauri ambayo yapo mahakamani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gekul. Mheshimiwa Gekul endelea na swali la nyongeza. Kuna Mheshimiwa Waziri anataka kujibu? Haya Mheshimiwa Waziri naomba majibu.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti,…

**MWENYEKITI:** Samahani naomba ukae Mheshimiwa Gekul. Naomba Mheshimiwa Waziri utupe majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba swali alilouliza ni swali mtambuka ambalo liko chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na vilevile Wizara ya Mambo ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kusisitiza yafuatayo na siyo lazima upende jibu lake lakini ndiyo ukweli wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nisahihishe kauli hatarishi sana kwa kwamba Tanzania haina tishio la ugaidi. Tumeshakabiliwa na matatizo ya

kigaidi, umeshalipuliwa ubalozi wa nchi kubwa sana hapa nchini na baadhi ya Watanzania wamehusika, lakini leo hii tukiona kuna usalama nchi hii tuelewe kwamba vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vinafanya kazi ndiyo maana huoni hayo matukio mara kwa mara. Naomba nichukue fursa hii kuvipongeza vikosi vyetu vya ulinzi na usalama kwa kazi nzuri ambayo vinafanya kuzima wimbi la ugaidi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, suala la….naomba...

**MWENYEKITI:** Naomba mtulie ili Mheshimiwa aweze kutueleza.

**MBUNGE FULANI:** Akae chini hana majibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa endelea.

**MBUNGE FULANI:** Huna majibu kaa chini.

**MWENYEKITI:** Dkt. endelea.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine ningemuomba Mheshimiwa Haji ajijibu mwenyewe lakini naomba mimi nijibu kama Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, suala la mtuhumiwa yeyote aliyeko mahakamni ni muda gani kesi yake ataruhusiwa kuendelea kukaa mahakamani kama upelelezi haujaisha? Naibu Waziri ameeleza ni siku 60. Lakini pale ambapo upelelezi haujakamilika Mkuu wa Upelelezi wa Mkoa analeta maombi mahakamani na inaweza kuongezwa hizo siku lakini siyo hivyo tu, baada ya hapo suala linakuwa chini ya Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai *(DPP)* ambaye kulingana na uzito wa suala lenyewe anaweza akaomba mahakama kuongeza muda na muda utaongezwa. Suala la ugaidi siyo suala dogo, ni suala ambalo upelelezi wake rahisi kwa sababu ni suala la kimtandao. Kutambua huo mtandao wa ugaidi siyo kitu rahisi tu. Usalama wa nchi hii…*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Mheshimiwa Mbunge leo aliyeuliza swali amekuja salama hapa kwa sababu kuna vyombo vya ulinzi vinamsimamia usalama wake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gekul naomba swali la nyongeza.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti tarehe 12 Januari, 2017 nilifika kwenye Gereza la Babati nikakuta watuhumiwa wa kesi ya mauaji na dawa za kulevya wamekaa zaidi ya miaka minne na sheria haijaweka *time frame,* hizo siku 60 ni kwa makosa ya kawaida. Mheshimiwa Waziri tuambie ni lini mtafanya marekebsho ya sheria ili hata kwa makosa haya ya mauaji na dawa za kulevya watu wasikae magerezani au mahabusu kwa muda mrefu kama ilivyo sasa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kuna baadhi ya makosa na hata makosa mengine yanawafanya Watanzania wengi walioko magerezani kukaa huko kwa muda mrefu. Lakini swali hili lilikuwa linauliza tunachukua hatua zipi? Naomba kumuelezea Mheshimiwa Mbunge hatua ambazo Serikali imezichukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, sasa hivi tunaangalia njia za kuboresha mifumo yetu ya adhabu mbadala ambayo mnafikiri wote Waheshimiwa Wabunge mnajua mmepitisha sheria nyie wenyewe hapa ya *Parole,* kuna suala la *community service* na vilevile kuna kitu kinaitwa *extra mural penal employment,* lakini vilevile ipo haja na hili ni suala pia linawahusu Waheshimiwa Wabunge tukiwaletea bajeti hapa kuongeza vikao vya Mahakama Kuu ambayo Mahakama Kuu ndiyo pekee inakaa kufanya *sessions* kwa ajili ya *murder cases* na wafungwa wengi kwa kweli, mahabusu wengi tunawakuta magerezani wa *murder cases* kwa kweli vikao vya mahakama ni vichache, inabidi tuongeze hiyo *frequency*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile tatu, kuna tatizo sasa siyo tu kwa wale wanao-*face murder cases* hata kwa watuhumiwa wengine kwamba kuna tatizo la ucheleweshaji wa hukumu za mahakama na mwenendo wa mashitaka ambao unawafanya watuhumiwa waweze kwenda mahakamani au wafungwa au mahabusu kwenda mahakamani kudai haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe wito sasa hivi kwa mahakama ku-*adhere*, kuheshimu au kufuata, kutekeleza waraka namba moja wa mwaka jana wa Jaji Mkuu unaotaka mashauri yote na mwenendo wake unapokwisha ichukue siku 21 tu kila kitu kiweze kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba suala la mrundikano wa kesi mahakamani na watu kukaa ndani tumelifanyia kazi kubwa mno na tukiangalia *record* ya nchi hii miaka mitatu iliyopita tulikuwa na mrundikano wa kesi zaidi ya asilimia 60 za zamani, lakini leo mrundikano wa kesi umebakia ni asilimia 5.8 hivi na ambao ni kesi hizo za jinai kama alizoziongelea Mheshimiwa Gekul. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria. Tunaendelea na Mheshimiwa Susan Limbweni Kiwanga, Mbunge wa Mlimba sasa aulize swali lake.

Na. 60

**Ukosefu wa Vituo Vya Polisi Mlimba**

**MHE. SUSAN L. KIWANGA** aliuliza:-

Katika Jimbo zima la Mlimba kuna kituo kimoja tu cha polisi cha Mngeta jambo linalofanya hali ya usalama kwa wananchi kuwa duni.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga vituo vya polisi katika Jimbo la Mlimba?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani naomba kujibu swali la Mheshimiwa Susan Limbweni Kiwanga, Mbunge wa Mlimba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua uhaba wa vituo vya polisi nchini na ili kuimarisha usalama nchini Serikali ina mpango wa kujenga vituo vya polisi hadi ngazi ya kata na tarafa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Mbunge avute subira hadi hapo hali ya fedha itakapokuwa nzuri na kutuwezesha kutekeleza mpango huo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan Limbweni swali la nyongeza.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa majibu ya kunakili kila swali anapoulizwa majibu yake ndiyo haya haya kwa hiyo ana-*copy* na ku-*paste*. Sasa kwa taarifa yako Waziri wa Mambo ya Ndani tarehe 5 Februari, 2017 alifanya ziara katika Jimbo la Mlimba na kuona hali halisi tete ilivyokuwa kule vituo vya polisi vimebandikwa pale TAZARA kwa hiyo hali ni mbaya zaidi ya kiusalama na akatoa ahadi kwenye mkutano wa hadhara baada ya kuona hali ni tete kwamba mwaka huu sisi tutafute kiwanja na kiwanja kimeshatafutwa karibuni ekari 80 kwa matumizi ya umma na sasa tulete ili iingie kwenye bajeti, nakushangaa unajibu swali huwasiliani na Waziri wako.

Sasa je, kwa ahadi aliyotoa Waziri wako tarehe 05 Februari, 2017 Serikali sasa iko tayari kuingiza kwenye mpango wa bajeti ya mwaka 2017/2018 ili Wananchi wa Mlimba wapate kituo cha polisi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu!

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Swali la pili…

**MWENYEKITI:** Nilifikiri umeshamaliza, nimeona unataka kukaa.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Hapana bado.

Kwa kuwa ndani ya Jimbo la Mlimba inafanana kabisa na Jimbo ya Kilombero, katika Makao Makuu ya Wilaya Ifakara, kituo cha polisi cha Wilaya kiko kwenye kituo cha maliasili na wakati wa mvua maji yanajaa askari wanaogelea kama bata. Ni lini sasa Serikali itapeleka pesa katika Mpango wa Bajeti wa mwaka 2017/2018 kuhakikisha wanajenga kituo cha Wilaya ya Polisi Ifakara maeneo ya Kibaoni ambapo kiwanja kimeshapatikana? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka nimhakikishie Mheshimiwa Susan kwamba hakuna kupingana wala kugongana kokote kati ya mimi na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, alichokifanya ndiyo tunakifanya ndiyo msimamo wetu. Alifanya ziara Mlimba na hivi juzi tu nimerudi kufanya ziara katika mikoa minne na nataka nikupe mfano ambao nimeuona katika Mkoa wa Mbeya kwenye Jimbo la

Mbeya Vijijini ambapo Mbunge wake Mheshimiwa Oran amehamasisha wananchi kuweza kutafuta kiwanja, kuchangia fedha za awali za ujenzi na tukaahidi kama ambavyo Mheshimiwa Waziri alivyokuahidi wewe kwamba tutaangalia kama ambavyo jibu langu la msingi nimejibu pale ambapo fedha zitapatikana tuweze kuingiza katika bajeti kwa ajili ya kumalizia nguvu hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi niseme tu kwamba Mheshimiwa Waziri alikuja na aliunga mkono jitihada hizo na naendelea kutoa wito tu kwa Waheshimiwa Wabunge wengine wote, wale ambao wataonakuna haja ya kufanya hivyo, kuongeza jitihada za Serikali kama ulivyotambua tuna upungufu mkubwa sana wa vituo katika nchi nzima. Wilaya, Tarafa na Kata tuna upungufu wa vituo 65 katika wilaya 65 nchi nzima. Kwa hiyo tatizo ni kubwa katika maeneo mengi nchini.

Kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Susan usivunjike moyo, wewe endelea hivyo hivyo kuhamasisha wananchi, wachangishe na Mheshimiwa Waziri ahadi yake iko pale pale kwamba fedha zitakapopatikana tutachangia nguvu hizo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Omary Badwel swali la nyongeza.

**MHE. OMARY A. BADWEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa wananchi wa tarafa ya Chipanga Wilaya ya Bahi, kwa takribani miaka 15 iliyopita waliamua kuchanga wao wenyewe na kujenga kituo cha polisi na wakakikamilisha kwa thamani ya wakati huo shilingi milioni 40.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimehangaika sana, nimempeleka Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani wakati huo alikuwa Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha akakiona kituo akashangaa kwa nini hakifunguliwi, nikampeleka Mheshimiwa Naibu Waziri Silima wakati huo akakiona kituo akaona kwanini hakifunguliwi, lakini pia nimemuandikia sasa barua Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani na Mheshimiwa Naibu Waziri lakini mpaka leo kituo kile hakijafunguliwa.

Sasa nilikuwa nataka kujua hapa leo ama Serikali inatoa kauli ya kufungua kituo cha polisi kile mara moja au itoe kauli ya kutokifungua sisi na wananchi wa tarafa ya Chipanga tukifanyie kazi nyingine? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Badwel pamoja na wananchi wake kwa jitihada hizo lakini nimhakikishie kwamba hili jambo aliwahi kulizungumza mimi sikuwa na hakika na taarifa kwamba mpaka leo bado kituo hicho hakijafunguliwa. Lakini Mheshimiwa Badwel nataka nikuahidi kwamba tukitoka hapa tukae, tufuatilie tuone lini tutafungua kituo hiki ili wananchi waendelee kupata moyo na wsivunjike moyo wa maeneo mengine na Jimbo lako kwa ujumla wake.

**MWENYEKITI:** Naona mko wengi na namuona mmoja tu hapa jirani yangu karibu.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jengo la Polisi la kituo cha Kingeja ni bovu, chakavu, linavuja na jengo hili Serikali walinyang'anya kutoka kwa hao wanaitwa Wakoloni. Kwa bahati mbaya sana wamenyang'anya kutoka kwa hawa wanaitwa wakoloni wakawa wameshindwa kueliendeleza na linahatarisha maisha ya polisi na Naibu Waziri amefika kituo cha Polisi cha Kingeja huku akiwa na ahadi lukuki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka utuambie leo Mheshimiwa Waziri, una mikakati gani ya ziada kuhakikisha kwamba kituo cha polisi cha Kingeja ambacho mlinyang'anya kwa wakoloni, jengo lile sasa hivi linapatiwa ukarabati wa hali ya juu ili polisi wale wasipate madhara yoyote? Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anachokizungumza Mheshimiwa Masoud ni sahihi, binafsi nilifanya ziara katika Jimbo hilo la Mtambile na nilikitembelea hiki kituo, kwa kweli hiki kituo kiko katika hali mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba hatujakaa kimya wala hatujadharau. Tunatambua changamoto kubwa ya ubovu wa kile kituo kama ambavyo vituo vingine vingi katika nchi yetu na kama ambavyo nimezungumza mwanzo kwamba pale ambapo tutapata fedha za ujenzi na ukarabati wa vituo hivyo tutafanya hivyo haraka sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano sasa namkaribisha Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mbunge wa Viti Maalum aulize swali lake.

Na. 61

**Ujenzi wa Barabara ya Old Moshi - Kidia**

**MHE. LUCY F. OWENYA** aliuliza:-

Barabara ya Old Moshi - Kiboriloni - Kikarara - Tsuduni - Kidia yenye urefu wa kilometa10.8 ni muhimu kwa uchumi wa wakazi wa Kata ya Old Moshi Mashariki na Taifa kwa ujumla hasa ikizingatiwa kuwa ni njia mojawapo ya kupanda Mlima Kilimanjaro.

Je, ni lini barabara hii itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami kwa kuzingatia ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne alitoa ahadi ya kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Old Moshi hadi Kidia yenye urefu wa kilometa 10.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Old Moshi - Kiboriloni - Kikarara - Tsuduni hadi Kidia ni barabara ya Wilaya inayohudumiwa na Halmashauri ya Moshi. Hata hivyo, ujenzi kwa kiwango cha lami utatekelezwa na Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* na kwa sasa kazi ya usanifu wa kina wa barabara hii upo katika hatua za mwisho kwa kuwa Mhandisi Mshauri tayari alishawasilisha rasimu ya usanifu ambayo tayari imepitiwa na *TANROADS*. Kwa sasa Mhandisi Mshauri anafanyia marekebisho ya rasimu ya usanifu ili kuzingatia maoni yaliyotolewa na *TANROADS*. Hatua itakayofuata baada ya kukamilika kwa marekebisho hayo ni kutangaza zabuni ili kumpata mkandarasi atakayetekeleza kazi ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami. Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali imetenga jumla ya Shilingi milioni 2,583 ili kuanza ujenzi. Aidha, matengenezo mbalimbali ya barabara hii yanafanywa na Halmashauri ya Wilaya ya Moshi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lucy swali la nyongeza.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kwamba barabara hii inasimamiwa na Halmashauri ya Moshi, lakini kwa kuzingatia kwamba ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais Mstaafu na aliyekuwa Waziri wa Ujenzi Mheshimiwa Magufuli, ambaye ni Rais kwa sasa, katika bajeti ya mwaka 2015 waliahidi kutoa shilingi milioni 810 kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami, lakini mpaka sasa hivi wananchi wa Old Moshi na wa Kilimanjaro kwa ujumla wake hawajaona chochote kinachoendelea zaidi ya ahadi ya pesa ambazo ziko kwenye makaratasi tu.

Sasa tunataka kujua, watupe *time frame,* ni lini barabara hii itaanza na ni lini hii zabuni itapitishwa ili barabara ile iweze kujengwa kwa kiwango cha lami, ukizingatia barabara ile kule Tsuduni kuna vivutio vya utalii, kuna vipepeo, kuna *waterfalls* na kadhalika? Sasa Mheshimiwa Waziri atueleze ni lini barabara hii itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami una hatua. Tunaanza na upembuzi yakinifu, baada ya hapo tunafuata usanifu wa kina na baadaye ndipo tunaingia kwenye ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu Mheshimiwa Fidelis Owenya kwamba barabara hii kutokana na ahadi ambayo Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne aliiitoa tayari imeingizwa katika mchakato. Tumemaliza hatua ya kwanza ya upembuzi yakinifu, sasa hivi tunakaribia kumaliza hatua ya pili ya usanifu wa kina ambapo kilichobakia sasa ni kupata tu taarifa ya mwisho ya msanifu na baada ya hapo barabara hii itaanza kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, isitoshe, kama ambavyo nilivyosema katika jibu langu la nyongeza, Mheshimiwa Owenya barabara hii imeshatengewa fedha kwa mwaka huu wa fedha na bahati nzuri sasa hatua zile za mwanzo ambazo zilikuwa ni za lazima zikamilike kabla ya ujenzi kuanza sasa zinakaribia kukamilika. Nimhakikishie ahadi tutaitekeleza kama ilivyoahidiwa na viongozi wetu wakuu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Seif Gulamali.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza na swali langu napenda kulielekeza kwa Waziri, Wizara ya ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Swali langu linafanana sana na swali lililoulizwa hivi punde; ni lini sasa Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Ziba kwenda Ikinga, Simbo mpaka Tabora na Ziba, Choma mpaka Shinyanga hasa ukizingatia hizi ni ahadi za Mheshimiwa Rais na huu ni mwaka wa 2017? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Seif Gulamali na wananchi wote wa Manonga na Wilaya ya Igunga kwa ujumla, kwamba ahadi zote ambazo viongozi wetu wamezitoa katika kipindi hiki cha miaka mitano tutazitekeleza. Lazima twende hatua kwa hatua, hatuwezi kutekeleza ahadi zote kwa mwaka mmoja wa fedha. Na nimhakikishie tu kwamba kabla ya kipindi hiki cha miaka mitano barabara hii tutakuwa tumeitendea haki kama ambavyo viongozi wetu wakubwa wa kitaifa walitolea ahadi.

**MHE. PASCHAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Barabara ya kutoka Mji Mdogo wa Mlowo Wilaya ya Mbozi kuelekea Kamsamba ni barabara muhimu sana kwa kuwa inaunganisha Halmashauri ya Mbozi lakini pia na Halmashauri ya Momba. Pia barabara hii inaunganisha Mkoa mpya wa Songwe na Mkoa wa Rukwa na Katavi. Je, ni lini Serikali itajenga barabara hii kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nadhani amewahisha swali hili kwa sababu anajua kuna swali lingine zuri kabisa la Mheshimiwa Silinde linakuja; lakini nimhakikishie tu kwamba kila ambapo Serikali hii imeahidi itatekeleza.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru sana. Kwa kuwa barabara inayokwenda katika mbuga za wanyama katika Mkoa wetu wa Iringa ni barabara ya kiuchumi pia na Serikali kwa mara ya mwisho nilipouliza swali hilo iliniambia kwamba inafanya upembuzi yakinifu.

Je, ni lini sasa Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara hiyo kwa sababu hii barabara tunategemea kwamba kama itakuwa imemalizika, uchumi wa Iringa kutumia utalii utaongezeka?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Ritta Kabati pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, walimchukua Waziri wangu wakaenda kuikagua barabara hii na nafahamu aliyowaahidi alipokuwa kule *site*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nikuhakikishie, yale ambayo Waziri wangu aliwaelezeni kule *site* ni lazima tutayatekeleza.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Momba, sasa aulize swali lake.

Na. 62

**Ahadi ya Ujenzi wa Daraja la Kamsamba - Kilyamatundu**

**MHE. DAVID E. SILINDE** aliuliza:-

Ahadi ya Rais wa Awamu ya Nne Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete ya ujenzi wa daraja la Kamsamba–Kilyamatundu bado haijatekelezwa tangu mwaka 2009.

Je, ni upi mpango wa Serikali ya Awamu ya Tano kukamilisha ujenzi wa daraja hilo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Momba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Daraja la Momba lililopangwa kujengwa katika barabara ya Mkoa ya Kibaoni - Muze - Ilemba - Kilyamatundu na barabara ya Mkoa ya Kamsamba hadi Mlowo ni kiunganishi muhimu cha Mkoa wa Rukwa katika eneo la Kilyamatundu na Mkoa wa Songwe katika eneo la Kamsamba. Kukamilika kwa ujenzi wa daraja hilo kutarahisisha usafirishaji wa abiria na mizigo kutoka sehemu moja kwenda nyingine, kuimarisha shughuli za kijamii na kiuchumi katika Bonde la Ziwa Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza azma hiyo, Serikali ya Awamu ya Tano imepanga kuanza ujenzi wa daraja hilo katika mwaka huu wa fedha 2016/2017. Zabuni za ujenzi wa daraja la Momba ziliitishwa tarehe 11 Januari, 2017 kwa ajili ya kumpata Mkandarasi. Mara baada ya hatua hii ya zabuni na tathmini kukamilika, mkataba kwa ajili ya kuanza ujenzi utasainiwa. Aidha, katika mwaka wa fedha 2016/2017 kiasi cha shilingi bilioni 2.935 zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa daraja hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Silinde swali la nyngeza.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Hili swali la ujenzi wa daraja ninaliuliza leo ni mwaka wa saba mfululizo nikiwa ndani ya Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada ambazo nimeanza kuziona ambazo zinaweza kuzaa matunda hivi karibuni, ni kwamba wametangaza *tender* tarehe 11.01.2017; sasa ninachotaka kujua ni kwamba, ili tupunguze maneno maneno mengi, je, Serikali itakamilisha lini utaratibu wa tenda ili ujenzi huo uanze? Wananchi wangu kule wameshachoka *story* hizi wanataka waone daraja likiwa limejengwa kwahiyo hicho ndiyo kitu cha kwanza, *commitment* ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la pili; ni kwamba palipokuwa na ahadi ya ujenzi wa daraja ilikuwa inaambatana na muendelezo wa ujenzi wa barabara ambayo Mheshimiwa Haonga alikuwa ameuliza katika swali la nyongeza kutokea pale Kamsamba mpaka Mlowo kilometa 166.

Sasa ninachohitaji kujua ni kwamba wakati wa awamu ya nne Waziri Mkuu alipokuwa analijibu hili swali alisema umeingizwa katika mradi wa *MCC 3* lakini bahati mbaya wale watu wa Marekani wa *MCC 3* walishajitoa katika kuhudumia miradi ya ndani ya nchi yetu. Sasa, je, Serikali ile miradi ambayo iliondolewa na *MCC* katika Serikali hii ya Awamu ya Tano itatekelezwa vipi ili kuhakikisha kwamba daraja linakamilika na liendane na ujenzi wa lami? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi Mheshimiwa Mbunge na ninaamini ni kwa niaba ya wananchi wake, wanahoji udogo udogo au utaratibu unaotumika, kwamba kasi yake kama ya konokono. Mimi nikuhakikishie, hii ni Serikali ya Awamu ya

Tano, Serikali hii iko tofauti, Serikali hii imewaahidi wananchi sehemu mbalimbali na umeshaanza kuona sehemu mbalimbali magoli yanaanza kufungwa. Ninakuhakikishia na goli lako litafungwa, daraja na hizo barabara ninazoongelea kabla ya miaka hii mitano haijakwisha. Tuache utaratibu huu wa kitaalam ukamilike na nina uhakika kwa kuwa wameshaanza haitachukua muda kuikamilisha hii kazi ya usanifu na mimi mara baada ya hapo, kwa kuwa fedha tayari tunazo nitahakikisha nalisimamia hili eneo likamilike na hasa kwa sababu mwenzako, jirani yako; na mimi nawasifu sana ninyi Wabunge wawili, wewe na Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha. Ninawasifu sana kwa ushirikiano mnaotumia katika kuhakikisha Daraja la Momba linajengwa.Ni daraja linalohudumia watu, halina Silinde wala halina Ignas Malocha. Mheshimiwa Ignas Malocha anakuja ofisini, Silinde anauliza hapa, wote wanawalenga wananchi wa Momba pamoja na watu wa Kwela.

Mimi niwahakikishie, kazi hii tutaifanya kwa umakini na kama ambavyo tumekuwa tukiwaahidi tutaikamilisha kwa wakati muafaka kabla hiki kipindi chetu hakijaisha.

**MWENYEKITI:** Haya nimeuona Mheshimiwa Komu.

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa hali ya Momba ni sawa sawa na Moshi Vijijini, kwa sababu Rais wa Awamu ya Nne Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete aliahidi kujenga barabara ya Kibosho kwa Raphael kupitia *central* mpaka *International School;* na kazi hiyo ilianza lakini mkandarasi ameondoka *site*. Vilevile Rais wa Awamu ya Tano Mheshimiwa John Pombe Magufuli aliahidi kujenga barabara ya Mamboleo mpaka Uru Shimbwe kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nijue ni lini ahadi hizi zitatekelezwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri kama unalo jibu hapo kuhusu hili swali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Mheshimiwa Komu tuonane ili anipe taarifa za zaidi hasa ya huyo mkandarasi ambaye anasema ameondoka *site*. Njoo ili tuhakikishe huyo mkandarasi anarudi kwa sababu tulishatoa maelekezo wakandarasi wote ambao walikuwa wamesimama kwa sababu ya kutolipwa warudi *site,* sasa nashangaa leo naambiwa kuna mkandarasi huku tena kwenye barabara muhimu sana ya ndugu zangu kule wa Kilimanjaro. Hebu njoo ofisini

tuongee kwa undani tulifanyie kazi na wataalam wetu wa Mikoa wa *TANROADS* au wa Halmashauri.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, naona Mheshimiwa Komu amefurahia hili suala. Mheshimiwa Flatei Massay.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti nikushukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Daraja la Magala na barabara yetu ya Karatu - Mbulu - Haydom - Sibiti Mheshimiwa Waziri aliahidi kwamba itaanza upembuzi yakinifu, sasa swali, je, barabara hii iko kwenye hatua gani, upembuzi yakinifu na lini anafikiri kwamba itaanza ujenzi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Mheshimiwa Massay, tulikubaliana kwamba twende *site* kwa sababu kuna mambo kama matatu ya msingi katika eneo lake. Mimi nimuombe, tutakapofika *site* tukaifanya kazi inayokusudiwa kuifanya baada ya hapo kama kutakuwa na maswali zaidi ndipo aulize, lakini kwa sasa nimhakikishie kwamba ahadi yangu ya kwenda *site* iko pale pale na tumekubaliana kipindi gani twende. Mimi naomba tuitumie fursa hiyo kushughulikia mambo makubwa yote matatu ikiwa ni pamoja na Daraja la Mto Ugala, barabara hiyo aliyoitaja Karatu - Mbulu - Haydom vilevile pamoja na wale watu wa Yaeda Chini ambao hawana mawasiliano ya simu.

**MWENYEKITI:** Tunaendela na Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde, Mbunge wa Mtera sasa aulize swali lake.

Na. 63

**Ahadi ya Barabara za Lami Katika Jimbo la Mtera**

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE** aliuliza:-

Rais wa Awamu ya Nne alipotembelea Jimbo la Mtera katika kijiji cha Mvumi Misheni aliahidi kutujengea barabara ya lami kutoka Mlowa barabarani hadi Mvumi Misheni kwenye Hospital Teule ya Wilaya ya Chamwino. Pia Rais wa

Awamu ya Tano katika kampeni zake alipofika Mvumi Misheni alisisitiza kuwa barabara hiyo itajengwa haraka iwezekanavyo.

Je, ujenzi huo utaanza lini?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimwa Livingstone Joseph Lusinde, Mbunge wa Mtera kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa Rais wa Awamu ya Nne alipotembelea Jimbo la Mtera katika Kijiji cha Mvumi Misheni aliahidi kujenga barabara ya lami kutoka Mlowa barabarani hadi Mvumi Misheni kwenye Hospitali Teule ya Wilaya ya Chamwino. Aidha, ni kweli kuwa wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, Rais wa Awamu ya Tano naye aliahidi kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumfahamisha Mheshimwa Mbunge kuwa Serikali inatambua umuhimu wa barabara hii kwa jamii na hususan katika kusaidia wagonjwa wanaoenda kupata huduma ya matibabu katika hospitali ya Mvumi Misheni. Kwa kuzingatia umuhimu huo, azma ya Serikali ya kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami iko pale pale na itatekelezwa kulingana na upatikanaji wa fedha. Aidha, kwa sasa barabara hiyo itaendelea kuhudumiwa na Serikali kupitia Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa kufanya matengenezo ya aina mbalimbali kwa kiwango cha changarawe kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara ili iendelee kupitika majira yote ya mwaka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lusinde swali la nyongeza.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake. Hata hivyo napenda niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, punde wakati akijibu maswali leo asubuhi, amesema barabara ili ijengwe kwa kiwango cha lami inapitia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina; na kwa muda aliouonyesha ni kama vile kila kitendo kinachukua zaidi ya miaka miwili.

Je, kwa miaka iliyobaki kabla hata ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina haujaanza kufanyika, Waziri anawahakikishiaje wananchi wa Jimbo la Mtera kwamba barabara hiyo itakamilika mwaka 2020?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Mheshimiwa Naibu Waziri amesema barabara hiyo itaendelea kujengwa kwa kiwango cha changarawe na sasa hivi barabara hiyo bahati nzuri inajengwa. Je, Naibu Waziri yuko tayari kuongozana na mimi ili akaone hicho kiwango cha changarawe anachokisema kwamba kinajengwa badala ya kiwango cha changarawe naona wanajenga kwa kiwango cha tope, yuko tayari twende tukaone *site?* Ahsante

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibi kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Lusinde kwa kazi kubwa anayofanya ya kuwatetea wananchi wa Mtera.

Mimi nimhakikishie, Serikali hii iko pamoja naye na hicho anachokidhania kwamba inachukua zaidi ya miaka minne kufanya hizi kazi mbili, kwanza hii barabara siyo ndefu sana kwa hiyo, haitaweza kuchukua miaka minne. Ni barabara fupi na tunaweza tukaingia kwenye hatua ya *design and build*, kwa maana ya unafanya yote kwa wakati mmoja. Nikuhakikishie tu ahadi yetu kwenye hilo tutaitekeleza kwanza hii barabara ni ndogo sana. Siamini kama wewe unafahamu ni barabara fupi inayohitaji gharama siyo kubwa sana kwa hiyo, tutaikamilisha kwa wakati kabla ya kipindi hiki cha miaka mitano hakijaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, kwa kweli naomba kwa heshima kabisa ikiwezekana hata leo jioni hebu twende tukalione hili ili tuweze kulishughulikia kwa haraka. Kama ni kweli ni tope siyo sahihi kabisa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa mmeshakuwa wengi sasa, Mheshimiwa Zakaria Issaay halafu baadaye Mheshimiwa Waitara.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba nichukue nafasi hii kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri hayakugusa ahadi ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa katika barabara ya Mji wa Mbulu na ahadi hiyo iliwagusa wananchi wa Mji wa Mbulu wakati wa uchaguzi. Je, Mheshimiwa

Naibu Waziri anatuambia nini kuhusu utekelezaji wa ahadi hii ambayo imesahaulika, hadi sasa mwaka mmoja umeisha baada ya uchaguzi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii hatujaisahau. Tulichokifanya katika mwaka wa kwanza ni kutekeleza barabara zile ambazo wakandarasi walikuwa wameondoka *site* kwa kutolipwa madeni yao, na unaona kwamba sasa hivi tumefanya kazi kubwa sana na barabara nyingi zinaanza kukamilika baada ya kulipa madeni ambayo walikuwa wanayadai. Nimhakikishie, kuanzia bajeti ijayo, tunaanza sasa, kwanza kukamilisha zile barabara zilizobakia za nyuma ili tusiwe tunadaiwa daiwa riba pamoja na usumbufu, lakini vilevile tuanze sasa kwa kiwango chochote tutakachoweza kwa mwaka ujao wa fedha barabara zile mpya tulizoziahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie katika safari yangu ambayo Mheshimiwa Massay tumekubaliana tutafika mpaka Mbulu na ninadhani nitalala Mbulu Mjini ili tuliangalie hilo kwa undani pamoja na hayo matatizo matatu makubwa ambayo nimeyaongea kabla.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waitara halafu tutamalizia na Mheshimiwa Hawa Ghasia.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida ya barabara ya Jimbo la Mtera inafanana sana na shida ya barabara ya Jimbo la Ukonga. Barabara ya kutoka Banana - Kitunda - Kivule - Msongora ni barabara ambayo imeahidiwa kwa miaka ishiri ambapo Mheshimiwa Rais wa sasa alikuwa Waziri kwenye eneo hilo aliahidi na haikutekelezwa, miaka kumi ya Mheshimiwa Kikwete iliahidiwa haikutekelezwa. Kwenye bajeti ya mwaka jana ilionyesha kuwa *TANROADS* wanasaida kujenga angalau kilometa 3.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapozungumza hapa walishaenda wakafanya *survey* wakapata na mkandarasi yupo anasubiri. Shida iliyopo ni kwamba fedha hazipo na ieleweke tu kwamba barabara hii ndiyo inayohudumia Kata ya Kitunda, Kata ya Mzinga, Kata ya Kivule, Kata ya Msongora na mojawapo ya shida ya barabara hii imeleta madhara makubwa kwa sababu shule zilizoongoza kwa kufanya vibaya, shule ya msingi Kitonga ipo eneo hili na shida

mojawapo ya watoto wale kufeli ni kwamba wanatoka mjini kati, wanaenda kule hakuna usafiri wanatembea kwa miguu, kwa hiyo wanatega shule na wamefeli ndiyo maana wakaomba walimu wasiadhibiwe kwa sababu hii.

Sasa naomba nimuulize Mhesimiwa Naibu Waziri ni lini baabara hii itaweza kutengenezwa kwa kiwango cha lami au hata changarawe ili magari yatoke Banana mpaka Msongora – Kitonga, walimu na watumishi wengine, wanafunzi waende shuleni kwa uhakika kupunguza shida iliyopo sasa? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waitara anafahamu kwamba tatizo hili aliliwasilisha kwangu vilevile kupitia kwa Afisa Elimu Sekondari ambaye naye alilalamika sana kuhusiana na kufeli shule zake, kuwa za mwisho katika Mkoa wa Dar es Salaam; na alisema kwamba mchango mmojawapo ni matatizo ya hii barabara na wanafunzi wanapangiwa kule mbali kwa sababu shule za karibu huwa zinajaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimuhakikishie, Serikali imelichukua hili, tutalishughulikia ili turekebishe haya. Naomba unipe fursa niwasiliane na *TANROADS* Mkoa wa Pwani nipate taarifa zao za karibuni maana yake nilishawaambia kuhusu hili tatizo baada ya kupata hiyo taarifa kutoka kwa Afisa Elimu wa Sekondari wa Wilaya ya Ilala, na baada ya kujua sasa alifanya nini baada ya malalamiko yale nitakuja nikuambie hatua ipi tunaichukua.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri, tunamalizia na Mheshimiwa Hawa Ghasia.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru kwa kunipa nafasi nilulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya kutoka Mtwara hadi Newala – Masasi kipande cha kutoka Mtwara hadi Nnivata *tender* ilishatangazwa, na kwa mujibu wa maelezo ya Meneja *TANROADS* Mtwara ni kwamba mkataba ulisainiwa tarehe 16 Januari, lakini ukimuuliza Waziri anasema hajui, Naibu Waziri hajui na wengine wanakwambia mara mkataba uko kwa Ofisi ya Mwanasheria wa Serikali. Sasa nilitaka kujua mkataba umesainiwa au haujasainiwa na inachukua muda gani kujua ndani ya ofisi hiyo hiyo inamchukua Waziri muda gani kupata taarifa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Ghasia na kupitia kwake na wananchi wake wa Mtwara Vijijini kwamba Serikali kama ambavyo imepanga kwenye bajeti ya kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami katika mwaka huu wa fedha itatekeleza ahadi hiyo na tofauti ambayo ameieleza kati ya tunachokifahamu sisi na anachoambiwa na *TANROADS* Mkoa kule kimetokana na sintofahamu iliyotokea kwa mkandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kila kitu kukamilika na *document* kuwa tayari kusainiwa kuna kipengele ambacho ilibidi Mwanasheria Mkuu wa Serikali akikamilishe kukiangalia na kukiweka sawa kabla mkataba haujasainiwa.

Kwa hiyo, ninavyofahamu mimi na kwa namna Mheshimiwa Waziri wangu alivyonieleza na namna nilivyoambiwa na *TANROADS* pamoja na Katibu Mkuu mkataba huu utasainiwa muda wowote katika wiki hii kwa sababu Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu namshukuru ametusaida kulitatua lile tatizo ambalo lilikuwa linatusumbua, kwa hiyo mkataba utasainiwa muda wowote kati ya wiki hii na wiki ijayo. Kikubwa na cha msingi fedha tumetenga, tuko tayari kuanza ujenzi, *process* za kumpata mkandarasi wa kujenga tayari sasa zimefikia mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba Mheshimiwa Ghasia pamoja na mengi anayotushauri kwenye hili atuvumilie kidogo, lakini kubwa ni kwamba zile fedha tulizozitenga shilingi bilioni 21 zitatumika katika mwaka wa fedha kuanza ujenzi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Nabu Waziri. Sasa tunaendelea Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, tunaanza na Mheshimiwa Steven Hilary Ngonyani Mbunge wa Korogwe Vijijini karibu uulize swali lako.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuuliza swali langu nataka kutoa neno la shukrani. Naomba niseme yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, Makamu wa Rais Mheshimiwa Samia Hasan Suluhu, Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Job Ndugai, Naibu Spika Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Katibu wa Bunge Ndugu Dkt. Thomas Kashililah, Waziri wa Afya Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Waheshimiwa Wabunge wote bila kujali vyama vyao pamoja

na Waheshimiwa Mawaziri. Nilitembelewa na Wabunge 265, haijawahi kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nisiwasahau wafanyakazi wa Ubalozi walioko India ambao walinipokea na kunidhibiti na kunifanyia kila kilichokuwa kinahitajika na leo hii nimerudi ndani ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya machache naomba swali langu namba 64 lipatiwe majibu. *(Makofi)*

Na. 64

**Kampuni ya Katani Kutowalipa Wakulima Fedha Zao**

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI** aliuliza:-

Wakulima wadogo wadogo wa mkonge wamekuwa wakiuza mkonge kwa Kampuni ya Katani lakini kampuni hiyo imekuwa haiwalipi wakulima fedha zao.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha wakulima wanalipwa fedha zao kwa wakati?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijajibu swali na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge wote kumkaribisha Mheshimiwa Ngonyani tena Bungeni, lakini zaidi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kumrejesha salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme vilevile kwamba kuna kitu ambacho mimi kimenigusa sana. Muda wote ambao Mheshimiwa Ngonyani amekuwa mgonjwa hakusita kuendelea na majukumu yake ya Kibunge kwani aliendelea kuwasiliana na Wizara yangu kuwatetea wananchi wake na hata hili swali ambalo ameuliza, amepiga simu mara nyingi sana kuulizia madeni ya wananchi wake wanaodai madai ya Katani, kwa hiyo, ameonyesha uwakilishi uliotukuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Steven Hilary Ngonyani, Mbunge wa Korogwe Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na malalamiko ya wakulima wadogo wa mkonge walio chini ya *scheme* ya *Sisal Smallholders and Outgrowers Scheme (SISO)* ya kutoridhika na ucheleweshwaji wa malipo yao kwa mkonge unaosindikwa na Kampuni ya *Katani Limited*. *Scheme* hii inaendesha kilimo cha mkataba ambapo chini ya mfumo huu *Katani Limited* ni mnunuzi na msindikaji wa mkonge wa mkulima wakati mkulima ana wajibu wa kupanda, kutunza, kuvuna na kusafirisha mkonge wake hadi kwenye kiwanda (Korona) inayomilikiwa na *Katani Limited* katika shamba husika kwa ajili ya kusindikwa.

Kwa mujibu wa mkataba kati ya mkulima na *Katani Limited*, Katani inapaswa kumlipa mkulima fedha zake ndani ya siku 60 baada ya kusindika mkonge wa mkulima, na inapotokea kampuni ya Katani kuchelewesha malipo zaidi ya siku 60, inalazimika kumlipa mkulima malipo hayo pamoja na riba ya asilimia 1.5 ya malipo hayo kwa kila mwezi uliocheleweshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumetokea ucheleweshwaji wa malipo haya kwa mwaka 2016 kutokana na kuyumba kwa masoko ya mkonge duniani na kushuka kwa bei za mkonge. Kampuni imelazimika kuuza shehena iliyokuwepo japo kwa hasara na hivyo hadi sasa wakulima wanadai malipo ya mkonge waliovuniwa ya miezi mitatu yaani Septemba hadi Novemba, 2016 ambayo hayajalipwa. Malipo ya miezi hiyo mitatu yanatarajiwa kufanyika mwezi Februari, 2017 yaani mwezi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Bodi ya Mkonge Tanzania imekuwa ikichukua hatua za kuhakikisha kwamba wakulima wanalipwa fedha zao kwa wakati.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri wa Kilimo. Nilikuwa na swali dogo tu la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa zao la mkonge ni moja ya mazao yanayoiingizia nchi yetu kipato, na kwa kuwa wakulima wa mkonge katika Jimbo la Korogwe Vijijini na hasa Mkoa wa Tanga wamekuwa wanajitahidi sana kulima mkonge ili wajinufaishe wao na familia zao na kuwasomesha watoto wao, je, Serikali itawasaidiaje ili wapate kulipwa haraka fedha walizokuwa wanadai kwenye Mamlaka ya Mkonge au *Katani Limited* ili ziweze kuwasaidia kuendesha na kustawisha zao la mkonge hapa nchini?

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi kabisa.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba zao la mkonge ni zao muhimu sana na linaloingizia wakulima pamoja na nchi fedha nyingi. Kwa taarifa tuilizonazo ni kwamba mwaka 2014/2015 mkonge uliingizia nchi dola za Kimarekani milioni 35.4 na kwa sasa uzalishaji umefikia kiwango cha tani 40,000. Kwa sasa sisi ni nchi ya pili baada ya Brazil inayozalisha tani 150,000 za mkonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itahakikisha kwamba wakulima wanaendelea kufaidika na kuinuka tena kwa zao la mkonge fahari ya watu wa Tanga ambapo kwa sasa tunafuatilia kuhakikisha kwamba wakulima wanalipwa fedha zao miezi mitatu na ndiyo maana nimemueleza Mheshimiwa Mbunge kwamba fedha zinategemewa kulipwa mwezi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nieleze tu kwamba kilio hiki cha wakulima kucheleweshewa fedha siyo cha Mheshimiwa Ngonyani peke yake, Wabunge karibu wote wa Mkoa wa Tanga wamekuwa wakiulizia kuhusu hizi fedha, na Mheshimiwa Mbunge wa Pangani amelalamika sana kuhusu hili na nimuahidi Mheshimiwa Nyonyani na Wabunge wote wa Tanga baada ya Bunge hili mimi mwenyewe naondoka naelekea Tanga kwenda kushughulikia kwa karibu zaidi kuhakikisha kwamba fedha za wakulima zinalipwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa vile Mwenyezi Mungu amejaalia Mheshimiwa wetu Stephen Hilary Ngonyani kurudi salama kwa dua zenu. Kwa hiyo, naomba swali hili tumuachie liishie kwake ili tumuombee dua zaidi awe na afya njema.

Tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango tunaingia sasa tunae Mheshimiwa Machano Othman Said kutoka Baraza la Wawakilishi naomba aulize swali lake.

Na. 65

**Malalamiko ya Utozwaji wa Riba Kubwa Kwenye Mabenki**

**MHE. MACHANO OTHMAN SAID** aliuliza:-

Kwa muda mrefu kumekuwa na malalamiko ya wananchi, watumishi wa umma na wafanyabiashara juu ya riba kubwa inayotozwa na benki zetu kwa wale wanaochukua mikopo hali ambayo inarudisha nyuma juhudi zao za kupunguza umaskini na kwa kuwa Benki Kuu ndiyo inayosimamia mabenki yote nchini.

(a) Je, ni lini Serikali kwa kupitia benki zetu nchini itaweka utaratibu wa kupunguza riba ya mikopo walau kufikia 10% -12% badala ya riba ya sasa ambayo ni 17% - 20%?

(b) Kwa kuwa mikopo inayotolewa kwa watumishi wa umma ni salama zaidi kwa mabenki, je, benki hizo haziwezi kuweka riba maalum?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Machano Othman Said, Mbunge Baraza la Wawakilishi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ya sekta ya fedha ya mwaka 1991 yalipelekea Serikali kujitoa katika uendeshaji wa moja kwa moja wa shughuli za kibenki nchini ili kuruhusu mfumo wa soko huria, hususan nguvu ya soko kuamua viwango vya riba za mikopo, riba za amana na gharama zingine za huduma za kibenki. Viwango vya riba za mikopo na riba za amana, pamoja na riba za mikopo kati ya benki na benki hupangwa kwa kuzingatia gharama za upatikanaji wa fedha, gharama za uendeshaji, riba za dhamana za Serikali, sifa za mkopaji na hatari ya mkopaji kutolipa mkopo, pamoja na kasi ya mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoa maelekezo kwa mabenki kutumia viwango fulani vya riba katika biashara zao kutaifanya Benki Kuu kukosa nguvu na mamlaka ya kuyachukulia mabenki hatua endapo yatapata hasara kwa kutumia riba ambayo Benki Kuu imeelekeza. Hivyo basi, kwa mujibu wa Sheria ya Taasisi za Fedha ya mwaka 1991, Serikali haina mamlaka kuweka ukomo wa riba au riba elekezi itakayotumiwa na mabenki katika kutoa mikopo.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwango cha hatari ya kutolipa mkopo ni miongoni mwa vigezo vinavyotumiwa na mabenki katika kupanga viwango vya riba za mikopo. Aidha, kwa sehemu kubwa gharama za riba za mikopo hutegemea zaidi gharama za upatikanaji wa fedha pamoja na gharama za uendeshaji.

Pili, ni muhimu kutambua kwamba kadri riba za mikopo zinapokuwa juu, ndivyo riba za amana zinapokuwa juu pia. Mfano; wastani wa riba za kukopa kwa mwaka mmoja mwezi Juni, 2016 ulikuwa ni asilimia 13.67 wakati wastani

wa riba za amana za mwaka mmoja ulikuwa ni asilimia 11.52 ikiwa ni tofauti ya asilimia 2.25

**MHE. MACHANO OTHMAN SAID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, naomba niulize maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza ni kwamba kutokana na kwamba hii Sheria ya Fedha ipo kwa muda mrefu tangu mwaka 1991, na kutokana na mabadiliko ya kidunia ya uchumi na baadhi ya nchi jirani kubadilisha sheria hizi katika nchi zao; je, haaoni kwamba umefika wakati kwa Serikali kubadilisha sheria hii?

Na la pili, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba riba katika mwezi wa Juni, 2016 ilikua kwa kiwango cha 13.46 lakini ukweli halisi ilikuwa ni kati ya 16 mpaka 18. Katika swali langu niliuliza je, haoni kwamba Serikali inahitaji ichukue juhudi maalum kwa wafanyakazi wa Serikali kwa sababu fedha zao kulipwa ni rahisi na zina dhamana zaidi, anaonaje Mheshimiwa Waziri?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza anauliza utayari wa Serikali kubadilisha sheria, naomba nilikumbushe Bunge lako Tukufu, tuko katika soko huria na tunafuata soko huria hivyo haiwezekani kurudi katika kuelekeza mabenki yetu. Kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, Benki Kuu ikifanya hivyo itakosa mamlaka sasa ya kuyasimamia mabenki hayo pindi yatakapopata hasara kutokana na riba elekezi iliyoyatoa. Hivyo nashauri tu tuendelee na mfumo uliopo kwa sababu tupo katika mfumo wa soko huria na hii pia ni *global practice* hivyo siamini kwamba ni njia njema kwa nchi yetu kuweza kurejea katika maelekezo kwa ajili ya riba zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, naomba niseme kwamba kuhusu kutoa riba elekezi kwa wafanyakazi pia haiwezekani kwa sababu riba tunazoziona zinakuwa ni wastani wa riba ambazo zimetolewa kutoka katika sekta na makundi mbalimbali, hivyo tukisema wafanyakazi tuwape riba nafuu itapelekea makundi mengine ambayo hasara yake au vihatarishi ni vya juu kupata riba kubwa sana na hivyo tutakuwa tumewaumiza.

Kwa hiyo, niliombe Bunge lako Tukufu na Wabunge kwamba tukubaliane na wastani huo ambao hutolewa na Benki Kuu baada ya kupata sasa riba zote kutoka katika mabenki yetu yote.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam Msabaha.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, na mimi naomba kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa wajasirimali wadogo wadogo hasa mama lishe na wamachinga na ambao wengine wana vipato vya chini wamekuwa wakikopa mikopo kwa ajili ya biashara zao na kutozwa riba kubwa na kushindwa kurejesha mikopo ile na kufilisiwa.

Je, Serikali ina mikakati gani kuhakikisha inatafuta fedha kwa ajili ya Wajasiriamal wadogo wadogo na kuwatoza riba ambayo inaendana na biashara zao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nilikumbushe Bunge lako tukufu kwamba tayari Serikali imeshatunga sera ya huduma ndogo za fedha za mwaka 2016 na sasa tupo katika hatua nzuri kuja na sheria katika Bunge lako tukufu ili kuwalinda wajasiriamali wadogo wanaokopeshwa kwa riba kubwa. Ni imani yangu sheria hii itakapokuwa imepitishwa watakopa katika viwango halisi ambavyo viko sokoni na sivyo ambavyo wanaonewa kwa sasa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, tunaendelea na Mheshimiwa Tauhida Cassian Galoss Nyimbo, Mbunge wa viti maalum sasa aulize swali lake.

Na. 66

**Uchongaji wa Vinyago na Biashara Zake**

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS NYIMBO** aliuliza:-

Kumekuwepo na malalamiko ya muda mrefu yanayotolewa na wachongaji wa vinyago hasa pale wanunuzi wa vinyago hivyo kutoka nje wanaponyang'anywa bidhaa hiyo wafikapo *airport* kwa madai mbalimbali ikiwemo kutolipa kodi.

(a) Je, vinyago hivyo ambavyo ni biashara ya wanyonge baada ya kuzuiliwa hupelekwa wapi?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kwa kufanya hivyo kunawapotezea wateja na soko kwa wanaofanya ujasiriamali wa aina hiyo lakini pia kuwaingizia hasara?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, vinyago sio miongoni mwa bidhaa zinazotozwa kodi au ushuru kwa bidhaa zinazosafirishwa nje ya nchi. Ikiwa vinyago vilizuiliwa uwanja wa ndege au mpakani, sio kwa sababu ya kutolipiwa kodi au ushuru wa forodha. Utaratibu unaotumika kimataifa ikiwemo nchi yetu katika kushughulikia bidhaa zozote zinazokamatwa kwenye sehemu za kuingia au kutokea nje ya nchi kama viwanja vya ndege na mipakani ni wa aina mbili:-

Moja, kuziharibu au kuziteketeza bidhaa hizo au kuzipiga mnada. Bidhaa zinazoharibiwa au kuteketezwa ni zile ambazo ni hatari kwa usalama wa nchi au kwa afya ya binadamu, kwa mfano, silaha, vyakula au kemikali zilizobainika kuwa si rafiki kwa matumizi ya binadamu na mazingira. Bidhaa nyingine ambazo haziangukii kwenye kundi hilo, ikiwa ni pamoja na vinyago hupigwa mnada na baada ya kuondoa gharama zozote za uhifadhi, mapato yake huingizwa Serikalini. Kwa kuwa swali la Mheshimiwa Tauhida halijabainisha ni lini na ni wapi vinyago hivyo vilikamatwa, idadi yake au taasisi au mamlaka ipi ilikamata vinyago hivyo ni vigumu kueleza vinyango hivyo vilipelekwa wapi.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuzuia vinyago au bidhaa nyingine yoyote inaposafirishwa nje ya nchi, hufanyika tu baada ya kubainika kuwa kuna ukiukwaji wa sheria na kanuni. Kwa hiyo, lengo la kufanya hivyo ni kujiridhisha kuwa wadau wote wa biashara au bidhaa hiyo wanafuata sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa ili asiwepo yeyote mwenye kupoteza mapato yanayotokana na biashara au bidhaa hiyo ikiwemo Serikali yetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tauhida swali la nyongeza.

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS NYIMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia fursa hii ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza pamoja na majibu aliyonipa Mheshimiwa Waziri lakini sikuridhika na majibu haya.

Mheshimiwa Waziri katika majibu yake ya msingi anasema kwamba kati ya bidhaa ambazo hazitozwi kodi pamoja na vinyago, lakini katika swali hilo hilo la msingi anabainisha kwamba kati ya vitu vinavyokamatwa na kupigwa mnada ni pamoja na vinyago. Mheshimiwa Waziri katika suala hili ulivyolijibu huoni kwamba umejichanganya? Kama vinakamatwa na kupigwa moto, vinakamatwa kwa kosa lipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kuuliza swali la pili, je, Serikali imetoa elimu yoyote kuhusiana na suala zima la uuzaji wa vinyago kwa wajasiriamali wadogo wadogo ukizingatia Mheshimiwa Rais ameondosha kodi ndogo ndogo kwa wajasiriamali?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, naomba nikiri kwamba sijamchanganya, vinyago tunafahamu ni bidhaa zinazotokana na maliasili za nchi yetu hivyo inawezekana watu wa Wizara ya Maliasili wanatozo zao ambazo wanazitoza. Mimi nimekanusha utozaji wa kodi ambao tunatoza sisi kama Wizara ya Fedha kwamba hizi hazipo katika orodha ya bidhaa tunazozitoza kodi *(extport duty)*. Kwa hiyo, ndiyo maana katika jibu langu la sehemu ya pili nilisema yawezekana zilikuwa zinatakiwa kulipiwa tozo mbalimbali kutoka katika Wizara ya Maliasili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, elimu ya ujasiriamali tunaendelea kuitoa, kuna kitengo ndani ya Wizara yangu ya Fedha na tunaendela kuifanyia kutoa elimu ya ujasiriamali kwa wajasirimali wote nchini wakiwepo wafanyabiashara wa vinyago.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mhesimiwa Naibu Waziri wa Fedha, tunaendelea sasa Wizara ya Nishati na Madini, tunaanza na Mheshimiwa Mussa Ramadhan Sima, Mbunge wa Singida Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 67

**Mahitaji Makubwa ya Umeme Jimbo la Singida Mjini**

**MHE. MUSSA R. SIMA** aliuliza:-

Kuna mahitaji makubwa ya umeme katika Jimbo la Singida Mjini hususani katika kata za pembezoni kama vile Kisaki, Mtama, Mtipa, Mwankoko, Uhamaka, Unyambwa, Unyamikombi na Unyianga.

(a) Je, Serikali ina mpango gani kuvipatia umeme vijiji katika mwaka huu wa fedha?

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kutumia rasilimali ya nguvu ya upepo iliyopo Singida ili kuongeza nishati ya umeme?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Ramadhan Sima, Mbunge wa Singida Mjini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata za Kisaki, Mtama pamoja na Mtipa pamoja na Mwankoko zimejumuishwa katika mradi kabambe wa *REA III* unaoanza mwezi Machi, 2017. Katika kazi hizi, maeneo haya yatapelekewa mradi kupitia *desification, grid extension* pamoja na *renewable* utakaoanza mwezi huo nilioutaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kupeleka umeme kwenye vijiji hivyo inajumuisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilometa 105, ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilometa 126.9, ufungaji wa transfoma 31, pamoja na kuwaunganishia wateja wa awali 1,111. Kazi hii itagharimu shilingi bilioni 8.15.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa muda mrefu wa Serikali ni kutumia vyanzo mbalimbali vya kuzalisha umeme ikijumuisha upepo uliopo katika eneo la Singida ambapo katika mpango kabambe wa kuendeleza sekta ya umeme wa mwaka 2016, mradi huu umepangwa kuanza kuzalisha megawati 50 za awamu ya kwanza mwaka 2018. Mradi huu unakadiriwa kugharimu dola za Marekani 136 na utatekelezwa katika maeneo ya Kisasida, Ipungi, Mughamo na Unyankhyanya. Kampuni ya *Geo Wind* pamoja na *Acciona* wameingia *exclusive agreement* kwa ajili ya kipindi cha miezi minne ambayo itaishia mwezi Februari mwaka huu kwa ajili ya kujiridhisha kwa wananchi kama watakubaliana na utekelezaji wa mradi huu ili waweze kupata umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni mbalimbali binafsi zimeonesha nia ya kuzalisha umeme kwa kutumia upepo katika Mkoa wa Singida ikiwa ni pamoja na Kampuni ya *Wind East-Africa* iliyojitokeza kuzalisha umeme wa megawati 50 kwa awamu ya kwanza na baadae kufikisha megawati 100. Mradi huu utatekelezwa katika eneo la Kititimo. Gharama ya mradi huu ni dola za Marekani milioni 264.77.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima, swali la nyongeza.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Singida Mjini imejaaliwa kuwa na rasilimali ya vyanzo vya umeme kwa maana ya upepo na jua na yako makampuni tayari yamekwishajitokeza kwa ajili ya kuzalisha umeme huo. Sasa na sisi wananchi wa Jimbo la Singida Mjini tumejitokeza kwa maana ya kutoa maeneo yetu kwa ajili ya uzalishaji. Serikali sasa ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba umeme huo unazalishwa ili Singida Mjini iweze kupata viwanda vya kutosha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Singida Mjini kunapita umeme wa kilovoti 40 kuelekea Shinyanga na Namanga na wananchi tayari wametoa maeneo yao kwa ajili ya kupisha mradi huo na wako ambao wameshalipwa fidia na wengine hawajalipwa fidia. Serikali inatoa tamko gani sasa kuhakikisha kwamba wananchi wote wanalipwa fidia kwa ajili ya kupisha umeme huo? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa, Serikali ina mpango mahususi wa kuendeleza wawekezaji binafsi katika umeme mbadala hasa katika maeneo ya Singida ambako kuna umeme wa upepo. Hata hivyo, mkakati wa Serikali wa kwanza, Serikali imetenga kupitia mradi wake wa *REA* shilingi milioni 42 kwa ajili ya kuendeleza wawekezaji binafsi watakaofanya katika uzalishaji wa umeme pamoja na mambo ya miradi ya maji. Kwa hiyo, wananchi wa Singida watapata pesa hizi kupitia mradi wa *REA* ambapo watawezeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mkakati mwingine badala ya kupitia mradi wake umeshafadhili sasa, nikizungumzia kwa nchi nzima miradi ya Lukonda kule

Njombe pamoja na Ndoya kule Mbinga kama wajasiriamali wa Kitanzania ambao wanawezeshwa kupitia miradi ya Serikali, miradi ya *REA*. Kwa hiyo, miradi ya Serikali kupitia miradi ya *REA* kutoa mahususi kwa ajili ya kuendekeza wawekezaji. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Sima na kama kuna wawekezaji wengine kule Singida Mheshimiwa Sima basi walete wataalam wetu watashirikiana na watu wa *REA* ili waweze kushirikiana zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili kuhusiana na mkakati wa Serikali kulipa fidia kwenye Mradi wa *backbone* wa kilovoti 400. Kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Sima alivyoshirikiana na Serikali mpaka wananchi takriban 200 wakalipwa fidia awamu ya kwanza. Awamu ya pili nimhakikishie Mheshimiwa Sima, hivi sasa vijiji vyake 13 ambavyo vinaingia kwenye mradi ule vitalipwa fidia jumla ya shilingi milioni 722.7, malipo yataanza mwezi Februari mwaka huu na yatakamilika mwezi Machi na nimhakikishie kwamba vijiji vyake vya Misuna ambavyo vilipitiwa na umeme pamoja na Mtipa pamoja na Kisaki pia vitalipwa fidia kwa utaratibu huo.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Tunaanza na Mheshimiwa Mwamoto na tunamalizia na Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na pamoja na kazi nzuri ambayo Wizara hii inafanya, naomba niulize swali dogo tu la nyongeza. Niliwahi kuuliza hili swali kwamba kwa kuwa Wilaya ya Kilolo ndiyo wilaya pekee ambayo maji mengi yanayojaza Kihansi yanatoka kule ambayo ndiyo yanasaidia kupelekea kuleta umeme nchi hii. Je, Kilolo inanufaikaje sasa? Naomba kwa nafasi hii atueleze hapa wananchi wa Kilolo watanufaika vipi ili kuhakikisha wanapata umeme.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa eneo la Kilolo linatupatia maporomoko ya maji ambayo yanatusaidia sana kuingiza kwenye Gridi ya Taifa. Lakini wananchi wa Kilolo pamoja na hasa wananchi wa Kihesa Mgagao watanufaika sana na umeme huu na nitaje tu Mheshimiwa Mwamoto, hivi sasa katika Mkoa wa Iringa, *REA* Awamu ya Tatu imeshaingia na eneo mojawapo ambalo linapelekewa umeme ni pamoja na Kihesa Mgagao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba wananchi wa Kilolo wataendelea kunufaika na miradi ya umeme.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Jimbo la Tarime Mjini lina kata nane na kati ya kata nane, kata nne ziko pembezoni na hazina umeme kabisa na kata mbili zina umeme kwa asilimia chache. Ningependa kujua *commitment* ya Serikali ya kuhakikisha kwamba wananchi wa Jimbo la Tarime Mjini wanapata umeme kwa asilimia zaidi ya 90.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Esther, tumeshirikiana naye sana kwenye mradi wa *REA* Awamu ya Pili na ni kweli kuna kata nne na kata nyingine mbili ambazo hazijaguswa kabisa. Hata hivyo, nimhakikishie Mheshimiwa Esther kwamba Jimbo lako pamoja na Mkoa wa Mara tumeshaanza kutekeleza Mradi wa *REA* Awamu ya Tatu wa *desification.* Hapa ninapozungumza wiki ijayo mkandarasi ata-*report* kwake ili amwelekeze maeneo mahususi. Kwa hiyo, kata zake nne na zile tatu ambazo anazungumza Mheshimiwa Mbunge zitapatiwa umeme kupitia mradi wa *REA* Awamu ya Tatu unaoanza mwezi wa Tatu na kuendelea.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Namwomba Mheshimiwa Martha Mlata sasa aulize swali la nyongeza kwa ufupi kabisa.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri akijibu swali mojawapo hapa Bungeni kuhusu mradi wa umeme wa upepo Singida alisema kwamba Serikali inakamilisha mkataba na taratibu za kusaini kati ya Kampuni ya *Wind East-Africa* na kwamba mwezi Februari mradi huo utaanza. Naomba atusaidie, je, maneno yale ni kweli au bado? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichowaeleza ni kweli kwanza, lakini cha pili nifafanue tu kwamba mradi wa *REA* unaokwenda kuendelea umeshaanza na mpaka tarehe 31 mwezi Machi, wakandarasi watakuwa wameshaingia mikoa yote kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa *REA* unaoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa upande wa umeme wa upepo kule Singida nimesema mradi wa *Wind East-Africa* pamoja na *Geo Wind*

wanakamilisha taratibu za kimikataba na kufikia mwezi Juni ndiyo wataanza rasmi. Kwa wanaoanza Februari na mwezi Machi ni miradi ya *REA* na ile miradi ya upepo itaanza kuanzia mwezi Juni na kuendelea.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunamalizia swali la mwisho, namuomba Mheshimiwa Abdul-Aziz Abood, Mbunge wa Morogoro Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 68

**Kupeleka Umeme Morogoro Mjini**

**MHE. ABDUL-AZIZ M. ABOOD** aliuliza:-

Maeneo mengi katika Jimbo la Morogoro Mjini bado hawajapata nishati ya umeme kama vile Kata za Mindu, Lugala, Mkundi, Kiegea A na B, Kihonda, Mafisa, Tungi, Kingolwira na Kauzeni A.

Je, ni lini Serikali itamaliza tatizo hili la muda mrefu?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdul-Aziz Abood, Mbunge wa Morogoro Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Shirika la Umeme *(TANESCO)* inatekeleza miradi ya kufikisha miundombinu ya umeme maeneo mbalimbali nchini ikiwa ni pamoja na Morogoro Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi unaoendelea katika Kata za Mindu, ujenzi wa njia ya umeme msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilometa 8.973, ujenzi wa njia ya umeme msongo wa kilovoti nne yenye urefu wa kilometa 35.4, lakini ufungaji wa transfoma saba pamoja na kuwaunganishia umeme wateja 834.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu utafikisha umeme kwenye maeneo ya Mindu, Kasanga na Madanganya ambapo ni transfoma nne zimefungwa tayari na baadhi ya wananchi pia wameshaunganishiwa umeme. Gharama za mradi ni shilingi bilioni 1.113. Unajumuisha Mindu -Lugala ambao unajumuisha ujenzi wa msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilometa 8.9, ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa voti 400 yenye urefu wa kilometa 10.7 na ufungaji wa

transfoma tatu. Hali kadhalika utaunganishwa umeme kwa wateja 206. Gharama za mradi huu ni milioni 106.784. Utekelezaji wa miradi hii utakamilika mwezi Juni mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yaliyobaki katika Mji wa Morogoro yataendelea kupatiwa umeme kupitia bajeti ya *TANESCO* zinazopangwa mwaka hadi mwaka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdul-Aziz Abood, swali la nyongeza.

**MHE. ABDUL-AZIZ M. ABOOD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; Morogoro inaelekea kuwa Jiji, je, Serikali ina mikakati gani ya kumaliza maeneo yote ya Mji wa Morogoro kuwa na umeme?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kuna maeneo ambayo umeme umeshafika, wananchi wameshalipia kuunganishiwa umeme, lakini majibu wanayopewa ni kuwa nguzo hakuna. Je, Serikali itaondoa lini kero hiyo ya nguzo katika Mji wa Morogoro ili wananchi waweze kupata umeme, maeneo waliyokwishapata umeme?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa Serikali kupeleka umeme ni kama ambavyo nimeeleza, ipo miradi ya *REA*, lakini pamoja na *REA* bado *TANESCO* wana bajeti zake za kupeleka umeme. Katika Mkoa wa Morogoro, hasa Morogoro Mjini, mkakati uliopo wa kwanza kabisa, Serikali imetenga shilingi milioni 106 kwa mwaka huu ambayo itapeleka umeme kwenye vijiji vya Mheshimiwa Abood ikiwemo Kihonda, Mafisa pamoja na maeneo mengine kama kule Kanisani ambako ameeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine ambayo Mheshimiwa Mbunge hajayataja pamoja na eneo lake lile ambalo amesema eneo la Bomba la Zambia. Kile Kijiji cha Bomba la Zambia ambacho kipo mbali sana kitapelekewa umeme mwaka huu. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Abood kwamba Serikali ina mkakati madhubuti wa kupeleka umeme kwenye vijiji vyake vyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili kuhusiana na nguzo, ni kweli kabisa yako maeneo Morogoro Mjini wananchi wamelipia, lakini hawajawahi kuunganishiwa umeme. Utaratibu unafanyika sasa na nimhakikishie

Mheshimiwa Abood hivi sasa tunapoongea hapa wananchi wake wa Lokole Juu pamoja na Lukobe Kanisani wanaunganishiwa umeme kwa sababu wameshalipia na nguzo zimeshakuja na vijiji vinne ambavyo amevitaja pamoja na Kauzeni na maeneo mengine wataendelea kuunganishiwa umeme mara baada ya nguzo kuingia mwezi ujao.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo.

**MWENYEKITI:** Naomba tutulizane.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo.

**MWENYEKITI:** Muda wetu wa maswali umefikia mwisho kwa siku ya leo. Kabla sijaanza na matangazo ya wageni, naomba kuwajulisha Waheshimiwa Wabunge kwamba tumepokea barua kutoka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba anasafiri kwenda Dar es Salaam kwa shughuli za kikazi kuanzia Jumapili tarehe 5 Februari, 2017. Wakati hayupo ambaye atakaimu nafasi hiyo ya Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni hadi atakaporejea atakuwa ni Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni ambao tunao Bungeni asubuhi hii ya leo wako katika makundi mawili:-

Kuna wageni waliopo Jukwaa la Spika ambaye ni Mheshimiwa Samwel Akon, Mbunge na Mwenyekiti wa Kamati ya Masuala ya Uhusiano ya Kibunge ya Bunge la Wawakilishi wa Nigeria ambaye pia alikuwa Spika wa Bunge la Jimbo la Akwan-Ivon, karibu sana Mheshimiwa Samwel Akon. *(Makofi)*

Mwingine ni mgeni ambae ni Mheshimiwa Larry Odey ambaye ni Mshauri wa Masuala ya Kibunge, pia alikuwa Spika la Jimbo la *Cross-River,* Nigeria, karibu sana Mheshimiwa Larry Odey. Wageni hawa wapo Bungeni kwa ziara ya kikazi na watakutana na Spika wa Bunge, Mheshimiwa Job Ndugai hapo baadaye, karibuni sana wageni wetu.

Wageni wengine ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge; tunao wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge pamoja na wageni waliokuja kutembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo Bungeni, tunawakaribisheni sana, karibuni katika Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Sasa yafuatayo ni matangazo; tangazo la kwanza linatoka kwa Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni, Mwenyekiti wa Kamati ya Utendaji *(CPA)* Tawi la Tanzania, anawatangazia kwamba kutakuwa na kikao cha Kamati leo tarehe 6 Februari, 2017 saa 8.00 mchana katika ukumbi namba 227, ghorofa ya pili, Jengo la Utawala, Ofisi za Bunge – Dodoma. Wajumbe wa Kamati wanaopaswa kuhudhuria kikao hicho ni hawa wafuatao; Mheshimiwa Tundu Antiphas Lissu ambaye ni Makamu Mwenyekiti na wajumbe ni Mheshimiwa Amina S. Mollel, Mheshimiwa Salum M. Rehani, Mheshimiwa Japhet N. Hasunga, Mheshimiwa Dkt. Immaculate S. Semesi, Mheshimiwa Khamis Mtumwa Ali, Mheshimiwa Zaynabu Matitu Vulu, Mheshimiwa Josephat Kandege, Mheshimiwa Juma Hamad Omar, Mheshimiwa Jitu Soni na Mheshimiwa Maria N. Kangoye. *(Makofi)*

Tangazo la mwisho linatoka kwa Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii anawaomba Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuwa leo tarehe 6 Februari, 2017 saa 7.00 mchana kutakuwa na kikao cha Kamati katika ukumbi wa 229, Jengo la Utawala.
Katibu!

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo ! Mwongozo!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwalimu.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. DOTO M. BITEKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7). Nikiwa hapa Bungeni na mapema leo nimeendelea kupata taarifa juu ya jambo ambalo limejitokeza na ambalo naomba niliombee mwongozo wako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimboni kwetu na Wilayani kwetu Bukombe, mwananchi anayeitwa Sizya Emmanuel mwenye umri wa miaka 30 ambaye anajishughulisha na kazi ya kufuga nyuki na ambaye amepewa kibali cha kufanya shughuli zake kwenye Hifadhi ya Kigosi alikwenda kufanya shughuli zake pamoja na wenzake wanne. Wakiwa huko, Ndugu Sizya Emmanuel akapigwa risasi na maaskari wa wanyamapori. Risasi hiyo amepigwa kisogoni ikatokea kwenye jicho lake la kulia na hivi ninavyoongea na wewe, Ndugu Sizya amepelekwa kwenye Hospitali ya Rufaa ya Bugando, hali yake ni mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kuomba Mwongozo wako kwa sababu mambo haya ya uonevu na unyanyasaji wa wananchi kwenye Wilaya

ya Bukombe na hili sio tukio la kwanza, yamekuwa yakijirudia mara kwa mara. Wananchi wa Bukombe hawana amani, hawana furaha, wana wasiwasi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwalimu.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7) na 46 zikisomwa kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo ninaouomba ni jambo lililotokea katika kujibu swali wiki iliyopita lililokuwa linaeleza juu ya madai ya walimu nchini. Wakati Naibu Waziri akijibu swali, alieleza walimu nchini wanadai madai yapatayo shilingi bilioni 26 na kwa takwimu zilizopo ambazo Chama cha Walimu kimezifikisha Serikalini, walimu wa nchi hii wanadai shilingi trilioni 1.06.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mwongozo ninaotaka unipe ni kwa nini deni kubwa la walimu halitajwi kikamilifu humu Bungeni na hivyo Serikali inataja kiasi kidogo sana kinachodaiwa na walimu? Sasa shida ni nini? Tupate Mwongozo, tunaficha hili deni kwa maslahi ya nani? Kwa nini Serikali inadanganya Bunge na madeni haya Chama cha Walimu kimejadiliana na Serikali tarehe 10 mwezi wa Kwanza, kwa hiyo Serikali inafahamu ina deni la shilingi trilioni 1.06. Naomba Mwongozo wako ni kwa nini Serikali haisemi ukweli katika madai ya Walimu wa nchi hii.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa miongozo yenu, Mheshimiwa Doto, naanza na Mwongozo ulioomba. Kwanza niwape pole wananchi wako wa huko Bukombe kwani hili jambo ni la hatari na Mwongozo wangu ni kwamba, naiagiza Serikali ifanye haraka iwezekanavyo ili kufuatilia suala hili tujue nini kinaendelea. Mheshimiwa Waziri wa Nchi una neno lolote kuhusiana na hili?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE WALEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa na mimi niungane na kauli yako, lakini niungane na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo kuwapa pole ama kumpa pole majeruhi ambaye amepatwa na tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kiti chako kinatoa miongozo na kuiagiza Serikali, naomba kwa niaba ya Serikali nipokee maagizo yako. Hata hivyo, naomba kulihakikishia Bunge hili toka asubuhi tulipopata taarifa, tumeshaiagiza Serikali ianze kufanya kazi ya kulijua jambo hili kwa upana wake, lakini

kushughulikia kwa kina matatizo yote yanayohusiana na askari wa wanyamapori katika kulinda mapori yetu ili kupata ufumbuzi wa kudumu wa pamoja.

**MWENYEKITI:** Nashukuru. Kwa hiyo, naamini kwamba agizo hilo litafanyiwa kazi kwa haraka iwezekanavyo. Suala la pili la Mheshimiwa Mwalimu, suala hili la walimu kuhusu deni nalichukua kwa mujibu wa Kanuni ya 68(10) na tutalitolea Mwongozo baadaye.

Katibu, tuendelee.

**NDG. CHARLES MLOKA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA KAMATI**

**Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI**
**na**
**Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa Kipindi cha Januari, 2016 hadi Januari, 2017**

**MWENYEKITI:** Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI aje kuwasilisha taarifa yake tafadhali.

**MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA MASUALA YA UKIMWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, napenda kuwasilisha kwako Taarifa ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kwa kipindi cha Januari, 2016 hadi Januari, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Shughuli zilizotekelezwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kwa kipindi cha Januari, 2016 hadi Januari, 2017.

Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu nne; sehemu ya kwanza inaelezea maelezo ya jumla; sehemu ya pili inaelezea utekelezaji wa majukumu ya Kamati; sehemu ya tatu imebainisha maoni na ushauri wa Kamati; na sehemu ya nne ni hitimisho la taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane ya Kanuni chini ya Kanuni ya 118(10) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Masuala ya UKIMWI imepewa majukumu yafuatayo:-

(a) Kuratibu masuala yanayohusu UKIMWI katika sekta zote.

(b) Kufuatilia utekelezaji wa sera na mipango ya Serikali kuhusu UKIMWI na udhibiti wa dawa za kulevya.

(c) Kujadili na kutoa mapendekezo na ushauri kuhusu hatua za kudhibiti dawa za kulevya; na

(d) Kushughulikia Bajeti za Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Madawa ya Kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi cha mwaka mmoja yaani Januari, 2016 hadi Januari, 2017, Kamati ilitekeleza majukumu yafuatayo:-

(a) Semina za mafunzo;

(b) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya taasisi zinazosimamiwa na Kamati;

(c) Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo; na

(d) Uchambuzi wa Taarifa na Utekelezaji wa Bajeti za Taasisi zinazosimamiwa na Kamati na pia sehemu ya pili inahusu uchambuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI ulizingatia masharti ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 hususan Kanuni ya 117 inayohusu utaratibu katika Kamati za Kudumu za Bunge. Hivyo, Kamati iliandaa Mpango Kazi uliotekelezwa katika kipindi cha Januari, 2016 hadi Januari, 2017, ambao matokeo ya utekelezaji wake yamefanyiwa uchambuzi katika sehemu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati, semina na mafunzo, katika hili Wajumbe wa Kamati walipata mafunzo ya kuwajengea uwezo katika maeneo yafuatayo:-

(i) Muundo wa majukumu ya Kamati;

(ii) Kanuni na taratibu za uendeshaji wa shughuli za Kamati;

(iii) Muundo na majukumu ya tume zinazosimamiwa na Kamati hii yaani Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya; na

(iv) Sheria na sera mbalimbali zinazohusu udhibiti wa UKIMWI na dawa za kulevya nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya taasisi zinazosimamiwa na Kamati; Kamati ya Masuala ya UKIMWI inasimamia taasisi mbili ambazo ni Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *TACAIDS* na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania, Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

(i) Ufinyu wa bajeti na ucheleweshaji wa fedha kutoka Serikalini;

(ii) Dosari katika Sera ya UKIMWI ya 2001; na

(iii) Kutokamilika kwa wakati mchakato wa muundo mpya wa Tume na hivyo….

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeangalia pia Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya. Katika kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Tume hii Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

(i) Ufinyu wa bajeti na uchelewaji wa fedha kutoka Serikalini;

(ii) Dosari katika Sera ya Dawa za Kulevya ya 2004; na

(iii) Kutokukamilika kwa muundo wa Tume hii ambayo kwa sasa imekuwa mamlaka kamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hii pia imepewa jukumu la kuratibu masuala yote yanayohusu UKIMWI katika sekta zote ikiwemo kufuatilia utekelezaji wa sera na mipango ya Serikali kuhusu UKIMWI na udhibiti wa dawa za kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilikutana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na kujadili mwongozo wa namna ya kuwahudumia watumishi wa umma wanaoishi na Virusi vya UKIMWI *(workplace intervention medical treatment and training to staff)* ambapo Kamati ilishauri mambo yafuatayo:-

(a) Waajiri kuhamasisha na kuwajengea watumishi ujasiri wa kupima VVU, kutoa elimu ya kujikinga dhidi ya maambukizi ya UKIMWI na kutekeleza afua za UKIMWI mahali pa kazi.

(b) Serikali kuwachukulia hatua waajiri wanaotumia fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya WAVIU kwa shughuli nyingine zisizohusiana na UKIMWI.

(c) Serikali kuongeza ajira katika viwanda vidogo vidogo na katika sekta binafsi ili kukuza uchumi na kuwawezesha vijana kupata ajira ili kuwaepusha kujihusisha na matumizi ya dawa za kulevya na tabia hatarishi zinazochochea kuongezeka kwa maambukizi ya VVU na UKIMWI.

(d) Serikali kuendelea kuwasisitiza vijana, waajiri katika utumishi wa umma kutumia fursa zinazowazunguka ili kudhibiti tatizo la unyanyapaa ambao huchangia kurudisha nyuma juhudi za Serikali katika mapambano dhidi ya maambukizi ya UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilikutana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ili kujadili hatua iliyofikiwa katika Utafiti wa Upatikanaji wa Chanjo ya UKIMWI Tanzania ambapo Kamati ilibaini kuwa wataalam wa utafiti wa tiba bado wapo kwenye hatua za awali za utafiti wa chanjo, hivyo kutokana na changamoto ya rasilimali fedha, rasilimali watu na teknolojia ya juu inayohitajika katika utafiti wa chanjo. Hivyo, kuifanya Tanzania kama zilivyo nchi nyingi za Afrika kutegemea kwa kiasi kikubwa tafiti zinazofanywa na nchi zilizoendelea kama Marekani. Kwa sababu hiyo, Kamati ilishauri mambo yafuatayo:-

(a) Serikali kuona umuhimu wa kuwekeza katika utafiti wa chanjo ya UKIMWI; kwa kuongeza bajeti ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

(b) Wizara kujielekeza zaidi katika kutoa elimu kwa wananchi juu ya kujikinga na maambukizi ya VVU na UKIMWI, pamoja na magonjwa sugu yasiyoambukizwa kwa maana Kinga ni bora kuliko Tiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilikutana na Bohari Kuu ya Madawa nchini pamoja na Baraza la Watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI ili kujadili mafanikio na changamoto zilizopo katika upatikanaji, usambazaji na utumiaji wa dawa za kufubaza makali ya VVU *(ARVs)* nchini ambapo, Kamati ilibaini uwepo kwa changamoto katika upatikanaji wa dawa hizo katika vituo vingi vya afya nchini inayosababishwa na malimbikizo ya madeni ya Bohari Kuu ya Madawa katika Mamlaka ya Bandari, hali iliyopelekea watumiaji wa dawa hizo kulazimika kununua dawa katika maduka ya dawa ya watu binafsi kwa bei za juu huku wengine wakishindwa kumudu gharama hizo na kujikuta wakidhoofika. Hivyo, Kamati ilishauri mambo yafuatayo:-

(a) Serikali kufanya jitihada za haraka za ulipaji wa deni kwa Bohari Kuu ya Dawa *(MSD)* ili kuwasaidia WAVIU kupata dawa za kufubaza makali ya VVU kwa wakati pia kutowakatisha tamaa wafadhili wanaotuletea dawa hizo;

(b) Serikali kuwekeza katika uzalishaji wa ndani wa dawa hizi ili kuondokana na utegemezi wa wafadhili katika ununuzi wa dawa kama jirani zetu wa Uganda wanavyofanya; na

(c) Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa itoe waraka utakaohusu halmashauri zote kushirikiana na Mabaraza ya WAVIU katika kubuni njia za kuwakwamua kiuchumi WAVIU na kusaidia katika mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilikutana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ili kujadili mafanikio, changamoto na matarajio ya Wizara hii katika udhibiti wa matumizi ya dawa za kulevya nchini ambapo Kamati ilibaini changamoto nyingi zilizotokana na ufinyu wa bajeti ya Wizara, hivyo kupelekea zoezi la udhibiti wa dawa za kulevya nchini kutokuwa na matokeo ya kuridhisha. Hii imetokana na bajeti ya Wizara hii kupungua kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na kufikia shilingi bilioni 30 kwa miradi ya maendeleo ikilinganishwa na kiasi cha sh. 65,757,261,000 zilizotengwa kwa mwaka wa fedha uliopita 2015/2016. Hivyo, Kamati ilishauri yafuatayo:-

(a) Jeshi la Polisi kuongezewa Bajeti ili kuwawezesha kununua vitendea kazi kama boti za doria ili kukabiliana na changamoto wanazopata katika kudhibiti uingizwaji wa dawa za kulevya nchini; na

(b) Jeshi la Polisi kuimarisha ulinzi hususan katika maeneo ya bandari, viwanja vya ndege na mipaka ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilikagua Mradi wa Ujenzi wa Ghala la Kuhifadhia Vielelezo vya Kesi za Dawa za Kulevya wenye thamani ya sh. 272,500,000 unaosimamiwa na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya uliopo Makao Makuu ya Jeshi la Polisi Kurasini, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika kipindi hiki pia Kamati ilifanya ziara katika taasisi mbalimbali ili kufuatilia utekelezaji wa sera za UKIMWI na dawa za kulevya, taasisi hizo ni pamoja na:-

(i) Hospitali ya Taifa Muhimbili na Hospitali ya Rufaa ya Mwananyamala katika vituo vya kutolea huduma ya dawa ya *methadone* kwa warahibu wa dawa za kulevya;

(ii) *Missana Foundation Sober House* iliyopo Kigamboni-Dar es Salaam;

(iii) Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali;

(iv) Bohari Kuu ya Madawa *(MSD);*

(v) Mgodi wa Buzwagi uliopo Kahama - Shinyanga; na

(vi) Kliniki ya WAVIU katika Kituo cha Afya cha Kambarage - Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Aprili, 2016, Kamati ilikutana na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya kwa mwaka wa fedha 2015/2016, kisha Kamati ilipitia na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya Fungu la 91 na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* Fungu la 92 kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kama ilivyoainishwa katika Nyongeza ya Nane ya Kanuni ya 118 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya, Kamati ilizingatia maelezo na fafanuzi mbalimbali zilizotolewa na Tume hizo kuhusiana na Makadirio ya Mapato na Matumizi yao ambapo Kamati ilipitisha sh. 2,340,236,000 kwa Matumizi ya Kawaida kwa Fungu 91. Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya na hakuna kiasi kilichotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Aidha, kiasi cha sh. 4,961,677,000 kilitengwa kwa matumizi ya kawaida na sh. 5,235,823,413 kwa miradi ya maendeleo kwa Fungu 92 - Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kwa mwaka wa 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu inahusu maoni na ushauri wa Kamati. Kutokana na shughuli za Kamati zilizofanyika katika kipindi cha mwaka mmoja yaani Januari, 2016 hadi Januari, 2017, kumekuwa na changamoto mbalimbali zilizojitokeza katika taasisi zinazosimamiwa na Kamati hii ambazo Kamati inazitolea maoni na ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza vyema majukumu ya Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya, Kamati inashauri mambo nane yafuatayo:-

Moja, KWA KUWA, Kamati imebaini dosari nyingi katika Sera ya Dawa za Kulevya ya mwaka 2004 ambayo imepitwa na wakati;

NA KWA KUWA, dosari hizo zimechangia ugumu katika utatuzi wa changamoto za sasa kuhusu udhibiti wa uingizwaji na matumizi ya dawa za kulevya, hali inayopelekea Taifa kuendelea kupoteza nguvu kazi;

KWA HIYO BASI, Kamati inashauri kuwa Serikali iharakishe mapitio ya sera hii ili kulinusuru Taifa na janga hili la dawa za kulevya.

Mbili, KWA KUWA, Kamati imebaini kuwa tangu Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya ibadilishwe kisheria kuwa Mamlaka ya Kupambana na Dawa za Kulevya, muundo wake bado haujakamilika;

NA KWA KUWA, kutokukamilika kwa muundo huo kunasababisha Tume kushindwa kuajiri watumishi wa kutosha, watumishi 37 kati ya 65 wanaohitajika;

KWA HIYO BASI, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha na kukamilisha mchakato wa muundo wa mamlaka hii ili uanze kutumika mara moja na kuongeza ufanisi katika kudhibiti uingizwaji na matumizi ya dawa za kulevya.

Tatu, KWA KUWA, imebainika kwamba ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa Tume umekuwa inakwamisha utendaji wa baadhi ya majukumu ya Tume hii kama vile:-

(a) Kudhibiti uingizwaji wa dawa za kulevya katika mipaka yote ya nchi ambayo ni mingi na ina vipenyo vingi vinavyofanya zoezi la udhibiti kuwa mgumu;

(b) Kushindwa kuteketeza mashamba ya bangi ambayo hulimwa sehemu zisizofikika kwa urahisi ambapo utekelezaji wa zoezi hilo uhitaji fedha nyingi; na

(c) Tume kushindwa kutoa elimu kwa wananchi kuhusu madhara yatokanayo na matumizi ya dawa za kulevya ili kunusuru afya za Watanzania na nguvu kazi ya Taifa;

NA KWA KUWA, kutotekelezwa kwa majukumu ya msingi ya Tume hiyo kutokana na ufinyu wa bajeti kunaathiri juhudi za udhibiti wa dawa za kulevya nchini jambo ambalo lina madhara makubwa kwa Taifa;

KWA HIYO BASI, Kamati inaishauri Serikali kuangalia uzito wa majukumu yanayotekelezwa na Tume hii katika kupambana na biashara haramu ya dawa za kulevya nchini, kwa kuongeza bajeti yao ili kuiongezea ufanisi Tume na kuhakikisha kuwa mafanikio yaliyofikiwa katika udhibiti wa dawa za kulevya hayapotei.

Nne, KWA KUWA, Kamati imebaini kukosekana kwa chombo cha kisheria cha kushughulikia udhibiti wa biashara na matumizi ya dawa za kulevya katika ngazi ya Halmashauri;

NA KWA KUWA, kukosekana kwa chombo hicho kunachangia udhibiti duni wa dawa za kulevya katika Halmashauri nchini;

KWA HIYO BASI, Kamati inaishauri Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kufanya maboresho ya Kamati za UKIMWI za Halmashauri ili kisheria ziwe na uwezo wa kusimamia shughuli za udhibiti wa dawa za kulevya katika ngazi ya Halmashauri kama ilivyo kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, kwa lengo la kusimamia kwa pamoja mambo haya yanayoendana.

Tano, KWA KUWA, Serikali imebaini changamoto katika upatikanaji wa tiba za utengemao *(rehabilitation)* na warahibu *(addicts)* wa dawa za kulevya nchini ambapo kwa sasa zinapatikana katika Mkoa wa Dar es Salaam na Zanzibar pekee;

NA KWA KUWA, changamoto hiyo inakwamisha juhudi za kuwawezesha warahibu kuacha matumizi ya dawa za kulevya, jambo linalochangia madhara ya kijamii nchini;

KWA HIYO BASI, Kamati inashauri kwamba huduma hii ihuishwe katika sera ya afya kama ilivyofanyika kwa suala la UKIMWI ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma hii kwa nchi nzima.

Sita, KWA KUWA, Kamati imebaini uwepo wa mwamko mdogo na ushiriki duni wa jamii katika mapambano dhidi ya biashara haramu ya dawa za kulevya;

NA KWA KUWA, hali hiyo kwa kiasi kikubwa imesababisha ongezeko la watumiaji wa dawa za kulevya, wagonjwa wa akili na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI;

KWA HIYO BASI, Kamati inashauri:-

(a) Tume ishirikiane na vyombo vya dola katika kuandaa kampeni endelevu ambazo mbali na kuwajengea uelewa Watanzania kuhusu umuhimu wa kushiriki katika mapambano haya, pia utawapa motisha ya kushiriki katika mapambano dhidi ya biashara ya dawa za kulevya; na

(b) Viongozi wakuu wa nchi kutoa kauli thabiti na kusimamia utekelezaji wa kauli hizo katika kukemea na kukomesha biashara na matumizi ya dawa za kulevya ili kuhamasisha ushiriki wa jamii nzima katika janga hili.

Saba, KWA KUWA, Kamati imebaini uwepo wa changamoto mbalimbali zinazowakabili warahibu *(addicts)* wa dawa za kulevya punde wanapoacha matumizi ya dawa hizo, kama kutengwa na jamii na kukosa ajira;

NA KWA KUWA, changamoto hizo husababisha warahibu kurudia matumizi ya dawa za kulevya au kujiingiza katika vitendo vya uhalifu;

KWA HIYO BASI, Kamati inashauri kuwa, Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu ianzishe programu maalum za kuwasaidia warahibu wa dawa za kulevya kuweza kujiinua na kujitegemeza kiuchumi mara tu baada ya kuachana na matumizi ya dawa za kulevya.

Nane, KWA KUWA, Kamati imebaini uwepo wa uhusiano mkubwa kati ya matumizi ya pombe za bei rahisi maarufu kama viroba na kuongezeka kwa tabia hatarishi zinazochangia ongezeko la vijana katika matumizi ya dawa za kulevya;

NA KWA KUWA, hali hiyo inaathiri ufanisi wa nguvu kazi ya Taifa kutokana na madhara ya matumizi ya dawa za kulevya;

KWA HIYO BASI, Kamati inaishauri Serikali kufungia kabisa uzalishaji na uuzwaji wa pombe za bei rahisi maarufu kama viroba ili kulinusuru Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa, Kamati inashauri mambo saba yafuatayo:-

Kwanza, KWA KUWA, Kamati imebaini dosari nyingi katika Sera ya UKIMWI ya mwaka 2001;

NA KWA KUWA, dosari hizo zinachangia kukosekana kwa mafanikio katika malengo ya sera, ikiwemo kushindwa kuendana na hali halisi ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI nchini;

KWA HIYO BASI, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha mchakato wa mapitio ya sera hii utakaoshirikisha wadau wote muhimu.

Pili, kwa kuwa marekebisho ya Sheria Namba 6 ya mwaka 2015 yalihitaji muundo mpya wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI nchini ili kuongeza ufanisi wa kiutendaji na kwamba mchakato wa kuandaa muundo huo haujakamilika;

NA KWA KUWA, kutokamilika kwa muundo huo kunasababisha kupunguza ufanisi katika mapambano dhidi ya UKIMWI;

KWA HIYO BASI, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha ukamilishaji wa muundo ili uanze kutumika mara moja na kuongeza ufanisi katika udhibiti wa UKIMWI.

Tatu, KWA KUWA, Kamati imebaini changamoto kubwa katika utengaji wa bajeti ya Mfuko wa UKIMWI ulioanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Namba 22 ya mwaka 2001 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2015;

NA KWA KUWA, changamoto hiyo inasababisha utegemezi uliokithiri kwa fedha za wafadhili katika utekelezaji majukumu ya udhibiti wa UKIMWI nchini ikiwemo upatikanaji wa uhakika wa dawa za kufubaza makali ya VVU *(ARV's)* na huduma nyingine zisizo za kitabibu;

KWA HIYO BASI, Kamati inashauri kuwa katika utengaji wa bajeti ya Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI *(ATF),* Serikali ianzishe kisheria chanzo mahususi cha kutunisha mfuko huu kama ilivyo katika mifuko mingine kama vile Mfuko wa Barabara *(Road Fund)* ili kupunguza utegemezi mkubwa kwa fedha za wafadhili ambazo mbali na kupambana na masharti magumu, hivi sasa zimeanza kupungua.

Nne, KWA KUWA, Kamati ilibaini changamoto ya ufinyu wa bajeti kwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* pamoja na ucheleweshaji wa fedha hizo kutoka Hazina;

NA KWA KUWA, hali hii inasababisha:-

(a) Tume kushindwa kuajiri watumishi wa kutosha katika ofisi zake, kwa sasa ina watumishi 83 kati ya 120 wanaohitajika.

(b) Tume kushindwa kuwaendeleza kitaaluma watumishi wake hasa katika maeneo ya ukaguzi wa ndani, tathmini na teknolojia ya habari na mawasiliano inayokuwa kwa kasi duniani; na

(c)Tume kushindwa kumudu gharama za uendeshaji wa ofisi kwa ujumla.

KWA HIYO BASI, Kamati inashauri kuwa:-

(a) Serikali itoe kipaumbele katika mapambano dhidi ya UKIMWI kwa kutenga bajeti ya kutosha kwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania ili kuhakikisha kuwa mafanikio yaliyofikiwa katika udhibiti wa UKIMWI nchini hayapotei; na

(b) Kwa kuzingatia kiwango cha bajeti inayotolewa na Serikali, Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania iweke utaratibu maalum wa kuwaendeleza watumishi wake ili kuendana na kasi ya ukuaji wa TEHAMA duniani.

Tano, KWA KUWA, Kamati imebaini changamoto ya ukosefu wa takwimu za Taifa kuhusu maambukizi ya UKIMWI nchini;

NA KWA KUWA, ukosefu wa takwimu sahihi na za kutumainiwa *(reliable)* unasababisha Serikali kushindwa kuchukua hatua sahihi katika mapambano dhidi ya UKIMWI;

KWA HIYO BASI, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania inaijengea uwezo thabiti Divisheni ya Ufuatiliaji na

Tathmini ili kwa kushirikiana na Ofisi ya Takwimu ya Taifa na taasisi nyingine za utafiti, Tume iweze kukusanya na kuchapa takwimu za maambukizi ya Virusi vya UKIMWI kwa nchi nzima.

Sita, KWA KUWA, baadhi ya Asasi Zisizo za Kiserikali (AZISE yaani *NGOs*) zinazofanya kazi za masuala ya UKIMWI kwa ufadhili wa watu wa nje, hutekeleza pia ajenda binafsi za wafadhili hao kama masharti ya ufadhili ambayo mara nyingi huenda kinyume na mila na desturi za Kitanzania;

NA KWA KUWA, mwenendo wa asasi hizo unachangia ukiukwaji wa maadili, mila na desturi bora za Kitanzania;

KWA HIYO BASI, Kamati inaishauri Serikali kuweka utaratibu maalum wa kufuatilia uendeshaji wa shughuli za Asasi Zisizo za Kiserikali zinazojishughulisha na masuala ya UKIMWI ili kuhakikisha kuwa zinafanya kazi kwa kuzingatia maadili, mila na desturi za Kitanzania.

Saba, KWA KUWA, imebainika kuwa makundi yaliyo katika hatari zaidi ya kupata maambukizi ya VVU bado yanahitaji elimu ya kinga dhidi ya maambukizi ya UKIMWI na kwa ushiriki wa vijana katika kuibua, kupanga na kutekeleza afua za UKIMWI nchini ni duni;

NA KWA KUWA, kukosekana kwa elimu ya kinga dhidi ya maambukizi ya UKIMWI kwa makundi hayo pamoja na ushiriki duni wa makundi hayo katika kuibua na kupanga afua za UKIMWI kunasababisha kutofanikiwa kwa juhudi za kutokomeza kabisa maambukizi mapya;

KWA HIYO BASI, Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

(a) Tume ijikite zaidi katika kutoa elimu ya kinga dhidi ya maambukizi ya UKIMWI katika makundi yaliyo katika hatari zaidi ya kupata maambukizi ya VVU ikiwemo watumiaji wa dawa za kulevya hasa kwa njia ya kujidunga, wanaume wanaofanya ngono ya jinsia moja, wafanyabiashara ya ngono, madereva wa magari ya masafa marefu na maeneo ya shughuli mbalimbali za kiuchumi ikiwemo migodi, mialo, ujenzi wa barabara na kadhalika; na

(b) Serikali itoe huduma rafiki kwa vijana hasa katika huduma za afya ili kuongeza ushiriki wa vijana katika kuibua, kupanga na kutekeleza afua za UKIMWI nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya nne inahusu hitimisho; napenda kukushukuru tena kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha taarifa ya Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu yake hadi kufikia Januari, 2017. Tunaamini kuwa fursa hii inayotokana na masharti ya Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, itasaidia kuliwezesha Bunge lako Tukufu kutekeleza wajibu wake ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Ajira, Vijana na Walemavu, Mheshimiwa Jenista Mhagama na aliyekuwa Naibu Waziri wake Mheshimiwa Dkt. Abdallah Possi. Aidha, nampongeza pia Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania, Dkt. Leonard Maboko na Kaimu Kamishna wa Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya, Ndugu Aida Tesha na watendaji wote wa Tume hizo kwa ushirikiano walioipa Kamati kwa kipindi cha mwaka mzima, kwa kufika mbele ya Kamati na kutoa ufafanuzi mara zote ulipohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah, kwa ushirikiano ambao amekuwa akitoa kwa Kamati. Pamoja na yeye, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndugu Athumani Hussein, Wakurugenzi Wasaidizi, Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Asia Msangi, Ndugu Happiness Ndalu na Ndugu Susan Ngole pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndugu Grace Mwenye, kwa kuratibu vyema Shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili taarifa hii na hatimaye kukubali maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hakuna anayeunga mkono hoja?

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Haya, imeungwa mkono hoja hiyo na wale pale wote.

# TAARIFA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI KWA KIPINDI CHA JANUARI, 2016 HADI JANUARI, 2017 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,**kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016; naomba kuwasilisha Taarifa ya Shughuli zilizotekelezwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kwa kipindi cha Januari, 2016 hadi Januari, 2017.

## *1.1 MAJUKUMU YA KAMATI NA SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA*

### 1.1.1 Majukumu

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane ya Kanuni chini ya 118 (10) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016, Kamati ya Masuala ya UKIMWI imepewa majukumu yafuatayo:

a) Kuratibu masuala yanayohusu UKIMWI katika sekta zote;

b) Kufuatilia utekelezaji wa sera na mipango ya Serikali kuhusu UKIMWI na udhibiti wa Madawa ya Kulevya;

c) Kujadili na kutoa mapendekezo na ushauri kuhusu hatua za kudhibiti madawa ya kulevya; na

d) Kushughulikia Bajeti za Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Madawa ya Kulevya.

### 1.1.2 Shughuli

**Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha mwaka mmoja yaani Januari 2016/Januari 2017 Kamati ilitekeleza majukumu yake kwa njia za vikao, semina na kongamano mbalimbalizilizohusu Masuala ya UKIMWI na Dawa za Kulevya, aidha Kamati ilifanya ziara za kazi katika Taasisi mbalimbali za Umma ili kujiridhisha na utekelezaji wa Sera za UKIMWI na Dawa za Kulevya katika maeneo hayo.

### a) Semina za Mafunzo

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia ugeni wa Wajumbe katika Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, katika kipindi cha Februari 2016

Kamati ilipata mafunzo mbalimbali yaliyoratibiwa na Ofisi ya Bunge kwa dhumuni la kuwajengea uwezo Wajumbe katika kutekeleza majukumu yao. Mafunzo hayo yalihusu mambo yafuatayo:

i. Muundo na majukumu ya Kamati;

ii. Kanuni na taratibu za uendeshaji wa shughuli za kamati;

iii. Muundo na majukumu ya Tume zinazosimamiwa na Kamati hii yaani, Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya; na

iv. Sheria na Sera mbalimbali zinazohusu udhibiti wa UKIMWI na Dawa za Kulevya nchini.

**b) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Taasisi zinazosimamiwa na Kamati.**
**Mheshimiwa Spika,** Nyongeza ya Nane chini ya Kanuni ya 118 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, imeipa Kamati jukumu la kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Taasisi mbili ambazo ni Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya. Aidha, Kanuni hiyo hiyo pia imeipa Kamati jukumu la kuratibu masuala yote yanayohusu UKIMWI katika sekta zote ikiwemo kufuatilia utekelezaji wa sera na mipango ya Serikali kuhusu UKIMWI na udhibiti wa dawa za kulevya.

**c) Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo**
**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016, Kamati ilikagua Mradi wa ujenzi wa ghala la kuhifadhia vielelezo vya kesi za dawa za kulevya wenye thamani ya shilingi milioni mia tatu hamsini (350,000,000) unaosimamiwa na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya uliopo Makao Makuu ya Jeshi la Polisi, Kurasini - Dar es Salaam. Aidha, katika kipindi hiki pia Kamati ilifanya ziara katika taasisi mbalimbali ili kufuatilia utekelezaji wa sera za UKIMWI na Dawa za Kulevya, Taasisi hizo ni pamoja na:

i. Hospitali ya Taifa Muhimbili na Hospitali ya Rufaa ya Mwananyamala katika Vituo vya Kutolea Huduma za Dawa ya *Methadone* kwa Warahibu wa Dawa za Kulevya;

ii. Pili Missana Foundation *Sobber House* iliyopo Kigamboni, Dar es Salaam;

iii. Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali;

iv. Bohari Kuu ya Madawa (MSD);

v. Mgodi wa Buzwagi uliopo Kahama, Shinyanga;

vi. Kituo cha Afya cha Kambarage, Shinyanga; na

**d) Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti za Taasisi zinazosimamiwa na Kamati**


**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016, Kamati ilikutana na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya ili kwa pamoja kujadili taarifa ya utekelezaji wa bajeti zao kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ambapo Kamati ilibaini changamoto mbalimbali za kiutendaji ambazo kwa kiasi kikubwa zilisababishwa na ufinyu wa bajeti zilizotengwa na Serikali kwa Tume hizi kama zinavyoonyeshwa katika majedwali na chati zifuatazo:

***JEDWALI NAMBA 1***

**MWENENDO WA BAJETI YA TUME YA KUDHIBITI UKIMWI TANZANIA KWA KIPINDI CHA MIAKA MITANO MFULULIZO KUANZIA 2011/2012 HADI 2016/2017**

| MWAKA | FEDHA ZA MAENDELEO | MATUMIZI YA KAWAIDA | JUMLA | MAONI |
|---|---|---|---|---|
| 2016/2017 | 5,235,823,413 | 4,961,677,000 | 10,197,500,443 | Bajeti inajumlisha Fedha za Mfuko wa UKIMWI Bilioni 5.6 |
| 2015/2016 | 2,744,438,000 | 6,387,068,000 | 9,131,506,000 | Bajeti inajumlisha Fedha za Mfuko wa UKIMWI Bilioni 3 |
| 2014/2015 | 5,341,286,000 | 3,358,663,400 | 8,699,949,400 | |
| 2013/2014 | 5,341,286,000 | 3,082,866,000 | 8,424,152,000 | |
| 2012/2013 | 15,341,286,000 | 2,809,683,657 | 18,272,734,455 | |
| 2011/2012 | 19,389,608,118 | 4,137,977,000 | 23,527,585,118 | |

**Chanzo: Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kwa miaka ya fedha 2011/12, 2012/13, 2013/14, 2014/15, 2015/16 na 2016/17**




*Chanzo: Jedwali Namba 1*


**Mheshimiwa Spika,** Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania ilianzakupungua katika kipindicha mwaka 2012/2013na kuwa katika hali yakupanda na kushuka hadi mwaka 2015/2016 kutokana na kupungua kwa mtiririko wa fedha za wafadhili katika bajeti ya miradi ya maendeleo. Aidha, kupanda na kushuka kwa mtiririko wa fedha za matumizi ya kawaida kwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania katika kipindi cha mwaka 2012/2013 hadi2016/2017, kumesababishwa na ukomo wa bajeti ya Serikali. Kwa kiasi kikubwa mwenendo huu wa bajeti umeathiri utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania katika mapambano dhidi ya maambukizi ya UKIMWI nchini.

***JEDWALI NAMBA 2:***

**MWENENDO WA BAJETI YA TUME YA KURATIBU UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA KWA KIPINDI CHA MIAKA MITANO MFULULIZO KUANZIA 2011/2012 HADI 2016/2017**

| MWAKA | FEDHA ZA MAENDELEO | MATUMIZI YA KAWAIDA | JUMLA | MAONI |
|---|---|---|---|---|
| 2016/2017 | 0 | 1,729,437,000 | 1,729,437,000 | |
| 2015/2016 | 860,000,000 | 2,159,488,359 | 3,019,488,359 | |
| 2014/2015 | 3,430,000,000 | 3,601,549,718 | 7,031,549,718 | Bajeti inajumlisha Fedha za Wafadhili |
| 2013/2014 | 2,798,000,000 | 2,587,176,826 | 5,385,176,826 | Bajeti inajumlisha Fedha za Wafadhili |
| 2012/2013 | 1,180,000,000 | 1,000,491,400 | 2,180,491,400 | |
| 2011/2012 | 1,254,767,000 | 1,150,000,000 | 2,404,767,000 | |

**Chanzo:** Bajeti za Tume ya Kuratibu Udhibiti waDawa za Kulevya kwa miaka ya fedha 2011/12, 2012/13, 2013/14, 2014/15, 2015/16 na 2016/17.




*Chanzo: Jedwali Namba 2*

**Mheshimiwa Spika,** bajeti ya Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya ambayo kwa sasa inajulikana kama Mamlaka ya Kudhibiti na

Kupambana na Dawa za Kulevya katika kipindi cha mwaka 2011/2012 na 2012/2013 likuwa chini kutokana na ukomo wa bajeti za Serikali ulioendana sawia na kiwango cha ushamiri wa biashara na matumizi ya dawa za kulevya katika kipindi hicho; ikilinganishwa na miaka 2013/2014 na 2014/2015, ambapo ushamiri wa biashara ya dawa za kulevya uliongezeka na bajeti ya Tume iliongezekakutokana na kuongezeka umakini wa Serikali na wafadhili katika kudhibiti biashara na matumizi ya dawa za kulevya nchini. Hata hivyo,katika kipindi cha mwaka 2015/2016 na 2016/2017, bajeti za Tume zilishuka hadi kufikia shilingi 0 kwa miradi ya maendeleo kwa mwaka 2016/2017 kutokana na ukomo wa fedha za wafadhili na kubadilika kwa vipaumbele vya bajeti ya serikali. Kwa ujumla, mwenendo mzimawa bajeti ya Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya umechangia kwa kiasi kikubwakupunguza ufanisi wa Tume katika kudhibiti biashara na matumizi ya dawa za kulevya nchini.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI

**Mheshimiwa Spika,**utekelezaji wa majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI ulizingatia masharti ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 hususan Kanuni ya 117 inayohusu utaratibu katika Kamati za Kudumu za Bunge. Hivyo,Kamati iliandaa Mpango Kaziuliotekelezwa katika kipindi cha Januari 2016 hadi Januari 2017, ambao Matokeo ya Utekelezaji wake yamefanyiwa Uchambuzi katika Sehemu hii.

### *2.1 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI*

### 2.1.1 Semina za Mafunzo

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia kuundwa upya kwa Kamati za Kudumu za Bunge mnamo Januari 15, 2016 Wajumbe wa Kamati ya Masuala ya UKIMWI walipata mafunzo mbalimbali yaliyolenga kuwajengea uwezo wa kutekeleza majukumu yao kwa ufasaha, namafunzo hayo yaligawanyika katika sehemu kuu mbili:

#### a) Taratibu za Uendeshaji wa Shughuli za Kamati

**Mheshimiwa Spika,** Wajumbe walipata elimu kuhusu mambo mbalimbali yanayohusu Kamati ikiwemo muundo, majukumu na taratibu za uendeshaji wa Shughuli za Kamati kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.Aidha, kupitia mafunzo haya Wajumbe walipata uelewa wa kina katika maeneo ya uchambuzi wa bajeti za wizara/taasisi, uchambuzi wa miswada na taratibu za miswada Bungeni, pamoja na mahusiano ambayo kwa kipindi cha nyuma Kamati ilifanikiwa kuyaanzisha na vyombo vingine vya ndani na nje ya nchi vilivyojikita katika mapambano dhidi ya maambukizi ya UKIMWI.

### b) Taratibu za Uendeshaji wa Tume zinazosimamiwa na Kamati

**Mheshimiwa Spika,** Wajumbe walipata elimu kuhusu mambo mbalimbali yanayohusu Shughuli za Kamati ikiwemo muundo na majukumu ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya, pia Wajumbe wa Kamati waliweza kupata ufahamu juu ya sheria na sera zinazosimamia uratibu na utekelezaji wa majukumu ya Tume hizo na taasisi nyingine zote zinazotekeleza Sera za UKIMWI na Dawa za Kulevya nchini. Mbali na kupata uelewa juu ya mipango na mikakati madhubuti ya Tume hizi katika kutekeleza majukumu yake, Wajumbe pia walipata ufahamu juu ya hali halisi ya maambukizi ya UKIMWI na udhibiti wa dawa za kulevya kwa mwaka 2015/2016.

## 3.0 KUFUATILIA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya Kamati kujengewa uwezo kupitia semina mbalimbali za Mafunzo, Kamati ilianza utekelezaji wa majukumu yake kwa kufuatilia kwa ukaribu utendaji kazi wa Taasisi zilizo chini yake pamoja na utekelezaji wa sera na mipango anuai inayohusu Udhibiti wa UKIMWI na Dawa za Kulevya katika Wizara na Taasisi za Umma nchini kama ifuatavyo:

### *3.1 TUME YA KUDHIBITI UKIMWI TANZANIA*

**Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania, Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

a. Changamoto kubwa inayoikumba Tume ni Ufinyu wa Bajeti na ucheleweshwaji wa fedha kutoka serikalini ambapo kwa sasa, zaidi ya asilimia 90 ya bajeti ya Tume inategemea fedha za wafadhili wa nje hali iliyopelekea kupunguza ufanisi wa Tume katika mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU na UKIMWI;

b. Mapungufu katika Sera ya UKIMWI ya 2001 ambayo imepelekea Tume na Wadau wa UKIMWI kushindwa kwenda na kasi inayohitajika sasa katika kudhibiti Maambukizi ya Virusi vya UKIMWI;

c. Kutokamilika kwa Muundo wa Tume unaopelekea uchache wa watumishi wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania unaoenda sambamba na uhaba wa fursa za kujiendeleza kitaaluma; na

d. Uelewa mdogo wa jamii hususan katika makundi maalumu, kuhusu namna ya kujikinga na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI.

#### 3.1.1 TUME YA KURATIBU UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA

**Mheshimiwa Spika,** katika kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Tume hii, Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

a. Ufinyu wa Bajeti inayotengwa na Serikali pamoja na ucheleweshwaji wa mtiririko wa fedha kutoka Wizara ya Fedha ambao unapelekea mambo yafuatayo:

i. Kukosekana kwa vitendea kazi vya kisasa vinavyopelekea kupungua kwa ufanisi katika udhibiti wa dawa za kulevya nchini;

ii. Tume kushindwa kutoa elimu kwa umma juu ya athari za matumizi ya dawa za kulevya;

iii. Tume kushindwa kufanya operesheni za ukamataji wa wafanyabiashara wa dawa za kulevya na uteketezaji wa mashamba makubwa ya Bangi katika mikoa inayoongoza kwa kilimo cha zao hilo ambalo ni haramu; na

iv. Kukosekanakwa programu maalum zenye lengo la kuwainua kiuchumi warahibu wa dawa za kulevya ambao huchangia kukwamisha juhudi zaokatika kuachana moja kwa moja na matumiziya dawa za kulevya.

b. Kutokamilika kwa Muundo wa Tume unaopelekea uchache wa watumishi wenye taaluma mbalimbali wanaohitajika katika kuongeza ufanisi wa Tume katika kudhibiti dawa za kulevya nchini.

### *3.2 TAASISI ZA UMMA ZA KISEKTA ZINAZOTEKELEZA SERA ZA UKIMWI NA DAWA ZA KULEVYA*

#### 3.2.1 Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikutana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na kujadili Mwongozo wa namna ya kuwahudumia Watumishi wa Umma wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (*Workplace Interventions, Medical Treatment and Training to Staff)* ambapo Kamati ilishauri mambo yafuatayo:
a. Waajiri kuhamasisha na kuwajengea watumishi ujasiri wa kupima VVU,kutoa elimu ya kujikinga dhidi ya maambukizi ya UKIMWI na kutekeleza afua za UKIMWI mahala pa kazi;

b. Serikali kuwachukulia hatua waajiri wanaotumia fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya WAVIU kwa shughuli nyingine zisizohusiana na UKIMWI;

c. Serikali kuongeza ajira katika viwanda vidogovidogo na katika sekta binafsi ili kukuza uchumi na kuwawezesha vijana kupata ajira ili kuwaepusha kujihusisha na matumizi ya dawa za kulevya na tabia hatarishi zinazochochea kuongezeka kwamaambukizi ya VVU na UKIMWI; na

d. Serikali kuendelea kuwasisitiza waajiri katika utumishi wa umma kutumia fursa zinazowazunguka ili kudhibiti tatizo la unyanyapaa ambao huchangia kurudisha nyuma juhudi za Serikali katika mapambano dhidi ya maambukizi ya UKIMWI.

### 3.2.2 Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee Na Watoto

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikutana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ili kujadili kuhusu hatua iliyofikiwa katika Utafiti wa Upatikanaji wa Chanjo ya UKIMWI Tanzania, ambapo Kamati ilibaini kuwa wataalamu wa utafiti wa tiba bado wapo kwenye hatua za awali za utafiti wa chanjo hiyo kutokana na changamoto ya rasilimali fedha, rasilimali watu na teknolojia ya juu inayohitajika katika utafiti wa chanjo. Hivyo, kuifanya Tanzania kama zilivyo nchi nyingi za Afrika kutegemea kwa kiasi kikubwa tafiti zinazofanywa na nchi zilizoendelea kama Marekani. Kwa sababu hiyo, Kamati ilishauri mambo yafuatayo:

a. Serikali kuona umuhimu wa kuwekeza katika utafiti wa chanjo ya UKIMWI; kwa kuongeza Bajeti ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto;

b. Wizara kujielekeza zaidi katika kutoa elimu kwa wananchi juu ya kujikinga na maambukizi ya VVU na UKIMWI, pamoja na Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa (MSY) kwa maana "*Kinga ni bora kuliko Tiba*".

### 3.2.3 Bohari Kuu ya Madawa (MSD) na Baraza la WAVIU (NACOPHA)

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikutana na Bohari Kuu ya Madawa nchini pamoja na Baraza la Watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI ili kujadili mafanikio na changamoto zilizopo katika upatikanaji, usambazaji na utumiaji wa dawa za kufubaza makali ya VVU (ARVs) nchini. Ambapo, Kamati ilibaini uwepo wa changamoto katika upatikanaji wa dawa hizo katika vituo vingi vya afya nchini inayosababishwa na malimbikizo ya madeni ya Bohari Kuu ya Madawa katika Mamlaka ya Bandari, hali iliyopelekea watumiaji wa dawa hizo kulazimika kununua dawa katika maduka ya dawa ya watu binafsi kwa bei za juuhuku wengine wakishindwa kumudu gharama hizo na kujikuta wakidhoofika.Hivyo, Kamati ilishauri mambo yafuatayo:

a. Serikali kufanya jitihada za haraka za ulipaji wa deni kwa Bohari Kuu ya Dawa (MSD) ili kuwasaidia WAVIU kupata dawa za kufubaza makali ya VVU kwa wakati pia kutowakatisha tamaa Wafadhili wanaotuletea dawa hizo;

b. Serikali kuwekeza katika uzalishaji wa ndani wa dawa hizi ili kuondokana na utegemezi wa wafadhili katika ununuzi wa madawa kama jirani zetu wa Uganda wanavyofanya; na

c. Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa itoe Waraka utakaohusu Halmashauri zote kushirikiana na Mabaraza ya WAVIU katika kubuni njia za kuwakwamua kiuchumi WAVIU na kusaidia katika mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU.

### 3.2.4 Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikutana na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ili kujadilimafanikio na changamoto zilizopo katika utekelezaji wa Afua za UKIMWI katika Ofisi hiyo, ambapo Kamati ilibaini yafuatayo:

a. Ufinyu wa bajeti iliyotengwa na Serikali kwa ajili ya kuwahudumia watumishi WAVIU na kuratibu masuala mbalimbali yanayohusu UKIMWI katika Ofisi hii;

b. Ufinyu wa bajeti nzima ya uendeshaji wa shughuli za Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, uliopelekea Ofisi hii kushindwa kutekeleza majukumu yake yote ipasavyo ikiwa ni pamoja na kufanya ukaguzi wa fedha za UKIMWI katika Ofisi/Taasisi zote za Umma na Asasi zisizo za kiserikali ambazo fedha zake zinapitia Wizara ya Fedha.

**Mheshimiwa Spika,**Kwa sababu hiyo, Kamati ilimshauri Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kufanya Ukaguzi wa "*Value-for-Money*" kwa Fedha zote za Masuala ya UKIMWI ili kuona kama pesa zinazotengwa mahususi kushughulikia Masuala ya UKIMWI zinatumika kama zilivyokusudiwa.

### 3.2.5 Wizara ya Habari, Utamaduni, Wasanii na Michezo

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikutana pia na Wizara ya Habari, Utamaduni, Wasanii na Michezo kwa lengo la kujadili Taarifa ya Wizara kuhusu Utekelezaji wa Afua za UKIMWI mahali pa kazi ambapo Kamati ilibaini kuwa utekelezaji wa Mwongozo huo katika wizara hii umejikita zaidi katika kuwapatia posho za kujikimu watumishi ambao ni WAVIU, lakini kuna jitihada ndogo sana zinazofanywa katika utoaji wa elimu ya kujikinga dhidi ya maambukizi mapya kwa watumishi wa wizara hiyo. Hivyo, Kamati ilishauri mambo makubwa mawili kwa Wizara hii:

a. Wizara kuweka matangazo mengi yanayohusu Mapambano dhidi ya UKIMWI kwenye viwanja vya michezo ili elimu kuhusu UKIMWI iweze kuwafikia wananchi wengi zaidi; na

b. Wizara kuweka mikakati madhubuti ya kuwasaidia wanamichezo na wasanii kwa ujumla kutokujihusisha na matumizi ya dawa zaa kulevya.

### 3.2.6 *Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikutana na Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi ili kujadili Taarifa yao ya Utekelezaji wa Mwongozo wa Afua za UKIMWI Mahali pa Kaziambapo changamoto kubwa iliyobainika naKamati ni utekelezaji mdogo wa afua za UKIMWI katika wizara yenyewe na taasisi inazozisimamia, hivyo Kamati ilishauri mambo yafuatayo:

a. Wizara isimamie vyema utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ya Mwaka 2014 kuhusu Malengo na Matamko yanayohusu Mapambano dhidi ya Maambukizi ya VVU kwa watumishi; na

b. Serikali kuziagiza shule zote nchini kuweka ajenda ya UKIMWI na dawa za kulevya kunapokuwa na vikao vya wazazi na wanafunzi ili kuhakikisha wanafunzi na wazazi wanapata uelewa juu ya kujikinga dhidi ya UKIMWI na matumizi ya Dawa za Kulevya.

### 3.2.7 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikutana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ili kujadili mafanikio, changamoto na matarajio ya Wizara hii katika Udhibiti wa Matumizi ya Dawa za Kulevya nchini ambapo, Kamati ilibaini changamoto nyingi zilizotokana na ufinyu wa bajeti ya wizara, hivyo kupelekea zoezi la udhibiti wa dawa za kulevya nchini kutokuwa na matokeo ya kuridhisha.Hii imetokana na bajeti yawizara hii kupungua kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na kufikia shilingi bilioni 30,000,000,000 kwa miradi ya maendeleo ikilinganishwa na kiasi cha shilingi bilioni 65,757,261,000 zilizotengwa kwa mwaka wa fedha uliopita 2015/2016. Hivyo, Kamati ilishauri yafuatayo:

a. Jeshi la Polisi kuongezewa Bajeti ili kuwawezesha kununua vitendea kazi kama boti za doria ili kukabiliana na changamoto wanazopata katika kudhibiti uingizwaji wa dawa za kulevya nchini; na

b. Jeshi la Polisi kuimarisha ulinzi hususan katika maeneo ya bandari, viwanja vya ndege na mipaka ya nchi.

## *4.0 UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO*

### 4.1 Mradi wa Ujenzi wa Ghala la Kuhifadhia Dawa za Kulevya

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikaguaMradi wa Ujenzi wa Ghala la Kuhifadhia Vielelezo vya Kesi za Dawa za Kulevya wenye thamani ya shilingi Milioni 272,500,000uliotekelezwa ndani ya Makao Makuu ya Jeshi la Polisi Kurasini, Dar es Salaam na kusimamiwa na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya.Kamati ilibaini mapungufu mengi katika Mradi yakiwemo:

a. Udogo wa eneo la ghala na ubora usioridhisha wa viwango vya ujenzi ikilinganishwa na mahitaji makubwa ya hifadhi za vidhibiti vya dawa za kulevya vilivyohifadhiwa ndani ya ghala hilo na vile vinavyoendelea kukamatwa; na

b. Mazingira magumu na hatarishi ya Watumishi wanaofanya kazi katika ghala hilo, kutokana na ukosefu wa vitendea kazi wengi wao wameathirika kwa kuvuta hewa iliyochanganyika na dawa za kulevya na wengine kunusurika na milipuko inayosababishwa na kemikali za madawa hayo.

**Mheshimiwa Spika,**kutokana na mapungufu haya, Kamati inashauri mambo yafuatayo:

a. Serikali kuona umuhimu wa kutenga fedha za kutosha ili kujenga ghala kubwa, imara na la kisasa litakalokidhi mahitaji ya sasa ya kuhifadhi vidhibiti vya sampuli mbalimbali za dawa za kulevya vinavyokamatwa (*ushahidi*);

b. Serikali iwekeze katika vitendea kazi vya kisasa vitakavyolinda afya za watumishi lakini pia vitakavyorahisisha zoezi la upekuzi na ukamataji wa dawa za kulevya zinazoingizwa nchini kupitia njia mbalimbali; na

c. Serikali kutoamotishakwa watumishi wa kitengo maalumu cha udhibiti wa dawa za kulevya kwa kuboresha mazingira wanayofanyia kazi ikiwemo posho, ofisi na vitendea kazi.

### 4.2 Ziara

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hiki pia Kamati ilifanya ziara za kazi katika taasisi mbalimbali ili kufuatilia utekelezaji wa sera za UKIMWI na Dawa za Kulevya, Taasisi hizo ni pamoja na Vituo vya Kutolea Huduma za Dawa ya Methadone kwa Warahibu wa Dawa za Kulevya vilivyopo katika Hospitali ya Taifa Muhimbili na Hospitali ya Mwananyamala, Pili Missana Foundation Sobber House,Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali,Bohari Kuu ya Madawa (MSD), Mgodi

wa Dhahabu wa Acacia, na Kliniki ya WAVIU katikaKituo cha Afya cha Kambarage.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na ziara hizi, Kamati inashauri mambo yafuatayo:
a. Serikali kutenga bajeti ya kutosha ili kuiwezesha Ofisi ya Mkemia Mkuu kumudu gharama za kuendesha ofisi kwa wakati na kwa ufanisi; ili kusaidia kupunguza mlundikano wa kesi za dawa za kulevya;

b. Serikali kuona umuhimu wa kupitisha sheria zitakazolinda uanzishwaji wa wakala mbalimbali wa serikali ili kuzipa mamlaka kamili wakala hizo katika maeneo yao ya utendaji;

c. Kudumisha ushirikiano wa kazi kati ya Jeshi la Polisi, Mahakama na Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali ili kuongeza ufanisi katika kushughulikia masuala yanayohusu udhibiti wa Dawa za Kulevya nchini;

d. Serikali itenge bajeti ya kutosha ili kuwezesha ujenzi wa vituo vingi vya huduma ya tiba ya utengemao kwa warahibu wa dawa za kulevya, ununuzi wa vitendea kazi, vifaa tiba na kuajiri watumishi ili kuleta ufanisi katika utoaji wa huduma;

e. Kuwepo na takwimu za WAVIU Mahala pa Kazi ili kuwezesha serikali kuchukua hatua sahihi.

**5.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI**

**Mheshimiwa Spika**, mwezi Aprili, 2016 Kamati ilikutana na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya kwa mwaka wa fedha 2015/2016, kisha Kamati ilipitia na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya – *Fungu 91* na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) – *Fungu* 92kwa mwaka wa fedha 2016/2017; kama ilivyoainishwa katika Nyongeza ya Nane ya Kanuni ya 118 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya, Kamati ilizingatia maelezo na fafanuzi mbalimbali zilizotolewa na Tume hizo kuhusiana na Makadirio ya Mapato na Matumizi yao ambapo Kamati ilipitisha shilingi bilioni 2,340,236,000kwa matumizi ya kawaida kwaFungu 91 - Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya na hakuna kiasi kilichotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Aidha, kiasi cha shilingi bilioni 4,961,677,000 kilitengwakwa

matumizi ya kawaidana shilingi bilioni 5,235,823,413 kwa miradi ya maendeleo kwaFungu 92 - Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kwa mwaka wa fedha 2016/2017.Ambapo, Kamati iliridhia na kupitisha Makadirio ya Tume zote mbili na kuwasilisha maoni yake ikiwa ni pamoja na kuliomba Bunge lipitishe Makadirio ya Tume hizo kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

## SEHEMU YA TATU

## 6.0 MAONI NA USHAURI

**Mheshimiwa Spika,** kutokana nashughuli za Kamati zilizofanyika katika kipindi cha mwaka mmoja (Januari, 2016 - Januari, 2017) kumekuwa na changamoto mbalimbali zilizojitokeza katika Taasisi zinazosimamiwa na Kamati hii ambazo Kamati inazitolea maoni na ushauri ufuatao:

### TUME YA KURATIBU UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA

**Mheshimiwa Spika,** ili kutekeleza vyema majukumu ya Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya, Kamati inashauri mambo Nane (8) yafuatayo:-
**1. Kwa kuwa,** Kamati imebaini dosari nyingi katika Sera ya Dawa za Kulevya ya mwaka 2004 ambayo imepitwa na wakati,

**Na kwa kuwa,**dosari hizozimechangia ugumu katika utatuzi wa changamoto za sasa kuhusu udhibiti wa uingizwaji na matumizi ya dawa za kulevya, hali inayopelekea taifa kuendelea kupoteza nguvu kazi.

**Kwa hiyo basi**, Kamati inashauri kuwa Serikali iharakishe mapitio ya sera hii ili kulinusuru taifa na janga hili la dawa za kulevya.

**2. Kwa kuwa,** Kamati imebaini kuwa tangu Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya ibadilishwe kisheria kuwa Mamlaka ya Kupambana na Dawa za Kulevya, muundo wake bado haujakamilika,

**Na kwa kuwa,**kutokukamilika kwa muundo huo kunasababisha Tume kushindwa kuajiri watumishi wa kutosha (*watumishi 37 kati ya 65 wanaohitajika*),

**Kwa hiyo basi,** Kamati inaishauri serikali kuharakishana kukamilisha mchakato wa muundo wa Mamlaka hii ili uanze kutumika mara moja na kuongeza ufanisi katika kudhibiti uingizwaji na matumizi ya dawa za kulevya.

**3. Kwa kuwa**, imebainika kwamba Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa Tume umekuwa unakwamisha utendaji wa baadhi ya majukumu ya Tume hii kama vile:

a) Kudhibiti uingizwaji wa dawa za kulevya katika mipaka yote ya nchi ambayo ni mingi na ina vipenyo vingi vinavyofanya zoezi la udhibiti kuwa gumu;

b) Tume kushindwa kuteketeza mashamba ya bangi ambayo hulimwa sehemu zisizofikika kwa urahisi ambapo utekelezaji wa zoezi hilo uhitaji fedha nyingi; na
c) Tume kushindwa kutoa elimu kwa wananchi kuhusu madhara yatokanayo na matumizi ya dawa za kulevya ili kunusuru afya za Watanzania na nguvu kazi ya taifa.

**Na kwa kuwa**, kutotekelezwa kwa majukumu ya msingi ya Tume hiyo kutokana na ufinyu wa bajeti kunaathiri juhudi za Udhibiti wa dawa za Kulevya nchini jambo ambalo lina madhara makubwa kwa taifa,

**Kwa hiyo basi,** Kamati inaishauri Serikali kuangalia uzito wa majukumu yanayotekelezwa na Tume hii katika kupambana na biashara haramu ya dawa za kulevya nchini, kwa kuongeza bajeti yao ili kuiongezea ufanisi Tume na kuhakikisha kuwa mafanikio yaliyofikiwa katika udhibiti wa dawa za kulevya hayapotei.

**4. Kwa kuwa**, Kamati imebaini kukosekana kwa chombo cha kisheria cha kushughulikia udhibiti wa biashara na matumizi ya dawa za kulevya katika ngazi ya halmashauri,

**Na kwa kuwa,** kukosekana kwa chombo hicho kunachangia udhibiti duni wa dawa za kulevya katika halmashauri nchini,

**Kwa hiyo basi**, Kamati inaishauri Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kufanya maboresho ya Kamati za UKIMWI za Halmashauri ili kisheria ziwe na uwezo wa kusimamia shughuli za udhibiti wa dawa za kulevya katika ngazi ya halmashauri kama ilivyo kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, kwa lengo la kusimamia kwa pamoja mambo haya yanayoendana.

**5. Kwa kuwa,** Serikali imebaini changamoto katika upatikanaji wa tiba za utengemao (*Rehabilitation*) wa warahibu (*Addicts*) wa dawa za kulevya nchini ambapo kwa sasa zinapatikana katika mkoa wa Dar es Salaam na Zanzibar pekee,

**Na kwa kuwa**, changamoto hiyo inakwamisha juhudi za kuwawezesha Warahibu kuacha matumizi ya dawa za kulevya, jambo linalochangia madhara ya kijamii nchini,

**Kwa hiyo basi**, Kamati inashauri kwamba huduma hii ihuisihwe katika Sera ya Afya kama ilivyofanyika kwa suala la UKIMWI ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma hii kwa nchi nzima.

**6. Kwa kuwa,** Kamati imebaini uwepo wa mwamko mdogo na ushiriki duni wa jamii katika mapambano dhidi ya biashara haramu ya dawa za kulevya,

**Na kwa kuwa,**hali hiyo kwa kiasi kikubwa imesababisha ongezeko la watumiaji wa dawa za kulevya, wagonjwa wa akili na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI,

**Kwa hiyo basi,**Kamati inashauri:
a) Tume ishirikiane na vyombo vya dola katika kuandaa kampeni endelevu ambazo mbali na kuwajengea uelewa watanzania kuhusu umuhimu wa kushiriki katika mapambano haya, pia utawapa motisha ya kushiriki katika mapambano dhidi ya biashara ya dawa za kulevya; na

b) Viongozi wakuu wa nchi kutoa kauli thabiti na kusimamia utekelezaji wa kauli hizo katika kukemea na kukomesha biashara na matumizi ya dawa za kulevya ili kuhamasisha ushiriki wa jamii nzima katika janga hili.

**7. Kwa kuwa**, Kamati imebaini uwepo wa changamoto mbalimbali zinazowakabili warahibu (*Addicts*) wa dawa za kulevya punde wanapoacha matumizi ya dawa hizo, kama kutengwa na jamii na kukosa ajira,

**Na kwa kuwa**, changamoto hizo husababisha Warahibu kurudia matumizi ya dawa za kulevya au kujiingiza katika vitendo vya uhalifu.

**Kwa hiyo basi**, Kamati inashauri kuwa, Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Ajira, Vijana na Walemavu ianzishe programu maalumu za kuwasaidia warahibu wa dawa za kulevya kuweza kujiinua na kujitegemeza kiuchumi mara tu baada ya kuachana na matumizi ya dawa za kulevya.

**8. Kwa kuwa**, Kamati imebaini uwepo wa uhusiano mkubwa kati ya matumizi ya pombe za bei rahisi maarufu kama "*viroba*" na kuongezeka kwa tabia hatarishi zinazochangia ongezeko la vijana katika matumizi ya dawa za kulevya,

**Na kwa kuwa**, hali hiyo inaathiri ufanisi wa nguvu kazi ya taifa kutokana na madhara ya matumizi ya dawa za kulevya,

**Kwa hiyo basi,**Kamati inaishauri Serikali kufungia kabisa uzalishaji na uuzwaji wa pombe za bei rahisi maarufu kama "*viroba*" ili kulinusuru taifa.

**TUME YA KUDHIBITI UKIMWI TANZANIA;**

**Mheshimiwa Spika,** ili Tume hii iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa, Kamati inashauri mambo Saba (7) yafuatayo:-

**1. Kwa kuwa**, Kamati imebaini dosari nyingi katika Sera ya UKIMWI ya mwaka 2001,

**Na kwa kuwa,** dosari hizo zinachangia kukosekana kwa mafanikio katika malengo ya Sera, ikiwemo kushindwa kuendana na hali halisi ya maambukizi ya Virusi vya UKIMWI nchini,

**Kwa hiyo basi**, Kamati inaishauri Serikali kuharakishamchakato wamapitio ya sera hii utakaoshirikisha wadau wote muhimu;

**2. Kwa kuwa,**Marekebisho ya Sheria Na. 6 ya mwaka 2015 yalihitaji Muundo Mpya wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI nchini ili kuongeza ufanisi wa kiutendaji na kwamba Mchakato wa kuandaa Muundo huo haujakamilika,

**Na kwa kuwa**, Kutokamilika kwa Muundo huo kunasababisha kupunguza ufanisi katika mapambano dhidi ya UKIMWI,

**Kwa hiyo basi**, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha ukamilishaji wa muundo ili uanze kutumika mara moja na kuongeza ufanisi katika udhibiti wa UKIMWI.

**3. Kwa kuwa**, Kamati imebaini Changamoto kubwa katika utengaji wa bajeti ya Mfuko wa UKIMWI ulioanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Na. 22 ya mwaka 2001 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2015,

**Na kwa kuwa** changamoto hiyo inasababisha utegemezi uliokithiri kwa fedha za wafadhili katika kutekeleza majukumu ya udhibiti wa UKIMWI nchini ikiwemo, upatikanaji wa uhakika wa Dawa za kufubaza makali ya VVU (ARVs) na huduma nyingine zisizo za kitabibu.

**Kwa hiyo basi**, Kamati inashauri kuwa katika utengaji wa bajeti ya Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI (ATF), Serikali ianzishe kisheria chanzo mahususi

cha kutunisha Mfuko huu kama ilivyo katika Mifuko mingine kama vile Mfuko wa Barabara (*Road Fund*) ili kupunguza utegemezi mkubwa kwa fedha za wafadhili ambazo mbali na kuambatana na masharti magumu, hivi sasa zimeanza kupungua.

**4. Kwa kuwa,** Kamati ilibaini changamoto ya ufinyu wa bajeti kwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) pamoja na ucheleweshaji wa fedha hizo kutoka Hazina,

**Na kwa kuwa,** hali hii inasababisha:

a) Tume kushindwa kuajiri watumishi wa kutosha katika Ofisi zake (kwa sasa ina watumishi 83 kati ya 120 wanaohitajika);

b) Tume kushindwa kuwaendeleza kitaalumawatumishi wake hasa katika maeneo ya Ukaguzi wa Ndani, Tathminina Teknolojia ya Habari na Mawasiliano inayokuwa kwa kasi duniani; na

c) Tume kushindwa kumudu gharama za uendeshaji wa ofisi kwa ujumla.
**Kwa hiyo basi**, Kamati inashauri kuwa:

a) Serikali itoe kipaumbele katika mapambano dhidi ya UKIMWI kwa kutenga bajeti ya kutosha kwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania ili kuhakikisha kuwa mafanikio yaliyofikiwa katika udhibiti wa UKIMWI nchini hayapotei;

b) Kwa kuzingatia kiwango cha bajeti inayotolewa na Serikali, Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzaniaiweke utaratibu maalum wa kuwaendeleza watumishi wake ili kuendana na kasi ya ukuaji wa TEHAMA duniani;

**5. Kwa kuwa**, Kamati imebaini Changamoto ya Ukosefu wa Takwimu za Taifa kuhusu Maambukizi ya UKIMWI nchini,

**Na kwa kuwa,** ukosefu wa Takwimu sahihi na za kutumainiwa (*Reliable*) unasababisha Serikali kushindwa kuchukua hatua sahihi katika mapambano dhidi ya UKIMWI,

**Kwa hiyo basi,** Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania inaijengea uwezo thabiti divisheni ya Ufuatiliaji na Tathmini ili kwa kushirikiana na Ofisi ya Takwimu ya Taifa na Taasisi nyingine za utafiti, Tume iweze kukusanya na kuchapa takwimu za maambukizi ya virusi vya UKIMWI kwa nchi nzima.

**6. Kwa kuwa,**Baadhi ya Asasi zisizo za Kiserikali (AZISE yaani NGOs) zinazofanya kazi za Masuala ya UKIMWI kwa ufadhili wa watu wa nje, hutekeleza pia ajenda binafsi za wafadhili hao kama masharti ya ufadhili ambayo mara nyingi huenda kinyume na mila na desturi za kitanzania;

**Na kwa kuwa,** mwenendo wa Asasi hizo unachangia ukiukwaji wa maadili, mila na desturi bora za kitanzania,

**Kwa hiyo basi**, Kamati inaishauri Serikali kuweka utaratibu maalum wakufuatilia uendeshaji wa shughuli za Asasi zisizo za Kiserikali zinazojishughulisha na masuala ya UKIMWI ili kuhakikisha kuwa zinafanya kazi kwa kuzingatia maadili, mila na desturi za kitanzania.

**7. Kwa kuwa,**imebainika kuwa makundi yaliyo katika hatari zaidi ya kupata maambukizi ya VVU bado yanahitaji elimu ya kinga dhidi ya Maambukizi ya UKIMWI, na kwamba ushiriki wa vijana katika kuibua, kupanga na kutekeleza afua za UKIMWI nchini ni duni,

**Na kwa kuwa,** kukosekana kwa elimu ya kingadhidi ya Maambukizi ya UKIMWI,kwa makundi hayo pamoja na ushiriki duni wa makundi hayo katika kuibua na kupanga afua za UKIMWI kunasababisha kutokufanikiwa kwa juhudi za kutokomeza kabisa Maambukizi mapya.

**Kwa hiyo basi,**Kamati inashauri mambo yafuatayo:

a) Tume ijikite zaidi katika kutoa elimu ya kinga dhidi ya Maambukizi ya UKIMWI katika makundi yaliyo katika hatari zaidi ya kupata maambukizi ya VVU ikiwemo watumiaji wa dawa za kulevya hasa kwa njia ya kujidunga, wanaume wanaofanya ngono ya jinsia moja, wafanyabiashara ngono, madereva wa magari ya masafa marefu na maeneo ya shughuli mbalimbali za kiuchumi ikiwemo migodi, mialo, ujenzi wa barabara, n.k; na

b) Serikali itoe huduma rafiki kwa vijana hasa katika huduma za afya ili kuongeza ushiriki wa vijana katika kuibua, kupanga na kutekeleza afua za UKIMWI nchini.

## SEHEMU YA NNE

### 7.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** napenda kukushukuru tena kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu yake hadi kufikia Januari, 2017. Tunaamini kuwa fursa hii inayotokana na masharti ya Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, itasaidia kuliwezesha Bunge lako tukufu kutekeleza wajibu wake ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** naombanachukua fursa hii kumpongeza Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Ajira, Vijana na Walemavu, Mhe. Jenista Mhagama,Mb na aliyekuwa Naibu Waziri wake Dkt. Abdallah Possi, Mb. Aidha, nampongeza pia Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania, Dkt. Leonard Maboko na Kaimu Kamishna wa Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya, Ndg. Aida Tesha; na Watendaji wote wa Tume hizo kwa ushirikiano walioipa Kamati kwa kipindi cha mwaka mzima, kwa kufika mbele ya Kamati na kutoa ufafanuzi mara zote ulipohitajika.

**Mheshimiwa Spika,**kwa namna ya pekee napenda niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati kwa uchapakazi wao wakati wote wa kutekeleza majukumu ya Kamati kwa Mwaka mzima. Wajumbe wamefanya kazi kubwa katika kuhakikisha Kamati inaisimamia na kuishauri vyema Serikali kwa mujibu wa Katiba ya nchi na Kanuni za Kudumu za Bunge. Napenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kwa majina kama ifuatavyo:

1. Mhe. Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, Mb –Mwenyekiti
2. Mhe. Dkt. Jasmine Tiisekwa Bunga, Mb –M/Mwenyekiti
3. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Dkt. Hadji Hussein Mponda, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Daniel Edward Mtuka, Mb -Mjumbe
6. Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Joseph Kizito Mhagama, Mb -Mjumbe
8. Mhe. Juliana Daniel Shonza, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Kemirembe Julius Lwota, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Lucia Ursula Michael Mlowe, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Mary Deo Muro, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Martha Mosses Mlata - Mjumbe
13. Mhe. Masoud Abdallah Salim, Mb - Mjumbe
14. Mhe.Oscar Rwegasira Mukasa, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo,Mb - Mjumbe

16. Mhe. Yussuf Kaiza Makame, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Zainab Matitu Vullu, Mb - Mjumbe
18. Mhe.Omary Ahmad Badwel, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashillilah, kwa ushirikiano ambao amekuwa akitoa kwa Kamati. Pamoja na yeye, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge,Ndg. Athumani Hussein, Wakurugenzi Wasaidizi, Makatibu wa Kamati hii, Ndg. Asia Msangi, Ndg. Happiness Ndalu na Ndg. Susan Ngole pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndg. Grace Mwenye, kwa kuratibu vyema Shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika.

**Mheshimiwa Spika,** sasa naliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili taarifa hii na hatimaye kukubali Maoni na Ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

…………………………………
Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI**
**06 FEBRUARI, 2017**

**MWENYEKITI:** Haya. Ahsante sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI. Sasa namkaribisha Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kukushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya mwaka ya shughuli zilizotekelezwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii katika kipindi cha mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane kifungu cha 5 iliyo chini ya Kanuni ya 118 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii imepewa jukumu la kusimamia shughuli za Wizara zifuatazo:-

(a) Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto;

(b) Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; na

(c) Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ni moja kati ya Kamati tisa za Kudumu za Bunge za Kisekta ambayo kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane iliyo chini ya Kanuni ya 118 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, Kamati hii imepewa jukumu la:-

(a) Kushughulikia Bajeti ya Wizara inazozisimamia;

(b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia;

(c) Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila mwaka za Wizara hizo; na

(d)Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati; Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii imefanya utekelezaji wa majukumu yake katika mwaka 2016 kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Majukumu hayo ni kama yalivyoelezwa katika uchambuzi na utekelezaji wake katika taarifa ambayo mmepewa. Majukumu hayo ni pamoja na:-

(i) Mafunzo kwa Wajumbe wa Kamati; katika kuhakikisha Kamati inatekeleza majukumu yake ipasavyo na kwa kuzingatia kuwa Wabunge, Wajumbe wengi wa Kamati wa Bunge la Kumi na Moja walikuwa wapya ilikuwa ni muhimu kuanza utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa kupokea mafunzo katika kufahamu muundo na majukumu ya Wizara zinazosimamiwa na Kamati ambayo yaliandaliwa na Ofisi ya Bunge.

(ii) Kupokea taarifa za utendaji wa Wizara na Taasisi mbalimbali; Kamati ilipata fursa ya taarifa za utendaji wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara hizo katika mwaka 2015/2016. Kamati ilipokea taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto pamoja na Taarifa ya Mfuko wa Bima wa Afya *(National Health Insurance Fund);* Taarifa ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na Taasisi iliyo chini ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu pamoja na Taarifa ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kama ilivyoelezwa kwenye taarifa ambayo mmepewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukaguzi wa miradi ya maendeleo kwa mwaka 2015/2016; Kamati ilikagua miradi mbalimbali iliyo chini ya usimamizi wa Wizara inazozisimamia ambayo ilitengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2015/2016 na ambayo taarifa yake ilikuwa hapa katika taarifa zilizowasilishwa na Kamati wakati wa uwasilishaji wa taarifa za bajeti za mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, miradi ambayo Kamati ilipata fursa ya kuitembelea kwa lengo la kufanya ukaguzi ni pamoja na mradi wa kujenga nyumba maalum kwa ajili ya kusimika mashine mpya za kisasa za kutibu saratani katika Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road,* mradi wa upanuzi wa Taasisi ya Mifupa *(MOI)* Awamu ya Tatu ambapo ni ujenzi wa jengo la ghorofa saba kwa ajili ya kutolea huduma ya uchunguzi ikiwemo *CT-Scan, MRI, X-Ray, Ultra Sound,* vyumba vya upasuaji, maabara, hifadhi ya damu, huduma za dharura za *ICU,* vyumba vya wagonjwa wanaohitaji uangalizi wa karibu na vyumba vya wagonjwa wa kulipia na kuchangia na mradi wa upanuzi wa ofisi za Bohari ya Dawa, Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili *(MUHAS),* Mloganzila na Mradi wa kutoa Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu *(Higher Learning Students Loans Board)* na mradi wa Upanuzi wa Usikivu wa Mitambo ya Shirika la Utangazaji la Tanzania *(TBC)* kule Kisarawe.

Kamati iliamua kukagua miradi hiyo kutokana na kuwa katika Miradi ya Wizara ambayo ilitengewa fedha bilioni tatu hakuna hata mmoja uliotekelezwa kwa kuwa haikutolewa fedha yoyote kutoka Serikalini. Kwa ujumla miradi karibu yote ambayo Kamati iliikagua ilikuwa na changamoto ya ucheleweshwaji au kutotolewa kabisa kwa fedha zilizotengwa hali ambayo iliathiri utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kwamba imekuwa ni kawaida kwa Serikali kutotimiza utoaji wa fedha kwa wakati katika Wizara zilizopo chini ya Kamati hii kama vielelezo vifuatavyo vya taarifa vilivyooneshwa hali ya upatikanaji wa fedha kwa kipindi cha miaka ya 2011 mpaka 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupokea, kuchambua na kujadili taarifa za utekelezaji na mpango wa bajeti kwa kipindi cha nusu mwaka; katika vikao vya Kamati vilivyofanyika kuanzia tarehe 16 hadi 18 Januari, 2017 mkoani Dodoma, pamoja na majukumu mengine, Kamati ilipokea na kuchambua na kujadili taarifa za utekelezaji na mpango wa bajeti wa Wizara kwa ajili ya kusimamia kwa kipindi cha nusu mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipokea, kuchambua na kujadili taarifa ya utekelezaji na mpango wa bajeti ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto kwa kipindi cha nusu mwaka ambayo ilionesha kuwa ukusanyaji wa maduhuli ni wa kuridhisha kwani mpaka kufikia Desemba, 2016 Wizara ilikuwa imekusanya kiasi cha shilingi bilioni 87.6 sawa na asilimia 55.6 ya kiasi cha shilingi bilioni 157 kilichopangwa kukusanywa kwa mwaka 2016/2017. Kamati inapongeza ukusanyaji huu wa maduhuli.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Ramadhan Sima, Mbunge wa Singida Mjini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata za Kisaki, Mtama pamoja na Mtipa pamoja na Mwankoko zimejumuishwa katika mradi kabambe wa *REA III* unaoanza mwezi Machi, 2017. Katika kazi hizi, maeneo haya yatapelekewa mradi kupitia *desification, grid extension* pamoja na *renewable* utakaoanza mwezi huo nilioutaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kupeleka umeme kwenye vijiji hivyo inajumuisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilometa 105, ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilometa 126.9, ufungaji wa transfoma 31, pamoja na kuwaunganishia wateja wa awali 1,111. Kazi hii itagharimu shilingi bilioni 8.15.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa muda mrefu wa Serikali ni kutumia vyanzo mbalimbali vya kuzalisha umeme ikijumuisha upepo uliopo katika eneo la Singida ambapo katika mpango kabambe wa kuendeleza sekta ya umeme wa mwaka 2016, mradi huu umepangwa kuanza kuzalisha megawati 50 za awamu ya kwanza mwaka 2018. Mradi huu unakadiriwa kugharimu dola za Marekani 136 na utatekelezwa katika maeneo ya Kisasida, Ipungi, Mughamo na Unyankhyanya. Kampuni ya *Geo Wind* pamoja na *Acciona* wameingia *exclusive agreement* kwa ajili ya kipindi cha miezi minne

ambayo itaishia mwezi Februari mwaka huu kwa ajili ya kujiridhisha kwa wananchi kama watakubaliana na utekelezaji wa mradi huu ili waweze kupata umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni mbalimbali binafsi zimeonesha nia ya kuzalisha umeme kwa kutumia upepo katika Mkoa wa Singida ikiwa ni pamoja na Kampuni ya *Wind East-Africa* iliyojitokeza kuzalisha umeme wa megawati 50 kwa awamu ya kwanza na baadae kufikisha megawati 100. Mradi huu utatekelezwa katika eneo la Kititimo. Gharama ya mradi huu ni dola za Marekani milioni 264.77.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima, swali la nyongeza.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Singida Mjini imejaaliwa kuwa na rasilimali ya vyanzo vya umeme kwa maana ya upepo na jua na yako makampuni tayari yamekwishajitokeza kwa ajili ya kuzalisha umeme huo. Sasa na sisi wananchi wa Jimbo la Singida Mjini tumejitokeza kwa maana ya kutoa maeneo yetu kwa ajili ya uzalishaji. Serikali sasa ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba umeme huo unazalishwa ili Singida Mjini iweze kupata viwanda vya kutosha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Singida Mjini kunapita umeme wa kilovoti 40 kuelekea Shinyanga na Namanga na wananchi tayari wametoa maeneo yao kwa ajili ya kupisha mradi huo na wako ambao wameshalipwa fidia na wengine hawajalipwa fidia. Serikali inatoa tamko gani sasa kuhakikisha kwamba wananchi wote wanalipwa fidia kwa ajili ya kupisha umeme huo? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa, Serikali ina mpango mahususi wa kuendeleza wawekezaji binafsi katika umeme mbadala hasa katika maeneo ya Singida ambako kuna umeme wa upepo. Hata hivyo, mkakati wa Serikali wa kwanza, Serikali imetenga kupitia mradi wake wa *REA* shilingi milioni 42 kwa ajili ya kuendeleza wawekezaji binafsi watakaofanya katika uzalishaji wa umeme pamoja na mambo ya miradi ya

maji. Kwa hiyo, wananchi wa Singida watapata pesa hizi kupitia mradi wa *REA* ambapo watawezeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mkakati mwingine badala ya kupitia mradi wake umeshafadhili sasa, nikizungumzia kwa nchi nzima miradi ya Lukonda kule Njombe pamoja na Ndoya kule Mbinga kama wajasiriamali wa Kitanzania ambao wanawezeshwa kupitia miradi ya Serikali, miradi ya *REA*. Kwa hiyo, miradi ya Serikali kupitia miradi ya *REA* kutoa mahususi kwa ajili ya kuendekeza wawekezaji. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Sima na kama kuna wawekezaji wengine kule Singida Mheshimiwa Sima basi walete wataalam wetu watashirikiana na watu wa *REA* ili waweze kushirikiana zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili kuhusiana na mkakati wa Serikali kulipa fidia kwenye Mradi wa *backbone* wa kilovoti 400. Kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Sima alivyoshirikiana na Serikali mpaka wananchi takriban 200 wakalipwa fidia awamu ya kwanza. Awamu ya pili nimhakikishie Mheshimiwa Sima, hivi sasa vijiji vyake 13 ambavyo vinaingia kwenye mradi ule vitalipwa fidia jumla ya shilingi milioni 722.7, malipo yataanza mwezi Februari mwaka huu na yatakamilika mwezi Machi na nimhakikishie kwamba vijiji vyake vya Misuna ambavyo vilipitiwa na umeme pamoja na Mtipa pamoja na Kisaki pia vitalipwa fidia kwa utaratibu huo.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Tunaanza na Mheshimiwa Mwamoto na tunamalizia na Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na pamoja na kazi nzuri ambayo Wizara hii inafanya, naomba niulize swali dogo tu la nyongeza. Niliwahi kuuliza hili swali kwamba kwa kuwa Wilaya ya Kilolo ndiyo wilaya pekee ambayo maji mengi yanayojaza Kihansi yanatoka kule ambayo ndiyo yanasaidia kupelekea kuleta umeme nchi hii. Je, Kilolo inanufaikaje sasa? Naomba kwa nafasi hii atueleze hapa wananchi wa Kilolo watanufaika vipi ili kuhakikisha wanapata umeme.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa eneo la Kilolo linatupatia maporomoko ya maji ambayo yanatusaidia sana kuingiza kwenye Gridi ya Taifa. Lakini wananchi wa Kilolo pamoja na hasa wananchi wa Kihesa Mgagao watanufaika sana na umeme huu na nitaje tu Mheshimiwa Mwamoto, hivi sasa katika Mkoa wa Iringa, *REA* Awamu ya Tatu

imeshaingia na eneo mojawapo ambalo linapelekewa umeme ni pamoja na Kihesa Mgagao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba wananchi wa Kilolo wataendelea kunufaika na miradi ya umeme.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Jimbo la Tarime Mjini lina kata nane na kati ya kata nane, kata nne ziko pembezoni na hazina umeme kabisa na kata mbili zina umeme kwa asilimia chache. Ningependa kujua *commitment* ya Serikali ya kuhakikisha kwamba wananchi wa Jimbo la Tarime Mjini wanapata umeme kwa asilimia zaidi ya 90.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Esther, tumeshirikiana naye sana kwenye mradi wa *REA* Awamu ya Pili na ni kweli kuna kata nne na kata nyingine mbili ambazo hazijaguswa kabisa. Hata hivyo, nimhakikishie Mheshimiwa Esther kwamba Jimbo lako pamoja na Mkoa wa Mara tumeshaanza kutekeleza Mradi wa *REA* Awamu ya Tatu wa *desification.* Hapa ninapozungumza wiki ijayo mkandarasi ata-*report* kwake ili amwelekeze maeneo mahususi. Kwa hiyo, kata zake nne na zile tatu ambazo anazungumza Mheshimiwa Mbunge zitapatiwa umeme kupitia mradi wa *REA* Awamu ya Tatu unaoanza mwezi wa Tatu na kuendelea.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Namwomba Mheshimiwa Martha Mlata sasa aulize swali la nyongeza kwa ufupi kabisa.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri akijibu swali mojawapo hapa Bungeni kuhusu mradi wa umeme wa upepo Singida alisema kwamba Serikali inakamilisha mkataba na taratibu za kusaini kati ya Kampuni ya *Wind East-Africa* na kwamba mwezi Februari mradi huo utaanza. Naomba atusaidie, je, maneno yale ni kweli au bado? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichowaeleza ni kweli kwanza, lakini cha pili nifafanue tu kwamba mradi wa *REA* unaokwenda kuendelea umeshaanza na mpaka tarehe 31 mwezi Machi,

wakandarasi watakuwa wameshaingia mikoa yote kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa *REA* unaoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa upande wa umeme wa upepo kule Singida nimesema mradi wa *Wind East-Africa* pamoja na *Geo Wind* wanakamilisha taratibu za kimikataba na kufikia mwezi Juni ndiyo wataanza rasmi. Kwa wanaoanza Februari na mwezi Machi ni miradi ya *REA* na ile miradi ya upepo itaanza kuanzia mwezi Juni na kuendelea.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunamalizia swali la mwisho, namuomba Mheshimiwa Abdul-Aziz Abood, Mbunge wa Morogoro Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 68

**Kupeleka Umeme Morogoro Mjini**

**MHE. ABDUL-AZIZ M. ABOOD** aliuliza:-

Maeneo mengi katika Jimbo la Morogoro Mjini bado hawajapata nishati ya umeme kama vile Kata za Mindu, Lugala, Mkundi, Kiegea A na B, Kihonda, Mafisa, Tungi, Kingolwira na Kauzeni A.

Je, ni lini Serikali itamaliza tatizo hili la muda mrefu?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdul-Aziz Abood, Mbunge wa Morogoro Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Shirika la Umeme *(TANESCO)* inatekeleza miradi ya kufikisha miundombinu ya umeme maeneo mbalimbali nchini ikiwa ni pamoja na Morogoro Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi unaoendelea katika Kata za Mindu, ujenzi wa njia ya umeme msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilometa 8.973, ujenzi wa njia ya umeme msongo wa kilovoti nne yenye urefu wa kilometa 35.4, lakini ufungaji wa transfoma saba pamoja na kuwaunganishia umeme wateja 834.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu utafikisha umeme kwenye maeneo ya Mindu, Kasanga na Madanganya ambapo ni transfoma nne zimefungwa tayari na baadhi ya wananchi pia wameshaunganishiwa umeme. Gharama za mradi ni shilingi bilioni 1.113. Unajumuisha Mindu -Lugala ambao unajumuisha ujenzi wa msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilometa 8.9, ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa voti 400 yenye urefu wa kilometa 10.7 na ufungaji wa transfoma tatu. Hali kadhalika utaunganishwa umeme kwa wateja 206. Gharama za mradi huu ni milioni 106.784. Utekelezaji wa miradi hii utakamilika mwezi Juni mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yaliyobaki katika Mji wa Morogoro yataendelea kupatiwa umeme kupitia bajeti ya *TANESCO* zinazopangwa mwaka hadi mwaka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdul-Aziz Abood, swali la nyongeza.

**MHE. ABDUL-AZIZ M. ABOOD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; Morogoro inaelekea kuwa Jiji, je, Serikali ina mikakati gani ya kumaliza maeneo yote ya Mji wa Morogoro kuwa na umeme?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kuna maeneo ambayo umeme umeshafika, wananchi wameshalipia kuunganishiwa umeme, lakini majibu wanayopewa ni kuwa nguzo hakuna. Je, Serikali itaondoa lini kero hiyo ya nguzo katika Mji wa Morogoro ili wananchi waweze kupata umeme, maeneo waliyokwishapata umeme?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa Serikali kupeleka umeme ni kama ambavyo nimeeleza, ipo miradi ya *REA*, lakini pamoja na *REA* bado *TANESCO* wana bajeti zake za kupeleka umeme. Katika Mkoa wa Morogoro, hasa Morogoro Mjini, mkakati uliopo wa kwanza kabisa, Serikali imetenga shilingi milioni 106 kwa mwaka huu ambayo itapeleka umeme kwenye vijiji vya Mheshimiwa Abood ikiwemo Kihonda, Mafisa pamoja na maeneo mengine kama kule Kanisani ambako ameeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine ambayo Mheshimiwa Mbunge hajayataja pamoja na eneo lake lile ambalo amesema eneo la Bomba la Zambia. Kile Kijiji cha Bomba la Zambia ambacho kipo mbali sana kitapelekewa umeme mwaka huu. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Abood

kwamba Serikali ina mkakati madhubuti wa kupeleka umeme kwenye vijiji vyake vyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili kuhusiana na nguzo, ni kweli kabisa yako maeneo Morogoro Mjini wananchi wamelipia, lakini hawajawahi kuunganishiwa umeme. Utaratibu unafanyika sasa na nimhakikishie Mheshimiwa Abood hivi sasa tunapoongea hapa wananchi wake wa Lokole Juu pamoja na Lukobe Kanisani wanaunganishiwa umeme kwa sababu wameshalipia na nguzo zimeshakuja na vijiji vinne ambavyo amevitaja pamoja na Kauzeni na maeneo mengine wataendelea kuunganishiwa umeme mara baada ya nguzo kuingia mwezi ujao.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo.

**MWENYEKITI:** Naomba tutulizane.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo.

**MWENYEKITI:** Muda wetu wa maswali umefikia mwisho kwa siku ya leo. Kabla sijaanza na matangazo ya wageni, naomba kuwajulisha Waheshimiwa Wabunge kwamba tumepokea barua kutoka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba anasafiri kwenda Dar es Salaam kwa shughuli za kikazi kuanzia Jumapili tarehe 5 Februari, 2017. Wakati hayupo ambaye atakaimu nafasi hiyo ya Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni hadi atakaporejea atakuwa ni Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni ambao tunao Bungeni asubuhi hii ya leo wako katika makundi mawili:-

Kuna wageni waliopo Jukwaa la Spika ambaye ni Mheshimiwa Samwel Akon, Mbunge na Mwenyekiti wa Kamati ya Masuala ya Uhusiano ya Kibunge ya Bunge la Wawakilishi wa Nigeria ambaye pia alikuwa Spika wa Bunge la Jimbo la Akwan-Ivon, karibu sana Mheshimiwa Samwel Akon. *(Makofi)*

Mwingine ni mgeni ambae ni Mheshimiwa Larry Odey ambaye ni Mshauri wa Masuala ya Kibunge, pia alikuwa Spika la Jimbo la *Cross-River,* Nigeria, karibu sana Mheshimiwa Larry Odey. Wageni hawa wapo Bungeni kwa ziara ya kikazi na watakutana na Spika wa Bunge, Mheshimiwa Job Ndugai hapo baadaye, karibuni sana wageni wetu.

Wageni wengine ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge; tunao wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge pamoja na wageni waliokuja kutembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo Bungeni, tunawakaribisheni sana, karibuni katika Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Sasa yafuatayo ni matangazo; tangazo la kwanza linatoka kwa Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni, Mwenyekiti wa Kamati ya Utendaji *(CPA)* Tawi la Tanzania, anawatangazia kwamba kutakuwa na kikao cha Kamati leo tarehe 6 Februari, 2017 saa 8.00 mchana katika ukumbi namba 227, ghorofa ya pili, Jengo la Utawala, Ofisi za Bunge – Dodoma. Wajumbe wa Kamati wanaopaswa kuhudhuria kikao hicho ni hawa wafuatao; Mheshimiwa Tundu Antiphas Lissu ambaye ni Makamu Mwenyekiti na wajumbe ni Mheshimiwa Amina S. Mollel, Mheshimiwa Salum M. Rehani, Mheshimiwa Japhet N. Hasunga, Mheshimiwa Dkt. Immaculate S. Semesi, Mheshimiwa Khamis Mtumwa Ali, Mheshimiwa Zaynabu Matitu Vulu, Mheshimiwa Josephat Kandege, Mheshimiwa Juma Hamad Omar, Mheshimiwa Jitu Soni na Mheshimiwa Maria N. Kangoye. *(Makofi)*

Tangazo la mwisho linatoka kwa Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii anawaomba Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuwa leo tarehe 6 Februari, 2017 saa 7.00 mchana kutakuwa na kikao cha Kamati katika ukumbi wa 229, Jengo la Utawala.

Katibu!

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo ! Mwongozo!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwalimu.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. DOTO M. BITEKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7). Nikiwa hapa Bungeni na mapema leo nimeendelea kupata taarifa juu ya jambo ambalo limejitokeza na ambalo naomba niliombee mwongozo wako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimboni kwetu na Wilayani kwetu Bukombe, mwananchi anayeitwa Sizya Emmanuel mwenye umri wa miaka 30 ambaye anajishughulisha na kazi ya kufuga nyuki na ambaye amepewa kibali cha

kufanya shughuli zake kwenye Hifadhi ya Kigosi alikwenda kufanya shughuli zake pamoja na wenzake wanne. Wakiwa huko, Ndugu Sizya Emmanuel akapigwa risasi na maaskari wa wanyamapori. Risasi hiyo amepigwa kisogoni ikatokea kwenye jicho lake la kulia na hivi ninavyoongea na wewe, Ndugu Sizya amepelekwa kwenye Hospitali ya Rufaa ya Bugando, hali yake ni mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kuomba Mwongozo wako kwa sababu mambo haya ya uonevu na unyanyasaji wa wananchi kwenye Wilaya ya Bukombe na hili sio tukio la kwanza, yamekuwa yakijirudia mara kwa mara. Wananchi wa Bukombe hawana amani, hawana furaha, wana wasiwasi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwalimu.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7) na 46 zikisomwa kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo ninaouomba ni jambo lililotokea katika kujibu swali wiki iliyopita lililokuwa linaeleza juu ya madai ya walimu nchini. Wakati Naibu Waziri akijibu swali, alieleza walimu nchini wanadai madai yapatayo shilingi bilioni 26 na kwa takwimu zilizopo ambazo Chama cha Walimu kimezifikisha Serikalini, walimu wa nchi hii wanadai shilingi trilioni 1.06.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mwongozo ninaotaka unipe ni kwa nini deni kubwa la walimu halitajwi kikamilifu humu Bungeni na hivyo Serikali inataja kiasi kidogo sana kinachodaiwa na walimu? Sasa shida ni nini? Tupate Mwongozo, tunaficha hili deni kwa maslahi ya nani? Kwa nini Serikali inadanganya Bunge na madeni haya Chama cha Walimu kimejadiliana na Serikali tarehe 10 mwezi wa Kwanza, kwa hiyo Serikali inafahamu ina deni la shilingi trilioni 1.06. Naomba Mwongozo wako ni kwa nini Serikali haisemi ukweli katika madai ya Walimu wa nchi hii.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa miongozo yenu, Mheshimiwa Doto, naanza na Mwongozo ulioomba. Kwanza niwape pole wananchi wako wa huko Bukombe kwani hili jambo ni la hatari na Mwongozo wangu ni kwamba, naiagiza Serikali ifanye haraka iwezekanavyo ili kufuatilia suala hili tujue nini kinaendelea. Mheshimiwa Waziri wa Nchi una neno lolote kuhusiana na hili?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE WALEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa na mimi niungane na kauli yako, lakini niungane na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo kuwapa pole ama kumpa pole majeruhi ambaye amepatwa na tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kiti chako kinatoa miongozo na kuiagiza Serikali, naomba kwa niaba ya Serikali nipokee maagizo yako. Hata hivyo, naomba kulihakikishia Bunge hili toka asubuhi tulipopata taarifa, tumeshaiagiza Serikali ianze kufanya kazi ya kulijua jambo hili kwa upana wake, lakini kushughulikia kwa kina matatizo yote yanayohusiana na askari wa wanyamapori katika kulinda mapori yetu ili kupata ufumbuzi wa kudumu wa pamoja.

**MWENYEKITI:** Nashukuru. Kwa hiyo, naamini kwamba agizo hilo litafanyiwa kazi kwa haraka iwezekanavyo. Suala la pili la Mheshimiwa Mwalimu, suala hili la walimu kuhusu deni nalichukua kwa mujibu wa Kanuni ya 68(10) na tutalitolea Mwongozo baadaye.

Katibu, tuendelee.

**NDG. CHARLES MLOKA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA KAMATI**

**Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI**
**na**
**Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa**
**Kipindi cha Januari, 2016 hadi Januari, 2017**

**MWENYEKITI:** Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI aje kuwasilisha taarifa yake tafadhali.

**MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA MASUALA YA UKIMWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, napenda kuwasilisha kwako Taarifa ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kwa kipindi cha Januari, 2016 hadi Januari, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Shughuli zilizotekelezwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kwa kipindi cha Januari, 2016 hadi Januari, 2017.

Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu nne; sehemu ya kwanza inaelezea maelezo ya jumla; sehemu ya pili inaelezea utekelezaji wa majukumu ya Kamati; sehemu ya tatu imebainisha maoni na ushauri wa Kamati; na sehemu ya nne ni hitimisho la taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane ya Kanuni chini ya Kanuni ya 118(10) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Masuala ya UKIMWI imepewa majukumu yafuatayo:-

(a) Kuratibu masuala yanayohusu UKIMWI katika sekta zote.

(b) Kufuatilia utekelezaji wa sera na mipango ya Serikali kuhusu UKIMWI na udhibiti wa dawa za kulevya.

(c) Kujadili na kutoa mapendekezo na ushauri kuhusu hatua za kudhibiti dawa za kulevya; na

(d) Kushughulikia Bajeti za Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Madawa ya Kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi cha mwaka mmoja yaani Januari, 2016 hadi Januari, 2017, Kamati ilitekeleza majukumu yafuatayo:-

(a) Semina za mafunzo;

(b) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya taasisi zinazosimamiwa na Kamati;

(c) Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo; na

(d) Uchambuzi wa Taarifa na Utekelezaji wa Bajeti za Taasisi zinazosimamiwa na Kamati na pia sehemu ya pili inahusu uchambuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI ulizingatia masharti ya Kanuni za Kudumu za

Bunge, Toleo la Januari, 2016 hususan Kanuni ya 117 inayohusu utaratibu katika Kamati za Kudumu za Bunge. Hivyo, Kamati iliandaa Mpango Kazi uliotekelezwa katika kipindi cha Januari, 2016 hadi Januari, 2017, ambao matokeo ya utekelezaji wake yamefanyiwa uchambuzi katika sehemu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati, semina na mafunzo, katika hili Wajumbe wa Kamati walipata mafunzo ya kuwajengea uwezo katika maeneo yafuatayo:-

(i) Muundo wa majukumu ya Kamati;

(ii) Kanuni na taratibu za uendeshaji wa shughuli za Kamati;

(iii) Muundo na majukumu ya tume zinazosimamiwa na Kamati hii yaani Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya; na

(iv) Sheria na sera mbalimbali zinazohusu udhibiti wa UKIMWI na dawa za kulevya nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya taasisi zinazosimamiwa na Kamati; Kamati ya Masuala ya UKIMWI inasimamia taasisi mbili ambazo ni Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *TACAIDS* na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania, Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

(i) Ufinyu wa bajeti na ucheleweshaji wa fedha kutoka Serikalini;

(ii) Dosari katika Sera ya UKIMWI ya 2001; na

(iii) Kutokamilika kwa wakati mchakato wa muundo mpya wa Tume na hivyo….

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeangalia pia Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya. Katika kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Tume hii Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

(i) Ufinyu wa bajeti na uchelewaji wa fedha kutoka Serikalini;

(ii) Dosari katika Sera ya Dawa za Kulevya ya 2004; na

(iii) Kutokukamilika kwa muundo wa Tume hii ambayo kwa sasa imekuwa mamlaka kamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hii pia imepewa jukumu la kuratibu masuala yote yanayohusu UKIMWI katika sekta zote ikiwemo kufuatilia utekelezaji wa sera na mipango ya Serikali kuhusu UKIMWI na udhibiti wa dawa za kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilikutana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na kujadili mwongozo wa namna ya kuwahudumia watumishi wa umma wanaoishi na Virusi vya UKIMWI *(workplace intervention medical treatment and training to staff)* ambapo Kamati ilishauri mambo yafuatayo:-

(a) Waajiri kuhamasisha na kuwajengea watumishi ujasiri wa kupima VVU, kutoa elimu ya kujikinga dhidi ya maambukizi ya UKIMWI na kutekeleza afua za UKIMWI mahali pa kazi.

(b) Serikali kuwachukulia hatua waajiri wanaotumia fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya WAVIU kwa shughuli nyingine zisizohusiana na UKIMWI.

(c) Serikali kuongeza ajira katika viwanda vidogo vidogo na katika sekta binafsi ili kukuza uchumi na kuwawezesha vijana kupata ajira ili kuwaepusha kujihusisha na matumizi ya dawa za kulevya na tabia hatarishi zinazochochea kuongezeka kwa maambukizi ya VVU na UKIMWI.

(d) Serikali kuendelea kuwasisitiza vijana, waajiri katika utumishi wa umma kutumia fursa zinazowazunguka ili kudhibiti tatizo la unyanyapaa ambao huchangia kurudisha nyuma juhudi za Serikali katika mapambano dhidi ya maambukizi ya UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilikutana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ili kujadili hatua iliyofikiwa katika Utafiti wa Upatikanaji wa Chanjo ya UKIMWI Tanzania ambapo Kamati ilibaini kuwa wataalam wa utafiti wa tiba bado wapo kwenye hatua za awali za utafiti wa chanjo, hivyo kutokana na changamoto ya rasilimali fedha, rasilimali watu na teknolojia ya juu inayohitajika katika utafiti wa chanjo. Hivyo, kuifanya Tanzania

kama zilivyo nchi nyingi za Afrika kutegemea kwa kiasi kikubwa tafiti zinazofanywa na nchi zilizoendelea kama Marekani. Kwa sababu hiyo, Kamati ilishauri mambo yafuatayo:-

(a) Serikali kuona umuhimu wa kuwekeza katika utafiti wa chanjo ya UKIMWI; kwa kuongeza bajeti ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

(b) Wizara kujielekeza zaidi katika kutoa elimu kwa wananchi juu ya kujikinga na maambukizi ya VVU na UKIMWI, pamoja na magonjwa sugu yasiyoambukizwa kwa maana Kinga ni bora kuliko Tiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilikutana na Bohari Kuu ya Madawa nchini pamoja na Baraza la Watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI ili kujadili mafanikio na changamoto zilizopo katika upatikanaji, usambazaji na utumiaji wa dawa za kufubaza makali ya VVU *(ARVs)* nchini ambapo, Kamati ilibaini uwepo kwa changamoto katika upatikanaji wa dawa hizo katika vituo vingi vya afya nchini inayosababishwa na malimbikizo ya madeni ya Bohari Kuu ya Madawa katika Mamlaka ya Bandari, hali iliyopelekea watumiaji wa dawa hizo kulazimika kununua dawa katika maduka ya dawa ya watu binafsi kwa bei za juu huku wengine wakishindwa kumudu gharama hizo na kujikuta wakidhoofika. Hivyo, Kamati ilishauri mambo yafuatayo:-

(a) Serikali kufanya jitihada za haraka za ulipaji wa deni kwa Bohari Kuu ya Dawa *(MSD)* ili kuwasaidia WAVIU kupata dawa za kufubaza makali ya VVU kwa wakati pia kutowakatisha tamaa wafadhili wanaotuletea dawa hizo;

(b) Serikali kuwekeza katika uzalishaji wa ndani wa dawa hizi ili kuondokana na utegemezi wa wafadhili katika ununuzi wa dawa kama jirani zetu wa Uganda wanavyofanya; na

(c) Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa itoe waraka utakaohusu halmashauri zote kushirikiana na Mabaraza ya WAVIU katika kubuni njia za kuwakwamua kiuchumi WAVIU na kusaidia katika mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilikutana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ili kujadili mafanikio, changamoto na matarajio ya Wizara hii katika udhibiti wa matumizi ya dawa za kulevya nchini ambapo Kamati ilibaini changamoto nyingi zilizotokana na ufinyu wa bajeti ya Wizara, hivyo kupelekea

zoezi la udhibiti wa dawa za kulevya nchini kutokuwa na matokeo ya kuridhisha. Hii imetokana na bajeti ya Wizara hii kupungua kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na kufikia shilingi bilioni 30 kwa miradi ya maendeleo ikilinganishwa na kiasi cha sh. 65,757,261,000 zilizotengwa kwa mwaka wa fedha uliopita 2015/2016. Hivyo, Kamati ilishauri yafuatayo:-

(a) Jeshi la Polisi kuongezewa Bajeti ili kuwawezesha kununua vitendea kazi kama boti za doria ili kukabiliana na changamoto wanazopata katika kudhibiti uingizwaji wa dawa za kulevya nchini; na

(b) Jeshi la Polisi kuimarisha ulinzi hususan katika maeneo ya bandari, viwanja vya ndege na mipaka ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilikagua Mradi wa Ujenzi wa Ghala la Kuhifadhia Vielelezo vya Kesi za Dawa za Kulevya wenye thamani ya sh. 272,500,000 unaosimamiwa na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya uliopo Makao Makuu ya Jeshi la Polisi Kurasini, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika kipindi hiki pia Kamati ilifanya ziara katika taasisi mbalimbali ili kufuatilia utekelezaji wa sera za UKIMWI na dawa za kulevya, taasisi hizo ni pamoja na:-

(i) Hospitali ya Taifa Muhimbili na Hospitali ya Rufaa ya Mwananyamala katika vituo vya kutolea huduma ya dawa ya *methadone* kwa warahibu wa dawa za kulevya;

(ii) *Missana Foundation Sober House* iliyopo Kigamboni-Dar es Salaam;

(iii) Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali;

(iv)Bohari Kuu ya Madawa *(MSD);*

(v) Mgodi wa Buzwagi uliopo Kahama - Shinyanga; na

(vi) Kliniki ya WAVIU katika Kituo cha Afya cha Kambarage - Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Aprili, 2016, Kamati ilikutana na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya kwa mwaka wa fedha 2015/2016, kisha Kamati ilipitia na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya Fungu la 91 na

Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* Fungu la 92 kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kama ilivyoainishwa katika Nyongeza ya Nane ya Kanuni ya 118 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya, Kamati ilizingatia maelezo na fafanuzi mbalimbali zilizotolewa na Tume hizo kuhusiana na Makadirio ya Mapato na Matumizi yao ambapo Kamati ilipitisha sh. 2,340,236,000 kwa Matumizi ya Kawaida kwa Fungu 91. Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya na hakuna kiasi kilichotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Aidha, kiasi cha sh. 4,961,677,000 kilitengwa kwa matumizi ya kawaida na sh. 5,235,823,413 kwa miradi ya maendeleo kwa Fungu 92 - Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kwa mwaka wa 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu inahusu maoni na ushauri wa Kamati. Kutokana na shughuli za Kamati zilizofanyika katika kipindi cha mwaka mmoja yaani Januari, 2016 hadi Januari, 2017, kumekuwa na changamoto mbalimbali zilizojitokeza katika taasisi zinazosimamiwa na Kamati hii ambazo Kamati inazitolea maoni na ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza vyema majukumu ya Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya, Kamati inashauri mambo nane yafuatayo:-

Moja, KWA KUWA, Kamati imebaini dosari nyingi katika Sera ya Dawa za Kulevya ya mwaka 2004 ambayo imepitwa na wakati;

NA KWA KUWA, dosari hizo zimechangia ugumu katika utatuzi wa changamoto za sasa kuhusu udhibiti wa uingizwaji na matumizi ya dawa za kulevya, hali inayopelekea Taifa kuendelea kupoteza nguvu kazi;

KWA HIYO BASI, Kamati inashauri kuwa Serikali iharakishe mapitio ya sera hii ili kulinusuru Taifa na janga hili la dawa za kulevya.

Mbili, KWA KUWA, Kamati imebaini kuwa tangu Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya ibadilishwe kisheria kuwa Mamlaka ya Kupambana na Dawa za Kulevya, muundo wake bado haujakamilika;

NA KWA KUWA, kutokukamilika kwa muundo huo kunasababisha Tume kushindwa kuajiri watumishi wa kutosha, watumishi 37 kati ya 65 wanaohitajika;

KWA HIYO BASI, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha na kukamilisha mchakato wa muundo wa mamlaka hii ili uanze kutumika mara moja na kuongeza ufanisi katika kudhibiti uingizwaji na matumizi ya dawa za kulevya.

Tatu, KWA KUWA, imebainika kwamba ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa Tume umekuwa inakwamisha utendaji wa baadhi ya majukumu ya Tume hii kama vile:-

(a) Kudhibiti uingizwaji wa dawa za kulevya katika mipaka yote ya nchi ambayo ni mingi na ina vipenyo vingi vinavyofanya zoezi la udhibiti kuwa mgumu;

(b) Kushindwa kuteketeza mashamba ya bangi ambayo hulimwa sehemu zisizofikika kwa urahisi ambapo utekelezaji wa zoezi hilo uhitaji fedha nyingi; na

(c) Tume kushindwa kutoa elimu kwa wananchi kuhusu madhara yatokanayo na matumizi ya dawa za kulevya ili kunusuru afya za Watanzania na nguvu kazi ya Taifa;

NA KWA KUWA, kutotekelezwa kwa majukumu ya msingi ya Tume hiyo kutokana na ufinyu wa bajeti kunaathiri juhudi za udhibiti wa dawa za kulevya nchini jambo ambalo lina madhara makubwa kwa Taifa;

KWA HIYO BASI, Kamati inaishauri Serikali kuangalia uzito wa majukumu yanayotekelezwa na Tume hii katika kupambana na biashara haramu ya dawa za kulevya nchini, kwa kuongeza bajeti yao ili kuiongezea ufanisi Tume na kuhakikisha kuwa mafanikio yaliyofikiwa katika udhibiti wa dawa za kulevya hayapotei.

Nne, KWA KUWA, Kamati imebaini kukosekana kwa chombo cha kisheria cha kushughulikia udhibiti wa biashara na matumizi ya dawa za kulevya katika ngazi ya Halmashauri;

NA KWA KUWA, kukosekana kwa chombo hicho kunachangia udhibiti duni wa dawa za kulevya katika Halmashauri nchini;

KWA HIYO BASI, Kamati inaishauri Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kufanya maboresho ya Kamati za UKIMWI za Halmashauri ili kisheria ziwe na uwezo wa kusimamia shughuli za udhibiti wa dawa za kulevya katika ngazi ya Halmashauri kama ilivyo kwa Kamati ya

Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, kwa lengo la kusimamia kwa pamoja mambo haya yanayoendana.

Tano, KWA KUWA, Serikali imebaini changamoto katika upatikanaji wa tiba za utengemao *(rehabilitation)* na warahibu *(addicts)* wa dawa za kulevya nchini ambapo kwa sasa zinapatikana katika Mkoa wa Dar es Salaam na Zanzibar pekee;

NA KWA KUWA, changamoto hiyo inakwamisha juhudi za kuwawezesha warahibu kuacha matumizi ya dawa za kulevya, jambo linalochangia madhara ya kijamii nchini;

KWA HIYO BASI, Kamati inashauri kwamba huduma hii ihuishwe katika sera ya afya kama ilivyofanyika kwa suala la UKIMWI ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma hii kwa nchi nzima.

Sita, KWA KUWA, Kamati imebaini uwepo wa mwamko mdogo na ushiriki duni wa jamii katika mapambano dhidi ya biashara haramu ya dawa za kulevya;

NA KWA KUWA, hali hiyo kwa kiasi kikubwa imesababisha ongezeko la watumiaji wa dawa za kulevya, wagonjwa wa akili na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI;

KWA HIYO BASI, Kamati inashauri:-

(a) Tume ishirikiane na vyombo vya dola katika kuandaa kampeni endelevu ambazo mbali na kuwajengea uelewa Watanzania kuhusu umuhimu wa kushiriki katika mapambano haya, pia utawapa motisha ya kushiriki katika mapambano dhidi ya biashara ya dawa za kulevya; na

(b) Viongozi wakuu wa nchi kutoa kauli thabiti na kusimamia utekelezaji wa kauli hizo katika kukemea na kukomesha biashara na matumizi ya dawa za kulevya ili kuhamasisha ushiriki wa jamii nzima katika janga hili.

Saba, KWA KUWA, Kamati imebaini uwepo wa changamoto mbalimbali zinazowakabili warahibu *(addicts)* wa dawa za kulevya punde wanapoacha matumizi ya dawa hizo, kama kutengwa na jamii na kukosa ajira;

NA KWA KUWA, changamoto hizo husababisha warahibu kurudia matumizi ya dawa za kulevya au kujiingiza katika vitendo vya uhalifu;

KWA HIYO BASI, Kamati inashauri kuwa, Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu ianzishe programu maalum za kuwasaidia warahibu wa dawa za kulevya kuweza kujiinua na kujitegemeza kiuchumi mara tu baada ya kuachana na matumizi ya dawa za kulevya.

Nane, KWA KUWA, Kamati imebaini uwepo wa uhusiano mkubwa kati ya matumizi ya pombe za bei rahisi maarufu kama viroba na kuongezeka kwa tabia hatarishi zinazochangia ongezeko la vijana katika matumizi ya dawa za kulevya;

NA KWA KUWA, hali hiyo inaathiri ufanisi wa nguvu kazi ya Taifa kutokana na madhara ya matumizi ya dawa za kulevya;

KWA HIYO BASI, Kamati inaishauri Serikali kufungia kabisa uzalishaji na uuzwaji wa pombe za bei rahisi maarufu kama viroba ili kulinusuru Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa, Kamati inashauri mambo saba yafuatayo:-

Kwanza, KWA KUWA, Kamati imebaini dosari nyingi katika Sera ya UKIMWI ya mwaka 2001;

NA KWA KUWA, dosari hizo zinachangia kukosekana kwa mafanikio katika malengo ya sera, ikiwemo kushindwa kuendana na hali halisi ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI nchini;

KWA HIYO BASI, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha mchakato wa mapitio ya sera hii utakaoshirikisha wadau wote muhimu.

Pili, kwa kuwa marekebisho ya Sheria Namba 6 ya mwaka 2015 yalihitaji muundo mpya wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI nchini ili kuongeza ufanisi wa kiutendaji na kwamba mchakato wa kuandaa muundo huo haujakamilika;

NA KWA KUWA, kutokamilika kwa muundo huo kunasababisha kupunguza ufanisi katika mapambano dhidi ya UKIMWI;

KWA HIYO BASI, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha ukamilishaji wa muundo ili uanze kutumika mara moja na kuongeza ufanisi katika udhibiti wa UKIMWI.

Tatu, KWA KUWA, Kamati imebaini changamoto kubwa katika utengaji wa bajeti ya Mfuko wa UKIMWI ulioanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Namba 22 ya mwaka 2001 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2015;

NA KWA KUWA, changamoto hiyo inasababisha utegemezi uliokithiri kwa fedha za wafadhili katika utekelezaji majukumu ya udhibiti wa UKIMWI nchini ikiwemo upatikanaji wa uhakika wa dawa za kufubaza makali ya VVU *(ARV's)* na huduma nyingine zisizo za kitabibu;

KWA HIYO BASI, Kamati inashauri kuwa katika utengaji wa bajeti ya Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI *(ATF),* Serikali ianzishe kisheria chanzo mahususi cha kutunisha mfuko huu kama ilivyo katika mifuko mingine kama vile Mfuko wa Barabara *(Road Fund)* ili kupunguza utegemezi mkubwa kwa fedha za wafadhili ambazo mbali na kupambana na masharti magumu, hivi sasa zimeanza kupungua.

Nne, KWA KUWA, Kamati ilibaini changamoto ya ufinyu wa bajeti kwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS)* pamoja na ucheleweshaji wa fedha hizo kutoka Hazina;

NA KWA KUWA, hali hii inasababisha:-

(a) Tume kushindwa kuajiri watumishi wa kutosha katika ofisi zake, kwa sasa ina watumishi 83 kati ya 120 wanaohitajika.

(b) Tume kushindwa kuwaendeleza kitaaluma watumishi wake hasa katika maeneo ya ukaguzi wa ndani, tathmini na teknolojia ya habari na mawasiliano inayokuwa kwa kasi duniani; na

(c)Tume kushindwa kumudu gharama za uendeshaji wa ofisi kwa ujumla.

KWA HIYO BASI, Kamati inashauri kuwa:-

(a) Serikali itoe kipaumbele katika mapambano dhidi ya UKIMWI kwa kutenga bajeti ya kutosha kwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania ili kuhakikisha kuwa mafanikio yaliyofikiwa katika udhibiti wa UKIMWI nchini hayapotei; na

(b) Kwa kuzingatia kiwango cha bajeti inayotolewa na Serikali, Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania iweke utaratibu maalum wa kuwaendeleza watumishi wake ili kuendana na kasi ya ukuaji wa TEHAMA duniani.

Tano, KWA KUWA, Kamati imebaini changamoto ya ukosefu wa takwimu za Taifa kuhusu maambukizi ya UKIMWI nchini;

NA KWA KUWA, ukosefu wa takwimu sahihi na za kutumainiwa *(reliable)* unasababisha Serikali kushindwa kuchukua hatua sahihi katika mapambano dhidi ya UKIMWI;

KWA HIYO BASI, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania inaijengea uwezo thabiti Divisheni ya Ufuatiliaji na Tathmini ili kwa kushirikiana na Ofisi ya Takwimu ya Taifa na taasisi nyingine za utafiti, Tume iweze kukusanya na kuchapa takwimu za maambukizi ya Virusi vya UKIMWI kwa nchi nzima.

Sita, KWA KUWA, baadhi ya Asasi Zisizo za Kiserikali (AZISE yaani *NGOs*) zinazofanya kazi za masuala ya UKIMWI kwa ufadhili wa watu wa nje, hutekeleza pia ajenda binafsi za wafadhili hao kama masharti ya ufadhili ambayo mara nyingi huenda kinyume na mila na desturi za Kitanzania;

NA KWA KUWA, mwenendo wa asasi hizo unachangia ukiukwaji wa maadili, mila na desturi bora za Kitanzania;

KWA HIYO BASI, Kamati inaishauri Serikali kuweka utaratibu maalum wa kufuatilia uendeshaji wa shughuli za Asasi Zisizo za Kiserikali zinazojishughulisha na masuala ya UKIMWI ili kuhakikisha kuwa zinafanya kazi kwa kuzingatia maadili, mila na desturi za Kitanzania.

Saba, KWA KUWA, imebainika kuwa makundi yaliyo katika hatari zaidi ya kupata maambukizi ya VVU bado yanahitaji elimu ya kinga dhidi ya maambukizi ya UKIMWI na kwa ushiriki wa vijana katika kuibua, kupanga na kutekeleza afua za UKIMWI nchini ni duni;

NA KWA KUWA, kukosekana kwa elimu ya kinga dhidi ya maambukizi ya UKIMWI kwa makundi hayo pamoja na ushiriki duni wa makundi hayo katika

kuibua na kupanga afua za UKIMWI kunasababisha kutofanikiwa kwa juhudi za kutokomeza kabisa maambukizi mapya;

KWA HIYO BASI, Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

(a) Tume ijikite zaidi katika kutoa elimu ya kinga dhidi ya maambukizi ya UKIMWI katika makundi yaliyo katika hatari zaidi ya kupata maambukizi ya VVU ikiwemo watumiaji wa dawa za kulevya hasa kwa njia ya kujidunga, wanaume wanaofanya ngono ya jinsia moja, wafanyabiashara ya ngono, madereva wa magari ya masafa marefu na maeneo ya shughuli mbalimbali za kiuchumi ikiwemo migodi, mialo, ujenzi wa barabara na kadhalika; na

(b) Serikali itoe huduma rafiki kwa vijana hasa katika huduma za afya ili kuongeza ushiriki wa vijana katika kuibua, kupanga na kutekeleza afua za UKIMWI nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya nne inahusu hitimisho; napenda kukushukuru tena kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha taarifa ya Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu yake hadi kufikia Januari, 2017. Tunaamini kuwa fursa hii inayotokana na masharti ya Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, itasaidia kuliwezesha Bunge lako Tukufu kutekeleza wajibu wake ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Ajira, Vijana na Walemavu, Mheshimiwa Jenista Mhagama na aliyekuwa Naibu Waziri wake Mheshimiwa Dkt. Abdallah Possi. Aidha, nampongeza pia Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania, Dkt. Leonard Maboko na Kaimu Kamishna wa Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya, Ndugu Aida Tesha na watendaji wote wa Tume hizo kwa ushirikiano walioipa Kamati kwa kipindi cha mwaka mzima, kwa kufika mbele ya Kamati na kutoa ufafanuzi mara zote ulipohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah, kwa ushirikiano ambao amekuwa akitoa kwa Kamati. Pamoja na yeye, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndugu Athumani Hussein, Wakurugenzi Wasaidizi, Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Asia Msangi, Ndugu Happiness Ndalu na Ndugu Susan Ngole pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndugu Grace Mwenye, kwa kuratibu vyema Shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili taarifa hii na hatimaye kukubali maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hakuna anayeunga mkono hoja?
**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Haya, imeungwa mkono hoja hiyo na wale pale wote.

**TAARIFA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI KWA KIPINDI CHA JANUARI, 2016 HADI JANUARI, 2017 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**SEHEMU YA KWANZA**

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,**kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016; naomba kuwasilisha Taarifa ya Shughuli zilizotekelezwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kwa kipindi cha Januari, 2016 hadi Januari, 2017.

## *1.1 MAJUKUMU YA KAMATI NA SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA*

### 1.1.1 Majukumu

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane ya Kanuni chini ya 118 (10) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016, Kamati ya Masuala ya UKIMWI imepewa majukumu yafuatayo:

a) Kuratibu masuala yanayohusu UKIMWI katika sekta zote;
b) Kufuatilia utekelezaji wa sera na mipango ya Serikali kuhusu UKIMWI na udhibiti wa Madawa ya Kulevya;

c) Kujadili na kutoa mapendekezo na ushauri kuhusu hatua za kudhibiti madawa ya kulevya; na

d) Kushughulikia Bajeti za Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Madawa ya Kulevya.

**1.1.2 Shughuli**

**Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha mwaka mmoja yaani Januari 2016/Januari 2017 Kamati ilitekeleza majukumu yake kwa njia za vikao, semina na kongamano mbalimbalizilizohusu Masuala ya UKIMWI na Dawa za Kulevya, aidha Kamati ilifanya ziara za kazi katika Taasisi mbalimbali za Umma ili kujiridhisha na utekelezaji wa Sera za UKIMWI na Dawa za Kulevya katika maeneo hayo.

**a) Semina za Mafunzo**

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia ugeni wa Wajumbe katika Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, katika kipindi cha Februari 2016 Kamati ilipata mafunzo mbalimbali yaliyoratibiwa na Ofisi ya Bunge kwa dhumuni la kuwajengea uwezo Wajumbe katika kutekeleza majukumu yao. Mafunzo hayo yalihusu mambo yafuatayo:

i. Muundo na majukumu ya Kamati;

ii. Kanuni na taratibu za uendeshaji wa shughuli za kamati;

iii. Muundo na majukumu ya Tume zinazosimamiwa na Kamati hii yaani, Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya; na

iv. Sheria na Sera mbalimbali zinazohusu udhibiti wa UKIMWI na Dawa za Kulevya nchini.

**b) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Taasisi zinazosimamiwa na Kamati.**

**Mheshimiwa Spika,** Nyongeza ya Nane chini ya Kanuni ya 118 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, imeipa Kamati jukumu la kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Taasisi mbili ambazo ni Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya. Aidha, Kanuni hiyo hiyo pia imeipa Kamati jukumu la kuratibu masuala yote yanayohusu UKIMWI katika sekta zote ikiwemo kufuatilia utekelezaji wa sera na mipango ya Serikali kuhusu UKIMWI na udhibiti wa dawa za kulevya.

**c) Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016, Kamati ilikagua Mradi wa ujenzi wa ghala la kuhifadhia vielelezo vya kesi za dawa za kulevya wenye thamani ya shilingi milioni mia tatu hamsini (350,000,000) unaosimamiwa na Tume ya Kuratibu

Udhibiti wa Dawa za Kulevya uliopo Makao Makuu ya Jeshi la Polisi, Kurasini - Dar es Salaam. Aidha, katika kipindi hiki pia Kamati ilifanya ziara katika taasisi mbalimbali ili kufuatilia utekelezaji wa sera za UKIMWI na Dawa za Kulevya, Taasisi hizo ni pamoja na:

i. Hospitali ya Taifa Muhimbili na Hospitali ya Rufaa ya Mwananyamala katika Vituo vya Kutolea Huduma za Dawa ya *Methadone* kwa Warahibu wa Dawa za Kulevya;

ii. Pili Missana Foundation *Sobber House* iliyopo Kigamboni, Dar es Salaam;

iii. Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali;

iv. Bohari Kuu ya Madawa (MSD);

v. Mgodi wa Buzwagi uliopo Kahama, Shinyanga;

vi. Kituo cha Afya cha Kambarage, Shinyanga; na

**d) Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti za Taasisi zinazosimamiwa na Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016, Kamati ilikutana na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya ili kwa pamoja kujadili taarifa ya utekelezaji wa bajeti zao kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ambapo Kamati ilibaini changamoto mbalimbali za kiutendaji ambazo kwa kiasi kikubwa zilisababishwa na ufinyu wa bajeti zilizotengwa na Serikali kwa Tume hizi kama zinavyoonyeshwa katika majedwali na chati zifuatazo:

***JEDWALI NAMBA 1***

**MWENENDO WA BAJETI YA TUME YA KUDHIBITI UKIMWI TANZANIA KWA KIPINDI CHA MIAKA MITANO MFULULIZO KUANZIA 2011/2012 HADI 2016/2017**

**Chanzo: Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kwa miaka ya fedha 2011/12, 2012/13, 2013/14, 2014/15, 2015/16 na 2016/17**

*Chanzo: Jedwali Namba 1*

**Mheshimiwa Spika,** Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania ilianzakupungua katika kipindicha mwaka 2012/2013na kuwa katika hali yakupanda na kushuka hadi mwaka 2015/2016 kutokana na kupungua kwa mtiririko wa fedha za wafadhili katika bajeti ya miradi ya maendeleo. Aidha, kupanda na kushuka kwa mtiririko wa fedha za matumizi ya kawaida kwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania katika kipindi cha mwaka 2012/2013 hadi2016/2017, kumesababishwa na ukomo wa bajeti ya Serikali. Kwa kiasi kikubwa mwenendo huu wa bajeti umeathiri utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania katika mapambano dhidi ya maambukizi ya UKIMWI nchini.

***JEDWALI NAMBA 2:***

**MWENENDO WA BAJETI YA TUME YA KURATIBU UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA KWA KIPINDI CHA MIAKA MITANO MFULULIZO KUANZIA 2011/2012 HADI 2016/2017**

**Chanzo:** Bajeti za Tume ya Kuratibu Udhibiti waDawa za Kulevya kwa miaka ya fedha 2011/12, 2012/13, 2013/14, 2014/15, 2015/16 na 2016/17.

*Chanzo: Jedwali Namba 2*

**Mheshimiwa Spika,** bajeti ya Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya ambayo kwa sasa inajulikana kama Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya katika kipindi cha mwaka 2011/2012 na 2012/2013 likuwa chini kutokana na ukomo wa bajeti za Serikali ulioendana sawia na kiwango cha ushamiri wa biashara na matumizi ya dawa za kulevya katika kipindi hicho; ikilinganishwa na miaka 2013/2014 na 2014/2015, ambapo ushamiri wa biashara ya dawa za kulevya uliongezeka na bajeti ya Tume iliongezekakutokana na kuongezeka umakini wa Serikali na wafadhili katika kudhibiti biashara na matumizi ya dawa za kulevya nchini. Hata hivyo,katika kipindi cha mwaka 2015/2016 na 2016/2017, bajeti za Tume zilishuka hadi kufikia shilingi 0 kwa miradi ya maendeleo kwa mwaka 2016/2017 kutokana na ukomo wa fedha za wafadhili na kubadilika kwa vipaumbele vya bajeti ya serikali. Kwa ujumla, mwenendo mzimawa bajeti ya Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya umechangia kwa kiasi kikubwakupunguza ufanisi wa Tume katika kudhibiti biashara na matumizi ya dawa za kulevya nchini.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI

**Mheshimiwa Spika,**utekelezaji wa majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI ulizingatia masharti ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 hususan Kanuni ya 117 inayohusu utaratibu katika Kamati za Kudumu za Bunge. Hivyo,Kamati iliandaa Mpango Kaziuliotekelezwa katika kipindi cha Januari 2016 hadi Januari 2017, ambao Matokeo ya Utekelezaji wake yamefanyiwa Uchambuzi katika Sehemu hii.

### *2.1 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI*

### 2.1.1 Semina za Mafunzo

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia kuundwa upya kwa Kamati za Kudumu za Bunge mnamo Januari 15, 2016 Wajumbe wa Kamati ya Masuala ya UKIMWI walipata mafunzo mbalimbali yaliyolenga kuwajengea uwezo wa kutekeleza majukumu yao kwa ufasaha, namafunzo hayo yaligawanyika katika sehemu kuu mbili:

### a) Taratibu za Uendeshaji wa Shughuli za Kamati

**Mheshimiwa Spika,** Wajumbe walipata elimu kuhusu mambo mbalimbali yanayohusu Kamati ikiwemo muundo, majukumu na taratibu za uendeshaji wa Shughuli za Kamati kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.Aidha, kupitia mafunzo haya Wajumbe walipata uelewa wa kina katika maeneo ya uchambuzi wa bajeti za wizara/taasisi, uchambuzi wa miswada na taratibu za miswada Bungeni, pamoja na mahusiano ambayo kwa kipindi cha nyuma Kamati ilifanikiwa kuyaanzisha na

vyombo vingine vya ndani na nje ya nchi vilivyojikita katika mapambano dhidi ya maambukizi ya UKIMWI.

**b) Taratibu za Uendeshaji wa Tume zinazosimamiwa na Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** Wajumbe walipata elimu kuhusu mambo mbalimbali yanayohusu Shughuli za Kamati ikiwemo muundo na majukumu ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya, pia Wajumbe wa Kamati waliweza kupata ufahamu juu ya sheria na sera zinazosimamia uratibu na utekelezaji wa majukumu ya Tume hizo na taasisi nyingine zote zinazotekeleza Sera za UKIMWI na Dawa za Kulevya nchini. Mbali na kupata uelewa juu ya mipango na mikakati madhubuti ya Tume hizi katika kutekeleza majukumu yake, Wajumbe pia walipata ufahamu juu ya hali halisi ya maambukizi ya UKIMWI na udhibiti wa dawa za kulevya kwa mwaka 2015/2016.

## 3.0 KUFUATILIA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya Kamati kujengewa uwezo kupitia semina mbalimbali za Mafunzo, Kamati ilianza utekelezaji wa majukumu yake kwa kufuatilia kwa ukaribu utendaji kazi wa Taasisi zilizo chini yake pamoja na utekelezaji wa sera na mipango anuai inayohusu Udhibiti wa UKIMWI na Dawa za Kulevya katika Wizara na Taasisi za Umma nchini kama ifuatavyo:

### *3.1 TUME YA KUDHIBITI UKIMWI TANZANIA*

**Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania, Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

a. Changamoto kubwa inayoikumba Tume ni Ufinyu wa Bajeti na ucheleweshwaji wa fedha kutoka serikalini ambapo kwa sasa, zaidi ya asilimia 90 ya bajeti ya Tume inategemea fedha za wafadhili wa nje hali iliyopelekea kupunguza ufanisi wa Tume katika mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU na UKIMWI;

b. Mapungufu katika Sera ya UKIMWI ya 2001 ambayo imepelekea Tume na Wadau wa UKIMWI kushindwa kwenda na kasi inayohitajika sasa katika kudhibiti Maambukizi ya Virusi vya UKIMWI;

c. Kutokamilika kwa Muundo wa Tume unaopelekea uchache wa watumishi wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania unaoenda sambamba na uhaba wa fursa za kujiendeleza kitaaluma; na

d. Uelewa mdogo wa jamii hususan katika makundi maalumu, kuhusu namna ya kujikinga na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI.

### 3.1.1 TUME YA KURATIBU UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA

**Mheshimiwa Spika,** katika kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Tume hii, Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

a. Ufinyu wa Bajeti inayotengwa na Serikali pamoja na ucheleweshwaji wa mtiririko wa fedha kutoka Wizara ya Fedha ambao unapelekea mambo yafuatayo:

i. Kukosekana kwa vitendea kazi vya kisasa vinavyopelekea kupungua kwa ufanisi katika udhibiti wa dawa za kulevya nchini;

ii. Tume kushindwa kutoa elimu kwa umma juu ya athari za matumizi ya dawa za kulevya;

iii. Tume kushindwa kufanya operesheni za ukamataji wa wafanyabiashara wa dawa za kulevya na uteketezaji wa mashamba makubwa ya Bangi katika mikoa inayoongoza kwa kilimo cha zao hilo ambalo ni haramu; na

iv. Kukosekanakwa programu maalum zenye lengo la kuwainua kiuchumi warahibu wa dawa za kulevya ambao huchangia kukwamisha juhudi zaokatika kuachana moja kwa moja na matumiziya dawa za kulevya.

b. Kutokamilika kwa Muundo wa Tume unaopelekea uchache wa watumishi wenye taaluma mbalimbali wanaohitajika katika kuongeza ufanisi wa Tume katika kudhibiti dawa za kulevya nchini.

## *3.2 TAASISI ZA UMMA ZA KISEKTA ZINAZOTEKELEZA SERA ZA UKIMWI NA DAWA ZA KULEVYA*

### 3.2.1 Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikutana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na kujadili Mwongozo wa namna ya kuwahudumia Watumishi wa Umma wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (*Workplace Interventions, Medical Treatment and Training to Staff)* ambapo Kamati ilishauri mambo yafuatayo:

a. Waajiri kuhamasisha na kuwajengea watumishi ujasiri wa kupima VVU,kutoa elimu ya kujikinga dhidi ya maambukizi ya UKIMWI na kutekeleza afua za UKIMWI mahala pa kazi;

b. Serikali kuwachukulia hatua waajiri wanaotumia fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya WAVIU kwa shughuli nyingine zisizohusiana na UKIMWI;

c. Serikali kuongeza ajira katika viwanda vidogovidogo na katika sekta binafsi ili kukuza uchumi na kuwawezesha vijana kupata ajira ili kuwaepusha kujihusisha na matumizi ya dawa za kulevya na tabia hatarishi zinazochochea kuongezeka kwamaambukizi ya VVU na UKIMWI; na

d. Serikali kuendelea kuwasisitiza waajiri katika utumishi wa umma kutumia fursa zinazowazunguka ili kudhibiti tatizo la unyanyapaa ambao huchangia kurudisha nyuma juhudi za Serikali katika mapambano dhidi ya maambukizi ya UKIMWI.

### 3.2.2 Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee Na Watoto

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikutana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ili kujadili kuhusu hatua iliyofikiwa katika Utafiti wa Upatikanaji wa Chanjo ya UKIMWI Tanzania, ambapo Kamati ilibaini kuwa wataalamu wa utafiti wa tiba bado wapo kwenye hatua za awali za utafiti wa chanjo hiyo kutokana na changamoto ya rasilimali fedha, rasilimali watu na teknolojia ya juu inayohitajika katika utafiti wa chanjo. Hivyo, kuifanya Tanzania kama zilivyo nchi nyingi za Afrika kutegemea kwa kiasi kikubwa tafiti zinazofanywa na nchi zilizoendelea kama Marekani. Kwa sababu hiyo, Kamati ilishauri mambo yafuatayo:

a. Serikali kuona umuhimu wa kuwekeza katika utafiti wa chanjo ya UKIMWI; kwa kuongeza Bajeti ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto;
b. Wizara kujielekeza zaidi katika kutoa elimu kwa wananchi juu ya kujikinga na maambukizi ya VVU na UKIMWI, pamoja na Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa (MSY) kwa maana "*Kinga ni bora kuliko Tiba*".

### 3.2.3 Bohari Kuu ya Madawa (MSD) na Baraza la WAVIU (NACOPHA)

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikutana na Bohari Kuu ya Madawa nchini pamoja na Baraza la Watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI ili kujadili mafanikio na changamoto zilizopo katika upatikanaji, usambazaji na utumiaji wa dawa za kufubaza makali ya VVU (ARVs) nchini. Ambapo, Kamati ilibaini uwepo wa changamoto katika upatikanaji wa dawa hizo katika vituo vingi vya afya nchini inayosababishwa na malimbikizo ya madeni ya Bohari Kuu ya Madawa katika Mamlaka ya Bandari, hali iliyopelekea watumiaji wa dawa hizo kulazimika kununua dawa katika maduka ya dawa ya watu binafsi kwa bei za juuhuku wengine wakishindwa kumudu gharama hizo na kujikuta wakidhoofika.Hivyo, Kamati ilishauri mambo yafuatayo:

a. Serikali kufanya jitihada za haraka za ulipaji wa deni kwa Bohari Kuu ya Dawa (MSD) ili kuwasaidia WAVIU kupata dawa za kufubaza makali ya VVU kwa wakati pia kutowakatisha tamaa Wafadhili wanaotuletea dawa hizo;

b. Serikali kuwekeza katika uzalishaji wa ndani wa dawa hizi ili kuondokana na utegemezi wa wafadhili katika ununuzi wa madawa kama jirani zetu wa Uganda wanavyofanya; na

c. Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa itoe Waraka utakaohusu Halmashauri zote kushirikiana na Mabaraza ya WAVIU katika kubuni njia za kuwakwamua kiuchumi WAVIU na kusaidia katika mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU.

### 3.2.4 Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikutana na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ili kujadilimafanikio na changamoto zilizopo katika utekelezaji wa Afua za UKIMWI katika Ofisi hiyo, ambapo Kamati ilibaini yafuatayo:

a. Ufinyu wa bajeti iliyotengwa na Serikali kwa ajili ya kuwahudumia watumishi WAVIU na kuratibu masuala mbalimbali yanayohusu UKIMWI katika Ofisi hii;

b. Ufinyu wa bajeti nzima ya uendeshaji wa shughuli za Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, uliopelekea Ofisi hii kushindwa kutekeleza majukumu yake yote ipasavyo ikiwa ni pamoja na kufanya ukaguzi wa fedha za UKIMWI katika Ofisi/Taasisi zote za Umma na Asasi zisizo za kiserikali ambazo fedha zake zinapitia Wizara ya Fedha.

**Mheshimiwa Spika,**Kwa sababu hiyo, Kamati ilimshauri Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kufanya Ukaguzi wa "*Value-for-Money*" kwa Fedha zote za Masuala ya UKIMWI ili kuona kama pesa zinazotengwa mahususi kushughulikia Masuala ya UKIMWI zinatumika kama zilivyokusudiwa.

### 3.2.5 Wizara ya Habari, Utamaduni, Wasanii na Michezo

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikutana pia na Wizara ya Habari, Utamaduni, Wasanii na Michezo kwa lengo la kujadili Taarifa ya Wizara kuhusu Utekelezaji wa Afua za UKIMWI mahali pa kazi ambapo Kamati ilibaini kuwa utekelezaji wa Mwongozo huo katika wizara hii umejikita zaidi katika kuwapatia posho za kujikimu watumishi ambao ni WAVIU, lakini kuna jitihada ndogo sana zinazofanywa katika utoaji wa elimu ya kujikinga dhidi ya maambukizi mapya kwa watumishi wa wizara hiyo. Hivyo, Kamati ilishauri mambo makubwa mawili kwa Wizara hii:

a. Wizara kuweka matangazo mengi yanayohusu Mapambano dhidi ya UKIMWI kwenye viwanja vya michezo ili elimu kuhusu UKIMWI iweze kuwafikia wananchi wengi zaidi; na

b. Wizara kuweka mikakati madhubuti ya kuwasaidia wanamichezo na wasanii kwa ujumla kutokujihusisha na matumizi ya dawa zaa kulevya.

### 3.2.6 *Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikutana na Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi ili kujadili Taarifa yao ya Utekelezaji wa Mwongozo wa Afua za UKIMWI Mahali pa Kaziambapo changamoto kubwa iliyobainika naKamati ni utekelezaji mdogo wa afua za UKIMWI katika wizara yenyewe na taasisi inazozisimamia, hivyo Kamati ilishauri mambo yafuatayo:

a. Wizara isimamie vyema utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ya Mwaka 2014 kuhusu Malengo na Matamko yanayohusu Mapambano dhidi ya Maambukizi ya VVU kwa watumishi; na

b. Serikali kuziagiza shule zote nchini kuweka ajenda ya UKIMWI na dawa za kulevya kunapokuwa na vikao vya wazazi na wanafunzi ili kuhakikisha wanafunzi na wazazi wanapata uelewa juu ya kujikinga dhidi ya UKIMWI na matumizi ya Dawa za Kulevya.

### 3.2.7 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikutana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ili kujadili mafanikio, changamoto na matarajio ya Wizara hii katika Udhibiti wa Matumizi ya Dawa za Kulevya nchini ambapo, Kamati ilibaini changamoto nyingi zilizotokana na ufinyu wa bajeti ya wizara, hivyo kupelekea zoezi la udhibiti wa dawa za kulevya nchini kutokuwa na matokeo ya kuridhisha.Hii imetokana na bajeti yawizara hii kupungua kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na kufikia shilingi bilioni 30,000,000,000 kwa miradi ya maendeleo ikilinganishwa na kiasi cha shilingi bilioni 65,757,261,000 zilizotengwa kwa mwaka wa fedha uliopita 2015/2016. Hivyo, Kamati ilishauri yafuatayo:

a. Jeshi la Polisi kuongezewa Bajeti ili kuwawezesha kununua vitendea kazi kama boti za doria ili kukabiliana na changamoto wanazopata katika kudhibiti uingizwaji wa dawa za kulevya nchini; na

b. Jeshi la Polisi kuimarisha ulinzi hususan katika maeneo ya bandari, viwanja vya ndege na mipaka ya nchi.

## *4.0 UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO*

### 4.1 Mradi wa Ujenzi wa Ghala la Kuhifadhia Dawa za Kulevya

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikaguaMradi wa Ujenzi wa Ghala la Kuhifadhia Vielelezo vya Kesi za Dawa za Kulevya wenye thamani ya shilingi Milioni 272,500,000uliotekelezwa ndani ya Makao Makuu ya Jeshi la Polisi Kurasini, Dar es Salaam na kusimamiwa na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya.Kamati ilibaini mapungufu mengi katika Mradi yakiwemo:

a. Udogo wa eneo la ghala na ubora usioridhisha wa viwango vya ujenzi ikilinganishwa na mahitaji makubwa ya hifadhi za vidhibiti vya dawa za kulevya vilivyohifadhiwa ndani ya ghala hilo na vile vinavyoendelea kukamatwa; na

b. Mazingira magumu na hatarishi ya Watumishi wanaofanya kazi katika ghala hilo, kutokana na ukosefu wa vitendea kazi wengi wao wameathirika kwa kuvuta hewa iliyochanganyika na dawa za kulevya na wengine kunusurika na milipuko inayosababishwa na kemikali za madawa hayo.

**Mheshimiwa Spika,**kutokana na mapungufu haya, Kamati inashauri mambo yafuatayo:

a. Serikali kuona umuhimu wa kutenga fedha za kutosha ili kujenga ghala kubwa, imara na la kisasa litakalokidhi mahitaji ya sasa ya kuhifadhi vidhibiti vya sampuli mbalimbali za dawa za kulevya vinavyokamatwa (*ushahidi*);

b. Serikali iwekeze katika vitendea kazi vya kisasa vitakavyolinda afya za watumishi lakini pia vitakavyorahisisha zoezi la upekuzi na ukamataji wa dawa za kulevya zinazoingizwa nchini kupitia njia mbalimbali; na

c. Serikali kutoamotishakwa watumishi wa kitengo maalumu cha udhibiti wa dawa za kulevya kwa kuboresha mazingira wanayofanyia kazi ikiwemo posho, ofisi na vitendea kazi.

### 4.2 Ziara

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hiki pia Kamati ilifanya ziara za kazi katika taasisi mbalimbali ili kufuatilia utekelezaji wa sera za UKIMWI na Dawa za Kulevya, Taasisi hizo ni pamoja na Vituo vya Kutolea Huduma za Dawa ya Methadone kwa Warahibu wa Dawa za Kulevya vilivyopo katika Hospitali ya Taifa Muhimbili na Hospitali ya Mwananyamala, Pili Missana Foundation Sobber House,Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali,Bohari Kuu ya Madawa (MSD), Mgodi wa Dhahabu wa Acacia, na Kliniki ya WAVIU katikaKituo cha Afya cha Kambarage.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na ziara hizi, Kamati inashauri mambo yafuatayo:
a. Serikali kutenga bajeti ya kutosha ili kuiwezesha Ofisi ya Mkemia Mkuu kumudu gharama za kuendesha ofisi kwa wakati na kwa ufanisi; ili kusaidia kupunguza mlundikano wa kesi za dawa za kulevya;

b. Serikali kuona umuhimu wa kupitisha sheria zitakazolinda uanzishwaji wa wakala mbalimbali wa serikali ili kuzipa mamlaka kamili wakala hizo katika maeneo yao ya utendaji;

c. Kudumisha ushirikiano wa kazi kati ya Jeshi la Polisi, Mahakama na Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali ili kuongeza ufanisi katika kushughulikia masuala yanayohusu udhibiti wa Dawa za Kulevya nchini;

d. Serikali itenge bajeti ya kutosha ili kuwezesha ujenzi wa vituo vingi vya huduma ya tiba ya utengemao kwa warahibu wa dawa za kulevya, ununuzi wa vitendea kazi, vifaa tiba na kuajiri watumishi ili kuleta ufanisi katika utoaji wa huduma;

e. Kuwepo na takwimu za WAVIU Mahala pa Kazi ili kuwezesha serikali kuchukua hatua sahihi.

**5.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI**

**Mheshimiwa Spika**, mwezi Aprili, 2016 Kamati ilikutana na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya kwa mwaka wa fedha 2015/2016, kisha Kamati ilipitia na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya – *Fungu 91* na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) – *Fungu* 92kwa mwaka wa fedha 2016/2017; kama ilivyoainishwa katika Nyongeza ya Nane ya Kanuni ya 118 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya, Kamati ilizingatia maelezo na fafanuzi mbalimbali zilizotolewa na Tume hizo kuhusiana na Makadirio ya Mapato na Matumizi yao ambapo Kamati ilipitisha shilingi bilioni 2,340,236,000kwa matumizi ya kawaida kwaFungu 91 - Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya na hakuna kiasi kilichotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Aidha, kiasi cha shilingi bilioni 4,961,677,000 kilitengwakwa matumizi ya kawaidana shilingi bilioni 5,235,823,413 kwa miradi ya maendeleo kwaFungu 92 - Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kwa mwaka wa fedha

2016/2017.Ambapo, Kamati iliridhia na kupitisha Makadirio ya Tume zote mbili na kuwasilisha maoni yake ikiwa ni pamoja na kuliomba Bunge lipitishe Makadirio ya Tume hizo kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

## SEHEMU YA TATU

## 6.0 MAONI NA USHAURI

**Mheshimiwa Spika,** kutokana nashughuli za Kamati zilizofanyika katika kipindi cha mwaka mmoja (Januari, 2016 - Januari, 2017) kumekuwa na changamoto mbalimbali zilizojitokeza katika Taasisi zinazosimamiwa na Kamati hii ambazo Kamati inazitolea maoni na ushauri ufuatao:

### TUME YA KURATIBU UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA

**Mheshimiwa Spika,** ili kutekeleza vyema majukumu ya Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya, Kamati inashauri mambo Nane (8) yafuatayo:-
**1. Kwa kuwa,** Kamati imebaini dosari nyingi katika Sera ya Dawa za Kulevya ya mwaka 2004 ambayo imepitwa na wakati,

**Na kwa kuwa,**dosari hizozimechangia ugumu katika utatuzi wa changamoto za sasa kuhusu udhibiti wa uingizwaji na matumizi ya dawa za kulevya, hali inayopelekea taifa kuendelea kupoteza nguvu kazi.

**Kwa hiyo basi**, Kamati inashauri kuwa Serikali iharakishe mapitio ya sera hii ili kulinusuru taifa na janga hili la dawa za kulevya.

**2. Kwa kuwa,** Kamati imebaini kuwa tangu Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya ibadilishwe kisheria kuwa Mamlaka ya Kupambana na Dawa za Kulevya, muundo wake bado haujakamilika,

**Na kwa kuwa,**kutokukamilika kwa muundo huo kunasababisha Tume kushindwa kuajiri watumishi wa kutosha (*watumishi 37 kati ya 65 wanaohitajika*),

**Kwa hiyo basi,** Kamati inaishauri serikali kuharakishana kukamilisha mchakato wa muundo wa Mamlaka hii ili uanze kutumika mara moja na kuongeza ufanisi katika kudhibiti uingizwaji na matumizi ya dawa za kulevya.

**3. Kwa kuwa**, imebainika kwamba Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa Tume umekuwa unakwamisha utendaji wa baadhi ya majukumu ya Tume hii kama vile:

a) Kudhibiti uingizwaji wa dawa za kulevya katika mipaka yote ya nchi ambayo ni mingi na ina vipenyo vingi vinavyofanya zoezi la udhibiti kuwa gumu;

b) Tume kushindwa kuteketeza mashamba ya bangi ambayo hulimwa sehemu zisizofikika kwa urahisi ambapo utekelezaji wa zoezi hilo uhitaji fedha nyingi; na
c) Tume kushindwa kutoa elimu kwa wananchi kuhusu madhara yatokanayo na matumizi ya dawa za kulevya ili kunusuru afya za Watanzania na nguvu kazi ya taifa.

**Na kwa kuwa**, kutotekelezwa kwa majukumu ya msingi ya Tume hiyo kutokana na ufinyu wa bajeti kunaathiri juhudi za Udhibiti wa dawa za Kulevya nchini jambo ambalo lina madhara makubwa kwa taifa,

**Kwa hiyo basi,** Kamati inaishauri Serikali kuangalia uzito wa majukumu yanayotekelezwa na Tume hii katika kupambana na biashara haramu ya dawa za kulevya nchini, kwa kuongeza bajeti yao ili kuiongezea ufanisi Tume na kuhakikisha kuwa mafanikio yaliyofikiwa katika udhibiti wa dawa za kulevya hayapotei.

**4. Kwa kuwa**, Kamati imebaini kukosekana kwa chombo cha kisheria cha kushughulikia udhibiti wa biashara na matumizi ya dawa za kulevya katika ngazi ya halmashauri,

**Na kwa kuwa,** kukosekana kwa chombo hicho kunachangia udhibiti duni wa dawa za kulevya katika halmashauri nchini,

**Kwa hiyo basi**, Kamati inaishauri Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kufanya maboresho ya Kamati za UKIMWI za Halmashauri ili kisheria ziwe na uwezo wa kusimamia shughuli za udhibiti wa dawa za kulevya katika ngazi ya halmashauri kama ilivyo kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, kwa lengo la kusimamia kwa pamoja mambo haya yanayoendana.

**5. Kwa kuwa,** Serikali imebaini changamoto katika upatikanaji wa tiba za utengemao (*Rehabilitation*) wa warahibu (*Addicts*) wa dawa za kulevya nchini ambapo kwa sasa zinapatikana katika mkoa wa Dar es Salaam na Zanzibar pekee,
**Na kwa kuwa**, changamoto hiyo inakwamisha juhudi za kuwawezesha Warahibu kuacha matumizi ya dawa za kulevya, jambo linalochangia madhara ya kijamii nchini,

**Kwa hiyo basi**, Kamati inashauri kwamba huduma hii ihuisihwe katika Sera ya Afya kama ilivyofanyika kwa suala la UKIMWI ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma hii kwa nchi nzima.

**6. Kwa kuwa,** Kamati imebaini uwepo wa mwamko mdogo na ushiriki duni wa jamii katika mapambano dhidi ya biashara haramu ya dawa za kulevya,

**Na kwa kuwa,**hali hiyo kwa kiasi kikubwa imesababisha ongezeko la watumiaji wa dawa za kulevya, wagonjwa wa akili na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI,

**Kwa hiyo basi,**Kamati inashauri:
a) Tume ishirikiane na vyombo vya dola katika kuandaa kampeni endelevu ambazo mbali na kuwajengea uelewa watanzania kuhusu umuhimu wa kushiriki katika mapambano haya, pia utawapa motisha ya kushiriki katika mapambano dhidi ya biashara ya dawa za kulevya; na

b) Viongozi wakuu wa nchi kutoa kauli thabiti na kusimamia utekelezaji wa kauli hizo katika kukemea na kukomesha biashara na matumizi ya dawa za kulevya ili kuhamasisha ushiriki wa jamii nzima katika janga hili.

**7. Kwa kuwa**, Kamati imebaini uwepo wa changamoto mbalimbali zinazowakabili warahibu (*Addicts*) wa dawa za kulevya punde wanapoacha matumizi ya dawa hizo, kama kutengwa na jamii na kukosa ajira,

**Na kwa kuwa**, changamoto hizo husababisha Warahibu kurudia matumizi ya dawa za kulevya au kujiingiza katika vitendo vya uhalifu.

**Kwa hiyo basi**, Kamati inashauri kuwa, Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Ajira, Vijana na Walemavu ianzishe programu maalumu za kuwasaidia warahibu wa dawa za kulevya kuweza kujiinua na kujitegemeza kiuchumi mara tu baada ya kuachana na matumizi ya dawa za kulevya.

**8. Kwa kuwa**, Kamati imebaini uwepo wa uhusiano mkubwa kati ya matumizi ya pombe za bei rahisi maarufu kama "*viroba*" na kuongezeka kwa tabia hatarishi zinazochangia ongezeko la vijana katika matumizi ya dawa za kulevya,

**Na kwa kuwa**, hali hiyo inaathiri ufanisi wa nguvu kazi ya taifa kutokana na madhara ya matumizi ya dawa za kulevya,

**Kwa hiyo basi,**Kamati inaishauri Serikali kufungia kabisa uzalishaji na uuzwaji wa pombe za bei rahisi maarufu kama "*viroba*" ili kulinusuru taifa.

**TUME YA KUDHIBITI UKIMWI TANZANIA;**

**Mheshimiwa Spika,** ili Tume hii iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa, Kamati inashauri mambo Saba (7) yafuatayo:-

**1. Kwa kuwa**, Kamati imebaini dosari nyingi katika Sera ya UKIMWI ya mwaka 2001,

**Na kwa kuwa,** dosari hizo zinachangia kukosekana kwa mafanikio katika malengo ya Sera, ikiwemo kushindwa kuendana na hali halisi ya maambukizi ya Virusi vya UKIMWI nchini,

**Kwa hiyo basi**, Kamati inaishauri Serikali kuharakishamchakato wamapitio ya sera hii utakaoshirikisha wadau wote muhimu;

**2. Kwa kuwa,**Marekebisho ya Sheria Na. 6 ya mwaka 2015 yalihitaji Muundo Mpya wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI nchini ili kuongeza ufanisi wa kiutendaji na kwamba Mchakato wa kuandaa Muundo huo haujakamilika,

**Na kwa kuwa**, Kutokamilika kwa Muundo huo kunasababisha kupunguza ufanisi katika mapambano dhidi ya UKIMWI,

**Kwa hiyo basi**, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha ukamilishaji wa muundo ili uanze kutumika mara moja na kuongeza ufanisi katika udhibiti wa UKIMWI.

**3. Kwa kuwa**, Kamati imebaini Changamoto kubwa katika utengaji wa bajeti ya Mfuko wa UKIMWI ulioanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Na. 22 ya mwaka 2001 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2015,

**Na kwa kuwa** changamoto hiyo inasababisha utegemezi uliokithiri kwa fedha za wafadhili katika kutekeleza majukumu ya udhibiti wa UKIMWI nchini ikiwemo, upatikanaji wa uhakika wa Dawa za kufubaza makali ya VVU (ARVs) na huduma nyingine zisizo za kitabibu.

**Kwa hiyo basi**, Kamati inashauri kuwa katika utengaji wa bajeti ya Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI (ATF), Serikali ianzishe kisheria chanzo mahususi cha kutunisha Mfuko huu kama ilivyo katika Mifuko mingine kama vile Mfuko wa Barabara (*Road Fund*) ili kupunguza utegemezi mkubwa kwa fedha za wafadhili ambazo mbali na kuambatana na masharti magumu, hivi sasa zimeanza kupungua.

**4. Kwa kuwa,** Kamati ilibaini changamoto ya ufinyu wa bajeti kwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) pamoja na ucheleweshaji wa fedha hizo kutoka Hazina,

**Na kwa kuwa,** hali hii inasababisha:

a) Tume kushindwa kuajiri watumishi wa kutosha katika Ofisi zake (kwa sasa ina watumishi 83 kati ya 120 wanaohitajika);

b) Tume kushindwa kuwaendeleza kitaalumawatumishi wake hasa katika maeneo ya Ukaguzi wa Ndani, Tathminina Teknolojia ya Habari na Mawasiliano inayokuwa kwa kasi duniani; na

c) Tume kushindwa kumudu gharama za uendeshaji wa ofisi kwa ujumla.
**Kwa hiyo basi**, Kamati inashauri kuwa:

a) Serikali itoe kipaumbele katika mapambano dhidi ya UKIMWI kwa kutenga bajeti ya kutosha kwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania ili kuhakikisha kuwa mafanikio yaliyofikiwa katika udhibiti wa UKIMWI nchini hayapotei;

b) Kwa kuzingatia kiwango cha bajeti inayotolewa na Serikali, Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzaniaiweke utaratibu maalum wa kuwaendeleza watumishi wake ili kuendana na kasi ya ukuaji wa TEHAMA duniani;

**5. Kwa kuwa**, Kamati imebaini Changamoto ya Ukosefu wa Takwimu za Taifa kuhusu Maambukizi ya UKIMWI nchini,

**Na kwa kuwa,** ukosefu wa Takwimu sahihi na za kutumainiwa (*Reliable*) unasababisha Serikali kushindwa kuchukua hatua sahihi katika mapambano dhidi ya UKIMWI,

**Kwa hiyo basi,** Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania inaijengea uwezo thabiti divisheni ya Ufuatiliaji na Tathmini ili kwa kushirikiana na Ofisi ya Takwimu ya Taifa na Taasisi nyingine za utafiti, Tume iweze kukusanya na kuchapa takwimu za maambukizi ya virusi vya UKIMWI kwa nchi nzima.

**6. Kwa kuwa,**Baadhi ya Asasi zisizo za Kiserikali (AZISE yaani NGOs) zinazofanya kazi za Masuala ya UKIMWI kwa ufadhili wa watu wa nje, hutekeleza pia ajenda binafsi za wafadhili hao kama masharti ya ufadhili ambayo mara nyingi huenda kinyume na mila na desturi za kitanzania;

**Na kwa kuwa,** mwenendo wa Asasi hizo unachangia ukiukwaji wa maadili, mila na desturi bora za kitanzania,

**Kwa hiyo basi**, Kamati inaishauri Serikali kuweka utaratibu maalum wakufuatilia uendeshaji wa shughuli za Asasi zisizo za Kiserikali zinazojishughulisha na masuala ya UKIMWI ili kuhakikisha kuwa zinafanya kazi kwa kuzingatia maadili, mila na desturi za kitanzania.

**7. Kwa kuwa,**imebainika kuwa makundi yaliyo katika hatari zaidi ya kupata maambukizi ya VVU bado yanahitaji elimu ya kinga dhidi ya Maambukizi ya UKIMWI, na kwamba ushiriki wa vijana katika kuibua, kupanga na kutekeleza afua za UKIMWI nchini ni duni,

**Na kwa kuwa,** kukosekana kwa elimu ya kingadhidi ya Maambukizi ya UKIMWI,kwa makundi hayo pamoja na ushiriki duni wa makundi hayo katika kuibua na kupanga afua za UKIMWI kunasababisha kutokufanikiwa kwa juhudi za kutokomeza kabisa Maambukizi mapya.

**Kwa hiyo basi,**Kamati inashauri mambo yafuatayo:

a) Tume ijikite zaidi katika kutoa elimu ya kinga dhidi ya Maambukizi ya UKIMWI katika makundi yaliyo katika hatari zaidi ya kupata maambukizi ya VVU ikiwemo watumiaji wa dawa za kulevya hasa kwa njia ya kujidunga, wanaume wanaofanya ngono ya jinsia moja, wafanyabiashara ngono, madereva wa magari ya masafa marefu na maeneo ya shughuli mbalimbali za kiuchumi ikiwemo migodi, mialo, ujenzi wa barabara, n.k; na

b) Serikali itoe huduma rafiki kwa vijana hasa katika huduma za afya ili kuongeza ushiriki wa vijana katika kuibua, kupanga na kutekeleza afua za UKIMWI nchini.

## SEHEMU YA NNE

### 7.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** napenda kukushukuru tena kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu yake hadi kufikia Januari, 2017. Tunaamini kuwa fursa hii inayotokana na masharti ya Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, itasaidia kuliwezesha Bunge lako tukufu kutekeleza wajibu wake ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** naombanachukua fursa hii kumpongeza Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Ajira, Vijana na Walemavu, Mhe. Jenista Mhagama,Mb na aliyekuwa Naibu Waziri wake Dkt. Abdallah Possi, Mb. Aidha, nampongeza pia Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania, Dkt. Leonard Maboko na Kaimu Kamishna wa Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya, Ndg. Aida Tesha; na Watendaji wote wa Tume hizo kwa ushirikiano walioipa Kamati kwa kipindi cha mwaka mzima, kwa kufika mbele ya Kamati na kutoa ufafanuzi mara zote ulipohitajika.

**Mheshimiwa Spika,**kwa namna ya pekee napenda niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati kwa uchapakazi wao wakati wote wa kutekeleza majukumu ya Kamati kwa Mwaka mzima. Wajumbe wamefanya kazi kubwa katika kuhakikisha Kamati inaisimamia na kuishauri vyema Serikali kwa mujibu wa Katiba ya nchi na Kanuni za Kudumu za Bunge. Napenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kwa majina kama ifuatavyo:

1. Mhe. Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, Mb –Mwenyekiti
2. Mhe. Dkt. Jasmine Tiisekwa Bunga, Mb –M/Mwenyekiti
3. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Dkt. Hadji Hussein Mponda, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Daniel Edward Mtuka, Mb -Mjumbe
6. Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Joseph Kizito Mhagama, Mb -Mjumbe
8. Mhe. Juliana Daniel Shonza, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Kemirembe Julius Lwota, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Lucia Ursula Michael Mlowe, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Mary Deo Muro, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Martha Mosses Mlata - Mjumbe
13. Mhe. Masoud Abdallah Salim, Mb - Mjumbe
14. Mhe.Oscar Rwegasira Mukasa, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo,Mb - Mjumbe

16. Mhe. Yussuf Kaiza Makame, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Zainab Matitu Vullu, Mb - Mjumbe
18. Mhe.Omary Ahmad Badwel, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashillilah, kwa ushirikiano ambao amekuwa akitoa kwa Kamati. Pamoja na yeye, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge,Ndg. Athumani Hussein, Wakurugenzi Wasaidizi, Makatibu wa Kamati hii, Ndg. Asia Msangi, Ndg. Happiness Ndalu na Ndg. Susan Ngole pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndg. Grace Mwenye, kwa kuratibu vyema Shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika.

**Mheshimiwa Spika,** sasa naliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili taarifa hii na hatimaye kukubali Maoni na Ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

......................................
Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI**
**06 FEBRUARI, 2017**

**MWENYEKITI:** Haya. Ahsante sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI. Sasa namkaribisha Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kukushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya mwaka ya shughuli zilizotekelezwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii katika kipindi cha mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane kifungu cha 5 iliyo chini ya Kanuni ya 118 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari,

2016, Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii imepewa jukumu la kusimamia shughuli za Wizara zifuatazo:-

(a) Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto;

(b) Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; na

(c) Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ni moja kati ya Kamati tisa za Kudumu za Bunge za Kisekta ambayo kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane iliyo chini ya Kanuni ya 118 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, Kamati hii imepewa jukumu la:-

(a) Kushughulikia Bajeti ya Wizara inazozisimamia;

(b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia;

(c) Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila mwaka za Wizara hizo; na

(d)Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati; Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii imefanya utekelezaji wa majukumu yake katika mwaka 2016 kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Majukumu hayo ni kama yalivyoelezwa katika uchambuzi na utekelezaji wake katika taarifa ambayo mmepewa. Majukumu hayo ni pamoja na:-

(i) Mafunzo kwa Wajumbe wa Kamati; katika kuhakikisha Kamati inatekeleza majukumu yake ipasavyo na kwa kuzingatia kuwa Wabunge, Wajumbe wengi wa Kamati wa Bunge la Kumi na Moja walikuwa wapya ilikuwa ni muhimu kuanza utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa kupokea mafunzo katika kufahamu muundo na majukumu ya Wizara zinazosimamiwa na Kamati ambayo yaliandaliwa na Ofisi ya Bunge.

(ii) Kupokea taarifa za utendaji wa Wizara na Taasisi mbalimbali; Kamati ilipata fursa ya taarifa za utendaji wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara hizo katika mwaka 2015/2016. Kamati ilipokea taarifa za utekelezaji wa majukumu ya

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto pamoja na Taarifa ya Mfuko wa Bima wa Afya *(National Health Insurance Fund);* Taarifa ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na Taasisi iliyo chini ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu pamoja na Taarifa ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kama ilivyoelezwa kwenye taarifa ambayo mmepewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukaguzi wa miradi ya maendeleo kwa mwaka 2015/2016; Kamati ilikagua miradi mbalimbali iliyo chini ya usimamizi wa Wizara inazozisimamia ambayo ilitengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2015/2016 na ambayo taarifa yake ilikuwa hapa katika taarifa zilizowasilishwa na Kamati wakati wa uwasilishaji wa taarifa za bajeti za mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, miradi ambayo Kamati ilipata fursa ya kuitembelea kwa lengo la kufanya ukaguzi ni pamoja na mradi wa kujenga nyumba maalum kwa ajili ya kusimika mashine mpya za kisasa za kutibu saratani katika Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road,* mradi wa upanuzi wa Taasisi ya Mifupa *(MOI)* Awamu ya Tatu ambapo ni ujenzi wa jengo la ghorofa saba kwa ajili ya kutolea huduma ya uchunguzi ikiwemo *CT-Scan, MRI, X-Ray, Ultra Sound,* vyumba vya upasuaji, maabara, hifadhi ya damu, huduma za dharura za *ICU,* vyumba vya wagonjwa wanaohitaji uangalizi wa karibu na vyumba vya wagonjwa wa kulipia na kuchangia na mradi wa upanuzi wa ofisi za Bohari ya Dawa, Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili *(MUHAS),* Mloganzila na Mradi wa kutoa Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu *(Higher Learning Students Loans Board)* na mradi wa Upanuzi wa Usikivu wa Mitambo ya Shirika la Utangazaji la Tanzania *(TBC)* kule Kisarawe.

Kamati iliamua kukagua miradi hiyo kutokana na kuwa katika Miradi ya Wizara ambayo ilitengewa fedha bilioni tatu hakuna hata mmoja uliotekelezwa kwa kuwa haikutolewa fedha yoyote kutoka Serikalini. Kwa ujumla miradi karibu yote ambayo Kamati iliikagua ilikuwa na changamoto ya ucheleweshwaji au kutotolewa kabisa kwa fedha zilizotengwa hali ambayo iliathiri utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kwamba imekuwa ni kawaida kwa Serikali kutotimiza utoaji wa fedha kwa wakati katika Wizara zilizopo chini ya Kamati hii kama vielelezo vifuatavyo vya taarifa vilivyooneshwa hali ya upatikanaji wa fedha kwa kipindi cha miaka ya 2011 mpaka 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupokea, kuchambua na kujadili taarifa za utekelezaji na mpango wa bajeti kwa kipindi cha nusu mwaka; katika vikao vya Kamati vilivyofanyika kuanzia tarehe 16 hadi 18 Januari, 2017 mkoani Dodoma,

pamoja na majukumu mengine, Kamati ilipokea na kuchambua na kujadili taarifa za utekelezaji na mpango wa bajeti wa Wizara kwa ajili ya kusimamia kwa kipindi cha nusu mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipokea, kuchambua na kujadili taarifa ya utekelezaji na mpango wa bajeti ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto kwa kipindi cha nusu mwaka ambayo ilionesha kuwa ukusanyaji wa maduhuli ni wa kuridhisha kwani mpaka kufikia Desemba, 2016 Wizara ilikuwa imekusanya kiasi cha shilingi bilioni 87.6 sawa na asilimia 55.6 ya kiasi cha shilingi bilioni 157 kilichopangwa kukusanywa kwa mwaka 2016/2017. Kamati inapongeza ukusanyaji huu wa maduhuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini upatikanaji wa fedha si wa kuridhisha kwani hadi kufikia Disemba 2016, Wizara imepokea jumla ya Shilingi bilioni 251.9 sawa na asilimia 31.6 tu ya kiasi cha Shilingi bilioni 796.1 ya fedha iliyoidhinishwa kwa mwaka mzima. Aidha, kwa kiasi hicho cha fedha kilichopokelewa na Wizara, fedha za miradi ya maendeleo ilikuwa ni bilioni 106.6 sawa na asilimia 20.6 tu nikiacha kiasi cha Shilingi bilioni 518.5 kilichotengwa cha mwaka mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji huu wa kusuasua wa fedha umesababisha baadhi ya miradi muhimu ishindwe kuanza kutekelezwa kwa wakati. Miradi hiyo ni Mradi wa Kununua Vifaa Tiba katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, *MOI, KCMC* na *Ocean Road*; ujenzi wa uzio katika Kituo cha Waathirika wa Dawa za Kulevya kilichopo Itega, kukarabati Wodi ya Wagonjwa wa Afya ya Akili wa Hospitali ya Mirembe, ujenzi wa Hospitali ya Kanda ya Kusini-Mtwara na Usimikaji wa Mashine za *LINAC* katika Hospitali ya Bugando-Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Kamati ilipokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya Utekelezaji na Mpango wa Bajeti ya Wizara kwa kipindi cha mwaka 2016. Taarifa ya ukusanyaji wa maduhuli ilionesha katika kipindi cha nusu mwaka Wizara imeweza kukusanya kiasi cha Shilingi milioni 425.8 sawa na asilimia 51.9 ya Shilingi milioni 820 cha ukusanyaji wa kipindi cha mwaka mzima. Kamati inapongeza ukusanyaji huu mzuri wa maduhuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Upatikanaji wa Fedha. Wizara imepokea bilioni 8.8 kati ya bilioni 20.3 zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu ambayo ni sawa na asilimia 43 tu. Aidha, kwa upande wa miradi ya maendeleo Wizara imepokea Shilingi milioni 190 kati ya Shilingi bilioni tatu zilizotengwa ambayo ni

sawa na asilimia 6.3 tu. Hali hii inasikitisha sana kwani licha ya Wizara hii kutengewa bajeti ndogo lakini utoaji wake pia si mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kipindi cha Julai–Disemba, 2016 ilionesha kuwa kwa mwaka 2016/2017, Wizara hii ilikadiria kukusanya maduhuli ya Shilingi bilioni 327.8. Hadi kufika mwezi Disemba 2016, makusanyo ya maduhuli yalikuwa bilioni 151.3 sawa na asilimia 46. Wizara haina budi kuongeza juhudi katika ukusanyaji ili iweze kufikia lengo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2016/2017, Wizara iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu kiasi cha Shilingi trilioni 1.4. Hadi kufikia Disemba, 2016, Wizara ilikuwa imepokea Shilingi bilioni 584.4 sawa na asilimia 42. Aidha, kwa upande wa Miradi ya Maendeleo kiasi cha Shilingi bilioni 897 kiliidhinishwa na Bunge na kilichotolewa mpaka Disemba 2016 ni bilioni 341 sawa na asilimia 38 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kupokea Taarifa Mahususi; Hali ya Dawa Nchini. Katika taarifa iliyotolewa na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ilionesha kuwa hali ya upatikanaji wa Dawa nchini ni ya kuridhisha na upatikanaji wa dawa ulikuwa ni asilimia 63. Aidha, kwa dawa zile muhimu *(Essential Medicines)* ambazo ni dawa 133, dawa 85 zipo za kutosha na tarehe 27 Oktoba, 2016, ilitarajiwa shehena nyingine ya dawa kuingia. Si hivyo tu bali kila mwezi ilitarajiwa shehena ya dawa itakuwa inaingia.

Pamoja na hayo Kamati ilijulishwa kuwa Serikali imeingia Mikataba yenye thamani ya Shilingi bilioni 73 na *Suppliers* ili kuhakikisha kunakuwa na dawa za kutosha. Ilitarajiwa kuwa ifikapo Disemba, 2016, Bohari ya Dawa itakuwa na dawa asilimia 85. Pamoja na hayo, Kamati ilibaini uwepo wa deni kubwa ambalo Serikali imekuwa ikidaiwa na Bohari ya Dawa na ilikiri ni kweli deni ambalo Serikali inadaiwa ni bilioni 154.8 ambalo Serikali inajipanga kulilipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati haikukubaliana na taarifa ya Waziri kutokana na takwimu za hali ya dawa katika vituo vya afya ambazo ziliwasilishwa na Wajumbe wa Kamati kutofautiana. Waziri alipokea hoja ya Kamati na kuomba kuifanyia kazi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hatua Zilizofikiwa na Mfuko wa Bima ya Afya Katika Utoaji wa Bima ya Afya Kwa Wote *(Universal Health Coverage)*. Kamati ilielezwa kuwa Muswada wa Bima ya Afya kwa wote ulishaandaliwa na

ulitarajiwa kuwasilishwa Septemba, 2016. Hata hivyo, ulikwama kwenye Baraza la Mawaziri kutokana na mapungufu waliyoyabaini. Aidha, Kamati ilijulishwa kuwa mchakato unaenda vizuri na inategemewa mwezi Februari, 2017 Muswada huu utaletwa Bungeni. Ni matumaini ya Kamati kwamba Muswada huu upo tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utoaji na Urejeshwaji wa Mikopo Kutoka Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Utoaji na Urejeshwaji wa Mikopo ya Elimu ya Juu ambayo ilionesha kuwa urejeshwaji wa mikopo umeongezeka kutoka Shilingi milioni 53.6 mwaka 2006/2007 hadi kufikia bilioni 30 mwaka huu. Inatarajiwa kuwa mara baada ya kufanyiwa marekebisho Sheria ya Bodi ya Mikopo marejesho yataongezeka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utendaji Tume ya Vyuo Vikuu *(TCU)*. Pamoja na maelezo yaliyotolewa na *TCU*; Kamati ilibaini kwamba, *TCU* kwa kiasi kikubwa imekuwa ikifanya kazi ya udalali kutokana na utaratibu wake wa kuwapangia vyuo wanafunzi na hasa vile vya binafsi ambavyo pia vimekuwa na gharama kubwa sana, kitu ambacho Kamati imeona siyo sawa na inatoa maoni yake katika taarifa hii. Maelezo ya kina ya taarifa hizi na mahususi yapo kwenye taarifa ambayo Wabunge wote mmegawiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Miswada na Mikataba ya Kimataifa. Katika kipindi cha Januari, 2016 hadi Januari, 2017, Kamati imejadili na kuchambua jumla ya Miswada ya Sheria minne na Azimio moja kama inavyoonesha katika taarifa ambayo Wabunge mmegawiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Semina kwa Wajumbe. Kamati imefawanyia Wabunge wote semina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tatu; Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati; Maoni ya Jumla. Kama ambavyo imeelezwa ndani ya Taarifa hii, changamoto kubwa ambayo imekuwa ikizikumba Wizara zilizo chini ya Usimamizi wa Kamati hii ni utolewaji wa fedha usioridhisha. Kamati inatambua umuhimu wa kila sekta hapa nchini, lakini Sekta ya Elimu na Afya ni msingi mkuu wa sekta nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa mnamo Mwaka 2000, Umoja wa Mataifa kupitia *World Summit* iliyofanyika Brazil ilikuja na Malengo ya Millenia *(Millennium Development Goals–MDG's)* kwa lengo la kupunguza umaskini ambayo kilele chake kilikuwa mwaka 2015. Baada ya kilele chake, mwaka 2015, *UN* ilikuja na malengo 17 endelevu ya maendeleo *(Sustainable*

*Development Goals)* na kukubaliana kwamba yawe yametekelezwa ifikapo mwaka 2030. Katika Malengo hayo malengo matatu yanazihusu sekta ambazo zipo chini ya usimamizi wa Kamati hii ambayo ni:-

Lengo namba 2 *(Good health and wellbeing),* lengo namba 3 *(Quality education)* na lengo namba 4 *(Achieve gender equality and empower all women and girls)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kuwa *UN* imetambua kuwa ili kufikia maendeleo endelevu ni lazima kuwekeza kwenye sekta hizi kwa kutenga bajeti za kutosha. Kamati inaishauri Serikali kuziangalia Wizara hizi kwa jicho la pekee na kuhakikisha kinachotengwa na Bunge kinatolewa chote na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfumo wa Ugatuaji Madaraka *(D by D)*. Mfumo wa Ugatuaji Madaraka umesababisha Wizara zote zinazosimamiwa na Kamati hii kukosa mamlaka ya kuwafuatilia kwa karibu ikiwa ni pamoja na kuwachukulia hatua mbalimbali Watendaji walioko chini ya Wizara husika pale ambapo inabainika wamekwenda kinyume na taratibu na hivyo kupunguza ufanisi katika Wizara hizo. Kwa mfano, Waganga, Wauguzi, Walimu, Maafisa Michezo, Maafisa Maendeleo ya Jamii wote wako chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaona ni vyema ukaandaliwa mfumo bora wa mawasiliano na ushirikiano kati ya Wizara na TAMISEMI na ikibidi kuwepo na msimamizi mmoja tu. Aidha, kuna umuhimu wa Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii na Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa-TAMISEMI kufanya vikao vya Kamati kwa pamoja linapotokea hitaji la kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Katika Wizara hii Kamati inatoa maoni na ushauri na mapendekezo yafuatayo:-

(a) Bohari ya Dawa; Bohari ya dawa licha ya umuhimu wake wa kuwa ndiyo inayotegemewa katika suala zima la uagizaji na usambazaji wa dawa nchini, lakini bado imekuwa ikitengewa bajeti ndogo ambayo haikidhi mahitaji yake na hivyo kuathiri hali ya upatikanaji wa dawa nchini.

(b) Kamati inashauri *MSD* iwe na fungu lake *(Separate vote)* kwani mahitaji yake ni makubwa sana na kutapunguza malimbikizo ya madeni yanayosababishwa na Serikali.

(c) Kamati imebaini kuwa changamoto nyingine ambayo *MSD* inakumbana nayo ni madeni makubwa inayozidai Halmashauri mbalimbali hali ambayo inaifanya ishindwe kuagiza dawa za kutosha na kwa wakati. Kamati inashauri kwa zile Halmashauri ambazo zinadaiwa zimewekewa utaratibu wa kuwa zinakatwa kiasi kidogo pale zinapoagiza dawa kupitia fedha za Serikali ili kupunguza deni hilo.

(d) Pamoja na kauli ya Serikali kuwa upatikanaji wa dawa nchini upo wa kuridhisha, kiuhalisia hali ya upatikanaji wa dawa katika maeneo mengi si ya kuridhisha. Ukosefu huu wa dawa unahatarisha maisha ya wananchi wengi ambao wengi ni maskini. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha bidhaa hii muhimu kwa maisha ya wanadamu inakuwepo wakati wote kwani uwepo wa dawa maana yake wananchi wanapata dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahatma Gandhi aliwahi kusema *"It is health that is real wealth and not pieces of gold and silver"* akimaanisha kwamba "Afya ndiyo utajiri wa kweli siyo dhahabu wala shaba". Hivyo basi hatuna budi kuhakikisha afya ya Watanzania ndicho kipaumbele chetu cha kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango iandaliwe ili kuwezesha mfumo wa ugawaji wa dawa uwe wa kielektroniki *(Computerized)* ambapo kila siku asubuhi ijulikane dawa zilizopo kwenye kituo cha afya, hospitali ili kumsaidia na kumwezesha Daktari kuwaandikia wagonjwa dawa zilizopo kituoni ili hospitali kupunguza malalamiko na kuishiwa kwa dawa wakati dawa mbadala zipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Bima ya Afya. Kamati imebaini kwamba pamoja na Mfuko huu wa Bima ya Afya kuwakata fedha kwa ajili ya matibabu wanachama wake, Bima ya Afya imekuwa na utaratibu wa kuchagua baadhi ya magonjwa kwa ajili ya kugharamia matibabu yake na kuacha baadhi yakiwemo magonjwa yanayohusiana na upasuaji wa moyo. Kamati inashauri *NHIF* kuboresha Bima hii ili iweze kugharamia magonjwa yote, lakini pia iweze kukubaliwa katika hospitali zote nchini. Ifike mahali mtu mwenye kadi ya *NHIF* ajisikie fahari kuwa nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatambua nia nzuri ya Serikali kuleta mpango wa Bima ya afya kwa wote *(Universal Health Coverage),* hata hivyo haiwezekani kutunga Sheria bila ya kuwa na Sera. Kamati inashauri Serikali kuanza kuandaa sera kwa ajili ya kusimamia suala hili ili baadaye mchakato wa utungaji wa Sheria nao ufuate.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete inafanya kazi kubwa ambayo kwa kiasi kikubwa imesaidia kupunguza gharama kubwa ambazo nchi ilikuwa inaingia katika kutibu wagonjwa wa moyo. Hata hivyo, Taasisi hii imekuwa haipatiwi fedha za kutosha za utekelezaji wa majukumu yake. Kwa mfano, katika kipindi cha nusu ya mwaka Taasisi hii imepata asilimia 12.5 tu ya bajeti yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha inaipa kipaumbele cha pekee Taasisi hii kwa kuitengea fedha za kutosha, lakini pia zitolewe kwa wakati ili iweze kusaidia kupunguza gharama ambazo Serikali imekuwa ikiingia katika kupeleka wagonjwa nchini India.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road*; Ugonjwa wa Saratani umekuwa tishio hapa nchini kutokana na kuongezeka kwa wagonjwa. Pamoja na kasi ya kusambaa kwa ugonjwa huu, kuna changamoto ya vifaa ambapo vingi ni chakavu, uhaba wa dawa ambazo ni ghali sana na ukosefu wa vifaa vya kupimia saratani katika Hospitali za Mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto hizi zimepelekea wagonjwa wengi kupoteza maisha wakati wakisubiri matibabu ikiwemo vipimo na wengine kukosa dawa kabisa. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inaongeza bajeti ya hospitali hii ili iweze kuwa na vifaa vingi na vya kisasa pia kuhakikisha Hospitali za Mikoa zinapatiwa wataalam na vifaa ili kupunguza msongamano katika Hospitali ya *Ocean Road.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mafunzo ya Juu ya Wataalam wa Afya Wabobezi *(Specialists)*. Nchi yetu inakumbana na uhaba wa wataalam wa afya wenye ubobezi kwenye fani mbalimbali *(Specialists)*. Kamati inashauri Serikali kuanza kusomesha wataalam hawa ili kuhakikisha katika kila Hospitali ya Mkoa kunakuwepo wataalam wa aina hii kama Daktari wa akinamama, watoto na magonjwa ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukatili wa Kijinsia. Matendo ya ukatili wa kijinsia yameendelea kukua hali inayohatarisha maisha ya wananchi hususan wanawake na watoto. Hivi karibuni kumetokea tukio la mwanamke kuchapwa mbele ya hadhara ya wanawake na wanaume Mkoani Mara kitendo ambacho ni ukatili wa kijinsia. Kamati inashauri Serikali ichukue hatua kali kwa wale wote wanaobainika kujihusisha na vitendo hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makazi ya Wazee. Wazee ni kundi ambalo limesahaulika licha ya kuwa ndilo lilileta ukombozi wa nchi hii. Wazee pamoja na umuhimu wa kujengewa makazi lakini makazi yao yamekuwa na hali mbaya sana. Kamati inashauri Serikali itenge fedha za kutosha kwa ajili ya kujenga makazi ya wazee nchini kuhakikisha wanawekewa huduma zote muhimu zikiwemo maji, afya na matunzo ya kisaikolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria Mbalimbali. Kumekuwepo na baadhi ya sheria kandamizi kama vile Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 ambayo Kamati inaishauri Serikali iharakishe na kukamilisha mchakato wa marekebisho ya sheria hii. Sambamba na hilo Kamati inashauri Serikali iharakishe mchakato wa utungaji wa Sheria ya Wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Wizara ya Habari na taasisi zake zinakumbana na changamoto mbalimbali ambazo Kamati inapenda kuzitolea maoni, ushauri na mapendekezo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TBC*. Kilio kikubwa cha *TBC* ni uhaba wa fedha kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake, miundombinu mibovu na uchakavu wa vifaa ambayo imesababisha washindwe kusikika kwenye masafa ya redio katika baadhi ya mikoa na wilaya 81. Licha ya kuwa ndiyo Shirika pekee la Utangazaji linalomilikiwa na Serikali, Kamati inaishauri Serikali ilipe Shirika hili hadhi yake kwa kulitengea fedha za kutosha ili kutekeleza majukumu yake ipasavyo ikiwemo Miradi ya Maendeleo; hususan uwekezaji kwani Sekta ya Habari inahitaji uwekezaji wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Michezo. Kamati inatambua umuhimu wa michezo, lakini hakuna mitaala ya michezo katika shule hapa nchini hali ambayo imekuwa ikidumaza kiwango cha michezo. Kamati inaishauri Serikali kuandaa mitaala ya michezo ili kuinua kiwango cha michezo na kukuza vipaji. Sambamba na hili, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutekeleza mapema ushauri wa Kamati wa kutenga shule za michezo, lakini ni lazima kuzipatia fedha za kutosha ili kuweza kufikia malengo ya kukuza vipaji vya vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera na sheria mbalimbali za masuala ya michezo. Kamati imebaini kuwa sera na sheria zinazohusu michezo zimepitwa na wakati zinahitaji kurekebishwa ili ziweze kuendana na wakati, mfano Sera ya Maendeleo ya Michezo ya Mwaka 1995 ambapo mambo mengi yamekwishabadilika. Kamati inashauri Serikali ikamilishe mchakato wa mapitio ya sera na sheria hizo mapema ili kuendana na wakati tulionao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kazi za Wasanii. Wizara ihakikishe kwamba unaandaliwa utaratibu wa wazi utakaowezesha kulinda kazi za wasanii kwani kumekuwepo na wizi wa waziwazi wa kazi za wasanii hali ambayo pia inapelekea kutopata faida ya jasho la kazi zao na hatimaye kukosesha mapato Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Wizara hii pamoja na Taasisi zake inakumbana na changamoto mbalimbali ambazo Kamati inapenda kuzitolea maoni, ushauri na mapendekezo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu. Fedha za Miradi ya Maendeleo za Wizara zitenganishwe na fedha za Bodi ya Mikopo kwa ajili ya wanafunzi wa elimu ya juu ili kubainisha kiasi halisi kinachotengwa kwa ajili ya maendeleo ya elimu na kwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bodi iweke mkakati madhubuti wa kuhakikisha inaongeza kiwango cha marejesho ya mikopo kwani wanufaika wengi wanajulikana walipo. Hii itasaidia kutoa mikopo kwa wengine baada ya kupata marejesho hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Vyuo Vikuu *(TCU)*. Kamati imebaini kuwa *(TCU)* imekuwa na utaratibu wa kuwapangia wanafunzi vyuo vya kwenda na hususan vile vya binafsi. Kamati inashauri utaratibu huu uachwe na badala yake wanafunzi waombe wao wenyewe moja kwa moja katika vyuo husika, kwani *TCU* imekuwa ikifanya kazi ya uwakala wa vyuo binafsi na vyuo hivi vimekuwa vikitoa elimu kwa gharama kubwa sana na kulazimika kuwalipia wanafunzi hao kwa kupitia Bodi ya Mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatambua jukumu kuu la *TCU* ni kusimamia ubora wa elimu katika vyuo vikuu nchini na hivyo Kamati inaendelea kusisitiza kwa kuishauri *TCU* kufanya jukumu lake la msingi la kuangalia ubora wa elimu inayotolewa nchini na hivyo TCU iachane na utaratibu wake wa sasa ambapo imejikita zaidi katika kufanya udahili wakati hiyo si kazi yao. Kazi ya udahili ifanywe na vyuo husika kulingana na vigezo vya chuo hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Kufundishia ya Mloganzila. Kamati inatambua umuhimu wa Hospitali ya Kufundishia ya Mloganzila katika harakati za kuongeza wataalam wa afya nchini. Serikali imewekeza fedha nyingi sana katika ujenzi wa hospitali hiyo, hivyo ni muhimu ikatoa matokeo yanayotarajiwa. Hata hivyo Kamati inapata mashaka kuhusu upatikanaji wa rasilimali watu na

vifaa tiba kwani mahitaji halisi ya hospitali ni watumishi 950 na mpaka sasa ina watumishi 50 tu ambao ndio wenye uhakika wa kupatikana na kwenda kufanya kazi katika hospitali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali ijipange ili kuhakikisha kuwa kunapatikana rasilimali watu wa kutosha na wenye vigezo mbalimbali kupitia mfumo sahihi badala ya kuokoteza tu; pamoja na vifaa tiba. Aidha, kwa kuanzia Serikali ifanye ushirikiano na nchi wahisani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela. Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela ni jukumu la kutoa elimu na mafunzo katika ngazi ya uzamili na uzamivu pamoja na kufanya utafiti katika ngazi za ubobezi. Taasisi hii tayari imefanya utafiti kwa ajili ya kuanzisha Kituo cha Ithibati *(centre of excellence)* katika Bara la Afrika kwa ajili ya kujibu changamoto na matatizo ya Afrika katika nyanja ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Kamati imebaini kuwa Chuo kimejikita zaidi katika kutoa elimu kama vilivyo vyuo vingine. Kamati inaona kuwa Taasisi ya Nelson Mandela inapaswa kuwa kama *Sillicon Valley,* ambalo ni makao makuu ya makampuni yenye teknolojia huko Marekani kwa ajili ya kutotoa (kuzalisha) teknolojia. Kitendo cha kuwepo eneo moja maalum la utafiti na ugunduzi wa sayansi na teknolojia pamoja na makampuni na viwanda kumesaidia kuzalisha watafiti wengi na vituo vya teknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri na inaona ni wakati sasa Taasisi hii kujikita zaidi katika kufanya utafiti na kuzalisha wataalam wengi zaidi ili kuweza kuwa *Silicon Valley* ya Tanzania na Afrika. Kwa ujumla na hiyo yatawezekana endapo tu, Serikali itaamua kuwekeza ipasavyo na kujenga Maabara za kutosha za utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madeni ya walimu tunaomba nayo pia yalipwe, mfumo wa elimu Tanzania tunaomba uangaliwe kwa uangalifu sana, shule binafsi tunaomba zisimamiwe vizuri sana, Tuzo za Udhamini *(Schoralship Awards)* ili kuweza kutoa *schorlaship*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inarudia ushauri wake ilioutoa wakati wa taarifa ya Bajeti ya Wizara ya Elimu juu ya umuhimu wa kutoa tuzo za udhamini kwa kuwapeleka katika vyuo bora duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uainishaji wa Vyuo Vikuu *(University Classification);* kwa sababu ya muda najua tumesambaza ripoti hii naomba kama ilivyo kwenye vitabu ichukuliwe yote kwa sababu hapa tumefanya *summary*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kwa kipekee naomba kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas D. Kashililah; Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndugu Athuman B. Hussein; na Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati hii Ndugu Dickson M. Bisile pamoja na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Pamela E. Pallangyo na Ndugu Agnes F. Nkwera pamoja na Msaidizi wao Gaitana Chima kwa kuratibu vyema bila kuchoka shughuli za Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuelezea shughuli zilizotekelezwa, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli za Kamati, maoni na mapendekezo mbele ya Bunge lako Tukufu, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, pamoja na maoni, ushauri na mapendekezo yaliyomo katika taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, ahsante. Hoja imeungwa mkono na watu wengi.

# TAARIFA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII KUANZIA JANUARI, 2016 HADI JANUARI 2017 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

---

## *SEHEMU YA KWANZA*

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kukushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Mwaka ya shughuli zilizotekelezwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii katika kipindi cha 2016/2017.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu nne (4). Sehemu ya kwanza inaelezea maelezo ya jumla, sehemu ya pili inahusu Uchambuzi na matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati, sehemu ya tatu imebainisha Maoni na Mapendekezo ya Kamati na sehemu ya nne ni Hitimisho la taarifa hii.

### 1.1 Muundo na Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Nyongeza ya nane 5 (5) iliyo chini ya Kanuni ya 118 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, imepewa jukumu la kusimamia shughuli za Wizara zifuatazo:-

a) Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto;
b) Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; na
c) Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

**Mheshimiwa Spika**, Aidha, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ni moja kati ya Kamati tisa (9) za Kudumu za Bunge za Kisekta ambayo kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane 7 (1) iliyo chini ya Kanuni ya 118 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, Kamati hii imepewa jukumu la:-

a) Kushughulikia Bajeti ya Wizara inazozisimamia;
b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia;
c) Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila Mwaka za Wizara hizo na;

d) Kufuatilia utekelezaji wa Majukumu ya Wizara hizo.

## 1.2 Utaratibu uliotumika kutekeleza Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha Kamati inatekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitumia utaratibu ufuatao:-

a) Kufanya vikao na Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara hizo kwa kuziomba kufika mbele ya Kamati ili kutoa Taarifa juu ya jambo au suala mahsusi ambalo Kamati ilipenda kupata taarifa zake kutoka kwa Watendaji wa Wizara na Taasisi hizo.

b) Kufanya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 ili kuweza kuona thamani ya miradi hiyo (***Value for Money***), hili lilifanyika kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016.

c) Kufanya mikutano na Wadau kwa lengo la kupokea maoni yao juu ya Masuala mbalimbali ambayo Kamati ilikuwa inayafanyia kazi ikiwemo Miswada ya Sheria na Maazimio.

## 1.3 Shughuli zilizotekelezwa na Kamati

**Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha kuna kuwa na usimamizi wa kutosha wa majukumu yake kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, katika kipindi cha Januari 2016 hadi Januari 2017, Kamati ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

i) Kupokea Mafunzo;
ii) Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa za Utendaji wa Wizara na Taasisi zake;
iii) Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo;
iv) Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Bajeti za Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016;
v) Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 na mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017
vi) Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa za Utendaji wa Wizara kwa kipindi cha nusu Mwaka (Julai – Disemba 2016)

vii) Kupokea Taarifa Mahsusi;
viii) Uchambuzi wa Miswada ya Sheria na Mikataba ya Kimataifa;na
ix) Kupokea Semina mbalimbali

***SEHEMU YA PILI***

## 2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI

### 2.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, imefanya utekelezaji wa majukumu yake katika Mwaka 2016 kupitia mbinu, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 kama ilivyoelezwa hapo awali. Majukumu hayo ni kama yalivyoelezwa ambayo pia Kamati itaeleza Uchambuzi wa utekelezaji wake katika Taarifa hii.

### 2.2 Utekelezaji wa Shughuli za Kamati

**Mheshimiwa Spika,** Katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa kipindi cha mwaka 2016 shughuli zifuatazo zilitekelezwa:-

#### 2.2.1 Mafunzo kwa Wajumbe wa Kamati

**Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha Kamati inatekeleza majukumu yake ipasavyo na kwa kuzingatia kuwa Wabunge (Wajumbe) wengi wa Kamati wa Bunge la 11 walikuwa wapya ilikuwa ni muhimu kuanza utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa kuwapatia mafunzo Wajumbe wake ambayo yaliandaliwa na Ofisi ya Bunge. Mafunzo hayo yalifanyika kuanzia tarehe 8 hadi 12 Februari 2016 katika Ukumbi uliopo Jengo la LAPF Kijitonyama, Jijini Dar es Salaam. **Mafunzo yalikuwa na faida kwani yaliwawezesha Wajumbe kufahamu muundo na majukumu yao kama Wabunge na kama Wajumbe wa Kamati.**

#### 2.2.2 Kupokea Taarifa za Utendaji wa Wizara na Taasisi mbalimbali

**Mheshimiwa Spika**, Mnamo tarehe 14 Machi hadi 15 Aprili, 2016, Wajumbe walipokea Taarifa za Utendaji wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara hizo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016. Kamati ilipokea taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto pamoja na Taarifa ya Mfuko wa Taifa wa Bima wa Afya (**National Health Insurance Fund**); Taarifa ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na taasisi iliyo chini yake ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (**Higher Learning Student's Loan Board**); pamoja na Taarifa ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

**a) Taarifa za Utendaji wa Wizara**

**i) Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea Taarifa ya Utendaji wa Wizara hii ambayo ilionesha kuwa hadi kufikia mwezi Machi 2016 wakati Kamati inapokea taarifa hiyo, Wizara ilikuwa imepokea **asilimia 30.5 tu** ya bajeti nzima kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. **Hali hii iliisikitisha Kamati kwani kiasi cha fedha kilichotolewa kisingewezesha Wizara kutekeleza majukumu yake ipasavyo.** Aidha, Kamati ilipokea taarifa ya makusanyo ya maduhuli ya Wizara ambayo ilionesha hadi kufikia Mwezi Februari 2016, makusanyo yalikuwa ni sawa na **asilimia 94.4** ya lengo. **Kamati inaipongeza Wizara kwa ukusanyaji huo mzuri wa kuweza kufikia lengo kwa mwenendo wa makusanyo hayo.**

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ilitoa taarifa kuhusu changamoto mbalimbali zinazoikabili katika utendaji kazi wake, ikiwemo:- **kutotolewa kwa wakati fedha za utekelezaji wa majukumu yake zikiwemo fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo hali inayopelekea miradi mingi kuchelewa kutekelezwa, kuwepo kwa madeni ambayo hayajalipwa kwa wakandarasi pamoja na watoa huduma katika Wizara na Taasisi zake, ongezeko la idadi ya watu wanaohitaji huduma katika Ustawi wa jamii wakiwemo wazee, watoto yatima na watu wenye ulemavu, kupungua kwa fedha kutoka kwa wadau wengine wa maendeleo hasa wa nje ya nchi pamoja na upungufu wa Rasilimali watu katika vituo vya kutolea huduma za Afya nchini.**

**ii) Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

**Mheshimiwa Spika**, taarifa ya utendaji wa Wizara hii ilionesha kuwa hadi kufikia mwezi Februari 2016, ni **asilimia 55.3** ya bajeti nzima ya Wizara ndiyo iliyokuwa imepokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Matarajio ya Kamati yalikuwa hadi kufikia mwezi Februari 2016 angalau Wizara ingekuwa imepata **asilimia 70** ya bajeti yake yote.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ilieleza mafaniko yao ikiwa ni pamoja na kukamilisha **Waraka wa Elimu Na.5 wa Mwaka 2015** wa utoaji wa elimu ya msingi na sekondari za umma bila malipo na kuondoa michango yote katika shule hizo na kuusambaza katika shule ambao ulianza kutekelezwa mara moja. Kamati inaipongeza Serikali kwa kukamilisha ahadi hiyo ya elimu bila malipo kwa watoto wa kitanzania kwani imepelekea watoto wengi kupata fursa ya kwenda shule hata kwa familia ambazo zina uwezo duni wa kifedha. **Kamati inaona kuna umuhimu wa Serikali kuendelea kusimamia waraka huo na kuhahakikisha inaimarisha miundombinu katika shule hizo ili kuwawezesha watoto hao kupata elimu iliyo bora ambayo ndiyo mwanga na ufunguo wa maisha yao.**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio mengi yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii, Kamati ilielezwa changamoto mbalimbali kama vile za **ucheleweshewaji wa fedha walizotengewa, uhaba wa walimu wa hisabati, Sayansi, ufundi na lugha, upatikanaji wa miundombinu kwa ajili ya elimu kwa wote hususani watu wenye ulemavu wa aina zote, uhaba wa mafundi sanifu wa maabara za sayansi na wasimamizi wa karakana za ufundi.**

**iii) Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo**

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Februari 2016, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ilikuwa imepokea **asilimia 45** tu ya bajeti nzima iliyotengewa kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016. Pamoja na utekelezaji wa majukumu mengine mengi, Wizara ilitekeleza ujenzi wa ofisi ya BAKITA, Ujenzi wa Ukumbi wa wazi wa maonesho ya Sanaa, Upanuzi wa Masafa ya Usikivu-TBC.

**b) Taarifa za Utendaji wa Taasisi**

**i) Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea Taarifa ya Utendaji wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ambayo ilionesha kuwa kumekuwa na ongezeko la wateja wa Bima ya Afya kwani hadi kufikia Februari 2016 ilikuwa imefanikiwa kuwasajili **asilimia 27 tu** ya Watanzania. Mfuko wa Bima ya Afya unaendelea na utaratibu wa maboresho ya Huduma zao kwa kuhakikisha kila mwananchi wa Tanzania anakuwa katika Bima ya Afya ambayo itakuwa ya uhakika.

**ii) Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea Taarifa ya Utendaji wa Bodi ya Mikopo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 ambayo ilionesha kuwa idadi ya wanufaika wa mikopo imeongezeka kutoka wanafunzi **42,729** Mwaka **2005/2006** hadi wanafunzi **123,798** Mwaka **2015/2016** sawa na ongezeko la **asilimia 189.7**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Kamati ilielezwa pia kuhusu changamoto ya mwitikio mdogo wa urejeshwaji wa mikopo ambapo wanafunzi wengi wanaona fedha walizokopeshwa ni kama walipewa (**Hisani**) na hivyo kuwa wagumu kurejesha. Hali hii imekuwa ikiathiri utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wengine kwani takwimu zinaonesha kuwa marejesho ambayo yameiva na yanapaswa kurejeshwa ni **shilingi bilioni 258** na tayari Bodi imekwisha kusanya kiasi cha **shilingi bilioni 91** sawa na **asilimia 35 tu.**

**2.2.3 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikagua Miradi mbalimbali iliyo chini ya usimamizi wa Wizara inazozisimamia ambayo ilitengewa fedha katika Mwaka

wa Fedha 2015/2016 na ambayo Taarifa ilikuwemo kwenye Taarifa zilizowasilishwa na Kamati wakati wa uwasilishaji wa Taarifa za Bajeti za Mwaka wa Fedha 2016/2017. Ukaguzi wa Miradi hii ulifanyika kwa mujibu wa Kanuni ya 97 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

**Mheshimiwa Spika,** miradi ambayo Kamati ilipata fursa ya kuitembelea kwa lengo la kufanya ukaguzi ni pamoja na iliyopo chini ya:-

**a) Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto**

Katika Wizara hii, Kamati ilifanya ukaguzi wa **Miradi mitatu (3)** ambayo ni:- Mradi wa kujenga vyumba maalumu (Bunkers) kwa ajili ya kusimika mashine mpya za kisasa za kutibu Saratani katika Taasisi ya Saratani ya ***Ocean Road***; Mradi wa upanuzi wa Taasisi ya Mifupa (MOI) awamu ya III ambao ni ujenzi wa jengo la ghorofa saba (7) kwa ajili ya kutolea huduma ya uchunguzi ikiwemo *CT-Scan, MRI, X-Ray, Ultra Sound,* vyumba vya upasuaji, maabara, hifadhi ya damu, huduma za dharura, ICU, vyumba vya wagonjwa wanaohitaji uangalizi wa karibu na vyumba vya wagonjwa wa kulipia na kuchangia; na Mradi wa upanuzi wa ofisi za Bohari ya Dawa.

**b) Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

Katika Wizara hii, Kamati ilifanya ukaguzi wa **miradi miwili** (**2**) ambayo ni Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili (MUHAS)- Mloganzila na Mradi wa kutoa Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu (***Higher Learning Students Loan Board)***.

**c) Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo**


Katika Wizara hii, Kamati ilikagua Mradi mmoja wa Upanuzi wa Usikivu wa Mitambo ya Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC) wa Kisarawe ambao nao haukuhusisha fedha za Serikali. Kamati iliamua kukagua mradi huo kutokana na kuwa katika Miradi ya Wizara ambayo ilitengewa fedha (**kiasi cha shilingi bilioni 3**) hakuna hata mmoja uliotekelezwa kwa kuwa haikutolewa fedha yoyote kutoka Serikalini.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla Miradi karibu yote ambayo Kamati iliikagua ilikuwa na changamoto ya ucheleweshwaji au kutotolewa kabisa kwa fedha zilizotengwa hali ambayo iliathiri utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba, imekuwa ni kawaida kwa Serikali kutotimiza utoaji wa fedha zinazotengwa kwenda kwa wakati katika Wizara zilizopo chini ya Kamati hii kama vielelezo vifuatavyo vinaonesha hali ya upatikanaji wa fedha kwa kipindi cha Miaka 5 (2011/2012- 2015/2016.

| MCHANGANUO WA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO YA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO KWA KIPINDI CHA MIAKA 5 (2011/2012 - 2015/2016) | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Na** | **MWAKA** | **BAJETI** | **KIASI KILICHOPOKELEWA** | **%** |
| 1 | 2011/12 | 4,480,851,000 | 3,600,000,000 | 80.3 |
| 2 | 2012/13 | 3,055,596,335 | 2,698,966,000 | 88.3 |
| 3 | 2013/14 | 12,700,000,000 | 8,327,500,000 | 65.6 |
| 4 | 2014/15 | 16,850,000,000 | 9,000,000,000 | 53.4 |
| 5 | 2015/16 | 3,000,000,000 | 1,800,000,000 | 60.0 |

***Chanzo: Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo***




**MCHANGANUO WA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO YA WIZARA YA ELIMU,**

| SAYANSI NA TEKNOLOJIA KWA KIPINDI CHA MIAKA 5 (2011/2012 - 2015/2016) | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Na** | **MWAKA** | **BAJETI** | **KIASI KILICHOPOKELEWA** | **%** |
| **1** | **2011/12** | **135,518,096,000** | **120,180,954,633** | **88.7** |
| **2** | **2012/13** | **92,581,317,000** | **59,510,044,937** | **64.3** |
| **3** | **2013/14** | **72,598,051,000** | **47,887,451,490** | **66.0** |
| **4** | **2014/15** | **453,613,333,000** | **359,543,290,904** | **79.3** |
| **5** | **2015/16** | **582,670,597,888** | **492,753,160,996** | **84.6** |

***Chanzo: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia***

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwenendo huu wa upatikanaji wa fedha kwa muda wa miaka mitano (5), kama vielelzo vinavyoonesha, Kamati inaona kwamba utekelezaji wa Miradi hiyo ya maendeleo inategemea sana upatikanaji wa fedha hasa zilizotengwa na kupitishwa na Bunge lako Tukufu zinakwenda katika Wizara husika na kwa kiasi ambacho kimepangwa, kwa kufanya hivyo Wizara itaweza kutekeleza majukumu yake kwa wakati na maendeleo hayo kuonekana kwa wakati pia. Kamati inaiomba Serikali kuendelea kutekeleza majukumu ya upelekaji wa fedha kwa wakati kama ambavyo ni matarajio ya walio wengi.

### 2.2.4 Kupokea na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni na wa Fedha wa 2015/2016 na mchakato wa Bajeti za Wizara hizo kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/2017

**Mheshimiwa Spika**, mara baada ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa mujibu wa Kanuni, Kamati ilichambua Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Bajeti za Wizara inazozisimamia kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hizo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Taarifa hizo ziliwasilishwa Bungeni kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) Toleo la Januari, 2016, tarehe tofauti mnamo mwezi Mei, 2016.

**Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa Bajeti imekuwa ni chagamoto kwani Wizara karibu zote zimekuwa hazipewi fedha kama zilivyoidhinishwa na Bunge** kama inavyoelezwa hapa chini:-

**a) Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee wa Watoto**

Kamati iliridhishwa na Utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati. Hata hivyo, mpaka Kamati inapokea Taarifa mwezi Machi 2016, hata nusu ya Bajeti ilikuwa haijatolewa. Kwa **Fungu 52 (Idara Kuu Afya)** kiasi kilichotengwa kilikuwa ni shilingi **780,740,723,000/=** lakini kilichopokelewa kilikuwa ni **shilingi 238,685,499,908/=** sawa na **asilimia 31 tu.** Aidha, **Fungu 53 (Idara Kuu Maendeleo ya Jamii)** kiasi kilichoidhinishwa ni **shilingi 27,501,007,000/=** na kilichopokelewa ni shilingi **8,576,148,561/=** ambayo sawa na **asilimia 31. 2 tu.**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na hayo Kamati ilichambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 na kutoa maoni yake ambayo yaliwasilishwa Bungeni tarehe 11 Mei, 2016.

**b) Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo**

Taarifa ya utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati ilikuwa ya kuridhisha. Utendaji wa Wizara ulikuwa wa kusuasua kutokana na changamtoto ya Bajeti kwani hadi Kamati inakutana na Wizara ilikuwa imepokea **asilimia 50 tu** ya Bajeti na fedha za kutekeleza Miradi ya Maendeleo kilikuwa hakijatolewa kama ilivyoelezwa awali. Kuhusu Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, Kamati ilifanya ulinganisho wa Bajeti ya Wizara pamoja na ile ya Bajeti Kuu ya Taifa. Katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kuwa Bajeti inayoombwa kwa Mwaka huu ni sawa na **asilimia 0.09** ya Bajeti Kuu ya Taifa ya shilingi **23,847,987,319,085/=** ambayo pia ni pungufu kwani katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 Bajeti ya Wizara ilikuwa ni sawa na **asilimia 0.14** ya Bajeti Kuu ya Serikali. Kamati haikupendezwa na hali hii kwani ilitaraji pale ambapo Bajeti Kuu inapoongezeka basi hata Bajeti ya Wizara hii nayo ingeongezwa hususan fedha ya Miradi ya Maendeleo.

**c) Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea Taarifa ya utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati ya Mwaka wa Fedha 2015/2016 ambapo ilibaini yapo baadhi ya maeneo ambayo hajatekelezwa ipasavyo ambapo Kamati iliendelea kuyasisitiza katika Taarifa yake ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 iliyowasilishwa Bungeni tarehe 26 Mei, 2016. Kamati pia ilipokea Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016. Kamati ilibaini kuwa hadi kufikia robo ya tatu ya Mwaka yaani Machi 2016, Wizara ilikuwa imepokea kiasi cha shilingi **316,402,868,828/=** sawa na **asilimia**

**61.8** tu. Aidha, kuhusu Bajeti ya Maendeleo, Kamati ilibaini kuwa katika robo tatu ya Mwaka wa Fedha, Wizara imepokea jumla ya shilingi 360,922,754,359.61 sawa na **asilimia 61.9** ya fedha iliyoidhinishwa 582,670,597,884.49. Kamati imebaini kuwa kiasi hiki cha fedha kisichokidhi mahitaji ni moja ya sababu ya kutotekelezwa kwa Miradi ya Maendeleo ipasavyo.


### 2.2.5 Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa za Utekelezaji na Mpango wa Bajeti kwa kipindi cha Nusu Mwaka (Julai – Disemba 2016)

**Mheshimiwa Spika**, katika vikao vya Kamati vilivyofanyika kuanzia tarehe 16 hadi 28 Januari, 2017 Mkoani Dodoma, pamoja na majukumu mengine, Kamati ilipokea, kuchambua na kujadili Taarifa za Utekelezaji na Mpango wa Bajeti kwa kipindi cha nusu Mwaka Julai – Disemba kama ifuatavyo:-

#### a) Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto

**Mheshimiwa Spika,** katika kikao chake kilichofanyika tarehe 21 Januari, 2017, Kamati ilipokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya Utekelezaji na Mpango wa Bajeti ya Wizara kwa kipindi cha nusu Mwaka (Julai – Disemba 2016) ambayo ilionesha kuwa ukusanyaji wa maduhuli ni wa kuridhisha kwani mpaka kufikia Disemba 2016, Wizara ilikuwa imekusanya kiasi cha shilingi **87,600,975,103/=** sawa na **asilimia 55.6** ya kiasi cha shilingi **157,504,060,366/=** kilichopangwa kukusanywa kwa mwaka wa Fedh 2016/2017.

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu upatikanaji wa fedha, Kamati imebaini siyo wa kuridhisha kwani hadi kufikia Disemba 2016, Wizara imepokea kiasi cha shilingi **251,909,023,832/=** sawa na **asilimia 31.6 tu** ya kiasi cha shilingi **796,115,856,780/=** ya fedha iliyoidhinishwa kwa mwaka mzima. Aidha, kati ya kiasi hicho cha fedha kilichopokelewa na Wizara, fedha za Miradi ya Maendeleo ni shilingi **106,608,597,155/=** sawa na **asilimia 20.6** tu ya kiasi cha shilingi **518,511,683,780/=** kilichotengwa kwa mwaka mzima. Upatikanaji huu wa kusuasua wa fedha umesababisha baadhi ya miradi muhimu ishindwe kuanza kutekelezwa kama Mradi wa kununua vifaa tiba katika hospitali ya Taifa ya Muhimbili, MOI, KCMC na ***Ocean Road***, ujenzi wa uzio katika kituo cha Waathirika wa dawa za kulevya kilichopo Itega, kukarabati wodi ya wagonjwa wa afya ya akili Hospitali ya Mirembe, ujenzi wa hospitali ya kanda ya Kusini Mtwara na Usimikaji wa Mashine za ***LINAC*** katia Hospitali ya Bugando-Mwanza.





| | MAENDELEO | KAWAIDA | JUMLA |
|---|---|---|---|
| KILICHOIDHINISHWA | 518,511,683,780 | 277,604,173,000.00 | 796,115,856,780 |
| KILICHOTOLEWA | 106,608,597,155 | 145,300,426,677.00 | 251,909,023,832 |

***Chanzo: Taarifa ya Wizara***

**b) Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo**

**Mheshimiwa Spika,** mnamo tarehe 25 Januari, 2017, Kamati ilipokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya Utekelezaji na Mpango wa Bajeti ya Wizara kwa kipindi cha nusu Mwaka (Julai – Disemba 2016). Taarifa ya ukusanyaji wa maduhuli ilionesha katika kipindi cha Nusu Mwaka Wizara imeweza kukusanya kiasi cha shilingi **425,775,120/=** sawa na **asilimia 51.9** ya shilingi **820,005,000/=** cha ukusanyaji wa kipindi cha Mwaka mzima. Aidha, kuhusu upatikanaji wa fedha, Wizara imepokea **8,869,789,331/=** kati ya shilingi **20,326,176,000/=** zilizoidhinishwa na Bunge sawa na **asilimia 43 tu.** Kiasi cha shilingi **190,324,000/=** zilipokelewa kati ya shilingi **3,000,000,000/=** ya fedha za Miradi ya maendeleo ambayo ni sawa na **asilimia 6.3 tu.**




| | MAENDELEO | KAWAIDA | JUMLA |
|---|---|---|---|
| KILICHOTOLEWA | 190,324,000 | 8,679,465,331.00 | 8,869,789,331 |
| KILICHOIDHINISHWA | 3,000,000,000 | 17,326,176,000.00 | 20,326,176,000.00 |

***Chanzo: Taarifa ya Wizara***


**c) Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

**Mheshimiwa Spika**, katika kikao kilichofanyika tarehe 27 Januari 2017, Kamati ilipokea Taarifa ya utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kipindi cha nusu mwaka (Julai – Disemba 2016). Taarifa ilionesha kuwa, kwa Mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara ilikadiria kukusanya maduhuli ya shilingi **327,887,974,585.87/=** hadi kufikia Disemba 2016, makusanyo ya maduhuli yalikuwa shilingi **151,381.478,191/=** sawa na **asilimia 46.**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka w Fedha 2016/2017, Wizara iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu kiasi cha shilingi **1,396,929,798,625/=** hadi kufikia Disemba 2016, Wizara ilikuwa imepokea shilingi **584,442,204,153.49/=** sawa na **asilimia 42**. Aidha kwa upande wa Miradi ya Maendeleo kiasi cha shilingi **897,657,547,625/=** kiliidhinishwa na Bunge na kilichotolewa mpaka Disemba 2016 ni **341,924,630,778/=** sawa na **asilimia 38 tu**.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na hayo Wizara ilieleza changamoto ambazo yenyewe na Taasisi zake imekuwa ikikumbana nazo kama: kutopata kwa wakati fedha za kutekeleza Miradi ya Maendeleo, madeni ya walimu, uhaba wa wahadhiri wenye sifa, miundombinu chakavu na isiyokidhi mahitaji kwenye vyuo

vikuu, ongezeko la vyuo vikuu ambavyo vinahitaji ukaguzi wa mara kwa mara, uhaba wa wanafunzi wa kike hasa katika masomo ya Sayansi na uhaba wa hosteli za wanafunzi.




***Chanzo: Taarifa ya Wizara***

### 2.2.6 Kupokea Taarifa Mahsusi

**Mheshimiwa Spika,** katika vikao vya Kamati vilivyofanyika Mwezi Oktoba, 2016, Kamati iliomba kukutana na Wizara mbili inazozisimamia kwa lengo la kupokea Taarifa Mahsusi ya masuala ambayo Kamati iliona ni muhimu kwa wakati huo. Taarifa hizo ni pamoja na**:**

**a) Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto**

**Mheshimiwa Spika,** katika Wizara hii Kamati ilipokea Taarifa tatu zifuatazo:-

**i) Hali ya dawa nchini (Upatikanaji na Usambazaji)**

**Mheshimiwa Spika,** katika Taarifa iliyotolewa na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ilionesha kuwa hali ya upatikanaji wa Dawa nchini ni ya kuridhisha kwani upatikanaji wa dawa ulikuwa ni **asilimia 63**. Aidha, kwa zile dawa muhimu (***Essential Medicines***) ambazo ni **dawa 135, dawa 85** zipo za kutosha na tarehe 27 Oktoba 2016, ilitarajiwa shehena nyingine ya dawa kuingia. Si hivyo tu, lakini kila mwezi ilitarajiwa shehena ya dawa itakuwa inaingia. Pamoja na hayo Kamati ilijulishwa kuwa

Serikali imeingia Mikataba yenye thamani ya shilingi **bilioni 73** na washitiri (*suppliers*) ili kuhakikisha kunakuwa na dawa za kutosha. Ilitarajiwa kuwa ifikapo **mwezi Disemba 2016** Bohari ya Dawa itakuwa na dawa asilimia 85. **Kamati ilibaini uwepo wa deni kubwa ambalo Serikali imekuwa ikidaiwa na Bohari ya Dawa na ilikiri ni kweli deni ambalo Serikali inadaiwa na ni shilingi Bilioni 154.8 ambalo Serikali inajipanga kulilipa.** Pamoja na hayo Kamati haikukubaliana na Taarifa ya Waziri kutokana na takwimu za hali ya dawa katika vituo vya Afya ambazo ziliwasilishwa na Wajumbe wa Kamati kutofautiana. Waziri alipokea hoja ya Kamati na kuomba kuifanyia kazi.

**ii) Hatua zilizofikiwa na Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF) katika utoaji wa Bima ya afya kwa wote (*Universal Health Coverage*)**

**Mheshimiwa Spika,** kabla ya kueleza hatua zilizofikiwa katika utoaji wa Bima ya Afya kwa wote, Waziri alieleza nia ya Serikali kuanzisha Huduma ya Bima ya Afya kwa wote (***Universal Health Coverage***) ambapo itazingatia mambo muhimu yafuatayo:-

- Kutakuwa na mfuko mmoja wa Bima ya Afya nchini ambao ni wa lazima kwa kila Mtanzania ili kuhakikisha kila Mtanzania ana uhakika wa kupata Matibabu. Aidha
- Mfuko huu haufuti Bima za Afya binafsi, ila kila mwananchi atalazimika kuwa na Bima hii na hizi binafsi ziwe ziada. Mfuko pia Utajumuisha watu wenye kipato na hali tofauti hii pia itaondoa matabaka na kuhakikisha huduma za matibabu kwa wananchi wote ikiwa ni pamoja na kupunguza gharama za matibabu. Aidha, inatarajiwa ifikapo **2020 asilimia 70** ya Watanzania wawe wanufaika wa Huduma hii.

**Mheshimiwa Spika**, Waziri alieleza kuwa Muswada wa Bima ya Afya kwa wote ulishaandaliwa na ulitarajiwa kuwasilishwa Septemba 2016, hata hivyo, ulikwama kwenye Baraza la Mawaziri kutokana na mapungufu yaliyobainika. Aidha, Kamati ilijulishwa kuwa mchakato unaenda vizuri na inategemewa mwezi Februari 2017 Muswada huu utaletwa Bungeni. Ni matumaini ya Kamati kwamba Muswada huu upo tayari.

**iii) Utendaji wa Hospitali ya Benjamin Mkapa iliyopo Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM)**

**Mheshimiwa Spika,** Katibu Mkuu aliwasilisha taarifa ya Hospitali ya Benjamin Mkapa kwa niaba ya Waziri wa Afya na Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Taarifa hiyo ilikuwa na baadhi ya mafanikio yaliyopatikana

katika Hospitali hiyo tangu kufunguliwa kwake Oktoba 2015 ikiwa ni pamoja na kutoa tiba kwa wagonjwa ndani na nje ya Mkoa wa Dodoma. Pamoja na mafanikio hayo Kamati ilielezwa changamoto ambazo Hospitali imekuwa ikikumbana nazo ambazo ni:-

- Uhaba wa Watumishi pamoja na muundo wake kwani mahitaji ni **750** na waliopo ni Watumishi **51** ambayo ni sawa na **asilimia 6.8** tu ya mahitaji ya Hospitali hiyo ambayo inasababisha utendaji wake kuwa hafifu.
- Mabadiliko kutoka kuwa Hospitali ya kawaida (ya chuo) kama ilivyokuwa imepangwa awali na kuwa Hospitali ya Taifa ambapo kunahitajika eneo kubwa zaidi.
- Ukosefu wa maeneo ya kuchomea taka (***Incinerator***)
- Ukosefu wa maabara (kwa ajili ya TB, Virus kama vya Ebola).
- Usafiri wa Watumishi kwa kuwa Hospitali ipo kilomita 25 kutoka makazi ya watumishi walio wengi.
- Uchache wa fedha kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa hospital ambazo zinatolewa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF).

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wake wa Taarifa hii, Kamati ilibaini kuwepo kwa Ufisadi katika manunuzi ya vifaa tiba katika Hospitali hiyo na Waziri alikiri katika maelezo yake alipokuwa anahitimisha na kuahidi kufanyia kazi suala hilo ikiwemo uchunguzi kufanywa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali na kuleta taarifa mbele ya Kamati.

**b) Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia**

**Mheshimiwa Spika,** katika Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia, Kamati ilipokea Taarifa za Taasisi mbili zilizo chini ya usimamizi wa Wizara hii ambazo ni:-

i) **Utoaji na urejeshwaji wa mikopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Elimu ya juu**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya utoaji na urejeshwaji wa mikopo ya Elimu ya juu ambayo ilionesha kuwa urejeshwaji wa mikopo umeongezeka kutoka shilingi **milioni 53.6 mwaka 2006/2007** hadi kufikia **Bilioni 30.3 mwaka 2015/2016** na inatarajiwa kuwa mara baada ya kufanyiwa marekebisho Sheria ya Bodi ya Mikopo marejesho yataongezeka zaidi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilihoji juu ya vigezo vinavyotumika kutoa mikopo kwa kuwa kumekuwepo na malalamiko mengi ya wanafunzi kukosa mikopo hiyo licha ya kuwa wanakidhi vigezo. Kamati ilijulishwa kuwa Vigezo vinavyotumika kutoa Mikopo ni **Ulemavu, Yatima na Wanafunzi wanaotoka kwenye familia duni.**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na hayo Kamati ilielezwa nia ya Bodi ya kutaka kufungua Ofisi za Kanda ili kutoa huduma kwa karibu. Lakini pia ilielezwa changamoto mbalimbali ambazo Bodi imekuwa ikukumbana nazo zikiwemo:-

- Ushirikiano mdogo kati ya Bodi ya mikopo na waajiri kwani hawatoi taarifa na hawakati mishahara ya waajiriwa hao ambao ni wanufaika wa mikopo.

- Ukosefu wa Kanzi data (***Database****)* kwaajili ya kuwapata wanufaika wa mikopo ili waweze kulipa madeni yao kwa wakati.

ii)**Utendaji wa Shirikisho la Vyuo Vikuu (TCU) na vigezo vinavyotumika katika kuchagua wanafunzi**

**Mheshimiwa Spika,** katika uwasilishaji wake Mkurugenzi Mtendaji alieleza vigezo vinavyotumika kuchagua wanafunzi pamoja na makosa yanayofanywa na wanafunzi hali inayowapelekea kushindwa kuchaguliwa. Makosa hayo mengi yanatoka na uelewa mdogo wa waombaji wa namna ya kujaza fomu za maombi kupitia mtandao na kutochukua muda wa kusoma na kuelewa maelekezo ya jinsi gani ya kujaza fomu hizo pamoja na vigezo vinavyoambatana na uchaguzi wa kozi anayoitaka na Chuo husika.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa TCU kwa kiasi kikubwa imekuwa ikifanya kazi ya udalali kutokana na utaratibu wake wa kuwapangia vyuo wanafunzi na hasa vile vya binafsi ambavyo pia vimekuwa na gharama kubwa sana.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Wizara kuisimamia TCU kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kuangalia ubora wa Elimu nchini inayotolewa na utitiri wa vyuo nchini badala ya kuhangaika na kipengele (*Component*) kimoja tu cha udahili wa wanafunzi jambo ambalo hata likiachwa halina madhara makubwa kwa Wizara.**

### 2.2.6 Uchambuzi wa Miswada na Mikataba ya Kimataifa (Maazimio)

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Januari 2016 hadi Januri 2017, Kamati ilijadili na kuchambua jumla ya Miswada ya Sheria minne (4) na Azimio moja kama ifuatavyo ambayo pia Taarifa zake ziliwasilishwa Bungeni.

### a) Miswada ya Sheria

**Mheshimiwa Spika,** Miswada ya Sheria iliyojadiliwa na kuchambuliwa na Kamati na hatimaye kuwasilishwa Bungeni na kupitishwa kuwa Sheria ni pamoja na:-

i) Muswada wa Wanataaluma wa Kemia wa Mwaka 2016 (***The Chemist Professionals Bill, 2016);***
ii) Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali wa Mwaka 2016 ( ***The Government Chemist Laboratory Authority Bill, 2016***);
iii) Muswada wa Huduma za Habari wa Mwaka 2016 (***The Media Services Bill, 2016); na***
iv) Muswada wa Sheria ya Madaktari, Madaktari wa Meno na Wataalam wa Afya Shirikishi wa Mwaka 2016 (***The Medical, Dental and Allied Professionals Bill, 2016***).

**b) Mkataba wa Kimataifa ( Maazimio)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijadili na kuchambua Mkataba mmoja wa Kimataifa wa Udhibiti wa Matumizi ya Dawa na Mbinu za kuongeza Nguvu Michezoni (***International Convention Against Doping in Sports***).

### 2.2.7 Semina kwa Wajumbe wa Kamati

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipewa semina mbalimbali kwa lengo la kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati. Semina hizo ni pamoja na:

**a) Semina ya Uchambuzi wa Bajeti**

Semina hii iliendeshwa na Shirika la Maendeleo la Kimataifa (UNDP) chini ya Mradi unaojulikana kama **Legislative Support Program** iliyo chini ya Ofisi ya Bunge. **Katika Semina hiyo wajumbe walijengewa uwezo wa namna ya kuchambua Bajeti ya Serikali na hasa upangaji wa vipaumbele vya Taifa.** Semina ilifanyika tarehe 10 Aprili, 2016 katika Ofisi za Bunge, Dar es Salaam.

**b) Semina ya Masuala ya Idadi ya Watu**

Semina hii iliendeshwa na Mtandao wa Kukuza Uelewa kuhusu Idadi ya Watu na Uwajibikaji Tanzania (TCDAA). Semina ilieleza kuhusu uhusiano uliopo wa ongezeko la Idadi ya watu na Uchumi hususan fursa na changamoto zake. **Semina iliwawezesha Wajumbe kuelewa umuhimu wa kudhibiti wa ongezeko la idadi ya watu** na semina hiyo ilifanyika tarehe 24 Aprili, 2016 katika Ukumbi wa Ngorongoro uliopo Hazina Ndogo- Mjini Dodoma.

**c) Semina ya Masuala ya Afya**

Semina hii iliendeshwa na Taasisi ijulikanayo kama Health Promotion Tanzania (HDT). Lengo la Semina lilikuwa ni pamoja na Taasisi hiyo kutambulika kwa Wajumbe wa Kamati ili kuwaeleza kazi zinazofanywa na Taasisi hiyo, pia kuwapa Taarifa ya uchambuzi uliofanywa na Taasisi hii kuhusu Bajeti ya Sekta ya Afya iliyotengwa katika Mwaka wa Fedha 2016/2017. **Semina ilisaidia kupanua**

**uelewa wa Wajumbe wa Kamati na hivyo kuweza kuishauri Serikali ipasavyo**. Semina ilifanyika katika Ukumbi uliopo Jengo la Hazina Dodoma tarehe 24 April, 2016.

**d) Semina ya Sera ya Pombe**

Semina hii iliendeshwa na TAMWA na ililenga kuhamasisha Wabunge kutaka kuwepo kwa Sera ya Udhibiti wa Matumizi mabaya ya Pombe. **Wajumbe wa Kamati walielewa kwa kina madhara ya kina nakuona kweli ipo haja ya kuwa na Sera**. Semina ilifanyika tarehe 26 Juni, Katika ukumbi wa Msekwa D, uliopo Ofisi ya Bunge Dodoma.

**e) Semina ya Masuala ya Elimu**

Semina hii iliendeshwa na Chuo Kikuu cha Aga Khan kwa lengo la kuainisha changamoto zilizopo kwenye Sekta ya Elimu na namna ya kutatua changamoto hizo. **Kamati ilibaini ni kweli kuna changamoto nyingi katika Sekta ya Elimu ambazo zinahitaji msukumo wa pamoja ili kuweza kuzitatua kwani suluhu yake ni mtambuka**. Semina hii ilifanyika tarehe 4 na 5 Septemba, 2016 katika Hoteli ya Morena Dodoma.

***SEHEMU YA TATU***

## 3.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapenda kutoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo kama ifuatavyo:-

### 3.1 Maoni ya Jumla

#### 3.1.1 Bajeti

**Mheshimiwa Spika**, kama ambavyo imeelezwa ndani ya Taarifa hii, changamoto kubwa ambayo imekuwa ikizikumba Wizara zilizo chni ya Usimamizi wa Kamati ni utolewaji wa fedha usioridhisha. Kamati inatambua umuhimu wa kila sekta hapa nchini lakini Sekta kama Elimu na Afya ni msingi mkuu wa sekta nyingine.

**Mheshimiwa Spika,** Itakumbukwa mnamo Mwaka 2000 UN kupitia *World Summit* iiyofanyika Brazil ilikuja na malengo ya millenia 8 (*8 Millenium Development Goasl –MDG's)* kwa lengo la kupunguza Umaskini ambayo kilele chake kilikuwa 2015. Baada ya kilele chake, mwaka 2015 UN ilikuja na malengo 17 endelevu ya maendeleo **(17 Sustainable Development Goals)** na kukubaliana yawe yametekelezwa ifikapo 2030. Kati ya Malengo hayo, malengo 3 yanahusu Sekta ambazo zipo chini ya usimamizi wa Kamati hii.

Lengo namba 2 ni ***Good health and well being***, lengo namba 3 ni ***Quality education***, na lengo namba 4 ni ***Achieve gender equality and empower all women and girls.***

**Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa UN imetambua kuwa ili kufikia maendeleo endelevu ni lazima kuwekeza kwenye sekta hizi kwa kutenga bajeti za kutosha. Kamati inaishauri Serikali kuziangalia Wizara hizi kwa jicho la pekee na kuhakikisha kiasi kinachotengwa na Bunge kinatolewa chote na kwa wakati**.

**3.1.2 Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa Miradi mingi ya Maendeleo iliyo chini ya Wizara zilizo chini ya usimamizi wa Kamati zimekuwa hazipati fedha zake kwa wakati hali ambayo imeathiri utekelezaji wa miradi hiyo, **Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha fedha zote zinazotengwa kwenye Miradi zinatolewa zote na kwa wakati na kama haiwezekani ni bora kupunguza miradi inayotekelezwa kwa wakati huo.**

**3.1.3 Mfumo wa ugatuaji madaraka (Development by Devolution)**

**Mheshimiwa Spika,** Mfumo wa Ugatuaji Madaraka (**D by D**) umesababisha Wizara zote zinazosimamiwa na Kamati kukosa mamlaka ya kuwafuatilia kwa karibu ikiwa ni pamoja na kuwachukulia hatua mbalimbali Watendaji walioko chini ya Wizara husika pale ambapo inabainika wamekwenda kinyume na taratibu na hivyo kupunguza ufanisi katika Wizara hizo. Kwa mfano Waganga, Wauguzi, Waalimu, Maafisa Michezo, Maafisa maendeleo ya Jamii wote wako chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (**TAMISEMI**). **Kamati inaona ni vyema ukaandaliwa mfumo bora wa mawasiliano na ushirikiano kati ya Wizara na TAMISEMI na ikibidi kuwepo na msimamizi mmoja tu. Aidha, kuna umuhimu kwa Kamati za Bunge za Huduma na Maendeleo ya Jamii na Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa kufanya vikao vya Kamati kwa pamoja pale linapotokea hitaji la kufanya hivyo.**

**3.1.4 Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto**

**Mheshimiwa Spika,** katika Wizara hii Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo yafuatayo:-

**a) Bohari ya Dawa (MSD)**

i) Bohari ya dawa licha ya umuhimu wake wa kuwa ndiyo inategemewa katika suala zima la uagizaji na usambazaji wa dawa nchini lakini bado imekuwa ikitengewa bajeti ndogo ambayo haikidhi mahitaji yake na hivyo kuathiri hali ya upatikanaji wa dawa nchini. **Kamati inashauri MSD iwe na**

**fungu lake (*Separate vote*) kwani mahitaji yake ni makubwa sana na kutapunguza malimbikizo ya madeni yanayosababishwa na Serikali.**

ii) Kamati imebaini kuwa changamoto nyingine ambayo MSD inakumbana nayo ni madeni makubwa inayozidai Halmashauri mbalimbali hali ambayo inaifanya ishindwe kuagiza dawa za kutosha kwa wakati**. Kamati inashauri kwa zile Halmashauri ambazo zinadaiwa ziwekewe utaratibu wa kuwa zinakatwa kiasi kidogo pale zinapoagiza dawa kupitia fedha za Serikali ili kupunguza deni.**

iii) **Mipango iandaliwe ili kuwezesha mfumo wa ugawaji dawa uwe wa kielektroniki (*computerized*) ambapo kila siku asubuhi ijulikane dawa zilizopo kwenye kituo cha afya au hospitali ili kumsaidia na kumuwezesha daktari kuwaandikia wagonjwa dawa zilizopo kituoni au hospitalini ili kupunguza malalamiko ya kuishiwa kwa dawa wakati dawa mbadala zipo.**

iv) Pamoja na kauli ya Serikali kuwa upatikanaji wa dawa nchini upo wa kuridhisha, kiuhalisia hali ya upatikanaji wa dawa katika maeneo mengi siyo ya kuridhisha. Ukosefu huu wa dawa unahatarisha maisha ya wananchi wengi ambao wengi ni maskini. **Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha bidhaa hii muhimu kwa maisha ya wanadamu inakuwepo wakati wote kwani Uwepo wa dawa maana yake wananchi wanapata dawa**. Mahatma Gandhi aliwahi kusema "***It is health that is real wealth and not pieces of gold and silver"*** akimaanisha kwamba ***"Afya ndiyo utajiri wa kweli siyo dhahabu wala shaba". Hivyo basi hatuna budi kuhakikisha afya ya Watanzania ndiyo kipaumbele chetu.***

v) Kamati imebaini kuwa kumekuwepo na wizi wa dawa za Serikali ambazo zimekuwa zikikutwa kwenye maduka ya dawa ya watu binafsi hali inayofanya wagonjwa wakienda hospitali wakose dawa na hivyo kuhatarisha maisha kwa wale wasio na uwezo, **Kamati inashauri hatua kali zichukuliwe kwa yale maduka binafsi ya dawa (*Pharmacy)* yanayokutwa na madawa za Serikali.**

**b) Taasisi ya Saratani *Ocean Road* (ORCI)**

**Mheshimiwa Spika**, ugonjwa wa Saratani umekuwa tishio hapa nchini kutokana na kuongezeka kwa wagonjwa. Pamoja na kasi ya kusambaa kwa ugonjwa huu, kuna changamoto ya vifaa kwani vingi ni chakavu, uhaba wa dawa ambazo pia ni aghali sana na ukosefu wa vifaa vya kupima saratani katika Hospitali za Mikoa.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto hizi zimepelekea wagonjwa wengi kupoteza maisha wakati wakisubiri matibabu ikiwemo vipimo na wengine kukosa dawa hivyo basi, **Kamati inashauri Serikali kuhakikisha inaongeza bajeti ya hospitali hii ili iweze kuwa na vifaa vingi na vya kisasa na pia kuhakikisha Hospitali za Mikoa zinapatiwa wataalam na vifaa ili kupunguza msongamano katika Hospitali ya Ocean Road.**

**c) Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)**

i) Kamati imebaini kwamba, pamoja na Mfuko huu wa Bima ya Afya kuwakata fedha kwa ajili ya matibabu wanachama wake, Bima ya Afya imekuwa na utaratibu wa kuchagua baadhi ya magonjwa kwa ajili ya kugharamia matibabu yake, na kuacha baadhi yakiwemo magonjwa yanayohusiana na upasuaji wa moyo. Utaratibu huu wa kuchagua magonjwa ya kulipia umekuwa unawawakatisha tamaa wananchi katika kuendelea kuchangia mfuko huo hasa pale wanaposhindwa kumudu matibabu hayo na hata kuwaingizia hasara Taasisi zinazotoa huduma hizo kama vile Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete kwa kujikuta inaingia gharama kubwa ya kununua vifaa ambavyo ni gharama ambapo jukumu hilo la kulipa matibabu ni la Bima ya Afya. **Kamati inashauri NHIF kuboresha Bima hii ili iweze kugharamia magonjwa yote, lakini pia iweze kukubaliwa katika hospitali zote nchini. Ifike mahali mtu mwenye kadi ya NHIF ajisikie fahari kuwa nayo.**

ii) Kamati inatambua nia nzuri ya Serikali ya kuleta mpango wa Bima ya afya kwa wote (***Universal Health Coverage***), hata hivyo, haiwezekani kutunga Sheria bila ya kuwa na Sera. **Kamati inashauri Serikali kwanza kuandaa sera kwa ajili ya kusimamia suala hili ili baadae mchakato wa utungaji wa Sheria hiyo ufuate.**

iii) Kamati iliona kwamba, kwa kuwa zaidi ya asilimia 50 ya Watanzania ni wategemezi, na hivyo hawataweza kulipia mfuko huu, **Serikali ihakikishe kuwa inajipanga vyema kuhakikisha wananchi walio katika kundi hili wanapata huduma hii bila tatizo kwa kuboresha vyanzo vyake vya mapato vitakavyowezesha kupatikana mapato ya kugharamia Mfuko huu. Aidha, muhimu dawa zikapatikana kwani bila hilo hata mfuko huu hauna maana.**

**d) Hospitali ya Benjamin Mkapa**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa ukiacha changamoto ambazo hospitali ya Benjamin Mkapa imekuwa ikikumbana nazo lakini kuna ufisadi mkubwa wa fedha ambao umefanyika na hivyo kusababisha hospitali ishindwe kujiendesha vizuri. **Kamati inaitaka Serikali kufanya Ukaguzi ili kubaini wahusika**

**wa ufisadi huo na kuwachukulia hatua. Pamoja na hayo Kamti inashauri Hospitali hii iwezeshwe kwa kupatiwa vifaa vya kutosha ili iweze kusaidia kutoa huduma kwa Watumishi wanaohamia Dodoma kufuatia agizo la Mhe. Rais Dkt. John Pombe Magufuli la kuifanya Dodoma Makao Makuu ya nchi kwa vitendo kwa kuhamishia shughuli zote za Serikali mkoani humu.**

**e) Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI)**

**Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) inafanya kazi kubwa ambayo kwa kiasi kikubwa imesaidia kupunguza gharama kubwa ambazo nchi ilikuwa inaingia katika kutibu wagonjwa wa moyo. Hata hivyo, Taasisi hii imekuwa haipatiwi fedha za kutosha za utekelezaji wa majukumu yake. Kwa mfano katika kipindi cha Nusu Mwaka (Julai – Disemba, 2016), Taasisi hii imepata **asilimia 12.5 tu** ya bajeti yake. **Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha inaipa kipaumbele cha pekee Taasisi hii kwa kuitengea fedha za kutosha lakini pia ambazo zinatolewa kwa wakati ili iweze kusaidia kupunguza gharama ambazo Serikali imekuwa ikiingia katika kupeleka wagonjwa wa moyo nchini India.**

**f) Mafunzo ya Juu ya Wataalam wa Afya Wabobezi (Specialists)**

**Mheshimiwa Spika**, nchi yetu inakumbana na uhaba wa wataalam wa afya wenye ubobezi kwenye fani mbalimbali (Specialists). **Kamati inashauri Serikali kuanza kusomesha wataalam hawa ili kuhakikisha katika kila Hospitali ya Mkoa kunakuwepo wataalam wa aina hii kama Daktari wa akina mama, watoto, magonjwa ya ndani n.k.**

**g) Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua kazi inayofanywa na TFDA katika kudhibiti ubora wa chakula na dawa nchini. **Kamati inashauri Mamlaka iendelee kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi juu ya umuhimu wa kununua bidhaa ambazo zimekaguliwa ili kuepuka madhara yatokanayo na ulaji au ununuzi wa bidhaa sizisokidhi viwango.**

**h) Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC)**

**Mheshimiwa Spika**, Taasisi ya Chakula na Lishe ni moja kati ya Taasisi muhimu sana hasa ikizingatiwa ina jukumu kuu la kusimamia lishe ya wananchi. Kwa miaka ya hivi karibuni Taasisi hii imekuwa kama imekufa. Kamati inatambua kuwa magonjwa mengi ambayo wananchi wanakumbana nayo kwa sasa mengi yanatokana na ulaji wa chakula usiozingatia lishe. **Kamati ina amini kwamba ni wakati sasa Taasisi hii ikawezeshwa ili iweze kutoa elimu ya kutosha juu ya uzingatiaji wa lishe bora ili kuepukana na magonjwa ambayo yanaweza kuepukika.**

**h) Uhaba wa Wataalam wa Afya**

Sekta ya Afya ni miongoni mwa Sekta mbazo zinakumbana na uhaba mkubwa wa Wataalam wa Afya ambao haukidhi mahitaji. Hata hivyo pamoja na uhaba huo lakini baadhi ya maeneo yana wataalam wengi ikilinganishwa na maeneo mengine. **Kamati inashauri kuwepo usawa wa kugawa Waganga Wakuu na Wataalamu wa afya katika maeneo mbalimbali ya nchi, ugawaji wa wataalam hao uzingatie mahitaji halisi ya eneo husika hasa katika maeneo ya pembezoni.**

**k) Elimu kuhusu Uzazi wa Mpango**

Tanzani ni moja kati ya nchi ambazo linakumbana na changamoto ya ongezeko la watu. Kwa wastani mwanamke mmoja ana uwezo wa kuzaa watoto 5. Takwimu zinaonesha Tanzania inaongezeka watu takribani **milioni moja (1,000,000)** kwa mwaka hali inayosababisha Serikali kushindwa kuwahudumia vizuri wananchi wake. **Kamati inaona ipo haja ya kudhibiti ongezeko hili la watu na hivyo inashauri Serikali kuandaa Mkakati wa kuwaelimisha wananchi kuhusu Uzazi wa Mpango na umuhimu wa kuwa na watoto wachache.**

**l) Ushiriki wa Sekta Binafsi katika kutoa huduma za vifaa tiba**

Ukuaji wa teknolojia umefanya nchi nyingi kuondokana na utaratibu wa kununua vifaa mbalimbali vya matibabu na badala yake imekuwa ikishirikisha sekta binafsi katika kutoa huduma hizi. **Kamati inaona ni wakati sasa Serikali ikaanza kufanya utafiti kuhusu namna ambavyo sekta binafsi inaweza kushiriki kwenye kutoa huduma za vifaa tiba kama MRI, CT SCAN n.k. Kwa kushirikisha sekta binafsi kwenye huduma hizi kutasaidia kupunguza tatizo la kukosekana mara kwa mara kwa huduma hizi zinazotolewa na vifaa tiba hivyo lakini pia itasaidia kupunguza gharama.**

**m) Ukatili wa Kijinsia**

Matendo ya ukatili wa kijinsia yameendelea kukua hali inayohatarisha maisha ya wanaanchi hususan wanawake na waoto. Hivi karibuni kumetokea tukio la mwanamke kuchapwa mbele ya hadhara ya wanawake na wanaume Mkoani Mara. **Kamati inashauri Serikali iwachukulie hatua kali wale wote wanaobainika kujihusisha na vitendo hivi.**

**n) Makazi ya Wazee**

Wazee ni kundi ambalo limesahaulika licha ya kuwa ndilo lilileta ukombozi wa nchi hii. Wazee pamoja na umuhimu wa kujengewa makazi lakini makazi yao mengi yamekuwa na hali mbaya sana. **Kamati inashauri Serikali itenge fedha za kutosha kwa ajili ya kujenga makazi ya wazee nchini na kuhakikisha wanawekewa huduma zote muhimu zikiwemo maji, huduma za afya na hata matunzo ya kisaikolojia**.

**o) Sheria Mbalimbali**

Kumekuwepo na baadhi ya Sheria kandamizi kama vile Sheria ya ndoa ya Mwaka 1971 ambayo **Kamati inashauri Serikali iharakishe na kukamilisha mchakato wa marekebisho ya sheria hii. Sambamba na hilo, Kamati inashauri Serikali iharakishe mchakato wa utungaji wa sheria ya Wazee.**

**3.1.5 Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo**

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Habari na Taasisi zake zinakumbana na changamoto mbalimbali ambazo Kamati inapenda kuzitolea maoni, ushauri na mapendekezo kama ifuatavyo:-

**a) Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC)**

**Mheshimiwa Spika**, kilio kikubwa cha TBC ni uhaba wa fedha kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake, miundombinu mibovu na uchakavu wa vifaa hali ambayo imesababisha washindwe kusikika kwenye masafa ya redio katika baadhi ya mikoa (Wilaya 81) licha ya kuwa ndiyo Shirika pekee la Utangazaji linalomilikiwa na Serikali. **Kamati inaishauri Serikali ililipe Shirika hili hadhi yake kwa kulitengea fedha za kutosha ili liweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo ikiwemo Miradi ya Maendeleo na hususan uwekezaji kwani Sekta ya Habari inahitaji uwekezaji wa kutosha.**

**b) Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliwahi kushauri juu ya umuhimu wa TSN kuwa wabunifu ili kuongeza vyanzo vyake vya mapato. Kamati inatambua jitihada zinazofanywa na TSN za kuanza utaratibu wa kufunga mtambo wa kibiashara (***Commercial Press***) utakaochapisha vitabu na machapisho mengine ili kuongeza mapato yake. **Kamati inaendelea kusisitiza mchakato huu ukamilike haraka ili mapato yaweze kupatikana mapema.**

**c) Chuo cha Sanaa Bagamoyo (TaSuBa)**

Kamati imebaini changamoto kubwa ambayo TaSuBa imekuwa ikikumbana nayo ya miundombinu isiyokidhi mahitaji. **Kamati inashauri Serikali itenge fedha za kutosha ili kuhakikisha kunakuwepo miundombinu ya kutosha**

**na yenye kukidhi mahitaji kwa ajili ya kutunza Sanaa ya Tanzania ambayo itatufanya tujivunie.**

**d) Mitaala ya Michezo shuleni na Shule za Michezo**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua umuhimu wa michezo lakini hakuna mitaala ya michezo katika shule hapa nchini hali ambayo imekuwa ikidumaza kiwango cha michezo. **Kamati inashauri Serikali kuandaa mitaala ya michezo ili kuinua kiwango cha michezo na kukuza vipaji. Sambamba na hili, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutekeleza mapema ushauri wa Kamati wa kutenga shule za michezo lakini ni lazima kuzipatia fedha za kutosha ili kuweza kufikia malengo ya kukuza vipaji vya vijana wetu.**

**e) Sera na sheria mbalimbali za masuala ya Michezo**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa Sera na Sheria zinazohusu michezo zimepitwa na wakati zinahitaji kurekebishwa ili ziweze kuendana na wakati, mfano Sera ya Maendeleo ya Michezo ya Mwaka 1995 ambapo mambo mengi yamekwisha badilika. **Kamati inashauri Serikali ikamalishe mchakato wa mapitio ya Sera na Sheria hizo mapema ili kuendana na wakati.**

**f) Uboreshaji wa viwanja vya michezo**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri Wizara iandae mkakati wa kuboresha viwanja vya michezo nchini, ikiwa ni pamoja na viwanja vinavyomilikiwa na Chama Cha Mapinduzi. Kamati inapendekeza Wizara ishirikishe sekta binafsi ili kuendesha na kuendeleza viwanja hivyo vitakavyosaidia kuinua kiwango cha michezo

**g) Maadili na Utamaduni wa Mtanzania**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini maadili na utamaduni wa Mtanzania yameendelea kuporomoka siku hadi siku kutokana na kukua kwa teknolojia. Kamati inashauri pamoja na jukumu la Serikali kutoa elimu juu ya umuhimu wa kutunza mila nzuri na tamaduni zetu na kuchukua hatua pale panapotokea ukiukwaji uliozidi kikomo lakini pia wazazi wanapaswa kuwa na jukumu la kwanza la kuangalia maadili ya watoto wao.

**h) Kazi za Wasanii**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa kumekuwepo na wizi wa waziwazi wa kazi za Wasanii hali ambayo pia inapelekea kutopata faida ya jasho la kazi zao na hatimaye kukosesha mapato Serikali, **Kamati inashauri Wizara ihakikishe unaandaliwa utaratibu wa wazi utakaowezesha kulinda kazi za wasani.**

**i) Idara ya Habari Maelezo**

**Mheshimiwa Spika**, Idara ya Habari Maelezo ndiye Msemaji Mkuu wa Serikali, hata hivyo kumekuwepo na Taarifa zinasambaa ambazo Idara hii inapaswa kutoa ufafanuzi kwa wananchi lakini mara nyingi imekuwa haifanyi hivyo. **Kamati inashauri Idara hii iweke utaratibu wa utoaji habari kwa Umma (*Press Conference*) ili kuweza kutoa ufafanuzi unaotakiwa na hivyo kupunguza mashaka kwa wananchi.**

**3.1.6 Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

**Mheshimiwa Spika,** Wizara hii pamoja na Taasisi zake inakumbana na changamoto mbalimbali ambazo Kamati inapenda kuzitolea maoni, ushauri na mapendekezo kama ifuatavyo:-

**a) Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu**

i) Kamati imebaini kuwa fedha nyingi takribani asilimia 50 ya fedha za miradi ya maendeleo zinaenda kwenye Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, **Kamati inashauri fedha za miradi ya maendeleo kwa Wizara hii zitenganishwe na fedha za Bodi ya Mikopo kwa ajili ya wanafunzi wa vyuo vya Elimu ya juu ili kubainisha kiasi halisi kinachotengwa kwa ajili ya maendeleo ya elimu na kwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya juu.**

ii) Kwa kuwa ukusanyaji wa marejesho ya mikopo ya Elimu ya Juu sio wa kuridhisha sana, **Kamati inashauri Bodi iweke mkakati madhubuti wa kuhakikisha inaongeza kiwango cha marejesho ya mikopo kwani wanufaika wengi wanajulikana walipo. Hii itasaidia kutoa mikopo kwa wengine baada ya kupata marejesho hayo**.

**b) Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA)**

Vyuo vya ufundi stadi (VETA) viwe na utaratibu wa kufundisha masomo kulingana na mahitaji ya nchi na soko na sera ya nchi (mfano: sera ya kuwa nchi ya viwanda) badala ya kujenga vyuo kila sehemu na na kujikuta wanafunzi walio wengi wanajifunza kitu hichohicho kama vile udereva ambao unafanywa na karibu vyuo vyote vya VETA nchini na hakuna fani nyingine.

**c) Taasisi ya Elimu Tanzania (TET)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua kuwa kuna uhaba wa vitabu nchini hali ambayo imeendelea kuzorotesha ubora wa Elimu. **Kamati inashauri Serikali ihakikishe vitabu vyote vinavyopaswa kutumika kwa walimu na wanafunzi vinapatikana kwa wakati.**

**d) Tume ya Vyuo Vikuu (TCU)**

i) Kamati imebaini kuwa (TCU) imekuwa na utaratibu wa kuwapangia wanafunzi vyuo vya kwenda na hususan vile vya binafsi. **Kamati inashauri utaratibu huu uachwe na badala yake wanafunzi waombe wao wenyewe moja kwa moja katika vyuo husika, kwani TCU imekuwa ikifanya kazi ya uwakala wa Vyuo binafsi na vyuo hivi vimekuwa vikitoa elimu kwa gharama kubwa sana na kulazimika kuwalipia wanafunzi hao kwa kupitia bodi ya mikopo.**

ii) Kamati inatambua jukumu kuu la TCU ni kusimamia ubora wa elimu katika vyuo nchini na hivyo Kamati inaendelea kusisitiza **kwa kuishauri TCU kufanya jukumu lake la msingi la kuangalia ubora wa elimu nchini inayotolewa na vyuo vikuu na iachane na utaratibu wake wa sasa ambapo imejikita zaidi katika kufanya udahili wakati hiyo sio kazi yao. Kazi ya udahili ifanywe na vyuo husika kulingana na vigezo vya chuo hicho.**

**e) Hospitali ya kufundishia ya Mloganzila**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua umuhimu wa Hospitali ya kufundishia ya Mloganzila katika harakati za kuongeza Wataalm wa Afya nchini. Hata hivyo Kamati inapata mashaka kuhusu upatikanaji wa rasilimali watu na vifaa tiba. Kwani mahitaji halisi ya Hospitali ni watumishi **950** na mpaka sasa ni watumishi **50** tu ndiyo wenye uhakika wa kupatikana wa kwenda kufanya kazi katika Hospitai hiyo. **Kamati inashauri Serikali ijipange ili kuhakikisha kuwa kunapatikana rasilimali watu wa kutosha na wenye vigezo kupitia mfumo sahihi badala ya kuokoteza tu, pamoja na vifaa tiba. Aidha, kwa kuanzia Serikali ifanye mashirikiano na nchi nyingine zenye Wataalam wazuri ili kuweza kuungana na watoaji wa huduma ya afya katika hospitali hiyo na kuwajengea uwezo (*beefing up*) wataalam wa afya nchini ili kuifanya Hospitali hii kuwa hospitali ya kisasa katika utoaji wa huduma wakati tukiendelea kusomesha wataalam wetu.**

**f) Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela- Arusha**

**Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela – Arusha ina jukumu la kutoa elimu na mafunzo katika ngazi ya uzamili na uzamivu pamoja na kufanya utafiti katika ngazi ya ubobezi. Taasisi hii tayari imefanya utafiti kwa ajili ya kuanzisha Kituo cha Ithibati (***centre of excellence)*** katika Bara la Afrika kwaajili ya kujibu changamoto na matatizo ya Afrika katika Nyanja ya Sayansi na Teknolojia.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, Kamati imebaini kuwa Chuo kimejikita zaidi katika kutoa elimu kama vilivyo vyuo vingine. Kamati inaona kuwa Taasisi ya Nelson Mandela inapaswa kuwa kama ***Sillicon Valley***, eneo ambalo ni Makao Makuu ya Makampuni yenye Teknolojia kubwa duniani ambayo yamewekeza kwa ajili ya kutotoa (kuzalisha) Teknolojia huko Marekani. Kitendo cha kuwepo eneo moja maalum la utafiti na ugunduzi wa Sayansi na Teknolojia pamoja na Makampuni na Viwanda kumesaidia kuzalisha watafiti wengi na vituo vya teknolojia.

**Mheshimiwa Spika**, **Kamati inashauri na inaona ni wakati sasa Taasisi hii kujikita zaidi katika kufanya utafiti na kuzalisha wataalam wengi zaidi ili kuweza kuwa *Silicon Valley* ya Tanzania na Afrika kwa ujumla na haya yatawezekana endapo tu, Serikali itaamua kuwekeza ipasavyo na kujenga Maabara za utafiti za kutosha.**

**f) Madeni ya Walimu**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua sana umuhimu wa Walimu katika Sekta ya Elimu na Maendeleo ya Taifa. Lakini walimu wamekuwa wanakumbana na changamoto nyingi ikiwemo ya kutolipwa stahiki zao, mfano walimu waliosimamia mitihani mwaka 2015 hali ambayo imepelekea Serikali kudaiwa fedha nyingi na walimu hawa. Kutolipwa fedha zao kwa wakati kunawafanya walimu wakose morali ya kufundisha vizuri na kwa bidii hali ambayo pia ina athari kwenye elimu ya watoto wetu, Mtaalam wa Elimu Bi. Theresa Grimm amewahi kusema "***Without teacher appreciation there can't be any student progress"*. Kamati inaitaka Serikali (Wizara ya Elimu na TAMISEMI) ijipange ikishirikiana na Chama Cha Walimu Tanzania kuhakiki na kulipa madeni yote ya walimu mapema iwezekanavyo yapatayo kiasi cha shilingi Trilioni 1.6**.

**g) Mkakati wa kuongeza Walimu**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa kuna upungufu wa Walimu na hususan wa masomo ya Sayansi, Hisabati na hali ambayo imekuwa ikiathiri kiwango cha Elimu nchini, kutokana na hali hiyo, Kamati inaazimia Wizara iandae Mkakati maalum wa kuendeleza waalimu wa masomo ya sayansi na hisabati ili kukabiliana na changamoto ya muda mrefu ya uhaba wa wataalam hao katika masomo hayo.

**h) Wanafunzi walioondolewa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM)**

**Mheshimiwa Spika**, itakumbukwa Mwaka 2016 kuna wanafunzi waliokuwa wanasoma Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) ukiwa ni mkakati wa kukabiliana na changamoto ya uhaba wa walimu wa masomo ya Sayansi waliondolewa

kwa kuwa hawakukidhi vigezo. Kamati inatambua kuwa wanafunzi hao waliingizwa chuoni kwa shinikizo la viongozi ili hali wakijua hawakidhi vigezo. **Kamati haipingani na zoezi la kuwaondoa wanafunzi hao lakini inashauri Serikali iache utaratibu wa kung'ang'aniza Wakuu wa vyuo kuchukua Wanafunzi wasio na vigezo ili kuepuka tukio kama hili. Kwani kwa kufanya hivyo kunaleta usumbufu kwa uongozi wa vyuo, wanafunzi, wazazi na hata mamlaka wa mahali husika kama vile uongozi wa mkoa kama ilivyo mfano wa tukio la UDOM 2016.**

**i) Uhaba wa Wahadhiri wa Vyuo Vikuu**

**Mheshimiwa Spika,** kumekuwepo na ongezeko la Vyuo vikuu ili hali idadi ya wahadhiri imeendelea kupungua kutokana na wengi kufikia umri wa kustaafu ambao ni miaka 60 kwa mujibu wa sheria na 70 kwa wale wenye PhD hali ambayo inahatarisha kiwango cha elimu nchini. **Kamati inaitaka Serikali kuandaa mkakati wa kuhakikisha inaongeza idadi ya wahadhiri nchini na wenye sifa ili kuweza kuinua kiwango cha elimu nchini. Pamoja na hayo Kamati inashauri uwepo utaratibu maalum kwa wahadhiri ambao wana uwezo na nguvu basi wapewe nafasi ya kufundisha hata miaka 80 kama ambavyo nchi za wenzetu wanafanya kwani kama nchi inakuwa imewekeza rasilimali nyingi kwa mtumishi huyo na faida (*return*) yake kwa nchi inakuwa kidogo sana kutokana na kigezo cha umri.**

**j) Vibali vya Wahadhiri**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati haipingani na utaratibu wa UTUMISHI wa kuomba kibali kwa Wahadhiri kwa Waziri pale wanapohitajika kusafiri kwenda nje ya nchi kwa manufaa ya chuo na nchi kwa ujumla. **Kamati inaona utaratibu huu unawanyima fursa wahadhiri pale wanapopata safari za dharura na hivyo basi inashauri Makamu Wakuu wa Vyuo wapewe mamlaka ya kutoa vibali kwa wahadhiri walio chini yao. Kwa kufanya hivyo vyuo husika watarudisha faida katika chuo kupitia miradi (projects) na hata kupata uzoefu wa masuala ya elimu.**

**k) Lugha ya Kiswahili**

**Mheshimiwa Spika,** tutambue kuwa Taifa hili haliwezi kuendelea kwa kujikita kwenye lugha moja tu ya Kiswahili, pamoja na nia njema ya kukuza Kiswahili, **Kamati inashauri Serikali ihimize watoto wajifunze Kiswahili fasaha pamoja na lugha nyingine kama Kingereza na Kifaransa ili kuendana na soko la dunia. Na hata ikiwezekana kulifanya somo la Kiswahii kuwa ni la lazima katika ngazi zote kwa maana ya kuanzia Elimumsingi mpaka chuo kikuu bila kujadili mwanafunzi anasoma mchepuo gani.**

**l) Miundombinu ya Elimu**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa miundombinu katika Sekta ya Elimu imekuwa chakavu na pia haikidhi mahitaji, **Kamati inashauri Serikali kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya Ujenzi wa miundombinu yakiwemo mabweni ya wanachuo na vyumba vya mihadhara. Aidha, Serikali inaweza kuishirikisha Mifuko ya Hifadhi za Jamii ili isaidie kujenga mabweni, hatua hii itasaidia kujenga utamaduni wa vyuo vikuu (*University Culture*) ambao umepotea kutokana na wanavyuo kuishi mitaani.**

**m) Mfumo wa Elimu Tanzania**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba Mfumo wa Elimu hapa nchini umevurugika kutokana na kuwepo kwa matamko mbalimbali ya Serikali ambayo yamekuwa yakiathiri mfumo mzima wa Elimu nchini. **Kamati inashauri Wataalam wa Elimu wafanye tathmini kuhusu mfumo wa elimu uliopo kuanzia elimu msingi, sekondari hadi vyuo vikuu kuja na mfumo ambao utaboresha kiwango cha elimu nchini**.

**n) Ofisi za Serikali kuhamia katika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaunga mkono shughuli za Serikali kuhamia Dodoma, lakini utaratibu huu wa Wizara kuhamishia Ofisi zao katika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) sio sawa**.** Kamati inaona kuna bomu kubwa linakuja kulipuka (***social disaster***) kwa kuwachanganya wanafunzi na wafanyakazi kwani kutapelekea kuwafanya wanafunzi wasijikite katika masomo. **Kamati inashauri Serikali itafute majengo mengine ikiwezekana kujenga majengo yao kwa shughuli za Ofisi za Serikali na siyo UDOM kwani lengo lake tangu mwazo halikuwa kukifanya chuo hicho kuwa ofisi za Wizara.**

**o) Shule Binafsi (*Private Schools*)**

**Mheshimiwa Spika,** uwepo wa shule binafsi umesaidia kuongeza ubora wa kiwango cha elimu nchini kwa kutoa elimu bora kutokana na kiwango cha elimu katika shule za Serikali kuzorota. Inasikitisha kuona Serikali inaziingilia shule binafsi hata katika masuala ya utendaji. **Kamati inashauri Serikali iboreshe shule zake kwani zikiboreshwa kwa vyovyote vile wazazi watawapeleka watoto wao katika shule za Serikali na hizi za binafsi zitakufa kifo cha asili au zenyewe (*natural death*) badala ya kuziingilia shule binafsi.Ikumbukwe zamani kila mzazi na mtoto alitamani kuingia katika shule ya serikali kwani ilikuwa fahari kwa sababu ya ubora wake kwa kipindi hicho, Kamati inaona ni vyema utamaduni huo wa ubora wa shule ukarejeshwa.**

**p) Tuzo ya Udhamini (Scholarship Award)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inarudia ushauri wake ulioutoa wakati wa taarifa ya Bajeti ya Wizara ya Elimu juu ya umuhimu wa kutoa tuzo za udhamini kwa wanafunzi wanaomaliza kidato cha sita ambao wamefanya vizuri katika mitihani yao ya Taifa. Serikali itoe ufadhili kwa wanafunzi waliofanya vizuri angalau 100 kila Mwaka ili wakasome katika vyuo ***vyuo bora duniani kama Havard, Cambridge, Yale n.k. Hii itasadia kuzalisha watanzania wenye elimu nzuri ambao watasaidia Taifa kusonga mbele.*** Aliyekuwa Rais wa 35 wa Marekani *John F. Kennedy* aliwahi kusema "***Our progress as a Nation can be no swifter than our Progress in Education. The human mind is our Fundamental Resource."***

**q) Uainishaji wa Vyuo Vikuu (*University Classification*)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inarudia ushauri ambao iliutoa wakati wa kuchambua Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 kuhusu uanishaji wa Vyuo Vikuu (***University classification***). Kamati inashauri **Serikali ifanye uanishaji wa vyuo hivyo kulingana na kiwango cha ubora wake katika utoaji wa Elimu. Hii itasaidia kuongeza ushindani wa wanafunzi waliopo sekondari na hivyo kusoma kwa bidii. Kamati ina amini kuwa wanafunzi wengi watapenda kusoma chuo chenye sifa ya juu. Kwa mfano Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kikawekewa kiwango cha kufanana na Havard au Yale au Chuo Kikuu cha Dodoma kiwango cha Oxford, n.k. Kwa kufanya hivyo, kutasaidia kupata wanafunzi wenye ufaulu wa juu (*academic creams*) ambayo mwisho wa siku itakuwa ni sifa kwanza kwa mwanafunzi mwenyewe, familia na hata nchi.**

***SEHEMU YA NNE***

**4.0 HITIMISHO**

**4.1 Shukrani**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mara nyingine napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa ya Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2016.

**Mheshimiwa Spika**, nachukua fursa hii kuwapongeza Mawaziri wote wa Wizara zilizo chini ya usimamizi wa Kamati hii Mhe. Ummy Mwalimu (Mb), Waziri wa Afya na Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Naibu wake Mhe. Hamis A. Kigwangalah (Mb), Mhe. Nape Moses Nnauye (Mb) Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Anastazia James Wambura (Mb), Naibu Waziri, na Mhe. Prof. Joyce Ndalichako (Mb), Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia na Naibu wake Mhe. Eng. Stella Manyanya (Mb) pamoja na

Makatibu Wakuu wa Wizara na Watendaji wote wa Wizara hizo kwa ushirikiano walioipa Kamati kwa kipindi cha mwaka mzima, kwa kufika mbele ya Kamati na kutoa ufafanuzi mara zote ulipohitajika. Namshukuru pia Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Watendaji wake kwa kazi nzuri waliyofanya ya kutoa miongozo ya kisheria wakati wote wa uchambuzi wa Miswada yote iliyochambuliwa na Kamati hii.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya kipekee nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati kwa weledi na umahiri waliouonesha wakati wote wa kutekeleza majukumu ya Kamati kwa mwaka mzima. Wajumbe wamefanya kazi nzuri kuhakikisha Kamati inaisimamia vyema Serikali kwa mujibu wa Katiba ya nchi na kwa maslahi ya Taifa zima. Napenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa majina kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Peter J. Serukamba, Mb | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Mussa A. Zungu, Mb | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Hussein Mohamed Bashe, Mb | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Peter Ambrose Lijualikali | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi, Mb | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Kasuku Samson Bilago, Mb | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Dkt. Elly Marko Macha, Mb | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Lucia Ursula Michael Mlowe, Mb | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Dkt. Jasmine Tiisekwa, Mb | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Ahmed Ally Salum, Mb | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Susan Anselm Lyimo, Mb | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Juma Selemani Nkamia, Mb | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Selemani Said Bungara, Mb | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Zitto Zuberi Kabwe, Mb | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Boniphace Mwita Getere, Mb | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Bernadetha K. Mushashu, Mb | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mb | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Sikudhani Yassin Chikambo, Mb | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Savelina Silvanus Mwijage, Mb | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb | Mjumbe |
| 22. | Mhe. Grace Victor Tendega, Mb | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika**, kwa kipekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashililah, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg.

Athuman B. Hussein na Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati hii Ndg. Dickson M. Bisile pamoja na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Pamela E. Pallangyo na Ndg. Agnes F. Nkwera pamoja na Msaidizi wao Gaitana Chima kwa kuratibu vyema bila kuchoka shughuli za Kamati kwa mwaka mzima na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

### 4.2 Hoja

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kueleza shughuli zilizotekelezwa, Uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli za Kamati, maoni na mapendekezo mbele ya Bunge lako Tukufu, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

Peter Joseph Serukamba, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII**
**06 Februari, 2017**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza hizi taarifa na sasa tunaingia kwenye mjadala wa jumla na tutaanza na Mheshimiwa Susan Lyimo atafuatiwa na Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, baadaye atakuja Mheshimiwa Stephen Ngonyani na Mheshimiwa Riziki Shahari ajiandae.

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ya kwanza ili niweze kuchangia hoja hizi tatu muhimu sana ambazo kimsingi zinahusiana na maisha ya Mtanzania. Kipekee nitajikita zaidi kwenye masuala ya elimu, lakini sitaacha kuzungumzia masuala ya UKIMWI, madawa ya kulevya pamoja na masuala ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianzia na masuala ya madawa ya kulevya; hapa kwenye Bunge lako Tukufu mwaka 2005 tulipitisha Sheria ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya na sheria ile ilianzisha Mamlaka ambayo pamoja na mambo mengine ni pamoja pia na kukamata (ku-*arrest)* pamoja na kushikilia mali zao. Hivi karibuni tunaona ni jinsi gani mamlaka hii inaingiliwa; Mkuu wa Mkoa anaamua tu kutaja majina ya watu bila kufuata utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tuliambiwa Mheshimiwa Rais Mstaafu Jakaya Kikwete alikuwa na majina hayo na vile vile tukaambiwa Waziri wa Mambo ya Ndani Mheshimiwa Kitwanga amepewa majina hayo. Ni kwa nini tume hiyo au mamlaka hiyo isishughulikie majina hayo ili tupate uhakika wa nani anatumia madawa ya kulevya. Ni kweli kwamba janga hilo ni kubwa sana, lakini lazima utafiti wa kina ufanyike, kwa sababu mtu na *brand* yake na kujijengea jina ni kazi kubwa lakini kulifuta ni jambo la haraka sana. Kwa hiyo, naomba utaratibu wa kisheria ufuatwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la elimu. Mambo mengi yameongelewa, lakini niseme tu, ni wazi kwamba elimu ndio msingi wa Taifa lolote; hakuna Taifa duniani hapa lililoendelea bila kuwekeza kwenye elimu. Hata hivyo, kwa muda mrefu nchi hii imekuwa ikichezea elimu sijui kama ndio sera ya Chama cha Mapinduzi lakini kwa kweli inasikitisha sana. Amezungumza Mwenyekiti wa Kamati kwamba, Tanzania mfumo wetu wa elimu ni matatizo makubwa sana; hakuna nchi duniani yenye mifumo zaidi ya miwili katika elimu; Tanzania ndio nchi pekee yenye mifumo miwili ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani kuwe na shule za msingi ambazo *medium of instruction* (lugha ya kujifundishia na kujifunzia) ni Kiswahili wakati shule nyingine za *level* hiyo hiyo *medium of instruction* ni kiingereza. Pia tukiangalia tuna elimu za aina mbili; tuna elimu bure na elimu inayouzwa na matokeo tumeyaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii shule iliyokuwa ya kwanza Tanzania *Feza* ambayo wanalipa takribani milioni tano wanafunzi wametoka na *division one* na *division two; division one* 56 na *division two* wanafunzi watano au sita tu, lakini shule ya mwisho haina *division one, two* wala *three*, ina *divison four* wachache na *zero* zaidi ya 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukiangalia unaona wazi kwamba tuna matatizo makubwa sana ya mfumo wetu wa elimu na ndio sababu nitakuja pia na mapendekezo ya kuona ni jinsi gani tutaboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa ni kutokana na fedha kutopelekwa kwa wakati na hata zinapopelekwa zinakuwa zimechelewa; na haya yanajitokeza zaidi kwenye miradi mikubwa; na matokeo yake ni nini! Tuna miradi mikubwa ya hospitali; Hospitali ya Bugando tulitegemea kwamba wataweza kusimika mashine kwa ajili ya uchunguzi wa saratani; tunatambua

kuwa kanda ya ziwa ina *population* kubwa sana; lakini jambo hilo halijafanyika; leo watu kutoka kanda ya ziwa wanakuja *ocean road* ya Dar es salaam; wakati huo huo tumekuwa na utayari wa kujenga *airport* Chato ambayo iko kwenye kanda hiyo hiyo ya ziwa. Kwa hiyo ni lazima tuangalie *priority* zetu ziko wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua juhudi kubwa ambazo zimekuwa zikifanywa na Serikali kwenye maeneo mbalimbali, lakini juhudi hizo ni za watu binafsi, wamekuwa wabunifu. Kipekee nimsifie sana Profesa Mohamed Janabi, amejitahidi sana kwenye Hospitali ya Moyo ya Jakaya Kikwete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na juhudi hizi binafsi bado Serikali haioni kuwa kuna haja ya kupeleka fedha nyingi. Leo Hospitali ya Moyo ya Jakaya Kikwete imepewa Shilingi milioni 500 tu kati ya Shilingi bilioni nne ambazo wanazihitaji; wakati tunajua kwamba huduma zikiboreshwa kwenye ile hospitali ni rahisi sana watu wetu kutibiwa ndani na kwa maana hiyo Serikali itaweza kupata fedha nyingi sana za ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ushauri wangu, nadhani labda ile hospitali ibadilishwe jina iitwe JPM, Rais aliye madarakani sasa badala ya Kikwete labda sasa fedha zitakuwa zinatoka kwa sababu atakuwa madarakani. Naamini labda alivyokuwa Kikwete iliwezekana, kwa hiyo nashauri kwamba labda tukibadili jina likawa la Rais itasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kuzngumzia ni madeni ya Walimu, hili suala ni kubwa sana. Na-*declare interest* mimi ni Mwalimu. Katika kuboresha elimu jambo la kwanza la kuliangalia ni Walimu na si madarasa wala vitabu. Walimu wa Taifa hili wamedharauliwa kiasi cha kutosha, wamenyanyaswa kiasi cha kutosha. Haiwezekani leo Walimu wadai hata kama ni trilioni 1.06 au milioni 800; ni kwa nini hawalipwi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tuulizane, kada gani nyingine hapa Tanzania ambayo ina madeni makubwa kiasi hiki? Yaani leo Mwalimu anaweza kwenda kituoni asilipwe mshahara kwa zaidi ya mwezi mmoja; nani anayeweza kukubali jambo hilo? Kwa hiyo, upole wa Walimu usiendelee kuifanya Serikali iache kulipa madeni yao na kuwafanya kama watu wa mitaani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kubwa zaidi ni hili suala la uhakiki. Mimi sielewi *definition* yake kwa sababu haiwezekani Walimu waitwe kwenda kusimamia mitihani, wamalize kusimamia mitihani, leo ni takribani miaka miwili wanaambiwa wanafanyiwa uhakiki. Hivi una mhakiki mtu kabla ya kufanya kazi

au baada ya kufanya kazi? Kwa hiyo, haya ni mambo ambayo tunaona yanaleta mushkeli katika elimu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze, na bahati mbaya sana Mheshimiwa Mwenyekiti wangu wa kamati, kwenye mapendekezo mwishoni kuna mengi hakuyasema lakini niseme; kuna suala la wanafunzi walioondolewa Chuo Kikuu cha Dodoma. Naamini kabisa kwamba kuondolewa kwa wanafunzi wale haikuwa bahati mbaya ilikuwa ni makusudi kwamba majengo yale sasa yawe wizara za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanini nasema hivyo? Nasema hivyo kwasababu ukiangalia mwaka 2014 ulile twa Muswada wa Mrekebisho ya Sheria ya Bodi ya Mikopo hapa ili tuweze kuwaingiza wanafunzi ambao wataenda kusoma *special education* kwa ajili ya masomo ya sayansi. Leo hakuna Mbunge humu ndani ataniambia kwamba kwenye Jimbo lake hakuna shida ya walimu wa sayansi; na Mheshimiwa Jenista wakati huo Naibu Waziri wa Elimu alilihangaikia sana hili jambo, lakini leo wanafunzi wale wameondolewa, tunapewa sababu za ajabu ajabu, tunaambiwa walikuwa vilaza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapoambiwa jambo, wewe mwalimu unapoambiwa kuwa wewe ni kilaza; kilaza kwa wale wasiojua hii ni terminology, na watoto wa University of Dar es Salaam huko nyuma, ni watu ambao hawaelewi chochote yaani wajinga. Kwahiyo, unapowaambia walimu wajinga…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan Lyimo, ahsante.

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, si ya kwanza?

**MWENYEKITI:** Umemaliza, ni ya pili hiyo. Ahsante sana, nashukuru; tunaendelea na Mheshimiwa Victor Mwambalaswa.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana nami kunipa nafasi hii niwe mchangiaji wa pili kwenye hoja ambazo zimeletwa na wenyeviti wa Kamati. Kamati hizi mbili zimefanya kazi nzuri sana na wenyeviti mmetuletea taarifa ambazo zipo kamili, nawashukuru sana na nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nianze kwa kutoa mifano kama miwili hivi au mitatu. La kwanza kuna mkoa hapa nchini ambao miaka ya 70 nyani walikuwa wengi sana mkoani huko na walikuwa wanashambulia sana mahindi kiasi cha kuleta njaa kwa wananchi. Wananchi wa Mkoa huo wakaamua sasa kwamba nyani ni kitoweo, wakaanza kula nyani; wanakamata nyani wanakula, nyani wakatoweka kabisa na chakula chao kwa miaka iliyofuata kikawa salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa pili kuna mkoa mwingine miaka hiyo hiyo ya 70 ilivamiwa sana na nzige; wananchi wa mkoa huo wakaamua kwamba nzige ni chakula wakawa wanakamata sana wanakaanga, wanakula; nzige wakatoweka. Maana yangu ni kwamba kukitokea maovu zipo njia nyingi za kuyashambulia ili yaishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano madawa ya kulevya ni ovu, yanaharibu wananchi na *society*; kwa hiyo, inaweza kutumia njia zozote kushambulia mpaka ziishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wizi ni dhambi; mwenye mamlaka ya kukamata mwizi ni polisi; sasa mtu akija shambani kwako anaiba mahindi unaogopa kukamata kwa sababu sio kazi yako kumkamata unasema ni kazi ya polisi utavuna mabua. Nadhani tutumie njia zote ili kuhakikisha kwamba maovu kama madawa ya kulevya yanatoweka nchini kwetu. Anakamata nani ni suala lingine, nani anayekamata ni kwenye vyombo vinavyohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka baada ya hapo niongelee masuala mawili tu machache ambayo Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ameweka mezani. Nianze na Hospitali ya Rufaa ya Benjamin Wiliam Mkapa ambayo ipo hapa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali za rufaa hapa nchini zipo tano au sita; Muhimbili, Bugando, *KCMC,* Mbeya na Benjamin Wiliam Mkapa. Hiyo hospitali ya Benjamin Wiliam Mkapa ni kama Jakaya Kikwete *Heart Institute;* ina vifaa vya kisasa kweli kweli lakini watumishi hakuna. Ile hospitali ilikuwa na madaktari wanajitolea; vijana kutoka vyuoni wanajitolea wako pale kama saba au nane, wamejitolea kwa zaidi ya mwaka mmoja; wanasubiri Serikali itakaporuhusu ajira waweze kufikiriwa nao, sio kulazimisha Serikali kuwaajiri bali waweze kufikiriwa kuajiriwa. Mkurugenzi wa hospitali hiyo baada ya vijana kutumika pale amewaondoa, halafu baada ya miezi miwili baada ya kuwaondoa amewarudisha baadhi yao wengine amewaacha huko mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wenyeviti wa Kamati mlishughulikie suala hili, naona kama si haki hata kama Serikali imesitisha ajira lakini hawa vijana wamejitolea kuokoa maisha ya wananchi; na hawasemi kwamba utakapokuwa tayari kuajiri waajiriwe wao, hapana; wanajitolea tu na uwape posho kidogo, naomba Wenyeviti mlichukue hilo na mlishughulikie ili muweze kuishauri Serikali vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye hospitali hiyo hiyo kama nilivyosema ina vifaa vya kisasa kweli kweli, sasa hapo mimi huwa naenda kutibiwa; kuna mashine ya *MRI (Magnetic Reasoning Imaging)* ya kisasa kweli kweli, haijafungwa bado ipo pale imekaa tu na mtu anayetaka kipimo cha namna hiyo inabidi umpeleke Muhimbili au kwingine lakini mashine iko hapa, kwa nini haifungwi? Tunahitaji lazima Mheshimiwa Rais atoe amri ya kufunga hiyo mashine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko mashine ya *CT Scan* ya kisasa kwelikweli, haijafungwa; iko mashine ya *X- Ray,* sasa hivi wanatumia *mobile mashine ya X-Ray; i*ko mashine ambayo ni *fixed*, kubwa, ya kisasa kweli haijafungwa; tunahitaji nani aje atuambie tufunge hizo mashine? Mheshimiwa Mwenyekiti na Kamati yake naomba sana walishughulikie suala hili, waishauri Serikali iweze kufunga vifaa hivi na kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye Hospitali ya Muhimbili, kama alivyosema Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii; Taasisi ya Jakaya Kikwete inafanya kazi nzuri sana, imepunguza Watanzania kwenda kutibiwa nje; unafanya vipimo na unatibiwa hapa hapa, naipongeza sana Serikali kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge mwenzangu aliyetangulia, tuiangalie taasisi hiyo, ipewe pesa ya kutosha ili lengo lake la kupunguza kabisa na kuweka sifuri ya Watanzania kwenda kutibiwa nje litimie. Kwa hiyo, namwomba Mwenyekiti wa Kamati waliangalie vizuri hilo na kuweza kuishauri Serikali; hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa hapo hapo, kuna Mturuki ambaye ametoa fedha kwa Muhimbili; amejenga maabara pale Muhimbili, Maabara ya *Hermatology* ya kupima kwa ndani sana vipimo vya mwili na damu mpaka kwenye *details* za vinasaba. Ameijenga maabara ile, iko pale, ame-*train* Watanzania sita au saba wa kuweza kui-*manage* hiyo maabara ili Serikali, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na hospitali nyingine ziachane na kupeleka sampuli Nairobi, Afrika Kusini, Uingereza na Marekani ambako tunatumia fedha

nyingi sana. Hiyo maabara ipo tayari na naambiwa Kamati wamepita hapo na kuna vifaa vingine amevituma vipo njiani vinakuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Hospitali ya Muhimbili haipeleki hizo sampuli kwenye maabara hiyo ambayo ipo mlangoni hapo, bado inapeleka Afrika Kusini, Uingereza na Marekani, kwa nini? Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati naomba hilo alishughulikie aishauri Serikali vizuri. Maabara iko pale, mtu wa Mungu ameijengea Tanzania; tuitumie hiyo ili iwe kama ilivyo Taasisi ya Jakaya Kikwete kupunguza kupeleka fedha zetu nje ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii, naomba kuunga mkono hoja za Kamati zote mbili.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Stephen Ngonyani na baadaye Mheshimiwa Riziki Shahari ajiandae.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mimi nianze kwa kurudia tena kuwashukuru Wabunge wenzangu wote ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile nirudi tena kuwashukuru kwa msaada mkubwa ambao Wabunge walinipatia nikiwa hospitalini nikiwa nimelazwa. Sitaacha kulisema hili kwa sababu wala sikutarajia, wala sikutegemea kama Wabunge wangejitokeza na kunipa misaada mbalimbali, Mungu awabairiki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nimshukuru sana Waziri wa Afya pamoja na Naibu wake, Katibu Mkuu pamoja na Daktari wa Muhimbili, wamefanya kazi kubwa sana ya ziada. Sitaacha kulisema hili kwa sababu unapopata nafasi lazima uliseme. Bila Waziri wa Afya kulisimamia kidete kunipeleka mpaka ofisini kwake na kunihakikishia barua yangu inapita, nisingefika na leo hii nikaja kusimama na Wabunge wenzangu ili nitoe neno la shukurani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisimamie suala moja tu la *insurance*, Bima ya Afya. Katika muda ambao nimekaa hospitalini nikiangalia bima ya afya inatakiwa iboreshwe kwa hali ya juu sana; kwa sababu kama sisi tunapewa vile vitambulisho vya *V.I.P* halafu kuna wengine wakulima ambao hawana vitambulisho vya *V.I.P*; lakini sisi tuliopewa vitambulisho vya *V.I.P* tunaambiwa tukanunue dawa nje za kutibiwa maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba unapokatwa hela yako ni kwamba utibiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Jubilee* walikuwa wanatukata hela hapa, tulikuwa tunasafiri mpaka India. Tunakwenda tunatibiwa wala hatupati shida ya aina yoyote. Leo tumesema haya mambo yote yarudi katika upande wa Serikali, lakini cha kushangaza leo hii mtu ameugua Mombasa, ameumia, anakwenda na *insurance* yake anaambiwa hii haitambuliki hapa, basi matokeo yake inafika mahali anafika mwingine anawekwa dhamana kwa sababu ya mtu. Kitendo hiki kimetudhalilisha sana sisi Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekaa hospitalini, nimetibiwa kwa muda wa karibuni siku 27 katika Hospitali ya Mikocheni, nimehudumiwa kila kitu lakini vipimo vya gharama kubwa nimelipiwa na *insurance*. Kipimo kidogo cha gharama ya 30,000 naambiwa nikanunue nje, sasa nini maana ya Bima ya Afya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Bima ya Afya sisi Wabunge ambao tunazipitisha hapa yanafanyika haya, je huyo Mtanzania wa chini ambaye hana uwezo kabisa atakuwa amefika wapi? Naomba Wenyeviti, mmetuletea hili jukumu, kwa kweli Serikali tunataka waiboreshe sana Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiini cha matatizo ni Wizara ya Afya kutengewa hela ndogo ndogo ambazo hazina msingi; kwa sababu Wizara ya Afya peke yake; nimetoka India juzi, kule Wizara inadaiwa zaidi ya bilioni 37 na bado wanatakiwa Wizara ya Afya itusaidie sisi Watanzania tulioko ndani ya nchi. Sasa hivi kule watu wanaanza kukata tamaa kutuhudumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo; hatukatai kwamba Serikali imejitolea sana kwa hali na mali na mimi naishukuru sana Serikali ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli inafanya kazi ya ziada sana; tunapofanya mambo haya tuangalie na utaratibu kwamba hii Wizara tunaisaidia kiasi gani. Hakuna kitu kibaya kama mtu; afadhali ukose chochote, lakini upate elimu na upate afya bora. Bila Wizara ya Afya kunisimamia kidete, bila Bunge kunisimamia kidete, bila ya Rais kunisimamia kidete, leo hii nilikuwa nakatwa mguu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba sana; Wenyeviti wa Kamati wametuletea mapendekezo lakini hii Wizara ya Afya inapata hela lakini hela zake hazitoshelezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii katika vijiji, wananchi wameamua kujenga zahanati lakini wameamua kujitolea wenyewe, kwangu wamejitolea kujenga zahanati lakini zahanati hizo hazisaidii chochote kwa sababu ukienda Wizara ya Afya unakuta watu wanakaa pale kusaidia lakini inafika mahali

watachukua wapi hela ili ziende kule vijijini zipeleke dawa? Dawa zipo kweli, lakini namna zile dawa zitakavyotumika vijijini lazima na sisi tuwaunge mkono hawa, lazima na sisi Wabunge safari hii tuhakikishe hii Wizara inapatiwa hela ya kutosha ambayo itatusaidia ili kuboresha mambo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitasema kweli daima fitina kwangu mwiko. Kwa kweli Wizara ya Afya ni kiungo muhimu sana kwa mwili wa binadamu. Leo hii angekuwa ameugua mtu mwingine ningesema labda wanatutania, nimekaa siku 27 Mikocheni, nimekwenda Muhimbili kwa Mkurugenzi wa mifupa nimeona shida wanayoipata. Nimeenda Wizarani nimeona wanavyohangaika, wanahangaika kweli kweli kutusaidia lakini hela hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wenyeviti mfanye mambo yenu yote lakini hebu jaribuni kumsaidia Dada Ummy. Yeye kama Ummy ni Waziri, yeye kama yeye hawezi kupitisha chochote lazima ninyi Wenyeviti na nyie mtilie mkazo. Sasa mnapotilia mkazo baadhi ya mambo wakati mnafikiria kwamba yeye atakwenda kutafuta hela sehemu nyingine tunakuwa tunamuumiza na Serikali hii tusitarajie kila kitu watufanyie Serikali na sisi wenyewe tujitume ili tufanye mambo mazuri ili tufanikiwe vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana hii *insurance;* na Mwenyekiti akija aje na jibu *Jubilee* ilifanya makosa gani na kwa nini iliondolewa? Kwa nini ilikatwa? Kama ilikatwa tukaamua kuliweka Shirika la Bima la Serikali ni tatizo gani lisiwe linafanya kazi katika nchi hizi tatu za Afrika Mashariki ili itusaidie hata wengine badala ya kwenda mbali zaidi; hata Afrika ya Mashariki unaweza kupata huduma ya kutosha tukashughulikiwa na *insurance*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya nirudie kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu, walinipa matumaini makubwa sana, hawakujali vyama vyao, hawakujali mimi ni nani, walinifanya nikawa najisikia kwamba si mnyonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nisiache kumshukuru Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, nisiache kumshukuru Naibu Spika, nisiache kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Kashililah, walikuwa wananipa moyo wa dhati. Hatua ya mwisho nilikuwa nakaa ofisini kwa Naibu Spika akiniambia subiri subiri na leo subiri hii nimeweza kuja hapa, Mungu awabariki sana Waheshimiwa Wabunge, Mungu awabariki sana Serikali ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitakuwa na mengi ya kuongea ila nilikuwa tu nataka nikazie hii *insurance* kwa sababu ikifika mahali hospitali nyingine ukienda hutibiwi bado hatujasaidia Watanzania. Kama umepewa *insurance* basi kila hospitali unayokwenda unatakiwa utibiwe kwa kutegemea ile kadi uliyopewa. Leo hii unachaguliwa baadhi ya hospitali, hospitali nyingine wakikuona wanakuona vile kama kituko, sasa kituko maana yake ni nini? Tunakatwa hela, wanazichukua halafu kwenye huduma unaambiwa dawa nyingine ukanunue wewe mwenyewe wakati umekaa hospitalini….

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa nakushukuru sana.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya Mungu atubariki, naunga mkono hoja ya viongozi hawa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Riziki Mngwali.

**MHE. RIZIKI S. MNGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi; nami nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia neema kubwa ya uhai na uzima na afya na tukawa hapa. Nimpongeze kaka yangu aliyemaliza kuzungumza Mheshimiwa Maji marefu kwa kutimiza ada muhimu sana. Mafunzo yanasema ukitendewa jema basi mshukuru yule aliyekufanyia jema mpaka ahisi kwamba ameshukuriwa. Naamini Waheshimiwa Wabunge na wote uliowashukuru walihisi kwamba umewashukuru na sisi tunamshukuru Mungu kukurejesha tena hapa hata tukawa na wewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, babu zangu wa Kimwera wanasema hizi Kamati hizi *they have seen it all.* Kwa kweli Kamati zimefanya kazi, Wenyeviti wao wametuletea hapa taarifa, hakuna kilichobaki humu; na wachangiaji walionitangulia nao wamechangia, wamesema waliyoyasema, sasa hayo nitakayoyasema mimi itakuwa ni nyongeza tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la kuchezea elimu. Elimu nchi hii tunaikoroga, elimu nchi hii tunaichezea na hatujiamini bado kama elimu ndiyo ufunguo wa maisha ingawa huo msemo upo kila mahali, elimu ni ufunguo wa maisha, lakini matendo yetu hayaendani na hilo. Naomba tu kwa msisitizo kabisa, hebu Serikali ibadilike. Waheshimiwa Wabunge humu wameshasema sana kuhusu suala la elimu, *its time now.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii ya CCM miaka yote hiyo iliyopita ni CCM tu hakuna ya Rais huyu, Serikali ya CCM, sasa ibadilike, ione kwamba ina jukumu la kusimamia elimu na elimu ni kweli iwe ufunguo wa mambo yetu yote yanayofuata. Dada zangu mmepewa Wizara hili tutawapima tu! Kwa hiyo, Profesa na Msaidizi wake wajipange kwenye elimu, mabadiliko tunayataka, yenye uweli si haya ya kutubadilishia mara mtaala, mara nini, hapana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la UKIMWI; na hili nalisema kwenye kipengele cha utegemezi. Wataalam wameimba kuhusu madhara ya kutotumia dawa ipasavyo. Mgonjwa wa UKIMWI ukishamkatizia dozi yake, iwe ile ya dozi yenyewe au ile inayoitwa dawa za kuondoa magonjwa nyemelezi, unamuathiri zaidi kwa sababu vile vijidudu vinajenga usugu; sasa tunashangaa nini inapoonekana kwamba haya maradhi hayaondoki na maambukizi yanazidi kwa sababu hata hiyo tiba yenyewe hatuifanyi swa sawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la utegemezi; kila mahali Kamati imetuambia hapa; kuanzia utafiti, kutoa hizo huduma zenyewe za madawa tunaambiwa wafadhili ndio wafanye hivyo. *MCC* hiyo arijojo, imeshaondoka sasa sijui tuna nini mbadala kwenye suala hili ambalo kwa kweli ni janga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla wake taasisi zetu za huduma muhimu haziko sawa. Tunajua hali za hospitali zetu, zahanati zetu, vituo vyetu vya afya, wamesema hapa na Kamati zimesema; lakini pia tunajua hali ya shule zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miezi kadhaa nilipita mahali kule Jimboni kwetu, kuna eneo Kaskazini kunaitwa Bweni nilikuwa nakwenda Bweni sasa hapo katikati unapita mahali panaitwa Kirongwe. Tulikuwa tunapita kwa haraka kwa gari lakini nikaona watoto kama wanacheza cheza hivi kwenye majengo mabovu sana. Sasa nikawa nauliza wale wenzangu, hiki hapa ni nini? Wakaniambia ndiyo shule ya msingi Kirongwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikasema watoto wanakuja kwenye majengo haya? Hizi ndiyo shule zetu lakini hapa Serikali Kuu inatuambia kwamba Halmashauri ndizo zishughulikie hizo, Halmashauri ambazo tayari zimeshaondolewa uwezo wa kusimamia hayo kwa maana ya kupunguziwa vyanzo vyao vya mapato. Sasa sidhani kama kweli tunataka kuleta maendeleo kwenye jamii hii kwa sababu mambo yetu maneno ni mengi kuliko utekelezaji na matendo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wimbo huu wa ufinyu wa bajeti na sasa umekuwa wimbo wa kutopeleka pesa zilizopangwa, sasa kuna haja gani ya kufanya hii *budgeting process?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkutano uliopita nilisema hapa kwamba hivi hii bajeti ya nchi yetu kwa nini isiwe mchakato unaojitegemea, yaani uliounganika yaani *intergraterd process* ya *budgeting?* Ndiyo maana tunapata haya matatizo. Tunazungumzia hiyo semina elekezi, semina elekezi si lazima tuambiwe A, B, C lakini semina elekezi pia isaidie kupanga pia vipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa Mawaziri wote wakikutanishwa pamoja waka-*brainstorm* kwa pamoja jamani vipaumbele mwaka huu ni nini? Haya matatizo, kwamba kule hakukupelekwa, huku hakikutolewa hayatotokea tena, au angalau yatapungua kwa asilimia kubwa; lakini kila mtu hapa anakaa peke yake, anasema ana vipaumbele, vipaumbele vyenyewe vinakuwa zaidi ya 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila anayesimama hapa kipaumbele, kipaumbele mwisho wake tunaimba hii kila siku nenda rudi ni yale yale hatubadiliki, tatizo ni nini jamani? Wasomi ndio hao na kama kuna Serikali imejaa maprofesa ndiyo hii, hebu tuone basi mabadiliko. Hizo elimu na ujuzi wenu wekeni kwenye vitendo ili tuone kweli ninyi mnataka, mnaambiwa mainjinia; tulikuwa tunawaita ma-*spanner boys;* basi na wao wafanye kazi ya vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezungumzwa pia suala la kutaka ufafanuzi kuhusu kuwepo au kutokuwepo kwa madawa; tena hili mimi naomba litolewe maelekezo kweli kweli. Huo ufafanuzi uwe ufafanuzi wa kweli. Kwa sababu Serikali ikizungumza kupitia Mawaziri wake iwe wa Afya au wa TAMISEMI unaona pepo kabisa kwenye zahanati, lakini wakisimama wale watumishi wetu walioko kule ma-*DMO* na wengine unaona ufukara uliokithiri, tatizo ni nini hapa? Mawaziri wanatuambia madawa yamejaa, sijui *basket fund* imeleta kila kitu, *DMO* akisimama akikwambia unaona kabisa ana-*negative* wala hata siyo *zero*, hili tatizo liko wapi? Hebu watupe maelekezo ya kutosha kwamba dawa zipo au hazipo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nimalizie kwa kusema kwamba na mimi ni-*declare interest* na mimi ni Mwalimu. Dada yangu Mwalimu Susan amesema Walimu wamedhalilishwa kiasi cha kutosha na kuonewa kiasi cha kutosha, sasa huu msemo unaishia kusema na tunasema sasa basi. Hebu Walimu wa nchi hii wapewe hadhi yao, wapewe haki zao, Walimu hawa wanadhalilika. Niliwataja siku moja hapa Walimu walionifundisha toka shule ya msingi wengine

wakasema wako hai, wako hai baadhi wa miaka 70 na, lakini ukiwaona unaona huyu mtu aliishi na anaendelea kuishi japo ameshazeeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu wetu wa sasa ndio watu dhalili, dhalili mpaka kwenye jamii yenyewe hawathaminiwi. Mwalimu anafika mahali anamwogopa mwanafunzi wake kwa sababu mwanafunzi anatoka kwenye hali ya juu kuliko Mwalimu. Kwa sababu gani Walimu wetu wanafanywa kuwa ombaomba, watu dhalili, watu wasiothaminiwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mateso wanayopata Walimu; Mwalimu Susan amesema kama unataka kuboresha elimu anza na Mwalimu. Mwalimu ambaye mmemjali yuko tayari kuchukua watoto wake akawafundishia chini ya mwembe na wakapata elimu bora, lakini Mwalimu ambaye umemdhalilisha, umemdharau, hata ungemjengea chumba ambacho kina feni na viyoyozi hatafundisha na watoto wale wakafundishika. Jamani hebu tuangalie mzizi wa tatizo uko wapi na tuutatue ule, tusihangaikie matawi, matawi hayajengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa nafasi uliyonipa na niwapongeze tena Kamati hizi kwa kazi nzuri na niseme naunga mkono hoja yao. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Riziki. Tunaendelea na Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani na baadaye atafuata Mheshimiwa Edward Mwalongo.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nomba nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia taarifa hii ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii na Kamati ya UKIMWI. Namshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenipa uhai ili niweze kusimama hapa siku hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la elimu bure. Nichukue nafasi hii kuipongeza sana Serikali kwa kuthubutu kuweza kutekeleza elimu hii bure. Dhamira ni njema, lakini katika mpango huu bado kumekuwa na changamoto nyingi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la elimu napenda kuzungumzia kwamba elimu bure sawa inatolewa, lakini pia ukienda kwenye shule zetu za *primary* na za *secondary* kumekuwa na changamoto ya upungufu wa madarasa; lakini bado katika Mkoa wangu wa Ruvuma kuna changamoto katika Wilaya ya Namtumbo katika sekondari ya Nungu Kata ya Hanga.

Kwenye hiyo sekondari ambayo sasa imeanza kidato cha tano; na changamoto iliyoko hapo inafanana kabisa na changamoto iliyoko katika Wilaya hiyo hiyo katika sekondari ya Nasulu Wilayani Namtumbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu sekondari hizi zilipoanzishwa kwa kidato cha tano hawajapelekewa pesa kwa ajili ya chakula. Kwa hiyo niombe, tunapoamua kutoa elimu bure ni vizuri basi tukajikita kwenye mambo ya msingi. Kwa mfano; mtoto hawezi kuendelea kusoma na akajituma vizuri zaidi na kuweza kuwa msikivu katika masomo kama hatakuwa amepata chakula. Wazabuni ambao wamejitokeza kutoa huduma katika shule hizi wameshafanya kwa kiasi walichoweza, lakini imefika mahali wanakwama kwa sababu hawajawezeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa Walimu pia unachangia kwa kiasi kikubwa. Hili ni eneo ambalo wajumbe wenzangu wengine Waheshimiwa Wabunge wamechangia; kwamba bado maboresho dhidi ya Walimu hawa yanatakiwa ili Walimu waweze kuwa na moyo wa kuendelea kutoa huduma hii ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende pia kwenye suala la afya katika Wilaya hiyo hiyo ya Namtumbo. Hospitali hiyo inajengwa kwa takribani miaka mitano sasa na haijakwisha. Mpaka sasa hivi ninavyozungumza, hospitali hii ya Wilaya ya Namtumbo bado ina jengo la *OPD* tu, hakuna wodi wala hakuna *theatre*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wilaya ya Namtumbo ni wilaya kubwa sana na imejumuisha kata nyingi, zaidi ya kata 23, bado wilaya hii inahudumia pia mji mdogo wa Lusewa; Wizara ingefanya jitihada za makusudi kuhakikisha kwamba hospitali hii ya Wilaya inakwisha ili iweze kuendelea kutoa huduma kwa sababu akinamama wengi wajawazito wanapata shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hizi kata zilizopo pale katika Wilaya ya Namtumbo nyingi zimekuwa kwenye maeneo ya mbali. Unakuta kutoka kwenye kituo au Makao Makuu ya Wilaya kwenda kwenye maeneo ya pembezoni, maeneo mengine yanafikia kama kilometa 100, kilometa 70 na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kwenye Wilaya hii ya Namtumbo, kwa maana ya Hospitali ya Wilaya, angalau ingekamilishwa wodi ya akinamama ili kuweza kuwafanya akinamama waweze kujifungua salama. Kwa mfano; kuna kituo hiki cha Lusewa; Kituo hiki cha afya cha Lusewa kimekuwa kikihudumia

wanawake ambao wakati mwingine wakizidiwa wanajikuta wanalazimika kwenda katika hospitali ya Mbesa ambayo iko karibu kilometa 150 kutoka Wilayani Namtumbo na usafirishaji wa akinamama hawa wakishakuwa kwenye hali mbaya mara nyingi wamekuwa wakibebwa na pikipiki. Yanatengenezwa matenga huku nyuma, wanawekwa kwenye matenga ili waweze kusafirishwa ili kufikishwa kwenye hospitali ya Mbesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana, mama yangu Ummy, naomba asikie kilio hiki cha wanawake wa Mkoa wa Ruvuma ili waweze kusaidiwa kwenye eneo hili ambalo imekuwa ni eneo tete sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende pia kwenye Wilaya ya Tunduru katika zahanati ya Legezamwendo. Zahanati ya Legezamwendo ni zahanati ambayo imezungukwa na vijiji karibu sita; zahanati hii bado haijakamilika na sasa hivi tayari inakaribia miaka minne. Niombe basi zifanyike jitihada za makusudi kuhakikisha kwamba fedha zinakwenda ili zimalizie zahanati ile ili iweze kutoa huduma kwa wananchi ambao kimsingi baadhi yao tayari wameshapewa hata zile kadi za *CHF* ili waweze kuzifanyia kazi hizo kadi zao na waweze kupata huduma ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika katika Hospitali ya Wilaya ya Tunduru. Hospitali ya Wilaya ya Tunduru ni ya muda mrefu sana ambayo inahudumia karibu Halmashauri mbili zenye zaidi ya Kata karibu 54; na unapoambiwa Kata zaidi ya 54 kwa Wilaya ya Tunduru ni eneo la kilometa za mraba nyingi mno kiasi ambacho kutoka kituo kimoja mpaka kufika Hospitali ya Wilaya ni parefu mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe miundombinu ya Hospitali ya Wilaya ya Tunduru iweze kuboreshwa ili wale wote wanaopata huduma katika hospitali ile waweze kupata huduma stahiki. Ingawaje sasa katika hospitali hiyo kumekuwa na mrundikano mkubwa sana wa wagonjwa kiasi ambacho hospitali inazidiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wakati tunaendelea kufanya miundombinu mingine, nadhani tuanze na hii Hospitali ya Wilaya tuiangalie ili tuweze kupata *theatre; theatre* ipo lakini ipanuliwe zaidi ili kuendelea kuboresha huduma hizi. Pia madawa na vifaa tiba viongezeke mara dufu ya vile vinavyotolewa sasa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa*

*muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani ahsante.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Edward Mwalongo na baadaye tutamalizia na huyu Waziri Kivuli wa Sera, Bunge, Kazi, Vijana na Dawa za Kulevya, Mheshimiwa Ester Bulaya kwa dakika tano.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia kwa Kamati ambazo zimewasilishwa mbele yetu leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la elimu. Kwanza kabisa niwaondoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge wenzangu na tuipongeze Serikali yetu kwamba mfumo wetu wa elimu ni mzuri sana, mfumo wa elimu ni mzuri sana. Tatizo kubwa tulilonalo ni jinsi ya kuusimamia, hapo ndipo shida inapoanzia kwamba uwezo wetu wa kuusimamia mfumo mzuri huu uko chini mno, hatuwezi kabisa kuusimamia huu mfumo. Kwa hiyo, sasa kinachokuja kutokea baadaye ndio maana tunapata matokeo mabaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano watu wanalalamika kusema watoto ujasiriamali, watu wanatoka wanamaliza mpaka vyuo vikuu hawawezi kujitegemea, sio kweli. Wasioweza kujitegemea baada ya kumaliza elimu hizi katika mfumo tulionao ni kwamba wao wenyewe tu hawako tayari kujituma, kwa sababu wanalazimisha kufanya vitu ambavyo wamesomea vilevile tu kama yeye amesoma *degree* ya sheria analazimisha akawe mwanasheria, lakini tunachosema kwenye elimu maana yake umepanua maarifa, licha ya kufanya hiyo taaluma maalum uliyosomea, lakini maarifa uliyapata, njia nzima uliyopita yanakuwezesha kuishi maisha mengine. Kwa hiyo, kila msomi anapaswa kuongeza akili ili aweze kutumia maarifa aliyopata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mfumo huu wa elimu ambao sasa tumeanza tunaita elimu msingi lipo jambo ambalo naiomba sana Serikali iangalie na ijaribu kutoa taarifa za mara kwa mara na kuna wakati nilishauri hapa kwamba kingekuwepo chombo fulani kinachoweza kuzungumza mara kwa mara juu ya hii elimu msingi; kwa sababu katika elimu msingi ifikapo mwaka 2021 itakuwa kwamba kidato cha kwanza kutakuwa na mikondo miwili, maana yake kutakuwa na wale walioishia darasa la saba na kutakuwa na wale

walioishia darasa la sita na hawa wote wanaenda kusomea shule hiyo hiyo ya sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ukiwauliza wataalam wa elimu wanasema kwa sababu tumefikia asilimia 75 ya ku-*recruit* watoto wote shuleni. *Definetly* watakapokuja hao wengine na wenyewe wataingia kwenye mfumo huo, lakini miundombinu tuliyonayo kwenye shule zetu za sekondari bado ni kidogo mno, hatuna madarasa ya kutosha, maabara zile hazitakaa zitoshe kama ni ma-*hall* au mabwalo yatakuwa hayatoshi. Lakini vilevile shule nyingi mpaka leo bado zinajengwa mpaka leo bado zinajengwa; shule nyingi hazina madarasa, misalani ya kutosha na miundombinu chungu mzima ambayo inatakiwa watoto hawa iwatosheleze. Sasa tunaenda na huu mfumo wa elimu msingi ambao watoto wote sasa kufikia mwaka 2021 wote watakuwa wanaendelea na sekondari bila kuwabakiza au bila kuchagua pale katikati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni muhimu sana serikali ikaona ni namna gani itajipanga vizuri. Niipongeze imejaribu kuwaelimisha walimu, tumeona; pamoja na changamoto zilizokuwepo za walimu kufanya migomo hawapati posho za kutosha na nini kwenye yale mafunzo ya kuwapa hii elimu msingi, lakini angalau mmeliona hilo na katika sera mpya ya elimu mnajaribu kulifanyia kazi. Lakini kazi iliyobaki sasa ni kufanya maandalizi ya kutosha kuandaa, miundombinu ya kutosha na kuelimisha wananchi kwasababu watoto wale na wazazi hawaelewi mpaka sasa kama wataishia darasa la sita; ni vizuri sasa wakaelimishwa wakajiweka tayari kwamba tunaishia darasa la sita halafu tunaendelea na kidato cha kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni kwamba Wizara ya elimu iache mikanganyiko; wapo maafisa kwenye Wizara ya Elimu wakiulizwa na wenyewe hawajui. Mahali kama Wizara ya Elimu na TAMISEMI ndipo tunapotegemea tupate majibu sahihi, wananchi wanapouliza maswali kama haya ya elimu msingi ni lazima watumishi na watendaji katika Wizara ya Elimu na TAMISEMI wawe na majibu sahihi. Kwa hiyo, nafikiri pamoja na hii sera ya elimu msingi ni vizuri sasa Wizara ya Elimu ikatengeneza hata vipeperushi tu kutoa hii elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuwa ipo Idara ya Ukaguzi ambayo ni idara ya udhibiti wa elimu; idara hii hatujaitendea haki; kwanza haina vitendea kazi na pili ina wakaguzi wachache sana. Sasa katika kuendesha elimu ndipo tunaposema mfumo wetu ndio wenye matatizo, kwenye elimu kuna mtaala, udhibiti ubora halafu kuna Baraza la Mitihani kwa ajili ya kutoa mitihani. Hawa wanaodhibiti ubora wao ndio wanaosimamia kuona mitaala inatekelezwa vilivyo? Halafu Baraza la Mitihani kazi yake ni kuleta

mtihani na kufanyisha mitihani. Sasa unakuta kwamba hii Idara ya Ukaguzi haifanyi chochote na matokeo yake ni kwamba hawa wanaosimamia mitaala kwa maana ya walimu, shule na wanafunzi wenyewe wanaosoma halafu wanakuja baraza wanatoa mtihani.

Sasa naomba Serikali iangalie itafanyaje kuwezesha hii Idara ya Udhibiti Ubora kweli iwe Idara ya Udhibiti Ubora, kinyume chake idara hii kama isipopewa vitendea kazi, wasipokuwepo wakaguzi wa kutosha haina uwezo wa kusimamia elimu yetu. Kwa hiyo, mapungufu mengi tunayoyaona yapo kwenye hii Idara ya Udhibiti Ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiacha suala la elimu, nije kwenye suala la afya. Suala la afya yapo matatizo sio makubwa sana lakini ningependa niyasemee kidogo kwamba ipo shida ya tiba kwa watoto, huduma ya bure kwa watoto, wazee na akinamama wajawazito. Huduma hizi zinapotolewa zinaingiza gharama na wanaoingia gharama ni wale wanaosimamia ile hospitali kama ni Halmashauri ndio inaingia gharama. Sasa utaratibu wa Serikali kurejesha zile gharama ambazo Halmasahauri zimeingia upo chini sana. Kwa hiyo, niombe sana Serikali ione ilete zile fedha ambazo Halmashauri zimeingia gharama kutoa huduma kwa watoto, wazee na wajawazito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine ambalo ningependa kuishauri Serikali itusaidie linaweza likawa ni la kwenye Halmashauri lakini tamko la Serikali lingeweza kutusaidia; matumizi ya magari ya wagonjwa. Mara nyingi sana tumeona magari ya wagonjwa ndio yanatumika kusafirishia wafu, sasa ni kinyume kabisa cha utaratibu yaani haiwezekani Halmashauri ina *ambulance* moja halafu *ambulance* hiyo hiyo bahati mbaya mtumishi amefariki inaondoka inaenda kilometa 800 kusafirisha mwili wa mtumishi aliyefariki, halafu Halamsahuri inabaki bila gari la mgonjwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeomba sana tamko la Serikali litolewe kwamba magari ya wagonjwayatumike kubebea wagonjwa, iwe ni bahati mbaya tu huyo ndugu yetu tunayemsafirisha kama mgonjwa amefariki ndio tunaweza kusema gari hiyo itumike kumrudisha alipotoka. Lakini kutumia gari la wagonjwa kwa lengo la kumpeleka marehemu kumsitiri hii sio sawa na wala sio sahihi kwa sababu inaacha pengo halafu Halmashauri inabaki haina gari la wagonjwa. Ningeomba sana Serikali ione hili na iweze kulikemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante, muda wako umekwisha.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naunga mkono hoja za Kamati kama zilivyowasilishwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, tunamalizia na Mheshimiwa Ester Bulaya dakika tano.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante kwa kunipa nafasi; wanasema mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. Kwa moyo wa dhati kabisa nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Jenista Mhagama, mimi mwenyewe, Dkt. Ndugulile ndio tulioanza kushughulikia dawa za kulevya humu ndani kwa kutunga sheria ya kupambana nao, sio kutafuta sifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba nizungumze yafuatayo, sipingani na watu wanaopingana na suala la kupambana na dawa za kulevya, wale wote wanaotaka kupambana na dawa za kulevya wasimuongopee Rais, tumshauri Rais amteue Kamishna wa chombo cha Kupambana na Kudhibiti Dawa za Kulevya ambacho tulipitisha sheria yake humu ndani na nilisema kabisa nimempongeza dada yangu Jenista Mhagama na Dkt. Ndugulile sisi ndio tulianza huu mchezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine tutakapohakikisha hiki chombo kinapata Kamishna kwa kumsaidia Mheshimiwa Rais tutakamata wale wanaoingiza dawa za kulevya, wale mapapa, hao wanaokamatwa sasa hivi waathirika wanatakiwa wapeleke Muhimbili na Mwananyamala wakapate tiba, wale ni waathirika sio kwenda sero. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ndio nililotaka niliseme na mdogo wangu Makonda akitaka kupambana na dawa za kulevya aende magerezani akakutane na akinamama Leyla atamwambia mapapa ili tuungane wote kwa pamoja na tunamkaribisha katika hili lindi kuhakikisha nchi yetu inapambana vikali dhidi ya dawa za kulevya kwa sababu mimi mwenyewe mdogo wangu anayenifuata yupo Mwananyamala anakunywa dawa *methadone*. Kwa hiyo, ninachokisema nina uchungu nacho na nimekifanyia utafiti wa kina na nilileta maelezo binafsi katika Bunge hili Tukufu na ninashukuru Mheshimiwa Jenista akalisikiliza alipoingia tu katika hiyo wizara tukaleta muswada na tukatunga sheria nzuri sana ambayo leo hii katika watu watakaokutwa nyumbani kwao wanafunga zile dawa za kulevya kuna *fine* lakini wanaenda jela zaidi ya miaka 20. Kwa hiyo, tulianza hiyo vita kwa vitendo kwa kutunga sheria kali sio kwa

kukamata waathirika ambao wanatakiwa waende wakanywe dawa kama ambavyo inafanyika hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine tangu mwaka jana mwezi wa kumi na moja hivi vituo vinavyorudisha watu katika hali yao ya kawaida, hawa waathirika ambao wapo sero sasa hivi, hivyo vituo tangu mwaka jana havijapokea watu wapya. Ningependa kujua kwa sababu gani hawajapokea watu wapya na inasemekana dawa ya *methadone* haiendi kwa wakati. Lakini pia mkifuata ile hoja yangu binafsi niliiambia Serikali ihakikishe hivi vituo viende nchi nzima, tusiishie Dar es Salaam peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunajua tatizo la dawa la kulevya yanachangia sana katika maambukizi mengine ya magonjwa ya *HIV*. Kwa mfano, watu tu wa kawaida maambukizi ya ugonjwa wa *HIV* ni asilimia 5.1; kwa watu ambao wanatumia dawa za kulevya ni asilimia 25 mpaka 50. Kwa hiyo, sio *issue* ya kuwapeleka waathirika sero, hili janga ni zito. Kwa hiyo, mtu anaetaka kupambana tupambane na mapapa na sio waathirika ambao wanawekwa sero badala ya kuwapeleka katika vituo vya kurudisha katika hali yao ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na haya ni maazimio ya *UN* ya mwaka 2006 ukitaka kupambana na dawa za kulevya pambana na watu wale mapapa wanaoleta nchini, hilo ndio jambo la msingi. Kwa hiyo, nilitaka niliweke hili sawa; tusifanye siasa katika vita ya dawa za kulevya. Tusimwongopee Rais kwa kutaka kuhakikisha vyeo vyetu, tumwambie ukweli na ili tumsaidie Rais amteue Kamishana wa hii Tume maana tangu tulipoipitisha hii sheria hiki chombo hakina Kamishna. Hilo ndio jambo la msingi ili tuungane kwa pamoja tuhakikishe tunatokomeza vita ya dawa za kulevya hapa katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imesema Tume ya Kuratibu na Kudhibiti Dawa za Kulevya haina fedha, ni aibu kwa nini hawa watu wengine wasiojua haya mambo wasifanye vitu kienyeji kama hatuwapi pesa za kutosha, tuipe hii Tume pesa ipambane na huu muziki kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna Mahakama ya Mafisadi, niliiomba Serikali hizi kesi zinachukua muda mrefu, kuwe na Mahakama Maalum ambayo itashughulika na hii mipapa ambayo wako ndani na haipelekwi mahakamani. Kuwe na Mahakama Maalum inayoshughulika na hizi kesi za dawa za kulevya, hilo ni jambo la msingi sana katika Taifa letu, lakini sio kutafuta sifa na sio kutaka kuhalalisha vyeo vyetu pasipo sababu katika janga ambalo linaharibu kizazi cha watu cha vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie kabisa Waziri anayehusika, hivi sasa hivi wale mapapa wanaoingiza wanataka kuanza kuangalia soko kwenye hizi *centre* zinazotoa huduma yaani dawa za *methadone*, wale ambao Serikali imeamua kuwarudisha katika hali ya kawaida wao sasa hivi wanataka kwenda kuwauzia dawa katika vile vituo. Serikali ina mkakati gani ya kuhakikisha hawa watu hawafanyi hivyo? Ni mbaya sana lakini sasa hivi baada ya kuona hii sheria kali na tumeweza kuhakikisha kwenye ile sheria zile kemikali na zenyewe tumeziingiza katika sheria kuwa ni moja ya makosa, sasa hivi zile kemikali hawa vijana wanatengeneza hapa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mdogo wangu Makonda watafute wale vijana wanaotengeneza hizi kemikali tuanze ku-*deal* nao, wanatengeneza viwanda vidogo vidogo halafu wale waathirika sasa tuwapeleke kwenye vituo tusiwaweke sero. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Kivuli anayehusika na dawa za kulevya, suala hili linatugusa watu wote humu Bungeni hata mimi mwenyewe, kwa hiyo, nakushukuru sana. Waheshimiwa Wabunge tumemaliza shughuli zetu kwa mchana wa leo, nawashukuru sana Mungu awabariki sana nawatakia mchana mwema. Sasa nasitisha Bunge hadi saa kumi leo jioni.

**WABUNGE FULANI:** Taja majina ya wachangiaji, taja majina.

**MWENYEKITI:** Eeeh! Naomba mnisamehe kwa hilo nilikuwa nimeghafirika; tutaanza na wachangiaji na nitawataja watano au sita wa mwanzo. Wa kwanza akiwa ni Mheshimiwa Zitto Kabwe, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salum, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Rashid Akbar, Mheshimiwa Halima Mdee na Mheshimiwa Hussein Bashe na wengine nitawataja hapo tutakapoendelea.

Sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi jioni.

*(Saa 6.56 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti*

**HOJA ZA KAMATI**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

*(Mwanzo wa Take, Sauti haikusikika kutokana na hitilafu ya mitambo)*

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** …..watu 20,000 wapelekwe kule wanafunzi waweze kusoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, chuo kikuu kingine napendekeza kijengwe Mtwara kwa ajili ya Mikoa ya Kusini. Na Chuo Kikuu cha *Lake Tanganyika* ama kijengwe Katavi au Kigoma au Tabora kwa ajili ya Mikoa ya Magharibi; hapa tutakuwa tumejenga uwezo wa kuwa na watu 60,000 zaidi kwenye vyuo vikuu vya umma na tukitanua vyuo vikuu ambavyo tunavyo sasa hivi, uwezo wa wanafunzi wote wanaostahili kuingia kwenye vyuo vikuu vya umma utakuwepo na hivyo tutaweza kuhakikisha ya kwamba tunaondokana na tatizo kubwa la ubora kwenye vyuo binafsi, ambalo tunalo sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ninalipendekeza, na hili ni kwa Kamati zote ni kwamba Kamati zinatoa maoni yao hapa na mapendekezo, mapendekezo yanapitishwa. Mfumo tulionao hivi sasa na mapendekezo haya kufuatiliwa na Kamati yenyewe, na kulingana na wingi wa kazi za Kamati jambo hili limekuwa halifanyiki. Wabunge ambao ni wazoefu wa muda mrefu wanafahmu hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani kuna haja ya kuhakikisha kwamba tunakuwa na Kamati Maalum ya Bunge ya Ufuatiliaji wa Mapendekezo ambayo yanakua yametolewa na Kamati za Bunge. Vinginevyo tutakuwa tunaongea hapa tunaonekana kama tunaimba tu. Kila mwaka tutakuja tutapokea taarifa, tutakuwa kama tunaimba tu na hatutakuwa na msaada wowote ambao tunakwenda nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo nataka kulizungumza lipo kwenye Kamati ya UKIMWI. Kamati hii imeshughulikia suala ambalo sasa hivi ndiyo ajenda. Sasa hivi kila mtu anazungumzia vita dhidi ya dawa za kulevya, ambayo imeanzishwa na mmoja wa Wakuu wa Mikoa hapa nchini katika eneo lake, lakini imekuwa kama vita ya kitaifa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Waheshimiwa Wabunge wakijielekeza kusoma kwenye ukurasa wa 11 wa Taarifa ya Kamati ya UKIMWI, imeeleza kinagaubaga kwamba, mamlaka ya kupambana na dawa za kulevya ambayo imeundwa kutokana na Sheria ya Bunge hapa haipewi uwezo kabisa wa kufanya kazi. Kwa hiyo, hata tukiendesha kampeni hizi namna gani, kila mtu atakuja na kampeni yake, lakini hatutaweza kuzifanya kampeni hizi kuwa

endelelevu kwa sababu, vyombo ambavyo tumeviweka kwa ajili ya kupambana na tatizo hili sisi wenyewe hatuvipi uwezo wa kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Tano ina ajenda ya kubana matumizi. Inabana matumizi mpaka kwenye vyombo ambavyo vinapaswa kufanya kazi ambayo sasa yanatoka matamko ambayo dhahiri kabisa yanaenda kinyume na mfumo wetu wa utoaji haki. Sasa jambo hili tusiliangalie kishabiki, tusiangalie ni mtu gani amesema, amepingwa na nani anaungwa mkono na nani, tutakuwa tunakosea sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii nchi hii kwa mujibu wa Katiba, *you are innocent until proven guilty*. Tunachojengewa sasa hivi moja ni kwamba *once you are accused you are guilty,* hili ni tatizo na hili ni tatizo ambalo Bunge hili lazima ilikemee, kwa sababu Waheshimiwa Wabunge hii ni kama mtego wa panya huu, leo hii kuna watu wamekamatwa, kesho Mkuu wa Mkoa mmoja ana chuki na Mbunge anasema nenda karipoti polisi una dawa, utasema nini? Na sisi kama hatukusimama kuhakikisha kwamba mfumo wa haki unafanya kazi hakuna atakayesimama kututetea atakapotufikia sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba sana, kwanza hakuna mtu anayeweza kuthubutu kukataa kwamba tuna tatizo la dawa na ni lazima kulifanyia kazi, hakuna mtu ambaye anakataa. Lakini ni lazima sisi kama watunga sheria, sisi kama wasimamizi wa Serikali tusimame kidete tuseme kwamba ni lazima taratibu zetu za kisheria na Katiba ziweze kufuatwa, na hii itatusaidia sana. Maana matamko ambayo wakati mwingine yanaweza kuwa ni matamko ya kawaida yanatoka lakini madhara yake yanakuwa ni makubwa sana katika vita yenyewe ambayo tunakuwa tunapambana nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi rai yangu, na mengine nimeyotoa kwa maandishi kwa sababu nilidhani kwamba muda utakuwa ni mfupi sana; rai yangu kubwa ni hiyo; na kwamba kama vita hii ni vita ya zaidi ya mkoa mmoja, basi vita hii iendeshwe na viongozi wa kitaifa wenye mamlaka katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Kigoma kule huwa tuna msemo, "ukiona kifaranga yuko juu ya chungu ujue chini kuna mama yake. Tukiendekeza hali hii tutakuja kupata matatizo makubwa sana; tulaani, lakini tuhakikishe haki inatendeka. Tushiriki kwenye kupambana, lakini tuhakikishe haki inatendeka. Hata siku moja tusionee mtu wala tusimfanye raia yeyote nchi hii aonekane kwamba anaonewa kwa sababu yeye hana madaraka, kwa sababu yeye ni

mnyonge, kwa sababu yeye hana vyombo vya ulinzi na usalama vya kuweza kuagiza na kufanya vitu ambavyo anaweza kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi yangu ni hayo. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Zitto, tunaendelea na Mheshimiwa Bobali badala ya Mheshimiwa Masoud Abdallah.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza niunge mkono hoja za Kamati. Kamati imeeleza mambo mengi na ya msingi, isipokuwa tatizo ni moja, kwamba hizi hoja ambazo Kamati wanazieleza katika Bunge hili la Taarifa za Kamati kwa mwaka mmoja, Kamati hizi hizi zingekuwa zinajenga hoja kama hivi wakati wa bajeti nadhani tungekuwa tuko mbali sana. Lakini inapofika wakati wa bajeti Kamati zote zinajigeuza, badala ya kusimamia na kuishauri Serikali kama ambavyo leo imefanya, zinajigeuza zinakuwa *caucas* ya vyama, hii ndiyo inakuwa changamoto kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukipitia taarifa ya Kamati, imejitosheleza kwa kiwango kikubwa ingawa yako maeneo mimi binafsi ningetaka kupata ufafanuzi zaidi. Kwa mfano kwenye ukurasa wa 33 wa Taarifa ya Kamati ya Huduma za Jamii, ukurasa wa 33 kipengele (b) anasema, katika Hospitali ya Benjamin Mkapa kuna ufisadi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Mwenyekiti wa Kamati angeeleza aina ya ufisadi huu anayotaja kwenye ukurasa wa 33 ni ufisadi wa nini. Ni kiwango gani cha fedha ambacho yeye anafikiria kwamba watu wamechukua, wameiba na wameiba katika mradi upi. Kwa hiyo, ukiangalia hii taarifa iliyoandikwa hapa katika ukurasa wa 33 haijitoshelezi, imesema tu kwamba, katika Hospitali ya Benjamin Mkapa kuna ufisadi. Kwa hiyo, naomba Mwenyekiti wa Kamati utakapokuja kuhitimisha hoja yako uje na maelezo kwamba ufisadi huu ulioueleza katika Hospitali ya Benjamin Mkapa ni ufisadi wa aina gani ili Bunge na Watanzania tuweze kufahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kuhusu suala la ongezeko la ugonjwa wa kansa. Ukisoma taarifa za Wizara, ukiingia kwenye *website* ya Wizara ya Afya, ukasoma taarifa inaumiza sana kwamba ugonjwa wa kansa unaenea kwa kiwango kikubwa kabisa. Taarifa zilizopo kwa mujibu wa *WHO* ambayo taarifa yao waliitoa mwaka 2002 ni kwamba kila mwaka zaidi ya watu 21,000 Tanzania wanapata ugonjwa wa kansa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine taarifa inaeleza kwamba ugonjwa wa kansa za uzazi takribani wanawake 7,515 wanapata ugonjwa wa kansa ya uzazi na kati ya hao 6,009 wanafariki kila mwaka kutokana na kansa ya uzazi. Kwa hiyo, ningetaka kujua na Kamati ingetueleza wao kwa kuwa wanaisimamia na kuishauri Serikali, Serikali ina mkakati gani wa kupambana na ugonjwa huu ambao kwa sasa unaenea kwa kasi kubwa kabisa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma taarifa za kansa namna unavyoenea na namna unavyosababisha vifo ni jambo ambalo linasikitisha sana kuona hatua ambazo Serikali wanazichukua. Lakini kinachosikitisha zaidi ni kuona kwamba hata hiyo Hospitali yenyewe ya *Ocean Road* katika bajeti ya mwaka 2016/2017 kile kiwango cha pesa ambacho ilitengewa hiyo pesa haikupelekwa, kiwango kilichopelekwa ni kidogo sana. Kwa hiyo, inaonesha kwamba dhamira ya Serikali ya kupambana na ugonjwa huu ambao ni hatari sana ni ndogo sana, lakini *WHO* wana-*estimate* kwamba tunakoelekea zaidi ya asilimia 25 ya Watanzania tuko hatarini kupata kansa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba karibu kwenye Watanzania wanne, mmoja yuko hatarini. Ni jambo la hatari na ni jambo *very serious,* tunahitaji Kamati kwa kuwa ndio inaisimamia Serikali ije itueleze wapi Serikali imekwama katika kuhakikisha inapambana na ugonjwa huu wa kansa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu Uganda naona wamechukua hatua kubwa kabisa na si vibaya Waziri akaenda akajifunza kwa zile *measures* ambazo Uganda wamezionesha na namna wanavyopambana imeonesha kwamba *is a serious issue* na *national problem* na Rais ame-*declare* kabisa kwamba kansa ni tatizo la Taifa na wameamua kupambana nalo. Sidhani kama Tanzania tumefikia kwenye *level* ya namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la ugonjwa wa UKIMWI. Sisi tunaotoka vijijini siku hizi ugonjwa huu ni kana kwamba umehama mjini umekwenda vijijini. Hali ya maambukizi vijijini ni makubwa kuliko hata mijini mimi nasema. Ukienda kule vijijini, mimi natokea Lindi, ukienda Lindi vijijini kabisa ukielezwa idadi ya watu wanaotumia dawa kule vijijini kabisa, inasikitisha sana. Inaonesha dhahiri kwamba inawezekana kuna tatizo kubwa la elimu ya namna ya kujikinga na ugonjwa huu ambayo wanayo wananchi wa vijijini?

Kwa hiyo, mimi naomba Kamati, kwasababu, ninyi ndio wenye hoja mtueleze pia, kwamba katika ushauri wenu kwa Serikali, Serikali wana mkakati gani wa kuongeza utoaji wa elimu vijijini? Suala la ugonjwa wa UKIMWI sasahivi

limekuwa kubwa vijijini kuliko mijini; na hii ni kwa sababu, wananchi kule vijijini wamezoea kuishi maisha yao yale ya kawaida. Inasikitisha sana, ukiwa kwenye vikao vya Halmashauri ukapewa takwimu za ugonjwa wa UKIMWI katika Halmashauri inasikitisha na inatisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi nimeshiriki Vikao vya Kamati ya UKIMWI juzi juzi tu kwenye Halmashauri yetu ya Wilaya ya Lindi, taarifa iliyopo ni mbaya sana. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba hili ulichukue kwamba hali ya maambukizi ya UKIMWI vijijini sasa hivi ni kubwa zaidi kuliko hata mijini. Sijui kama takwimu zako zinasemaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa nilizungumzie ni suala la Bodi ya Mikopo. Tulizungumza hapa wakati wa bajeti kwamba bajeti hii ni ndogo, lakini pia, utaratibu unaotumika kupima vigezo vya nani apate na nani akose bado ni utaratibu ambao hauridhishi. Kwa hiyo, tunaomba, Kamati muendelee kuishauri na kuisisitiza Serikali kwamba katika mwaka na ninadhani Kamati mngekuja na orodha ama idadi kwamba ni wanafunzi wangapi ambao walistahili kupata mikopo lakini wamekosa katika mwaka wa masomo 2016/2017. Idadi ni kubwa na waliokosa wengi ni maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda vijijini unawakuta watu ambao walifaulu kwa *division one, division two,* lakini wanatoka kwenye familia maskini wako vijijini wamekosa mkopo. Kwa hiyo, Kamati tunaomba mngekuja na takwimu walao mkatueleza kwamba kukosekana kwa mikopo kumeathiri kiwango gani cha vijana wetu wa Kitanzania katika mwaka wa masomo wa 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona muda wangu umekwisha, nakushukuru na ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Bobali, tunaendelea na Mheshimiwa Felister Bura na baadaye Mheshimiwa Rashid Akbar Ajali na Mheshimiwa Halima James Mdee ajiandae.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi ya kusimama katika Bunge lako Tukufu, lakini nikushukuru wewe pia kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze Kamati zote mbili kwa kazi nzuri walizofanya. Wamefanya kazi nzuri kwa muda mfupi sana, lakini wamefanya kazi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapopitisha bajeti hapa kila Wizara tunapitisha bajeti zake tukiamini kwamba fedha zitakwenda kwenye Wizara hizo kwa wakati muafaka. Lakini kwa Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii, nimesikitika jinsi mtiririko wa fedha ulivyo na hasa katika Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania milioni 45 tunategemea kuhudumiwa na Wizara ya Afya kuhusu huduma ya afya. Wazee wanaitegemea Wizara ya Afya, wanawake, watoto, vijana, kwa hiyo, milioni 45 fedha zinapopelekwa asilimia 21 kwa muda wa miezi sita ina maana Watanzania hawana pa kukimbilia na hasa wale ndugu zangu ambao wanaishi vijijini na hawana uwezo wa kujitibu na hawana bima ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika kweli ninaposema hili kwa sababu tunapata matatizo tunapokwenda vijijini, unamkuta mtu anaumwa na anaumwa kweli kweli na hana fedha, na zahanati au kituo cha afya jirani yake hakuna dawa. Kwa hiyo, mzigo unakuwa kwa Mbunge ambaye amekwenda kutembelea pale au mzigo unakuwa kwa Diwani aliyeko eneo lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sana kwamba tunapopitisha bajeti hapa basi fedha ziende kwa wakati. Utakuta mwezi wa tano au wa sita ndipo Wizara ya Fedha inapeleka fedha katika Wizara mbalimbali na mwisho wa mwaka unapofika fedha zinarudi nyingi tu Wizara ya Fedha kwa sababu fedha zimepelekwa muda umekwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna deni la *MSD* tangu Bunge lililopita; tangu mwaka wa jana wakati tunapitisha bajeti tuliomba sana kwamba deni la *MSD* lilipwe ili *MSD* wawe na uwezo wa kununua dawa na kuzisambaza mikoani, lakini hili deni linapungua kidogo kidogo mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Waziri wa Fedha afya za watanzania ni muhimu kwa hiyo, deni la *MSD* lilipwe ili *MSD* wawe na uwezo wa kuagiza dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na Wazee fedha za maendeleo wamepelekewa asilimia 21, nimeshangaa kweli. Mwaka jana tulipitisha bajeti tukiomba fedha kwa ajili ya kukarabati Hospitali ya Rufaa ya Mirembe; wanaotibiwa pale wana ugonjwa wa afya ya akili, wameshawapiga manesi na madaktari wengi tu pale, lakini mpaka leo hospitali ile haijakarabatiwa. Hospitali ile ilijengwa tangu mwaka

1926, kwa hiyo, miundombinu ya hospitali ile imechakaa kweli; wauguzi na madaktari hawatoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea kabla ya mwezi wa kumi na mbili Wizara itakuwa imepeleka watumishi wa kutosha, lakini mpaka leo watumishi ni wale wale, wauguzi wakiingia asubuhi ni mpaka jioni saa moja ndipo wabadilishane na posho za *overtime* hazilipwi kwa wakati. Na mimi simlaumu Mheshimiwa Ummy kwa sababu hana fedha. Posho za wauguzi hazilipwi, fedha za safari na za likizo hazilipwi kwasababu Wizara haina fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani tuwakumbuke Wizara ya Afya. Naona tunawatetea sana walimu lakini hata wauguzi na waganga hawana watetezi, watetezi wao ni sisi. Pamoja na walimu, wauguzi na waganga nao wanateseka; hawana nyumba, *overtime* na fedha za likizo hazilipwi kwa wakati, na wao watizamwe kwa jicho la huruma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais John Pombe Magufuli alipomteua mdogo wangu Ummy Mwalimu kuwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Watoto na Wazee alijua umahiri wake katika kazi, na mimi nampenda kwa sababu anafanya kazi nzuri. Mheshimiwa Ummy nakupenda kwa sababu unafanya kazi nzuri, lakini nina tatizo moja, najua huna fedha lakini takwimu ambazo zimeoneshwa hivi karibuni zinaonesha kwamba kati ya wanawake wajawazito 100,000 wanawake 556 wanapoteza maisha.

Mheshimiwa Waziri ninajua una uwezo wa kuja na mkakati madhubuti kabisa kuhakikisha kwamba hivi vifo vinapungua. Tusiwafanye watoto wetu wasichana wakaogopa kuzaa kutokana na vifo. Ninaomba sasa leo ukijibu hoja za Wabunge useme mkakati ambao umeandaa kwa ajili ya kupunguza vifo vya wanawake na hata vifo vya watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inahamia Dodoma lakini kwenye Taarifa ya Kamati inaonesha kwamba Hospitali za Rufaa tulizonazo hazina watumishi wa kutosha; Hospitali ya Benjamin Mkapa kati ya watumishi 751 wapo 51 tu. Kama uhakiki wa watumishi umekamilika basi waajiriwe; hao wanaotoka Dar es Salaam wanaiacha Muhimbili kule wanaacha Hospitali za Rufaa kule Dar es Salaam wanakuja dodoma, tuna hospitali moja tu hapa ya *General*. Lakini Hospitali ya Benjamin Mkapa ambayo ina vifaa vya kutosha vya kazi, hakuna watumishi, watumishi 700 wanahitajika pale na wale wanatibu wagonjwa wa ndani na wa nje; wagonjwa wa Dodoma na wa nje ya Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuomba kama uhakiki umeshamalizika basi waajiriwe wafanyakazi wa kutosha pale Benjamin Mkapa, Hospitali ya Mirembe na Hospitali yetu ya Mkoa ili kuhakikisha kwamba huduma inayoendelea kutolewa pale iwe ya kuridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niungane na msemaji, Mbunge aliyepita kuhusu ugonjwa wa kansa. Mimi kwa miaka mitatu nimepoteza ndugu watatu kwa ugonjwa wa kansa. Lakini hatujajua ugonjwa wa kansa unaambukizwaje, na tunatakiwa kujikinga vipi, na unasambaa au hausambai? Si mimi tu, wako wananchi wengi wa Tanzania ambao wanatamani kupata elimu kuhusu ugonjwa wa kansa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kusema habari ya viroba vilivyojaa madukani. Vijana wetu hasa waendesha bodaboda asubuhi anapiga viroba vitatu na ndio maana ajali za pikipiki haziishi, viroba sasa viuzwe kwenye *bar*, tuache kuviuza madukani. Kwa sababu wengine wataogopa kuingia kwenye *bar*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze pia kuhusu elimu. Sisi Kamati yetu ya *PAC* tulitembelea Chuo cha Ufundi Arusha; tuliona kazi kubwa ambayo inafanywa na kile chuo, wamebuni mambo mengi sana, wametengeneza mashine za kilimo cha kumwagilia, wamechukua kiwanda cha kuzalisha umeme kule Kikuletwa Wilaya ya Hai lakini hawana fedha. Pamoja na juhudi kubwa na kuwafundisha vijana namna ya kujitegemea, wavulana kwa wasichana wanajifunza mambo mengi sana pale lakini hawana fedha. Ninakuomba Waziri wa Elimu kiangalie kile chuo kwa jicho la huruma sana. Pamoja na kwamba tuna *VETA* lakini wanafunzi wanaweza wakatoka *VETA* wakaenda wakajifunza mambo makubwa sana pale *Arusha Technical College*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna malalamiko kwamba wanafunzi ambao hawastahili kupata mikopo na wanapata mikopo wanaweza wakarudishwa majumbani. Ninaomba hili Waziri wa Elimu aliweke wazi kwa sababu wanafunzi wetu wapo wengi vyuoni, lakini hawajui hatima yao. Tumeambiwa uhakiki bado unaendelea, hatujui uhakiki utakamilika lini, na je, kama watapatikana ambao hawastahili kupata mikopo itakuwaje, watarudishwa majumbani au Serikali itaendelea kuwahurumia na wakaendelea na masomo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako watoto wa maskini wengi tu,wengine walikuwa na wafadhili wakasoma shule ya sekondari *private school* lakini

anapoanza chuo mfadhili anamuacha. Mwingine baba au mama alikuwa na uwezo kipindi hicho lakini amebaki yatima hawezi kulipa chuo kikuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri aliangalie hilo kwa umakini na wanafunzi wasirudishwe kwa kuwa hawastahili kupata mikopo kwa kuwa wameshaanza kusoma. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Asante Mheshimiwa Felister Bura, tunaendelea na Mheshimiwa Rashid Akbar, baadae Mheshimiwa Halima James Mdee ajiandae.

**MHE. AJALI R. AKBAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nichukue nafasi hii kukushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi hii, lakini pili nichukue nafasi hii pia kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuweka hai sisi Waheshimiwa Wabunge. La tatu nikipongeze chama changu Chama cha Mapinduzi jana kwa kutimiza miaka 40, ni umri wa mtu mzima kwa kweli. Maana sijasikia kama Chama cha Mapinduzi kimepongezwa, kwa hiyo nitoe taarifa kwamba jana ndio kilikuwa kinatimizia miaka 40 kakweli nakipongeza sana, nampongeza Katibu Mkuu na Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jingine nipongeze kamati zote mbili kwa maana ya Kamati ya UKIMWI pamoja na Kamati ya Huduma za Jamii. Ukiangalia mustakabali wa hizi kamati zote mbili kwenye taarifa zao yaani utaona kabisa hizi Kamati zote zimefanya kazi kubwa sana tena kwa muda mfupi na kila kitu kimeelezwa humu, hakuna jambo ambalo ni geni ambalo sisi Waheshimiwa Wabunge tunaweza tukalizungumza nje ya yale ambayo Kamati imeyazungumza; kwakweli Kamati nazipongeza sana kwa ufanisi wenu wa kazi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yale mapungufu ambayo yanazungumzwa na mimi ningechukua nafasi hii kuchangia mapungufu ambayo nimeyaona hasa yale ambayo nimeona kuhusu dawa za kulevya. Upungufu inaonesha kabisa kwamba kulikuwa na mamlaka ambayo imeanzishwa kisheria ambayo ilikuwa imepitishwa kutoka mwaka jana lakini ukamilishwaji wa hii Kamati ndipo yote haya yanatokea leo kamata kamata inakuwa nani hajulikani akamatwe na yule ambaye asikamatwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaonesha kwamba ile mamlaka ambayo ilikuwa imeanzishwa ule mchakato mpaka leo haujakamilika; haina *commissioner,* ina upungufu wa vitendea kazi na rasilimali watu. Japo kuwa

kuna watu tumewasomesha lakini watu hao hawafanyi kazi, tuna polisi wa kutosha, lakini hawawezeshwi hawa watu ili wafanye kazi leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sisi ambao tumewahi kuwa Waheshimiwa Madiwani Jijini Dar es Salaam hili suala la kamata kamata la unga ni suala la muda mrefu sana. Vinginevyo watu watakuwa wanatuhumiwa, Wabunge wengine watakuwa wanakamatwa au watakuwa wanatajwa lakini wataambiwa wamehusika. Huu mchezo tusipokuwa makini sana itakuwa sawasawa na mchezo wa chura maana watoto walikuwa wanarusha mawe kwenye maji halafu ule mchezo watoto wanacheka, lakini chura wanalia; wakawaambia nyie watoto huo mchezo mnaoufanya ni mauti yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hatujui kwamba ni nani ambaye anawajibika moja kwa moja, kwa hiyo Kamati sababu ile watu wenye mamlaka hawajapewa mamlaka wala hawajawezeshwa kufanya kazi. Kwa hiyo, wale Mawaziri wanaohusika na tasnia hii waje waileze Kamati kwamba je, ni lini sasa hizi taasisi na hizi zinaanza kufanya kazi kwa ufanisi ili tujue nani anaewajibika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusifanye masihara ni gharama kubwa sana kutengeneza majina lakini kuyaua unaweza kuyaua kwa muda mfupi sana, tusifanye masihara kutengeneza jina. Lakini vile vile tulikuwepo pale tuliona watu ambao wametengeneza majina wameharibiwa hayo majina, lakini je, ni nani ambaye atakuja kuwajibika kwa kuharibiwa jina? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kamati imezungumza vilevile kuhusu udhaifu ambao umejitokeza wa ukosefu wa fedha. Inaonesha kabisa kwenye tasnia ya afya, kwa sababu afya ndio lango kuu la nchi hii, tunategemea afya na elimu. Lakini utaona kabisa kwamba afya pamoja na elimu zote hizi zimepelekwa TAMISEMI. Kwa hiyo, maana yake ni kwamba Wizara ya Elimu yenyewe inakuwepo pale *ceremonial* kama *policy makers,* lakini hawasimamii moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati sisi tunasoma tulikuwa tunajua kwamba kila kitu ambacho kilikuwa kinahusu elimu tulikuwa tunaenda Wizara ya Elimu lakini leo ukitaka kujua nini kuhusu elimu ukienda Mkoani au ukienda Wilayani Wizara ya Elimu kule, kule wewe utakuta tu TAMISEMI pamoja na *Local Government* kwa kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ina maana huwezi kujua kwamba kwenye ubovu wa elimu ni nani anaewajibika? Anaewajibika ni TAMISEMI au Wizara ya

Elimu moja kwa moja? Kwahiyo, ningeomba hawa Mawaziri wawili wanapokuja hapa waje watueleze kwamba ni nani ambaye anawajibika moja kwa moja ili tujue kwamba ile idara ya ukaguzi iliyopo pale TAMISEMI nani ambaye anasimamia kuiwezesha fedha ili ikafanye ukaguzi ili ubora wa elimu uwe juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo hivyo upande wa afya; utadhani kana kwamba Wizara ya Afya nao ni *policy makers* wao wanatengeneza tu sera, lakini moja kwa moja vile vituo vya afya ambavyo vipo vijijini ambavyo havina dawa; huku tunaambiwa kwamba dawa zipo lakini ukienda vijijini dawa hazipo kabisa. Lakini vilevile tuna sera za wazee tunasema kabisa tunapokwenda kule tunaenda kujinadi kwamba aaah, sasa hivi matibabu kwa wazee zipo bure; Lakini tunaulizwa sasa hivi imeshachukua muda mrefu sisi wazee bado tunapata shida ya kupata tiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwahiyo, Mheshimiwa Waziri wa Afya aje atueleze kwamba ni lini hii sera itakuwa imeshakamilika na hawa wazee watapata tiba ambayo moja kwa moja itakuwa bure ili nasi tuweze kujikimu kama Waheshimiwa Wabunge wamewahi kuzungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Elimu na Wizara ya Afya isipokuwa makini; mimi nadhani kwamba Wizara ambayo ninaipongeza ni Wizara ya Maji. Ukienda hata huko kwenye *Local Government* unakuta kabisa Wizara ya Maji inakuwa na uwajibikaji, ukienda kwenye Idara ya Maji unaona kabisa kwamba hawa watu wa maji wanajishughulisha moja kwa moja. Kwahiyo, ningeomba kwamba hizi Wizara mbili, kwa maana ya Wizara ya Afya pamoja na Wizara ya Elimu na yenyewe ichukue mfumo huo huo, kwa maana kwamba wawe wanasimamiwa wanafika mpka huko chini ili kwenda kusimamia kuhakikisha kwamba haya mambo yetu yanakwenda badala ya kuwa yamesimama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi michango yangu ilikuwa ni hiyo miwili ya kuhakikisha kwamba hawa Mawaziri wanatupa taarifa ni nani ambaye ambaye anawaibika kati ya Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja kwa kuwa hoja yangu ilikuwa ni fupi, asante sana!

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Akbar, tunaendelea na Mheshimiwa Halima James Mdee na baadaye Mheshimiwa Hussein Bashe na Mheshimiwa Hawa Ghasia wajiandae.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, na mimi mchango wangu utaongezea yale ambayo yamezungumzwa kuhusiana na dawa za kulevya; na nitarejea ukurasa wa saba na wa nane wa taarifa ya Kamati, naomba kunukuu inahusiana na mwenendo wa bajeti ya Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya, ukurasa wa saba unasema; "Hata hivyo katika kipindi cha mwaka 2015/2016, 2016/2017 bajeti za Tume zilishuka hadi kufikia sifuri kwa miradi ya maendeleo kwa mwaka 2016/2017 kutokana na ukomo wa fedha za wafadhili na kubadilika kwa vipaumbele vya Bajeti ya Serikali."

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati hotuba ya Kamati inasema haya leo Mheshimiwa Rais wakati anamuapisha Mkuu wa Majeshi amesema kinaga ubaga kwamba anaunga mkono vita ambayo kwa mtazamo wake yeye imeanzishwa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam na kwamba hakuna atakayepona na kwamba wote wawekwe ndani na haangalii umaarufu. Ifike kipindi hii nchi yetu tuache kuiendesha kwa sanaa. Ninarudia, ifike kipindi hii nchi yetu tuache kuiendesha kwa sanaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya mwaka 2016/2017 ambayo Rais Magufuli anayetoa tamko la kumuunga mkono Makonda ndiyo alikuwa ameshakuwa Rais; bajeti ya maendeleo ni sifuri, na bajeti ya maendeleo ndio tunatarajia ikafanye hizi shughuli; leo anasimama Ikulu anadai eti anaunga mkono hii vita. Isipofika kipindi kama nchi tukaamua kutembelea ama kusimamia maneno tunayoyasema ama kutembelea kauli zetu haya majanga hayawezi kuisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *President* Nickson mwaka 1971 wakati anaanzisha vita dhidi ya madawa ya kulevya Marekani mpaka sasa Taifa la Marekani limetumia si pungufu ya dola trilioni moja na bado wanapambana. Kwa mwaka mmoja Taifa la Marekani linatumia sio pungufu ya dola bilioni moja angalia *GDP* yetu halafu linganisha na dola bilioni 51; lakini vita bado ni kubwa. Leo bajeti sifuri halafu anasimama mkuu wa nchi anasema eti vita ipiganwe; tutapigana kwa viboko? Tutapiganaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwahiyo ifike kipindi tuache kutafuta *headlines* na tuache kucheza na vichwa vya Watanzania kwa kutengeneza *headlines* kwa sababu hii vita si ya jana, si ya leo na wala si ya juzi na wala si ya mtu mmoja.

Kwa hiyo, lazima tuwe na *political will* na dhamira ya kisiasa haipimwi zaidi ya kwenye maandiko, huna pesa huwezi kufanya kitu, tuache usanii, tuache sanaa na tulisaidie hili Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninyi hatuwaji wauza unga sisi? Hatuwajui wanaoagiza unga sisi? Si ndio wanaotuchangia kwenye kampeni sisi? Hatuwajui? Si ndio tunakula nao sisi? Si ndio tunalala nao sisi? *(Makofi)*

Leo tunaenda tunakamata vitoto vya watu eti vinatumia unga; Rais anasema kamateni hao watumiaji watatusaidia kutuambia wanaouza, mzee kama hawajakwambia ukweli inawezekana kampeni zako ulichangiwa na hawa watu, hii vita ni kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, inawezekana Rais amezungukwa na watu ambao anadhani anawaamini, mimi naamini hili Baraza lina watu makini, lakini naamini kuna watu anaowasikiliza zaidi na wengine anawapuuza. Tuanze kupima na kuangalia Rais anazungukwa na watu gani. Kwa hiyo, kama leo kwa sababu kuna mtu amesema hapa inawezekana Rais ametuma tu, labda Makonda ndiyo msemaji wake siku hizi anaambiwa tangulia halafu mimi nafuata, kwa sababu haiwezekani ikawa ni *coincidence*. Yaani anatokea anasema kitu halafu Mzee anafuata! Hii vita *if we are serious,* waliokuwepo kwenye Bunge lililopita, mnakumbuka Mheshimiwa Lukuvi alipokuwa Waziri anayeshughulika na masuala ya Bunge, alituingiza kule akatuonesha sinema, anasema watu wanawajua, iko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kikwete alisema anawajua na sisi tunaamini Rais akiondoka Ikulu mafaili yanabaki Ikulu, kwa hiyo, tusikimbie vivuli vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais John Pombe Magufuli na wasaidizi wake mnanisikia, *list* ya waagizaji siyo watumiaji, waagizaji, wafanyabiashara wa dawa za kulevya wanaotuma watu huko nje unayo Ikulu, tunaomba fanyia kazi *list* iliyokuwa Ikulu, tusicheze na akili za Watanzania kwa kutafuta *headlines.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila siku tunakwepa masuala ya msingi, wanaona uchumi unadorora wanamwambia mzee toka na hiki ili tu-*divert minds* za Watanzania, wanaona kuna njaa wanasema toka na hiki tu-*divert* akili za Watanzania, msitupotezee muda. Mmepewa hii nchi kwa dhamana, *more than 50 years now,* jana wametimiza *40 years* kama chama, watu wazima yaani *40 years* maana yake mtu mzima, shababi. Tu-*behave* kama watu wazima, tulisaidie hili Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba, niambiwe kabisa na Waziri wa Afya, kwa hizi mbwembwe mnazoanza hizi, hii kutoka *zero* itakuja ngapi ili tuweze basi kuanza kupambana na hili tatizo. Akina Amina Chifupa walizungumza sana humu wakaja akina Mheshimiwa Ester Bulaya na hoja zao binafsi wakaungwa mkono na Waziri Mheshimiwa Jenista, tukatunga sheria, sheria ukiisoma ni kali kwelikweli, na ile sheria ukiisoma *between the lines* inalenga wale mashababi, ambao inawezekana wengine, ndiyo maana yule dogo alikuwa yuko Marekani siku 20, hakuna anayejua nani kamfadhili Marekani siku 20, hana ubavu wa kuishi Marekani siku 20. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana hawa wauza unga ndiyo wanampeleka huko, anakuja anamkamata Wema, Wema kweli! Alizunguka na ninyi kwenye kampeni mlikuwa hamjui, alikuwa na Makamu wa Rais miezi mitatu, sijui Mama na Mtoto, mkapata kura za ma-*teenagers* kwa kumpitia huyo dogo. Kwa hiyo, siku zote yuko na Makamu wa Rais kumbe ananusa kitu Makamu wa Rais hajui, acheni usanii. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetumia muda wangu mwingi kulizungumzia suala hili, nirudie tumuogope Mungu, tuache usanii. Tunadhamira ya kuwasaidia watoto wetu hawa, tuwasaidie watoto kwa kuwapa tiba tukamate majambazi na majangili wanaoharibu Taifa letu, tumechoka maneno, tunataka vitendo sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la *HIV*…….

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mdee. Tunaendelea na Mheshimiwa Hussein Bashe na baadae Mheshimiwa Hawa Ghasia ajiandae.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuchangia. Na mimi ni-*declare interest* kwanza ni Mjumbe wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kusema, kama Taifa tunakabiliwa na mambo matatu makubwa, nina imani sana na Serikali ya Awamu ya Tano, kwamba mambo haya matatu, ukiwa na *collective work* mambo haya tutayamaliza. Jambo la kwanza ni suala la dawa za kulevya, jambo la pili ni jambo la ushoga, jambo la tatu ni tatizo la elimu ya hovyo kwenye nchi yetu, haya mambo matatu yanaliumiza Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa Serikali ya Awamu ya Nne, Mheshimiwa Rais Kikwete alisema anayo *list* ya wauza dawa za kulevya, naomba nieleweke Rais Kikwete alisema anayo *list* ya majina ya wauza dawa za kulevya. Mimi ningeomba kupitia Bunge hili Waziri wa Mambo ya Ndani amfuate Mzee Kikwete pale Msoga akamuombe ile *list* ili waweze kuungana na kazi ya Makonda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali, kama alivyosema Mheshimiwa Rais, vita ya madawa ya kulevya, na mimi naamini anachokifanya Mheshimiwa Makonda ana-*collect* taarifa, vita ya dawa za kulevya siyo vita ya Paul Makonda peke yake, ni vita ya Serikali dhidi ya *cartel* ya dawa za kulevya. Kwa hiyo, naamini hataachwa Makonda na vita hii kama alivyoachwa alivyoanza kuongelea suala la *lesbians* na ushoga, alibaki nayo peke yake, kwa hiyo naamini kwamba Serikali itamuunga mkono katika jitihada hii aliyoanza, *he started somewhere,* ninaamini watumiaji wataachiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili kwenye *issue* ya dawa za kulevya, nadhani lazima tuelewe, kama nchi tunataka kupigana vita hii tupigane in *it's totality*. Kwa sababu tunatunga sheria dhidi ya dawa za kulevya halafu tunaruhusu kuanzisha vituo vya kutibu watumiaji wa dawa za kulevya, *you prohibit in the left hand side,* unakataza kwa mkono wa kulia unaruhusu kwa mkono wa kushoto, mnaanzisha vita mnaita *sober house*. Mimi ingekuwa amri yangu ningefunga *sober house* na kila mtu anayekula unga akienda hospitali apimwe, akionekana anakula aanze kushughulikiwa yeye kutusaidia aliyemuuzia, *distributor* ni nani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu; nataka tuangalie hizi takwimu Waheshimiwa Wabunge humu ndani tumeongea sana, kwamba madai ya walimu, walimu wana matatizo. Tatizo la msingi la sekta ya elimu katika nchi yetu ni mfumo. Leo elimu yetu inasimamiwa na *almost* Wizara tano, TAMISEMI, kama Kamati ya Huduma madai ya walimu anayasema sana Mheshimiwa Mwalimu Bilago kwa sababu ni mwalimu, na dada yangu Mheshimiwa Susan na Wajumbe wengine, lakini hili liko chini ya TAMISEMI. Kwa hatua ya awali Bunge hili liazimie, linapokuja suala la elimu, Waziri wa TAMISEMI na Waziri wa Elimu waje mbele ya Kamati kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu matokeo ya mwaka huu asilimia 93 ya shule zilizofanya vizuri ni shule za *private, government* ni *only seven percent*. Lakini *division one mpaka division three* ni asilimia 28 tu ya wanafunzi, asilimia 72 ni *division four na division zero*. Hali ya vyuo vyetu vikuu tunasema

kwamba tunatanua elimu ya msingi matokeo yake idadi ya watoto wanaofaulu ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu tumeweza kuwapa *sponsorship* au kuwapa mikopo watoto 25,000 tu kati ya karibu watoto 60,000 ambao walikuwa wamedahiliwa kwenda vyuo vikuu, kuna watoto 35,000 hawajapata fursa ya kwenda *higher learning institution* ni tatizo. Kamati imesema *TCU* badala ya kusimamia suala la ubora amebaki kuwa dalali wa vyuo vikuu. Nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge, *East Africa Community* iliunda *commission* ya kupitia vyuo vikuu vinavyotoa elimu ya madaktari, vyuo vinne vimefungwa Tanzania kwa sababu *quality* ya elimu yake iko chini, *this is a crisis! (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hatutakuwa *serious* kwenye suala la elimu ya nchi hii hatuwezi kupiga hatua tunayotaka kupiga na mimi niwaombe Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Spika hapa alisema kuna hoja nilipeleka ya kutazama mfumo wa elimu, basi kwa kuanza tu tuazimie, Serikali ikautazame mfumo wa elimu wa nchi hii wote. Vyuo vikuu angalau by *standard*, wahadhiri wenye *Ph.D* wanaotakiwa kuwa kwenye vyuo vikuu, tulionao sasa hivi ni *only 25 percent* wakati *standard* ni angalau asilimia 60, lakini vyuo vyetu vina asilimia 25 tu ya wahadhiri wenye sifa ya kuweza kufundisha katika vyuo vikuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *sometimes* unajiuliza, nimeona takwimu za *BEST,* ukichukua takwimu za Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia za mwaka 2012 mpaka 2016….

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda umeisha?

**MWENYEKITI:** Ndiyo, Ahsante Mheshimiwa Bashe. Tunaendelea na Mheshimiwa Hawa Ghasia na baadaye Mheshimiwa Ester Michael Mmasi ajiandae.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami ningependa kuchangia hoja. Niwapongeze watoa hoja wote na hivyo nianze kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwanza ningependa kuzungumzia suala la elimu na hasa masuala mazima ya ufaulu. Katika wilaya nyingi na mikoa mingi ambapo matokeo ya kidato cha pili na kidato cha nne yamekuwa siyo ya kuridhisha, asilimia kubwa uamuzi au hatua zilizochukuliwa ni kushusha vyeo

walimu wakuu au wakuu wa shule. Mimi sidhani kama mwalimu peke yake anaweza akawa ndiyo sababu ya shule kufeli au kufaulu. Mimi napenda nishauri katika zile Wilaya ambazo kila mtihani uliofanywa zimekuwa za mwisho hebu tufanye utafiti wa kina tujue kwa nini wilaya hizo zimefanya vibaya. Haiwezekani kwenye Mkoa wangu Wilaya moja hiyo hiyo matokeo ya kidato cha nne wa mwisho, matokeo ya darasa la saba ya mwisho halafu tuone hatua ya kuchukua ni kushusha vyeo tu walimu, sidhani! Naomba tufanye tathmini ya kina ili tujue tatizo tuweze kuwasaidia na zile Wilaya na zenyewe zifanye vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwenye sekta ya afya na nianze kuzungumzia suala la uchache wa watumishi katika sekta ya afya. Kwa kweli hali ni mbaya, ukienda katika vituo vyetu vingi vya afya, hospitali majengo ni yanaridhisha, unakuta hospitali zetu sasa hivi nyingi ni safi, madaktari wanajitahidi hata wauguzi, kauli zinaridhisha lakini uchache wao unawaangusha. Katika baadhi ya Wilaya tunashindwa kutoa baadhi ya huduma kama upasuaji, kufungua baadhi ya zahanati, kwa sababu ya uchache wa watumishi. Niombe Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, wakati tukiendelea na uhakiki basi kama tulivyofanya kwa sekta ya elimu na sekta ya afya nayo tuiangalie, hali ni mbaya hasa katika Mkoa wangu wa Mtwara ambao ninaufahamu. Nina vituo vyangu vya afya ambavyo vimeshindwa kuanza huduma za upasuaji kwa sababu hatuna watumishi wa kuweza kutoa huduma hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la vifo vya akina mama limezungumziwa sana hasa kutokana na changamoto za uzazi. Mojawapo ikiwa kuzalishwa na watumishi ambao kwa kweli hawana utaalamu. Niombe hivi vituo vya afya, mlishaanza kuvifanyia tathmini na kuvipa madaraja, zoezi hili likamilike nchi nzima ili vile vituo ambavyo havina uwezo wa kuzalisha akina mama waambiwe kwamba siku zako zikifika pale huwezi kusaidiwa, wajue ili ajiandae, ikiwezekana aende akakae karibu na eneo ambalo ataweza kusaidiwa. Kwa sababu kama atahitaji damu wakati wa kujifungua, kama atahitaji *operation* wakati wa kujifungua ndiyo kusema kama atakuwa eneo ambapo hakuna huduma hizi huyo mama ndiyo tumeshampa cheti cha kifo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nilitaka kulichangia ni tafiti zinaonesha maeneo ambayo wanaume wanafanyiwa tohara maambukizi ya UKIMWI yako chini sana kuliko maeneo ambayo hayafanyiwi tohara ambapo maambukizi ya UKIMWI yako juu sana, na hivyo hivyo maeneo ambayo tohara haifanyiki maambukizi ya kansa ya shingo ya kizazi pia yako juu. Niiombe Wizara ya Afya hili suala la tohara kwa wanaume lisiwe la hiari liwe la lazima. Kwa

sababu kama tafiti zote zinatuambia maeneo mengine wanaume ambao hawajatahiriwa maambukuzi wako zaidi ya asilimia 21 kuliko wale ambao wametahiriwa. Kwa nini tusiseme ni lazima? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba, ile Mikoa ambayo wanatahiriwa, lile tendo wasiite suna, maana yake mtu anasema anakwenda kutahiriwa unaita suna, kitu kama ni suna maana yake siyo lazima, niwaombe kwa wale wanaotahiriwa tuseme faradhi ili kila mtu ahamasike. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana wote tulikuwa Morena, tumeambiwa haya, siyo kama nimeyatoa kichwani, ni taarifa zilizotolewa na Shirika la Afya Duniani, Wizara ya Afya wanazo. Tupeleke taarifa sahihi, kuhusu suala la tohara kwa wanaume. Tutawanusuru akina mama wetu tutapunguza maambukizi ya virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Wizara ya Afya, tunazo hospitali zetu za Kanda, Kanda ya Kaskazini tunayo *KCMC,* Kanda ya Magharibi au ya Ziwa tunayo Bugando na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini tunayo Hospitali ya kule Mbeya, Kanda ya Kusini peke yake ndiyo imebaki ambayo haina Hospitali ya Rufaa ya Kanda, ujenzi umeanza lakini ni wa kusuasua. Nikuombe Mheshimiwa Waziri, tusaidie katika hilo, gharama ya kumsaidia mgonjwa mmoja kuja hospitali kutibiwa kwa kumsafirisha kwa ndege kutoka Mtwara, *Precision Air* inafika mpaka shilingi milioni 12. Mimi mwenyewe nimesafirisha kijana ambaye alipata ajali ya gari kwa shilingi milioni nane kwa *ATC,* kutoka Mtwara kwenda Dar es Salaam, ni wangapi wanaweza gharama hizo? Kwa hiyo, tuwaombe wenzetu wa Wizara ya Afya mkamilishe ujenzi wa Hospitali ya Kanda ya Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo Hospitali za Rufaa za Mikoa, naomba tuzifanye ziwe kweli Hospitali za Rufaa za Mikoa. Unakwenda Hospitali ya Rufaa ya Mkoa unakuta ina *oxygen machine* moja, wakija wagonjwa wawili mmoja anakuwa kwenye mashine mwingine hata kama anahitaji ile huduma hawezi kupata. Tuombe muweke *MRI,* muweke *CT Scan, X-ray machines,* angalau hata kwa Kanda. Kwa sababu tunazungumzia suala la ugonjwa wa kansa ya kizazi ndiyo ugonjwa ambao unaua sana akina mama, lakini huduma hiyo inapatikana hospitali ya *Ocean Road* peke yake, na ugonjwa huo mgonjwa akiwahi unatibika. Kwa hiyo, niombe basi huduma hii ipelekwe angalau kwenye Kanda. Hivi ni wangapi wenye uwezo, unatoka Rukwa, unatoka Kagera kwenda Dar es Salaam na kila dozi inapokuja uende, kwa kweli, ndiyo kule utatibiwa bure, lakini mara nyingi gharama za kwenda kule huwa wanajigharamia. Kwa hiyo niombe kwa kweli hili lifanyiwe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la kuweka vifaa *MRI, CT Scan* na *X ray machines* siyo lazima Serikali ifanye, tunaelewa kwamba Serikali haina uwezo wa kugharamia kila kitu na tunaona unapokwenda kwenye hospitali pale Muhimbili kama mashine haifanyi kazi unaambiwa ukapime nje, kwa nini msiingie ubia mkafanya *PPP,* hizo mashine wakaja kuziweka kwenye hospitali zetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe Wizara ya Afya mshirikiane muingie ubia, vitu kama *MRI, CT Scan, X-Ray,* kila baada ya miaka mitano teknolojia inabadilika na hatuwezi kwenda na kasi hiyo, lakini akiweka mtu binafsi ikipita muda wake unamwambia hamisha leta nyingine inayoendana na teknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante, muda wako umemalizika. Tunaendelea na Mheshimiwa Ester Michael Mmasi na baade atakuja Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya dakika tano amegawana na Mheshimiwa Haonga.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru na mimi kunipa nafasi hii niweze kuchangia kwenye Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe walionitangulia utaona wengi wameonesha kusikitishwa ama kuwa na mkanganyiko fulani kwenye masuala haya ya *D by D* yaani ugatuzi wa madaraka. Leo hii Wizara ya Elimu tunaambiwa kwamba wao ni wabeba sera lakini utekelezaji wa azma hii ya kutoa elimu bora kwa Watanzania wameachiwa TAMISEMI.

Mheshimia Mwenyekiti, ifike mahali hebu tuone hili suala linahitaji umakini mkubwa sana kwa upande wa Serikali, kwa nini ninasema hivyo? Ukiangalia hapa michango yetu mingi kwenye elimu tunaongelea vyuo vikuu lakini tunapwaya sana au tunakuwa na machache sana ya kusema ama tunakuwa na *insight* finyu sana kwenye masuala mazima ya elimu kwa upande wa shule za misingi lakini hata sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wenzangu watakubaliana na mimi, yako mambo mengi ambayo bado yanahitaji michango yetu, michango mikubwa ambayo tunaweza kusema na ifike mahali Serikali iweze kutuelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala zima ya uendeshaji wa shule za msingi na sekondari zipo changamoto nyingi lakini *solution* zinazokuja hapa tunashangazwa kusikia kwamba Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa wanachukua madaraka kwa kuwafukuza walimu kuona kwamba walimu hawa ndiyo wanaosababisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najiuliza hivi viongozi hawa waliwahi kukaa chini na kufanya tathmini kujiuliza hata hii *standard* ambayo imekubalika kwenye mpango wa *BEST* taarifa ya mwaka 2012/2015 ile *student ratio* yaani mwalimu mmoja kwa wanafunzi 44 haya wanayasemea wapi?

Tunachosikia ni walimu kufukuzwa mashuleni hili hatutakubaliana nalo. Lakini wamejiuliza kuhusu miundombinu? Lakini wamesahau walimu wanadai satahiki zao miaka na miaka. Ifike mahali tuone kwamba tunahitaji kauli ya mwisho kabisa ya Serikali juu ya hatma ya walimu wetu, stahili za walimu, haki za walimu wetu zinalipika na tunahama kwenye hii ajenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ni shahidi na mimi pia ni shahidi na Wabunge wenzangu ni mashahidi. Mwaka jana kwenye uwasilishaji wa bajeti ya Serikali nilipata taarifa kwa Dada yangu ninayempenda sana, Kiongozi wangu mahiri, Mheshimiwa Angellah Kairuki ambaye ni Mheshimiwa mwenye dhamana Ofisi ya Rais, Manejimenti ya Utumishi wa Umma akisema kwamba kuna Bodi ya Mishahara na wamejipanga *comes this February* kwamba madai ya walimu yatakuwa yamefika sehemu ambapo Serikali itakuwa na kauli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafikiri tutakapofika kwenye majumuisho tunahitaji kauli ya Serikali ni lini masuala haya yatakwisha? Tumechoka kuimba nyimbo hii miaka kenda mia, tumechoka, inasikitisha na inaumiza sana. Ukiangalia wengi hapa tumefika kwa sababu ya uwezo wa walimu wetu. Hatukufika hapa kwa sababu ya ngonjera, midomo mizuri ya kuimba ngonjera hizi, tulikaa darasani, tukaelimishwa, tukaelemika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa lililoelimika ni Taifa ambalo litafika kuthamini nguvu kazi ya Serikali na kufanya tafsiri yenye maana kwenye masuala mazima ya maendeleo. Kwa nini nasema hivi? Tumeongea masuala ya mikopo na Wabunge wengi wamechangia kwenye upande huu.

Mimi nimeenda pale chuo cha *NIT* majuzi hapa nikakuta pale kuna vijana wa mwaka wa pili na mwaka wa tatu, wananfunzi 38. Wanafunzi hawa hawajalipiwa ada ambao kwa ujumla wao wanafunzi hawa wanasoma programu ya uinjinia wa vyombo vya angani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana hawa wanaosoma *Engineering Maintenance in Aircraft* wamefika mahali wako *stucked* hawana pa kwenda. Mimi najiuliza kweli tunafika mahali tunashindwa kutafsiri hatua ya Serikali katika masuala mazima ya maendeleo? Leo tumeagiza ndege mbili, tuna mpango wa kuongeza ndege, lakini tumerudi nyuma kutafsiri rasilimali yetu ambayo itakwenda kuwezesha hatua hizi za Serikali. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Waambie.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli! Leo hatujajipanga pengine tunafikiria kwenye *ku-poach* lakini ni gharama sana. Sisi tunaweza kuajiri mtu wa *Emirates?* Hatuwezi. Tunapoanza hapa tumemchukua Mkurugenzi wa *ATCL* Senegal lakini pia *Technical Manager* wa *ATCL* tumemchukua Rwanda. Hawa watu tutashindwa kufika mahali kuona ufanisi wao kwa sababu tumefika mahali ambapo tunashindwa kutafsiri *investment* inayofanywa na Serikali kwenye masuala mazima ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifike mahali tuone kwamba hawa vijana wetu wa *NIT* wanaosomea uinjinia na urubani pale wafike mahali Serikali iwalipie ada yao. Ada yao ni shilingi 10,500,000/=, shilingi 400,000,000 Serikali inapata ugumu gani kulipa hawa watoto wakasoma? Tutawaacha yatima mpaka lini? Lakini hatuoni unyeti, hatuoni nguvu ya Serikali tunayo *invest* pale na hata kuweza kuwakomboa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni gharama sana kumsomesha mwanafunzi ambaye anasoma *course* hii hapa *NIT* ukimpeleka Rwanda ni shilingi milioni 80, lakini kweli tunafika hapa kudharau na kuona kwamba *comes rain, comes sun* mambo yatakuwa sawa? Siyo sawa, ifike mahali tuone kwamba sisi kama Wabunge, sisi kama viongozi wenye dhamana tuna kila sababu ya kuisemea Serikali yetu na kuonesha njia pale inapobidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala haya ya mikopo ni masuala ambayo inabidi kwa kweli tuweze pia kuoanisha. Leo wanamaliza wanafunzi 250,000 mathalani, lakini tunajiuliza baada ya hapa ni vipi? Tunasema hii *fund* iweze kuzunguka na kuweza kufikia watoto maskini zaidi na zaidi lakini mbona hakuna uwiano hapa? Wanaomaliza ajira zao ziko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *last year* hapa tumekaa, tumeongea masuala mengi, kutakuwa na Benki ya Wakulima, leo hii katika zile shilingi bilioni 55 nakumbuka, zimetoka *only three percent* tukasema kutakuwa na dirisha la

vijana, mimi nikauliza hapa, dirisha la vijana likiwepo wanakopeshekaje hawa watu? Wakiwa na Hati za Kimila watakopesheka, *God forgive!* Mashamba haya nani kawapa watoto?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifike mahali tupunguze ngonjera tuende kwenye vitendo. Tuna mengi ya kujibu tutakapokwenda kuomba kura majimboni. Ninarudia kusema kwamba Taifa lililoelimika ni Taifa ambalo litafika kukaa chini na kufanya tathmini ambayo inalenga maendeleo chanya katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni pesa nyingi sana zinapotea pale Bodi ya Mikopo. Mimi nimesikiliza, ninyi ni mashahidi, tulipitisha hapa sheria mbili juzi tu hapa, kulikuwa na ile *Valuation and Valuer Registration Act* ya mwaka 2016, lakini pia tulipitisha ile *Procurement Act*. *Procurement Act* ilikuwa inatambua asilimia 30 ya vijana waweze kutambulika Serikalini, waweze kufanyakazi na Serikali kwa maana kwamba kutoa *service,* kufanya *consultancy* na vitu kama hivyo. Uwezo mmewajengea wapi? Mikopo wakatoe wapi hawa vijana? Wavunje ofisi zetu? Tupunguze maneno tuende kwenye vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani, tutakuwa hatutendei haki Taifa hili kama ujana wangu huu nakuja Bungeni kupaka *lipstick* na kupaka wanja na kurudi nyumbani, haiwezekan! Mimi sitakuwa tayari kupaka *lipstick* hapa ndani na wakati vijana hawana kazi, tutakuwa hatutendei haki Taifa hili. Sisi ni vijana akina Mheshimiwa Bulembo mnisikilize, tusimame hapa na tuisemee Serikali yetu kwa nia njema kabisa, lazima vijana watambuliwe, lazima vijana wapewe *status* yao katika hii nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mengi ya kusema nafikiri nikiendelea naweza nikatoa machozi, naomba niishie hapo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Ester. Tunaendelea na Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya dakika tano na Mheshimiwa Haonga dakika tano na baadae Mheshimiwa Esther Matiko ajiandae.

**MHE. LUCY F. OWENYA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia. Mimi nitachangia katika suala zima la UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa zinaonesha kwamba UKIMWI bado maambukizi yapo nami ninaona kama ni janga la Taifa. Watu zaidi ya milioni 1.4 sasa hivi wameambukizwa *HIV* na watu 54,000 wana maambukizi mapya na watu 36,000 wamekufa na *AIDS,* asilimia 53 wanatumia dawa za *ARV*. Takwimu

hizi zinatisha, lakini kitu kinachonisikitisha, Mfuko wa UKIMWI bado haujatoa fedha za kutosha. Zamani tuliona kwamba waliweza kutoa matangazo, kuweka vibao kwa ajili ya kutoa elimu kwa ajili ya UKIMWI, lakini sasa hivi matangazo yale hayapo na tumeona mara nyingi nimekuwa nikizungumzia suala zima la maambukizi ya UKIMWI kutokana na wanawake wanavyoenda saluni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake huwa wanakwenda saluni kutengeneza kucha na wakitengeneza kucha wana-*share* vile vyombo, zile *nail cutters* kwa ajili ya kusafishia kucha. Ni hatari sana sababu vyombo vile havisafishwi ni chuma na huwa saa nyingine mtu anaweza akajitoboa na kuambukiza yule ambaye alikuwa ameenda saluni kutengeneza kucha. Sijui ni kwa jinsi gani mpaka leo hii Wizara imeweza kuwapelekea wale wenye saluni elimu hii ili waweze kutumia vifaa vya kinga, maana saa nyingine wanafanya hata *scrub*, anaweza akam-*scrub* yule mtu lakini yule mtu ukute ana kidonda au yule anayefanya ile *scrubing* na yeye ana kidonda, kwa namna moja au nyingine anamuambukiza yule ambaye alikuwa anamfanyia hiyo *scrubing.(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile hizi *treatment centre,* unakuta watu wenye UKIMWI wanaenda sehemu moja kwenye kitengo ambacho wanakwenda kupata ushauri nasaha pamoja na kupewa dawa, lakini wamekuwa wanapata unyanyapaa na unyanyapaa bado unaendelea. Mimi ningeshauri, ni kwa jinsi gani Serikali inaweza ikajumlisha magonjwa sugu kama kisukari, shinikizo la damu na hawa wenye magonjwa ya UKIMWI wakakaa pamoja, wakapewa zile *treatment,* wakapewa dawa na hii itawafanya wale wagonjwa wenye UKIMWI kuwa na ari zaidi ya kuweza kwenda kupimwa na wale ambao wana magonjwa ya kisukari na magonjwa ya shinikizo la damu wataweza kukubali kupimwa kwa urahisi kwa sababu watajisikia kwamba hawanyanyapaliwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo hii inaenda sambamba na dawa za kulevya  na viroba. Hivi ni vitu ambavyo vinapunguza sana nguvu kazi katika nchi yetu, vijana wengi sana wameathirika, tunajaribu kujenga shule lakini sijui hawa watoto watakaokwenda kwenye hizo shule ni nani kama hatutalichukulia janga hili kama janga la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha vijana zaidi ya 550,000 wameathirika na dawa za kulevya . Kati ya hao 550,000 ni 50,000 ni kwa ajili ya kujidunga zile sindano na tunajua kabisa wakijidunga sindano wanaweza wakapata maambukizi ya UKIMWI. Mimi nafikiri Serikali ingewachukulia hawa mateja kama wagonjwa badala ya kuwakamata na kwenda kuwafunga *lock*

*up*. Hawa ni watu ambao wanahitaji kutibiwa kwa sababu ni wagonjwa na mara nyingi hawa mateja badala ya kuwapeleka hospitali za watu wenye magonjwa ya akili, mimi nashauri mtengeneze *centres* za kuwapeleka hawa vijana kwa sababau vijana hawa siyo vichaa, unakuta tu wamekuwa mazombi fulani wala hawamdhuru mtu lakini ukienda kuwachanganya na wale wagonjwa wenye matatizo ya akili wale wanakuwa *hyper* wanaweza wakawapiga, wanachukua vyuma wanapiga watu, lakini hawa wanahitaji kwamba wawekwe mahali vizuri, wapewe dawa, wapewe elimu ili waweze kuondokana na dawa za kulevya .

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na wenzangu wote kabisa hii habari ya kukamata vijana ambao wanatumia dawa za kulevya wale ni *innocent,* wanatumia tu zile dawa mimi nafikiri ni vizuri mkawakamata wale wanao-*supply* na hawa vijana wapelekwe waende wakatibiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka naomba nizungumzie suala zima la saratani; Saratani tunajua kutokana na taarifa ni zaidi ya watu 27,000 wanafariki kwa ajili ya magonjwa ya saratani. Kuna baadhi ya saratani kama elimu ikitolewa ya kutosha yanaweza yakatibika, kama tezi dume, saratani ya shingo ya kizazi, saratani ya matiti inayotokana na ulaji mwingi wa mafuta, kuna Saratani nyingine za ngozi ambazo wanawake wanatumia vipodozi vya kujichubua wanapata ugonjwa wa kansa kutokana na vipodozi. Wizara itoe elimu, wanawake waache kutumia hivi vipodozi vya kemikali kali ili...

*(Hapa kengele ililia kuashiri kwisha kwa muda wa Mzungumzaji )*

**MWENYEKITI:** Ahsante umeisha muda wa dakika tano, tunamuita sasa Mheshimiwa Haonga na baadae Mheshimiwa Esther Matiko halafu kuna wawili wamegawana hawa; Mheshimiwa Mlinga na Mheshimiwa Kadutu wamegawana dakika tano wajiandae.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti na mimi naomba nichangie, lakini naomba nianze kwa kusema kwamba taarifa hii ya Kamati, vitu vingi wamezungumza kusema ule ukweli kabisa vitu ambavyo ni vya ukweli japo kuna baadhi ya vitu naona kwamba kidogo kuna shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taarifa hii ukurasa wa nane, wamegusia Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu na Waziri wa Elimu yuko hapa. Miongoni mwa vitu ambavyo Mheshimiwa Waziri vitakuja kukuondoa siku za hivi karibuni nadhani ni Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Mheshimiwa Waziri kusema ule ukweli kabisa ameshawahi kuzungumza na ndugu yangu Heche hapa Bungeni, ulipokuwa Baraza la mitihani pale ulikuwa na heshima kubwa sana Mheshimiwa

Waziri lakini leo umeletwa kuwa Waziri wa Elimu kwa kweli *to be honestly* heshima yako imeshuka sana kutokana na yale ambayo yanaendelea katika Taifa hili hasa kwenye elimu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wale watoto wetu ambao walikuwa wanadahiliwa siku za nyuma kwa mfano mwaka 2014/2015 walidahiliwa wanafunzi 58,000 na *TCU;* lakini waliopata mikopo ni zaidi ya 40,000 zaidi ya nusu ya wanafunzi walipata mikopo. 2016/2017, wamedahiliwa wanafunzi 58,000 waliopata mkopo ni wanafunzi 20,000. Ukiangalia Awamu ya Nne walifanya vizuri zaidi katika suala hili la kutoa mikopo kwenye elimu ya juu lakini Awamu ya Tano ime-*prove failure* kabisa na Mheshimiwa Ndalichako hili unatakiwa ujipime, ujitathmini uone kama unatosha kuendelea kuiongoza Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema ule ukweli wako wanafunzi ambao walikuwa wanaendelea na masomo, wameshakopeshwa, yupo mwaka wa pili, mwaka wa tatu leo unasema kwamba hana sifa, unamuondoa kwenye mkopo. Sijajua vizuri kama hizi ni akili au ni matope lakini najua kabisa kwamba ni Serikali ambayo haipo makini kabisa katika kuhakikisha kwamba wanaboresha elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema ukweli kabisa kwenye hii mikopo wapo wanafunzi ambao wanadai haki baada ya kuona mikopo imecheleweshwa, wanapokuwa wanadai haki wanafunzi hawa wanafukuzwa chuo, wanaonekana kwamba ni wakorofi, hawafai kuendelea kusoma. Kuna mwanafunzi mmoja anaitwa Alphonce Lusako, huyu kijana amefukuzwa chuo mwaka 2011 kwa sababu alikuwa anadai fedha za wale ambao wamecheleweshewa mkopo mwaka 2011, kijana huyu amerudishwa chuoni mwaka jana 2016, lakini mwaka huu 2017 amefukuzwa tena kwa sababu ya kudai haki ya wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri leo ulitakiwa uwe wa kwanza kuondolewa kwenye nafasi yako kuliko kusimamisha wanafunzi wanaodai mkopo, chanzo cha kudai mkopo ni kwa sababu ninyi mnachelewesha, mikopo yenyewe haitoshi, wanapokuwa wanadai haki mnawafukuza badala ya kwamba Serikali iweze kuwajibika.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Elimu ya Juu kwa kweli hapa lazima iondoke na watu, kama Taifa tuweze kujitathmini upya tuangalie ni akina nani wanaweza wakaongoza. Naomba niseme tu kwamba yapo mambo mengi na madudu mengi sana kwenye Bodi ya Elimu ya Juu wamezungumza wengi sitaki nirudie sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala lingine japokuwa kuna mmoja amesema suala hili la TAMISEMI ni kweli kabisa. Kuna mambo ya TAMISEMI na kuna mambo mengine ya Wizara ya Elimu, lakini mambo haya ni kama mapacha yanaenda pamoja. Leo watoto wetu wanafeli kwa sababu walimu walishakata tamaa. Leo walimu wanaidai Serikali fedha nyingi sana. Serikali inawaambia walimu kwamba asiyetaka kazi aache. Ni kweli walimu wengi leo wameacha kazi wamebaki na utumishi. Kilichotufikisha leo hapa ni kwa sababu ya walimu kukata tamaa na ndiyo maana mmoja ametoa takwimu hapa shule za binafsi zinafanya vizuri kwa sababu kule hakuna madai. Shule zetu za Serikali, hizi za umma zinafanya hovyo kwa sababu walimu wetu tunawakatisha tamaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukiangalia kwa mfano Mkoa wa Songwe madai zaidi ya shilingi bilioni mbili hayajalipwa kwa walimu wetu, Wilaya ya Momba, Wilaya ya Mbozi na Wilaya ya Ileje, shilingi bilioni mbili hawajalipwa. Waziri ninaomba katika hili tafadhali muweze kuliangalia muone kama mnaenda sawasawa.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Haonga muda wako umeisha.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni kuhusu *TBC*..

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haonga naomba ukae chini tafadhali, naomba ukae chini…

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *TBC* tunailipia kodi zetu lakini inatangaza habari za Chama cha Mapinduzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haonga muda wako umekwisha naomba ukae chini. Mheshimiwa Esther Matiko tuendelee.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia fursa hii niweze kuchangia. kwanza kabisa, naunga mkono ripoti za Kamati zote mbili lakini nitajielekeza sana kwenye suala la elimu kama ambavyo tunajua elimu ya Tanzania iko *ICU.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaenda kushauri baadhi ya maeneo ambayo Serikali inatakiwa iyafanyie kazi ili walau tuweze kuwa na elimu iliyo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Dunia ilishauri ili Taifa liweze kuwa na elimu bora walau tuweze kuwekeza 5% ya Pato la Taifa. Ukiangalia nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, wenzetu wamewekeza vya kutosha. Kwa mfano, Kenya wamewekeza 6% ya pato la Taifa, Rwanda wamewekeza 5%, Uganda wamewekeza 4%, Burundi wamewekeza 3% lakini sisi Tanzania tumewekeza 1% tu ya Pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutashikana uchawi hapa, Wakuu wa Mikoa watawafukuza walimu kama tulivyosikia Mtwara, wanasiasa wataingilia, watawaghadhibu walimu lakini uhalisia ni kwamba hatujawekeza vya kutosha kwenye elimu ya Watanzania. Kama Taifa lazima tuwekeze vya kutosha. Kamati hapa imesema tunatenga fedha lakini haziendi.

Kwa hiyo, naomba kabisa Waheshimiwa Wabunge tuazimie na kwenye bajeti ya 2017/2018 tuhakikishe walau tunatenga 3% ya Pato la Taifa kwenye elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kushauri Rais aone kwamba ni wakati muafaka sasa wa kuunda tume ya kuweza kuchunguza hali ya elimu nchini ili waje na mbadala wa nini kifanyike kuweza kufufua elimu yetu. Pia ni wakati sasa Waziri aweze kuteua Wajumbe wa Baraza la Kumshauri kwa mujibu wa sheria ya mwaka 1978 na marekebisho yake ya mwaka 1995 ambao watakuwa wanamshauri Waziri kitaalamu maana tumekuwa tukishuhudia sasa hivi Mawaziri wanatoka tu na matamko. Kwa hiyo, tunaomba kabisa aunde lile Baraza liweze kumshauri kitaalam ni vipi tuweze kusonga mbele katika elimu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuwathamini walimu, mimi ni mwalimu. Walimu wasipokuwa na motisha hatuwezi kuwa na elimu bora. Imeelezwa hapa kwa mujibu wa takwimu za CWT ni zaidi ya shilingi trilioni 1.06 walimu wanadai. Wale ambao wamerekebishiwa mishahara ni walimu 5,000, walimu 80,000 bado hawajarekebishiwa mishahara wanadai zaidi ya shilingi bilioni 300, kuna wale walimu ambao wamestaafu takriban 6,000 wanadai zaidi ya shilingi bilioni 480 na kuna wanaodai madeni ya likizo ambayo hata bado hayajaboreshwa. Malengo ya *BRN* walisema walimu waweze kulipwa madeni yao ndani ya siku 90, sasa ni kwa nini Serikali inachukua muda mrefu sana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ni kuhusu utekelezaji wa Sera ya Elimu kwa Wote *(Universal Secondary Education)*. Kwa maoni yangu nashauri sera hii tusiitekeleze sasa hivi kwa sababu Serikali haijajiandaa. Kwa mfano, ukisema elimu ya msingi iishie darasa la sita na waendelee kwenda sekondari

kwa wote, tumejenga sekondari zipi za kuweza ku-*absorb* hawa watoto wanaotoka shule ya msingi na kuendelea moja kwa moja, bado hatujajiandaa! Ni dhahiri sasa tuweze kujiandaa kwanza kama nchi, kwa baadaye ndiyo tuweze kutekeleza hii Sera ya Elimu kwa Wote.

Kwa hiyo, iendelee watoto kujiandikisha shule wakiwa na miaka saba na elimu ya msingi iendelee kuwa darasa la saba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni wanasiasa kuingilia masuala ya kitaalam ya walimu. Utakuta Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Mkoa anajaziwa mafuta eti anaenda kukagua shule wakati huo huo wakaguzi ambao ni wataalam wanakagua kwa 30% tu na wanasema hawana fedha za kuweza kuwazungusha kukagua shule. Sasa hawa Wakuu wa Wilaya na Mikoa wengine hata hawana utaalamu huo, wako *busy* wanajaziwa mafuta kuzunguka kukagua shule. Tusiingilie kabisa kwenye masuala ya kitaalamu tupeleke fedha kwa wakaguzi waweze kukagua na kutoa mapendekezo ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ni kwenye afya kuhusu Taifa la vijana kuteketea na viroba. Kamati hapa imesema na mimi Jimboni kwangu kabisa waliniambia nilete Hoja Binafsi. Hivi viroba na sasa hivi hali imekuwa ngumu vijana asubuhi tu na mmewakataza wasiende kwenye *bar* mpaka saa kumi, kwa hiyo, wenyewe wakiamka tu asubuhi na pikipiki zao wamekamatwa na polisi na wengine kazi ngumu ngumu wanakunywa viroba vile. Viroba kwanza havina *standard! (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimboni kwangu nilivyokuwa nimekwenda baada ya hii likizo fupi tumezika vijana zaidi ya wanne na wananchi wamenituma kama Bunge tuazimie viroba vifutwe Tanzania, visizalishwe wala visiingizwe Tanzania.

Kwa hiyo, naunga mkono kabisa mapendekezo ya Kamati kuhusiana na viroba viweze kupotea kabisa vinginevyo tunateketeza Taifa letu, vijana ambao ni nguvu kazi ya Taifa wanateketea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine na cha mwisho ni kuhusu dawa za kulevya, zimezungumzwa kwa upana wake. Kama Taifa tujiulize ni kwa nini tumekuwa tukiimba, hatutekelezi. Kabla ya mwaka 2010 hata sijawa Mbunge tunaona kuna ma-*champions* walikuwa humu wakizungumzia dawa za kulevya na wengine wakataja kabisa, Marehemu Amina alitaja baadhi ya watu hapa. Tukaja Bunge la Kumi wengine tukawa Wabunge, Mheshimiwa Dkt. Ndugulile,

Mheshimiwa Bulaya, Mheshimiwa Jenista, Mheshimiwa Rais Kikwete akasema ana orodha….

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Lakini tunaona Awamu ya Tano wanaibuka na orodha nyingine wasitumie ileile... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Esther muda wako umekwisha. Tunaendelea na Mheshimiwa Goodluck Mlinga dakika tanona Mheshimiwa Kadutu dakika tano baadaye wajiandae Mheshimiwa Gashaza na Mheshimiwa Msukuma dakika tano, tano.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Jambo langu la kwanza naomba nitoe shukrani kwa Serikali kwa kunifanyia ukarabati Kituo cha Lupilo na kunijengea *theatre.* Hii inadhihirisha uchaguzi wao wa kumchagua Rais jembe na Mbunge jembe. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nije kwenye suala la elimu. Wizara ya Elimu kila siku inatoa miongozo, juzi hapa wamesema *private school* wapunguze ada, wawawekee kiasi cha ada yaani wao Serikali ndiyo wawe waamuzi, lakini hao hao Serikali wanaziwekea kodi nyingi hizi shule za *private,* sasa tunafanya nini? Ninyi Serikali si mna shule zenu na si mna shule nyingi, kwa nini msiwe mnatoa miongozo kwa shule zenu ili zifaulishe? Ada tunalipa sisi wazazi ninyi nini kinawakereketa? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mzazi mwenyewe ataamua, atachagua mwenyewe shule ya kumpeleka motto wake. Hawa wanapandisha ada kwa sababu *demand* imekuwa kubwa wasingekuwa wanapandisha ada. Wazazi wenyewe wawe waamuzi, waamue wapeleke au wasipeleke watoto wao katika shule hizo. Kwa hiyo, fanyeni maamuzi kwa shule zenu. Mlikuwa na shule Mzumbe, Pugu, ziko wapi sasa hivi, sifuri tupu! Kwa hiyo, fanyeni maamuzi kwa shule zenu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili kwenye hizo hizo shule za *private,* kwa mfano Jimboni kwangu mimi kuna shule inaitwa *Kasita Seminary,* Regina Mundi zinafaulisha kweli! Shule hizi zinafaulisha kwa sababu wanaweka madaraja kutoka kidato kimoja kwenda kidato kingine. Mwanafunzi asipofikia wastani wanamrudisha darasa. Sasa ona wanafaulisha, ninyi mnawaamuru

watu waende tu, mbona wanapata sifuri? Halafu mnakuja mnalalamika oh, wanapata sifuri; wenzenu wana mikakati na nyie pangeni shule zenu, wekeni mikakati vizuri, faulisheni! Wazazi wenyewe ndiyo wataamua, watakubali watoto wao waende mbele au warudi nyuma. Kwa hiyo, fanyeni ya kwenu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi hatujaja kugombana na wazazi. Mama yangu Ndalichako, mwaka juzi wakati wa kampeni hukuwepo. Sisi tuliokuwepo tulitoa ahadi hizi nzuri kwa wananchi wetu. Hatujaja kugombana na wamiliki wa shule za *private,* tumekuja ku-*entertain,* tunataka elimu ya Tanzania iwe juu, lakini sio kwa hiyo miongozo mnayotoa kila siku. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu ni kwenye mikopo. Serikali ya Chama cha Mapinduzi jamani nyote ni mashahidi, Mheshimiwa Rais alisema kitu chenyewe ni mkopo halafu kinacheleweshwa lakini sasa hivi hakipo kabisa, siyo kinacheleweshwa hakipo kabisa, ndiyo. Hatujaja kugombana na wanafunzi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii wanasema ukisoma shule ya *private* hupati mkopo. Wengine wamesoma shule za *private* kwa *sponsor* na ni wengi. Kwa mfano, shule ya mama yangu Tibaijuka karibu nusu wanakuwa na ma-*sponsor* sasa leo hii anafauli kwenda chuo kikuu amepata *divison one,* eti mnamwambia kwa sababu umesoma shule ya *private* haupati mkopo. Hatuko kwa ajili ya hiyo, hatujaja kugombana na wanafunzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la nne ni hili ambalo sasa hivi limekuwa kama linashika *headlines* la dawa za kulevya. Jamani mimi naomba niwaambie, sisi viongozi na naomba ni-*quote* Ahadi Namba 8 ya mwana TANU, nitasema ukweli uongo kwangu mwiko. Kwa hiyo, nitakachosema mtu yeyote akitaka anihukumu akihukumu chama changu kwanza na kama wewe mwana CCM utanichukia, rudisha kadi ndiyo unichukie. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyabiashara wa dawa za kulevya hamna asiyewajua, tunawajua! Humu ndani wapo, nje ya Bunge wapo, kwa nini hatuwataji tunakaa kimya?

**MBUNGE FULANI:** Sema sema.

**WABUNGE FULANI:** Wataje.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kwa ridhaa yako unaniruhusu mimi nitawataja hata humu ndani.

**WABUNGE FULANI:** Wataje.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dawa za kulevya ni pamoja na bangi. Kuna Mbunge alisimama humu alisema bangi hazina madhara, alijuaje kama hazina madhara kama hatumii? Tungeanza na huyu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, viongozi wenzangu, naomba niwahakikishie kama tutakuwa wanafiki mbinguni sisi ndiyo tutakaokuwa kuni. Tunawafumbia macho wafanyabiashara wa dawa za kulevya na tunakula nao. Nimpongeze sana ndugu ya Makonda wa Dar es Salaam kwa kuthubutu kutaja neno dawa za kulevya lakini nimhakikishie katika kila marafiki watano wanaomzunguka, watatu ni wafanyabiashara ya dawa za kulevya, aanze na hao! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais watu wasikuchezee akili…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Goodluck.

**MBUNGE FULANI:** Aaaaah! *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Kadutu dakika tano.

**MHE. JOHN P. KADUTU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kunipa fursa hii ya kuchangia jioni hii kwa ajili ya ripoti ya Kamati zetu hizi mbili, Kamati ya Kudumu ya masuala ya UKIMWI pamoja na Huduma na Maendeleo ya Jamii. Nizipongeze sana Kamati hizi mbili kwa kuja na taarifa ambayo inatupa mwanga nini kinaendelea kwenye Kamati hizi lakini ndani ya Serikali pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mimi nichangie eneo ambalo nadhani ndani ya Bunge humu leo au siku mbili, tatu halijazungumzwa. Kwa niaba ya wanamichezo wote tuipongeze timu ya *Serengeti Boys* kwa kufaulu rufaa yake na sasa itashiriki fainali za *under 17* kule Cameroon. Fainali hizi zilikuwa zifanyike Madagascar na sasa zitafanyika Cameroon. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kutoa ushauri kwa Serikali na bahati nzuri mdogo wangu Mheshimiwa Nape yupo, ni vyema yakafanyiwa kazi haya tunayosema. Tumekuwa watu wa kufurahia matokeo. Tunapokuwa na matokeo mazuri kila mmoja anafurahia. Juzi tulipopata taarifa ya *Serengeti Boys*

kufaulu kwenda kucheza fainali tumepongezana sana, lakini hatufikirii maandalizi sasa ya michuano hii. Ni juu ya Serikali kuanza kuona ni namna gani inaweza kuweka mkono wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1980 kwa wale mliokuwepo, Serikali yetu ilikuwa bado ina matatizo ya uchumi. Tutakumbuka tulikuwa tumetoka kwenye vita ya Uganda ya Nduli Iddi Amin, uchumi wetu ulikuwa umeparaganyika sana na Mwalimu alikuwa ametupa miezi 18 ya kufunga mkanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Serikali ya Mwalimu ambaye tulidhani labda hapendi michezo, ilitia mkono wake tukafika Lagos kwa ajili ya *AFCON,* wakati ule tunaita fainali za nchi huru za Afrika. Hata matokeo tunayoyaona ya Cameroon, Ghana na nchi nyingine hazipati matokeo mazuri tu kwa kuachia vyama vya mpira, Serikali lazima iweke mkono wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nashauri, tuanze sasa. Mheshimiwa Nape wakati wa bajeti lete mapendekezo hapa tuone kama yatakwama. Tupo Wabunge tuta-*support* ili Serikali itie mkono wake isiwe Serikali ya kusubiri matokeo mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitawapa mfano, mwaka 2014 mimi niliongoza msafara kwenda Brazil na kikosi cha watoto wanaoishi katika mazingira magumu kwenye *World Cup.* Mashindano hayo huwa yanatangulia *World Cup* yenyewe. Tulikwenda na tukachukua ubingwa wa dunia na tukakaribishwa hapa Bungeni, Waziri Mkuu wakati ule alikuwa Mzee Pinda, Serikali ikatoa ahadi nyingi tu mpaka leo hata ahadi moja haijatekelezwa. Sasa tunaanza kujiandaa kwa kombe la dunia lingine mwaka kesho. Mwaka kesho ni *World Cup,* sisi tutatangulia kwenda Urusi na timu ile kwenda kutetea ubingwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuiombe Serikali basi itie mkono pale tutakapohitaji msaada hata nauli. Maana yake tunagharamia wenyewe, tunakuja na kikombe tunafurahia wote kwa pamoja. Iko haja ya Serikai kuliona hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli tunataka kushinda, tunataka kwenda kufanya vizuri kule Cameroon na watoto hawa wa *under 17*…..

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Muda wako umemalizika, tunashukuru.

**MHE. JOHN P. KADUTU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Gashaza kwa dakika tano na baadaye Mheshimiwa Musukuma dakika tano halafu tutaendelea na Mheshimiwa Ikupa na Mheshimiwa Amina Mollel kwa dakika tano, tano.

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia taarifa za Kamati hizi mbili, Kamati ya UKIMWI na Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nianze kwa kupongeza Kamati hizi kwa kazi nzuri walioifanya na niwapongeze waliotangulia kuchangia. Mengi wameyagusa, mimi nijielekeze tu kwanza kwenye suala la elimu.

Mheshimiwa Mwenekiti, kama wengine walivyotangulia kusema hakuna namna ambavyo Taifa lolote lile linaweza kuendelea kama bado halijaweza kuelimisha watu wake. Kwa kutambua kwamba kupitia elimu ndipo unapoweza kuwa na rasilimali watu iliyo bora na zaidi hasa katika kujenga msingi. Ukijaribu kuangalia rasilimali hii muhimu tunaanza kuipoteza kuanzia darasa la saba, tunakuja sekondari kwa maana kidato cha nne pale ambapo tunajikuta tumehamasisha, tumejenga shule nyingi za kata tukitegemea watoto wetu waweze kupate elimu hii na waweze kuendelea hadi vyuo vikuu lakini kwa matokeo kwanza ya mwaka huu ya kidato cha nne unaweza ukaona ni rasilimali kiasi gani ambayo itabaki nyuma huku vijijini ambayo ni nguvu kazi vijana kama hatukuweka mpango mahsusi kwa ajili ya kuona ni namna gani ambavyo rasilimali hii tunaweza tukaiboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishukuru Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia wamejaribu kuweka mpango wa kuanzisha vyuo vya *VETA*. Niombe mpango huu usiwe katika karatasi tu, uwe ni mpango unaotekelezeka, vinginevyo kama tutaendelea kupoteza rasilimali hii muhimu, kila mwaka vijana wetu wanamaliza kidato cha nne, zaidi ya 60%, 70% wanabaki vijijini, hawana ujuzi wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoteza rasilimali hii muhimu na hasa ukizingatia tunajipanga sasa Taifa hili liweze kuwa linajenga uchumi kuelekea kwenye uchumi wa kati kupitia viwanda. Hakuna namna tunaweza kufaulu kama tusipoweza kuiandaa hii rasilimali muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na huduma zinazotolewa katika shule zetu, kuna kitu ambacho napenda Kamati wajaribu kuangalia. Sijui maeneo mengine lakini katika Jimbo langu la Ngara mara kadhaa kumekuwepo na tatizo la radi hususani katika maeneo ya shule. Mwaka jana tulipoteza wanafunzi watatu katika shule ya sekondari Kanazi kwa kupigwa na radi, lakini pia katika Kata ya Nyamagoma tulipoteza wananchi watatu kwenye familia moja ambao wako karibu na shule ya msingi na maeneo kadha wa kadha. Kwa hiyo, niombe…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, muda wako umemalizika. Tunaendelea na …

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga hoja za Kamati zote mbili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunamalizia na Mheshimiwa Msukuma dakika tano halafu tutakuja na Mheshimiwa Ikupa na Meshimiwa Amina Mollel.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwa ufupi dakika tano. Nianze kwa kumshukuru mdogo wangu Mlinga kwa kunitaja pengine na mimi kesho naweza kuwa mahabusu kwa amri ya Makonda. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie tu na mimi kwenye sehemu ya dawa za kulevya. Niliwahi kuchangia wakati nazungumzia kuhusu bangi na mirungi, nilieleza Taifa hili lina vyombo vya ulinzi na usalama, tuna Polisi, Usalama wa Taifa, Majeshi, vyombo vinavyoweza kutujua tabia zetu na vina utaalamu wa kuweza kumfuatilia mtu na kugundua kama kweli hiki kilichosemwa anahusika nacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napata mshtuko sana kwa hiki kinachoendelea, ni haki yangu kuzungumza kama Mbunge, kama Waziri Chikawe akiwa Waziri wa Mambo ya Ndani alisema ana orodha ya wauza unga, ameingia Mheshimiwa Kitwanga akatuaminisha mwezi mzima anataja, amewapa siku 21, hawakutaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Taifa linafanyia kazi orodha ya Makonda, napata wasiwasi. Hii ndiyo tulikuwa tunaisubiri awamu zote kuanzia kwa akina

Marehemu Amina Chifupa kwamba hawa ndiyo waliofanyiwa uchunguzi wakakutwa kweli wanauza dawa za kulevya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli ndivyo, basi hili Taifa tunakokwenda hatuendi sawasawa. Hivi kweli Watanzania tunaambiwa kuna msururu wa wauza dawa za kulevya wamekamatwa anatajwa Chid Benz na Ray C, watu ambao Taifa hili limeingia gharama ya mabilioni kumsaidia Ray C na watu walichanga kwenye M-pesa, mgonjwa unamchukua unamtia mahabusu, hatuko *serious* kumaliza suala la dawa za kulevya. *(Makofi)*

Mhehimiwa Mwenyekiti, hili tuongee lugha moja wote kwa pamoja kuondoa hata uvyama, wauza dawa za kulevya wanajulikana na hata wengine walio vigogo wa kukamata wenzao wanashinda nao na wanawasafirisha kwenda Marekani. Kwa nini vyombo vya ulinzi na usalama visimhoji Makonda, mtu ambaye siyo mfanyabiashara ameenda Marekani, Paris, Dubai kwa mshahara wa u-*RC* huu? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani ndugu zangu hiki kitu lazima tupate muda tuzungumze. Mheshimiwa Rais mimi nakuunga mkono, inawezekana Mheshimiwa Rais ana uchunguzi sahihi kuliko wa Makonda. Kama amesema kila mtu akamatwe hata mke wa Rais akamatwe na Makonda aanzie wa kwake aliowapangishia majengo. Kwa nini wa kwake wako nje na wametajwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Dar es Salaam mitaa ya wauza unga inajulikana…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Musukuma, muda wako umemalizika.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Makao Makuu ya CHADEMA ndiyo wauza unga wamejaa pale mateja.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Musukuma naomba ukae chini.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Tunaenda kuchukua mateja tunajaza magereza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma muda wako umeisha naomba ukae chini.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walimshangilia Mhe. Joseph Musukuma)*

**MBUNGE FULANI:** Na Makonda naye.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walimshangilia Mhe. Joseph Musukuma)*

**MBUNGE FULANI:** Makonda, Makonda, Makonda naye.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walimshangilia Mhe. Joseph Musukuma)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunamaliza upande wa Wabunge…

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Makonda anatumia Lexus…

**MWENYEKITI:** Majina yako mengi hatuwezi kumaliza wote kwa hiyo tunamalizia na Mheshimiwa Amina Mollel pamoja na Mheshimiwa Ikupa.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa sababu ya muda nitaenda haraka haraka. Nikiwa kama kijana, napenda na mimi niweze kuongelea kwa uchache kuhusiana na dawa za kulevya kwa sababu ni janga ambalo linaharibu ama linapoteza nguvu kazi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja niiombe sana Serikali kuitengea hii Tume ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya fedha za kutosha na kuipelekea ili iweze kufanya kazi yake vizuri kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niongelee suala la ulinzi kwenye mipaka yetu kwa sababu tunaona kwenye *airport* nyingi imeshadhibitiwa lakini bado kwenye mipaka yetu ulinzi hauko vizuri. Kwa hiyo, niiombe Serikali iimarishe ulinzi kwenye mipaka ya nchi yetu ikiwa ni pamoja na kupeleka vifaa vya kitaalamu ambavyo vitaweza ku-*detect* dawa hizi za kulevya kwa wale wanaopita kwenye hii mipaka yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja niongelee suala la elimu hasa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Kwanza kabisa, napenda niishukuru Serikali kwa kuweka ulemevu kama ni kigezo kimojawapo cha utoaji wa mikopo ya elimu ya juu. Naomba nitoe mapendekezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa watu wenye ulemavu kwa kuwa idadi ya watu wenye ulemavu ambao wanapata fursa ya kufika chuoni ni ndogo sana, hivyo niombe kabisa Serikali isitoe kama mikopo kwa watu wenye ulemavu bali itolewe kama ruzuku.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tupunguze sauti, tumsikilize Mheshimiwa aweze kumaliza.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niombe kwa habari ya elimu ya kuanzia shule ya awali mpaka kidato cha sita. Watu wenye ulemavu ambao wanapata fursa ya kwenda shule ni wachache sana na ipo ndani ya uwezo wa Serikali kuwapa elimu bure watoto wenye ulemavu kuanzia darasa la kwanza ama *kindergarten* mpaka kidato cha sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba niende ukurasa wa 45 wa Taarifa ya Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii. Ukurasa huu unaongelea mkakati wa kuongeza walimu. Naomba ninukuu; "Kamati imebaini kuwa, kuna upungufu wa walimu hususani wa masomo ya sayansi na hisabati, hali ambayo imekuwa ikiathiri kiwango cha elimu nchini. Kutokana na hali hiyo, Kamati inaazimia Wizara iandae mkakati maalum wa kuendeleza walimu wa masomo ya sayansi na hisabati ili kukabiliana na changamoto ya muda mrefu ya uhaba wa wataalamu hao katika masomo hayo."

Mheshimiwa Mwenyikiti, mimi napendekeza kwamba kifungu hiki kisomeke kwamba; "Kamati imebaini kuwa kuna upungufu wa walimu hususani wa masomo ya sayansi, hisabati na elimu maalum hali ambayo imekuwa ikiathiri kiwango cha elimu nchini. Kutokana na hali hiyo, Kamati inaazimia Wizara iandae mkakati maalum wa kuendeleza walimu wa masomo ya sayansi, hisabati na elimu maalum ili kukabiliana na changamoto ya muda mrefu ya uhaba wa wataalamu hao katika masomo hayo."

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa haraka haraka, naiomba Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ijitahidi kutembelea shule…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Ikupa, tunamalizia na Mheshimiwa Amina Mollel.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kwa hizi dakika tano zilizosalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na wale wote walio katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya na michango iliyotolewa Bungeni nawashukuru sana, niendelee katika vipengele vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la miundombinu ni tatizo na wengi wamezungumzia katika vyuo vikuu ambako pia kuna changamoto kubwa lakini pia tukiangalia katika shule za msingi na sekondari changamoto bado ni kubwa sana, mfano mabinti wengi hasa vijijini kutokana na uhaba wa mabweni hawafiki mbali zaidi. Pia kama tunavyofahamu mabinti wanakabiliwa na changamoto mbalimbali mfano tu binti anapokuwa katika siku zake za hedhi nayo ni changamoto kubwa hata Kamati imeeleza basi Wizara iangalie ni jinsi gani inaweza kusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwa wototo wenye ulemavu ambao ni changamoto kubwa sana. Naishukuru Serikali kwa suala zima la elimu bure kwa wote ambalo limesaidia kwa kiasi kikubwa wazazi wenye watoto wenye ulemavu kuwaandikisha watoto hawa shule. Siku za nyuma mzazi kama ana watoto wawili, watatu lakini ana mtoto mwenye ulemavu ni afadhali awapeleke hawa wengine, mwenye ulemavu anabaki nyuma. Kwa utafiti mdogo ambao binafsi nimeufanya watoto wenye ulemavu wengi hivi sasa wameandikishwa shule lakini changamoto ni nyingi katika shule zetu mbalimbali. Kwa hiyo, niiombe tu Wizara ihakikishe kwamba watoto wanaweza na wao kupata haki yao ya msingi ya kupata elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliuliza hata juzi katika vyuo vyetu vikuu changamoto bado ni kubwa kwa wale wanafunzi wenye ulemavu wanaopata bahati ya kwenda vyuo vikuu. Niiombe tu Serikali kupitia Wizara husika hasa katika vyuo vikuu na mfano mojawapo ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambacho miuondombinu ni tatizo. Kwa wanafunzi wanaopata bahati kwenda katika vyuo vikuu na hasa chuo hiki cha Mlimani ni tatizo kubwa kutoka darasa moja kwenda darasa lingine. Ukiangalia mazingira yenyewe katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hawawezi kupata elimu ipasavyo na wanafunzi hawa wengi wao hata matokeo yanapokuja siyo mazuri sana. Wanaopata matokeo mazuri ni bahati.

Kwa hiyo, kutokana na changamoto hii, naiomba Serikali kuangalia ni jinsi gani itaboresha miundombinu ili wanafunzi wenye ulemavu waweze kusoma pasipo changamoto yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niangalie pia katika Shirika la Utangazaji Tanzania na ni-*declare* tu *interest* kwamba mimi mwenyewe nimetoka huko. Nasikitika sana kwa Serikali kwa jinsi ambavyo kwa muda mrefu imekuwa ikisuasua kupeleka fedha na hata katika ripoti hii ukiangalia ni kwamba kila mwaka bajeti hiyo inapungua. Mimi nina imani sana na viongozi wetu walioko katika Wizara hii lakini watawezaje kutekeleza majukumu yao endapo bajeti hizi haziwezi kufika? Mheshimiwa Rais amemteua Ayub Rioba kuwa Mkurugenzi nina imani naye, lakini kama hakuna bajeti miundombinu ni chakavu, mitambo imechoka na iliyopo imezeeka ya tangu mwaka 1999...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba tu Serikali kuhakiksha kwamba bajeti hii inaifikisha katika Wizara hii ili waweze kutoa kwa *TBC. (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Amina Mollel.

Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza upande wa Wabunge kuna majina zaidi ya 50 hatuwezi kuwataja wote wengine wataendelea kuchangia siku zinazofuata. Tunaingia upande wa Waheshimiwa Mawaziri na tutaanza na Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Stella Manyanya, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla kwa dakika tano, tano. Karibu Mheshimiwa Stella Manyanya.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza, niipongeze sana Kamati kwa ushauri mkubwa ambao imetupatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la *VETA,* napenda kusema kwamba tunakubaliana kwamba lazima tuangalie *course* zake zinazoendelea kutolewa ili kuendana na hali halisi ya uhitaji wa soko na ujuzi tunaohitaji katika uchumi wa viwanda na biashara. Mfano tu kwa siku za nyuma katika baadhi ya maeneo watu binafsi walikuwa wanaruhusiwa kufanya kazi za umeme wa majumbani tu lakini sasa hivi wanaruhusiwa kufanya kazi hata za kuweka vituo vya umeme, jenereta na hata ujenzi wa laini. Kwa hiyo, na sisi tutarekebisha mitaala yetu kadri tunavyoenda ili kuweza kufikia hali inayoendana na soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kuhusiana na *UDOM*. Serikali haikuwaondoa wanafunzi wa *UDOM* ili tuweze kuhamia pale. Nachotaka kusema tu ni kwamba Serikali itaendelea wakati wote kuboresha mambo yote ambayo inaona kwamba yana tija kwa nchi. Kimsingi Chuo cha *UDOM* tuliweka nia njema ya kupeleka wale wanafunzi pale ili tupate hawa wanafunzi kwa ajili ya masomo ya sayansi na hisabati lakini likajitokeza tatizo kubwa la walimu jambo ambalo liliashiria hata kuleta migomo ya walimu yaani wahadhiri. Nafahamu kwamba hata Mheshimiwa aliyetoa hoja aliwahi kunielezea kuna tatizo gani kuhusiana na hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipotafakari tukaona kwamba wanafunzi hawa wanaweza wakapelekwa kwenye vyuo ambavyo tayari kuna walimu, ndivyo tulivyofanya, vilevile katika vyuo hivyo tulikuja kugundua kwamba hata ada yao ni pungufu kuliko hata ile ambayo ilikuwa inalipwa *UDOM* kwa kozi ileile. Kwa misingi hiyo unakuta kwamba ada iliyokuwa inalipwa *UDOM* inatosha kulipia watu wanne. Kwa hiyo, imekuwa ni tija kuwapeleka huko na wanafunzi wenyewe wanakiri kuwepo kule wanapata ufundishwaji unaostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niseme tu kwamba kwa Serikali kuhamia na kutumia majengo yale kwa sasa ni jambo ambalo lina tija, kwa sababu majengo yale yalijengwa kwa mkopo unaolipwa na Serikali na Serikali haioni tija kupanga majengo mengine wakati kuna majengo ambayo kwa sasa hayatumiki yakingojea kuendelea kuongeza walimu wa kutosheleza majengo yote.

Kwa hiyo, niseme tu kwamba pale Serikali ipo kwa muda na tunaendelea kupokea ushauri wa Kamati ya Bunge kwamba baada ya hapo tutaendelea na ujenzi katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kidogo suala hili la ufaulu. Nitoe mfano wa maisha ya kawaida. Unaweza ukawa kila siku unamwona mume au mke wako siyo mzuri ukafikiria mume au mke wa jirani mzuri kwa sababu anakula nyama kila siku, ukafikiria wa kwako sivyo. Tumezisema sana na kuzisimanga shule hizi ambazo ni za kwetu za kata kwamba labda hazifanyi vizuri. Nataka tu niwaeleze ukweli na hili nalisema kwa ajili ya kusaidia kuiona Serikali imefanya nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda mnielewe naposema hivi simaanishi kwamba shule hizo zinafanya vizuri sana, hapana, nakubaliana kabisa kuendelea kuboresha. Nachojaribu kusema ni kwamba ukienda ndani katika matokeo ya hizi shule, kwa mfano shule ya Kibaha utakuta watoto waliofaulu *division one* ni 72, *division two* ni 22, *division three* ni nne na *division four* mmoja.

Kutokana na hiyo *division four* na *one* wamewavuta kwenye ufaulu wao kiasi cha kuwaweka ni watu wa 16, lakini ukienda Feza hiyo ambayo tunasema imekuwa ya kwanza yenyewe ina wanafunzi 65 na *division one* ni 59 na *division two* ni sita. Kwa hiyo, ukiangalia kwa idadi ya watu utakuta kwamba shule imefanya kazi kubwa. Hali kadhalika ukienda katika shule nyingine, kama shule ya Kilimanjaro utaona hivyo hivyo, inaonyesha hapa *division one* ni 44, *division two* ni 44, na *division three* ni 31…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Stella.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** ...lakini kuna 68 ambao ndio wanawavuta wenzao. Kwa hiyo, si kwamba shule za Serikali hazichangii zina mchango mkuwa sana.

**MBUNGE FULANI:** Simama.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** ...toka shule za kata zimeanzishwa zimechangia jumla ya watu waliopata *division one* mpaka *three* 180,542, hayo ni mafanikio makubwa sana kwa Serikali yetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Stella Manyanya tunamkaribisha Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla na baadaye Mheshimiwa Profesa Ndalichako ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hoja ya kwanza ambayo nitaanza nayo ni ya viroba kwa sababu nilielekezwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu niongoze kikosi kazi cha Serikali cha kushughulikia suala hili ambacho kilihusisha Wizara na taasisi mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka hivi tunavyoongea suala hili linaelekea ukingoni na pengine baada ya miezi mitatu viroba vitapigwa marufuku kabisa katika nchi hii na wala sio suala la kusema viroba vitaruhusiwa kuuzwa labda kwenye maeneo maalum kama *bar* ama kwenye vioski na vitu kama hivyo na vitoke kwenye maduka ya kawaida, tunaelekea kwenda ku-*ban* kabisa *(total ban)* ya matumizi ya viroba katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia suala la usagaji na mambo ya ushoga, nalo tumelishughulikia sana ndani ya Serikali na mimi mwenyewe nimeongoza kikosi kazi cha kufanya tathmini ya suala hili. Hivi tunavyoongea kuna taasisi mbalimbali ambazo zilikuwa zinajihusisha na uhamasishaji wa vitendo vya ushoga zipo katika uchunguzi na nyingine tumezifutia usajili na hazifanyi kazi katika nchi yetu. Tutaendelea kuchukua hatua dhidi ya watu wote wale ambao watapingana na tamaduni zetu ambazo zinalindwa na sheria ambayo tuliipitisha hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hapa kuna Wabunge wameniletea taarifa za shoga mmoja maarufu kwa jina la James Delicious ambaye anajiuza kwenye mitandao. Namuagiza Katibu Mkuu afuatilie taarifa hizi ili shoga huyu aweze kuchukuliwa hatua haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu kwamba watumiaji wa dawa za kulevya huku tunawakamata lakini kwa upande mwingine tunawapa tiba. Hii inajulikana kama *public health approach* kwamba hatuwezi kuwakamata watu wanaotumia na tukawachukulia hatua badala yake tuna jukumu la kibinadamu la kuwahudumia kama wameamua kufuata huduma kwenye vituo vya kutolea huduma. Kwa hiyo, suala la udhibiti lina sheria na taratibu zake, lakini pia suala la kuhudumia waliothirika lina taratibu zake kwa mujibu wa sheria na kanuni mbalimbali za afya za kitaifa na za kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la watumishi kwenye sekta ya afya, ni kweli tunakiri upungufu kwa sababu katika miaka miwili iliyopita, kwa tathmini tuliyoifanya mwaka 2016 tulipaswa kuwa na watumishi wapatao 179,509 lakini tunao 90,000 tu sawa na 51%. Kwa hiyo, tuna upungufu mkubwa, tunaufahamu na tunaendelea kuushughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine lililojitokeza ni suala la *Ocean Road Cancer Institute* kuwa na vifaa vilivyochakaa. Suala hili tunalifahamu na tayari Serikali imeweka kipaumbele cha kipekee kwenye taasisi hii inayotibu magonjwa ya saratani na hivi ninavyoongea hapa, bajeti ya dawa kwenye kituo hiki imepanda kutoka shilingi milioni 700 mwaka uliopita mpaka shilingi bilioni saba mwaka wa fedha ambao unaendelea. Mpaka kufikia Disemba tayari *Ocean Road* walikuwa wamepatiwa bajeti ya shilingi bilioni tatu na sasa hivi upungufu wa dawa kwa kweli umepungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tumeongeza idadi ya vitanda kutoka 40 mpaka 100 kwa wagonjwa wanaopokea tiba ya saratani kwa njia ya dawa na hivyo msongamano umepungua sana. Kwa sasa Serikali ina mikakati ya

kuanzisha huduma za tiba ya saratani kwenye vituo vingine mbalimbali kwenye kanda nne za nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *KCMC* kufikia Disemba walianzisha huduma ya tiba kwa dawa *(chemotherapy),* lakini Bugando mwezi Machi wataanza kutoa tiba ya mionzi kwa mara ya kwanza toka tupate uhuru ya ugonjwa wa saratani ambayo ilikuwa haijawahi kutolewa hata siku moja nje ya Kituo cha *Ocean Road.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi Hospitali yetu ya Kanda ya Rufaa ya Nyanda za Juu Kusini, pale Mbeya na yenyewe kufikia Julai itaanza kutoka huduma za tiba ya sarani kwa njia ya mionzi pale pale ili ku-*off load* mzigo wa wagonjwa ambao wangelazimika kuja mpaka *Ocean Road* kwa ajili ya kupata tiba hiyo. Sasa watapata kule kule Nyanda za Juu Kusini na tutaendelea kushusha huduma hizi karibu zaidi na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kulikuwa kuna hoja ya makazi ya wazee kwamba yamechakaa. Hili tunalifahamu na tulishalichukulia hatua. Hivi sasa tunavyoongea hapa vituo kumi vya kuhudumia wazee vinafanyiwa ukarabati kwenye maeneo ya majiko na vyoo, lakini pia tutavipelekea bajaji kwa ajili ya kuwasaidia wazee waweze kupata huduma za kupelekwa hospitali na maeneo mengine kirahisi zaidi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kigwangalla. Tunaendelea na Mheshimiwa Profesa Ndalichako.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nina dakika ngapi?

**MWENYEKITI:** Una dakika saba.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia fursa ya kuchangia kuhusu hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza kabisa napenda nianze kwa kuishukuru Kamati yangu ya Kudumu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa ushauri na mapendekezo ambayo imeyatoa katika Wizara yangu. Niseme tu kwamba kwa sababu ya muda niliopewa, haitakuwa rahisi kujibu hoja zote zilizojitokeza, kwa hiyo, naomba nijielekeze kwenye masuala machache, kadri ya muda utakavyoruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na suala la mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu, ambalo limezungumzwa na Kamati, lakini pia

limezungumzwa na wachangiaji wengi. Kuna vipengele vingi ambavyo vimezungumzwa kuhusiana na mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu. Kwanza ni suala la vigezo vya utoaji mikopo ambavyo kwa sasa tunaangalia uyatima, uhitaji, ulemavu, pamoja na vipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri kwamba hivi vigezo vina matatizo na ninafurahi kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba tayari Wizara yangu imeshaunda Kamati ambayo imepitia hivi vigezo na kuleta mapendekezo ambapo tarehe 28 tulikaa na Kamati yangu ya Kudumu na kuvipitia, nawahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba tunapoanza mwaka 2017/2018 katika bajeti hii, tutakuja na vigezo ambavyo vitakuwa vimeboreshwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la utoaji wa mikopo na kwamba kuna baadhi ya wanafunzi ambao walikuwa wanapata mikopo lakini mikopo yao imefutwa, niseme kwamba Wizara yangu imekuwa ikihakiki wanafunzi wa elimu ya juu ambao wana sifa za kupata mikopo. Wale wote ambao hawana sifa, bila kujali kwamba yuko mwaka wa ngapi, tunawafutia mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili nililisema hata katika Bunge la mwezi Novemba. Nasisitiza kwamba huo ndiyo msimamo wa Serikali. Kuna wengine ambao walikuwa wamepata mikopo kwa sababu walidai kwamba wao ni yatima; tumepeleka vile vyeti vya vifo vya wazazi *RITA* na tukabaini kwamba ni vyeti vya kughushi. Kwa hiyo, tumefuta na tutaendelea kuhakiki na wale wote ambao wamepata mikopo kwa njia ya udanganyifu, hao tutaendelea kuwaondoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la urejeshaji mikopo. Ninakubaliana na Kamati kwamba kwa kweli kasi ya urejeshaji mikopo hairidhishi kabisa. Napokea ushauri wa Kamati kwamba kama Serikali kwa kweli tunapaswa kuimarisha urejeshaji wa mikopo kwa sababu hadi kufikia Juni, 2016 Serikali ilitoa jumla ya shilingi trilioni 2.5 lakini ambazo zimekwisharejeshwa ni shilingi bilioni 147.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utaratibu huu hatuwezi kutegemea kwamba Serikali iendelee kuongeza wigo wa utoaji mikopo wakati urejeshwaji hauko imara. Kwa hiyo, hatua ambazo Serikali tunazichukua, kwanza tumeongeza kato badala ya 8% kuanzia mwezi huu ni 15%. Nitumie fursa hii kuwataka waajiri wahakikishe kwamba wanafanya makato ya mikopo na kuyawasilisha kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nihamie katika eneo lingine ambalo limezungumzwa ambalo ni suala la udahili wa wanafunzi katika elimu ya juu. Hili suala limezungumzwa sana kwamba *TCU* amegeuka kuwa dalali wa udahili katika vyuo vya binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba Serikali inaliangalia suala hilo. Katika udahili wa mwaka 2017/2018 Serikali itafanya mapitio na kuja na mfumo ambao utakuwa na tija zaidi ili vyuo binafsi navyo vijione kwamba vina jukumu la kuboresha elimu yao na kuhakikisha kwamba vinajitangaza kutokana na ubora wa elimu na siyo kutegemea kupata wanafunzi kupitia mgongo wa *TCU.* Ushauri umepokelewa na utafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo limezungumzwa ni suala la upatikanaji wa vitabu. Nikiri kwamba kumekuwa na uchelewaji wa usambazaji wa vitabu kutokana na changamoto ambazo zilijitokeza katika suala zima la manunuzi. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba leo Wizara yangu imeanza kusambaza vitabu 2,426,135 kwa ajili ya kidato cha nne mpaka cha sita. Tunategemea kusambaza vitabu takribani milioni 5.5 kuanzia wiki mbili zijazo. Kwa hiyo, hilo suala la upatikanaji wa vitabu, changamoto ambazo ni za manunuzi zilizochelewesha tutazifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala moja tu kuhusu elimu ya msingi kwa sababu limezungumzwa sana. Kuna suala ambalo limeulizwa kwamba, je, hii Sera ya Elimu Msingi ya kwamba wanafunzi wanamaliza mpaka kidato cha nne imeanza kutekelezwa au la?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine wamekuwa na maoni tofauti, napenda kutoa ufafanuzi kwamba suala la elimu ya msingi kwamba mwanafunzi atasoma kuanzia darasa la kwanza mpaka kidato cha nne limeainishwa katika Sera ya Elimu ya mwaka 2014. Ili matamko ya sera yaanze kutekelezwa, inahitaji kutungwa sheria, kanuni na taratibu. Kwa sasa sheria inayoongoza jambo hilo bado. Nawahikikishia Watanzania kwamba jambo hili litakapoanza kutekelezwa mtajulishwa, lakini kwa sasa hivi bado halijaanza kutekelezwa, elimu yetu bado ni miaka saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Ndalichako. Tunaendelea na Mheshimiwa Ummy Mwalimu na baadaye Mheshimiwa Nape Nnauye atagawana dakika na Mheshimiwa January Makamba.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami jianze kwa kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa Taarifa yao, lakini nawashukuru kwa ushauri na maoni ambayo wamekuwa wakitupatia mara kwa mara katika kuboresha utendaji wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua hii niseme kwamba Wizara yangu inapokea maoni na ushauri wa Kamati kama walivyoyawasilisha hapa na ninaahidi kwamba tutayafanyia kazi masuala yote waliyoyabainisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, napenda kutoa ufafanuzi katika masuala makuu matatu kama muda utatosha na suala la kwanza ni kuhusu hali ya upatikanaji wa dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa ya upatikanaji wa dawa nchini ilikuwa inasababishwa na upatikanaji wa fedha, lakini hivi ninavyosema tumetoka katika kutaja bajeti ya Afya ya shilingi bilioni 251 na kusema pesa ambazo Wizara ya Afya imepokea; mpaka sasa hivi tumepokea shilingi bilioni 91 kwa ajili ya kununua dawa, vifaa na vifaa tiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia mwaka 2016 *MSD* ilipokea shilingi bilioni 24 tu kwa mwaka mzima kwa ajili ya kununua dawa. Sasa hivi kila mwezi Wizara ya Fedha inatuletea shilingi bilioni 20. Tumetoka kwenye kupokea shilingi bilioni mbili kila mwezi tunapokea shilingi bilioni 20 kila mwezi kwa ajili ya dawa. Kwa hiyo, baada ya kuwa tunapata fedha, hali ya dawa kwa kiasi kikubwa inazidi kuimarika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme tunapimaje upatikanaji wa dawa? Tunaangalia upatikanaji wa dawa katika Bohari Kuu ya Dawa. Hivi sasa *MSD* ana aina za dawa 105 kati ya dawa 135 muhimu za kuokoa maisha. Hii ni sawa na 78%. Nakiri kwamba sasa hivi kazi inayoendelea ni kuhakikisha dawa hizi sasa zinashuka katika zahanati zetu na vituo vya afya.

Waheshimiwa Wabunge, nimewaandikia barua na kesho mtaipata kuainisha mchanganuo wa kila fedha ya dawa ambayo tumebajeti katika Halmashauri yako ili uweze kupima. Kubwa tunawaomba msimamie matumizi ya fedha za dawa na matumizi ya dawa. Hali ya upatikanaji wa dawa kama wote hatutaimarisha Kamati za Vituo, basi hatutaweza kuwa na upatikanaji wa dawa hasa katika ngazi za chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nitoe angalizo, hatuwezi kuwa na upatikanaji wa dawa kwa asilimia 100 kwa sababu ya ongezeko la watu kila siku, ongezeko la magonjwa na vituo. Kwa hiyo, kubwa ambalo Wizara ya Afya tunalifanya sasa hivi ni kujikita kwenye kinga badala ya tiba. Maana inakuwa ni Taifa la kujikita kwenye tiba badala ya kinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ambayo tumeibaini ni *MSD* anabajeti fedha ya kununua dawa kutoka kwenye Fungu 52 - Wizara ya Afya, lakini kuna fedha za Mfuko wa Pamoja wa Afya, kuna vyanzo vya makusanyo tumeomba wenzetu wa TAMISEMI, maana *MSD* ananunua dawa za wateja za shilingi bilioni 70, lakini wateja wake wana fedha za kununua dawa za shilingi bilioni 300. Kwa hiyo, haiwezekani *MSD* kuweza kutosheleza soko lake. Nawaahidi Waheshimiwa Wabunge kwamba tutafanyia kazi suala hili la kuhakikisha dawa zinafika kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwamba *MSD* ipewe fungu, tulipokea ushauri wa Kamati na tukamwandikia Waziri anayehusika na masuala ya Utumishi na Utawala Bora kwa sababu wao ndio wanatoa *Vote*. Wakatushauri tuombe *line item*. Sasa hivi tuna *line item* katika Bajeti ya Wizara ya Afya kwa ajili ya *MSD*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Halmashauri ambazo zinadaiwa fedha na *MSD* ziruhusiwe zilipe kidogo kidogo; tumepokea pia ushauri wa Kamati. Sasa hivi katika ile fedha ambayo tunaingiza katika bajeti ya Halmshauri, tunakata asilimia 25 tu, asilimia 75 tunawapa kwa ajili ya kusaidia upatikanaji wa dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu deni la *MSD,* mpaka sasa hivi tumelipa shilingi bilioni 11, lakini tumeona chanzo kinachofanya deni hili likawa kubwa ni tozo. Kwa hiyo, tayari tumewaelekeza tupitie tozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Kamati inashauri kwamba i-*cover* magonjwa yote. Nataka kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge kwamba kuanzia mwezi Septemba tumeingiza kitita cha huduma za upasuaji wa moyo na matibabu mengine ya hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *NHIF* kusimamia kuweza kutumika Bima zao mpaka nchi za Afrika Mashariki, sheria iliyoanzisha *NHIF* inaruhusu *NHIF* kufanya kazi ndani ya nchi. Tumepokea ushauri na tutaleta. Waheshimiwa Wabunge ni mapendekezo yenu, tutayaleta hapa ili *NHIF* itumike ndani ya nchi

za Afrika Mashariki, nasi tuko tayari na ninaamini kwamba Muswada huu mtaweza kuupitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti,…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, muda wako umemalizika. Nilikuachia kidogo.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalize neno moja tu. Kuhusu uzazi wa mpango, nakubaliana na ushauri wa Kamati kwamba ni changamoto kubwa, Waheshimiwa Wabunge mtuunge mkono. Ni asilimia 32 tu ya wanawake wanaotumia uzazi wa mpango. Lengo letu ni kuhakikisha huduma hizi zinapatikana mitaani badala tu ya kwenye vituo vya afya na hospitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uzazi salama ni kipaumbele chetu. Nawathibitishia Waheshimiwa Wabunge, nikiwa Waziri mwanamke na mama wa watoto wawili, tutasaidiana kupunguza vifo vya akina mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ummy Mwalimu. Tunamkaribisha Mheshimiwa Nape Nnauye kwa muda wa dakika nne.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na ahsante kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kuishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kwa jinsi ambavyo wameandika ripoti yao vizuri na ushirikiano wanaotupa katika kufanya na kutimiza majukumu yetu. Niwahakikishie kwamba mapendekezo yao mazuri sana waliyoyatoa kwenye ripoti yao tutayafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na Mheshimiwa Kadutu kuwapongeza sana *Serengeti Boys* kwa mafanikio makubwa waliyoyapata na kuipa heshima nchi yetu kwa kufanikiwa kwenda kwenye fainali za Afrika kwa vijana chini ya umri wa miaka 17. Niwahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge kwamba hata kufika pale walipofika kuna mkono mkubwa sana wa Serikali. Wakati mwingine siyo kila jambo unalisema hadharani, lakini ni hakika kwamba mkono wa Serikali umesaidia wao kucheza na kufika pale walipofika, lakini pia

kusukuma rufaa yao mpaka wakapata kushinda na kwenda kwenye fainali za mashindano haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahakikishie Watanzania kwa pamoja, bila kujali tofauti zetu tuungane kwa pamoja, tuwatie moyo vijana hawa na kuwasaidia. Tunaamini watafanya vizuri kwenye mashindano haya na bila shaka tunaweza tukarudi na kombe. Wakifika nusu fainali, basi tuna uhakika wa kwenda kwenye Kombe la Dunia la Vijana chini ya miaka 17. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo mazuri ya Kamati na wameainisha humu changamoto ambazo zinaikabili sekta ya michezo, niseme tu moja ya eneo kubwa ambalo linatusumbua sana ni namna ya ku-*finance* michezo katika nchi yetu. Niahidi katika Bunge hili kwamba tutaleta hapa Bungeni mpango mahsusi wa ku-*finance* michezo katika nchi yetu na hili litakuwa jibu la tatizo hili la kuendelea kwa michezo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapitia Sera ya Michezo kama walivyoeleza katika taarifa yao na baada ya muda sera hii itakamilika, iko katika michakato ya mwisho. Ikikamilika, tutaleta sheria na kanuni zake hapa na bila shaka itasaidia sana katika ukuaji wa sekta ya michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja la mwisho ambalo nilipenda nilizungumzie ni suala la usikivu na utendaji kazi wa Shirika la Utangazaji la Taifa. Ni kweli kama ilivyooneshwa kwenye ripoti ya Kamati, Wilaya 81 za nchi yetu *TBC* haisikiki kabisa. Waheshimiwa Wabunge, tukumbuke wakati fulani *TBC* ilikuwa inasikika nchi nzima wakati tukitumia teknolojia ya zamani. Bahati mbaya wakati wa mabadiliko haya ya teknolojia mpya, vifaa vingi vile vya zamani sasa havifanyi kazi tena na uwekezaji ulikuwa haujafanyika wa kutosha na ndiyo maana ukweli ni huo kwamba nusu ya nchi yetu inasikika na nusu ya nchi yetu haisikiki. Sasa kwa Shirika la Utangazaji la Taifa kusikika nusu ya nchi, nadhani ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilihakikishie Bunge lako kwamba bajeti ijayo nadhani tutafanikiwa kuleta hapa mpango wa kupata fedha za kutosha wa ku-*finance TBC*. Uwekezaji mkubwa unahitajika ili kusaidia katika teknolojia, lakini pia kuboresha studio zao na vipindi vyao. Nina hakika Bunge hili likituunga mkono tutakapoleta mapendekezo hayo tutapata pesa za kutosha na tutaliondoa Shirika letu la Utangazaji pale lilipo na ndoto zetu kwamba liwe shirika bora kabisa katika nchi yetu. Inahitajika uwekezaji mkubwa, naamini Bunge litatuunga mkono wakati utakapofika na tutakapoleta hapa wakituunga mkono, tunaamini Watanzania watafurahia huduma nzuri na kazi nzuri ya Shirika la Utangazaji la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuunga mkono mapendekezo mengi yaliyoletwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge. Nakushukuru sana kwa nafasi uliyonipa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Nape Nnauye. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa January Makamba. Unazo dakika tatu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwa kuzipongeza Kamati zote mbili kwa kazi nzuri walizofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niongezee kwenye maelezo ya Naibu Waziri wa Afya kuhusu suala la viroba na vifungashio vya plastiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili liko chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais na kanuni tuliandika kwa sababu linapigwa marufuku kwa kanuni za chini ya Sheria ya Mazingira. Suala hili ni mtambuka, lina upande wa kodi, kwa maana ya Wizara ya Fedha, lina upande wa viwanda, Wizara ya Viwanda na Biashara, lina upande wa Wizara ya Afya kwa maana ya *TFDA* na Udhibiti wa Vyakula na Vinywaji, lakini pia upande wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunachofanya sasa ni Wizara zote kuandika karatasi ya pamoja ambayo itawezesha hatua tutakazochukua ziweze kutekelezwa kwa msukumo na mtazamo wa pamoja na kutapatikana *balance* kati ya haja ya kuhakikisha kwamba mapato yanaendelea kupatikana kwa nchi, lakini tunalinda afya za watu wetu na mazingira ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, suala hili linataka tafakuri ya kina ya pamoja ndani ya Serikali na ndiyo kinachofanyika na taarifa rasmi ya mwisho ya maamuzi hayo italetwa ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa January. Tunaendelea sasa na Mheshimiwa Jenista Mhagama na baadaye tutamalizia na Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi kwa haraka haraka lakini siyo kwa umuhimu, nianze kwa kuipongeza sana Kamati inayosimamia masuala

ya UKIMWI na masuala ya mapambano dhidi ya dawa za kulevya inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Ndugulile na Makamu Mwenyekiti Dkt. Tiisekwa na Wabunge wote Wajumbe wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hii kwa kweli imeanza kazi vizuri na ninaomba niseme kwamba inatushauri vizuri sana. Kwa hiyo, naomba niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati hiyo. Sitakuwa nimejitendea haki kama sitakumbuka mchango mkubwa uliotolewa na Mheshimiwa Dkt. Ndugulile na Mheshimiwa Ester Bulaya wakati wa kutungwa kwa Sheria Namba 5 ya mwaka 2015 ambayo imetupelekea katika azma ya Serikali ya kupambana na dawa za kulevya katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nichukue nafasi pia ya pekee kabisa kuwapongeza sana Wabunge wote ambao tulikuwa wote pamoja katika Bunge la Kumi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nakumbuka sheria hiyo ilikuwa ni sheria yangu ya kwanza nilipoteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, lakini Waheshimiwa Wabunge waliniunga mkono sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli sheria hii mpya ni sheria nzuri na imeweka adhabu za kutosha kabisa za kupambana na tatizo la dawa za kulevya katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa labda niseme yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la dawa za kulevya katika nchi yetu ya Tanzania lina historia. Historia ya ongezeko la tatizo hili ilianza toka miaka ya 1990 na miaka ya 1990 Serikali imekuwa ikihangaika sana kuona ni namna gani itaweka mifumo ya kisheria na taratibu za kupambana na dawa za kulevya katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1995 Serikali kupitia Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilitunga Sheria Namba 9 ya mwaka 1995 lakini sheria ile ilikuwa na kazi ya kuratibu tu masuala haya ya tatizo la dawa za kulevya nchini na ilionekana kwamba sheria ile haina nguvu yoyote. Watu wakikamatwa, sheria ilikuwa haiipi Tume ya Dawa za Kulevya nguvu ya kupekua, kupeleleza na kushitaki. Kwa hiyo, tulikuwa tunaona kulikuwa na upungufu mkubwa sana katika Sheria ya mwaka 1995. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Serikali ilianza kujionesha mwaka 2014. Mwaka 2014 tulifanya utafiti wa nguvu kazi katika nchi yetu ya Tanzania na tukagundua kwamba nguvu kazi ya vijana kwa miaka 14 mpaka 35 ni

asilimia 56. Hiyo asilimia 56 ya nguvu kazi ya vijana ndio hao ambao wanaathiriwa na madawa ya kulevya katika nchi yetu ya Tanzania. Kwa dhamira ya dhati, mwaka 2015 ndipo tukaamua kuja na Sheria Namba 5 ya mwaka 2015; lakini sheria hiyo sasa ikaweka nguvu nyingine ya ziada; hiyo sasa ikawa na ajenda ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme jambo hapa, mchakato sasa wa kuunda hii mamlaka ambayo itafanya kazi yake vizuri ambayo inategemewa na Watanzania wengi, mchakato huu umefika mahali pazuri sana. Mwaka 2015 Serikali ya Awamu ya Nne, kazi kubwa Serikali hiyo ilifanya ni kutunga sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge, jamani mapambano haya ya dawa za kulevya ni ya kwetu Watanzania wote, yasichague mtu yeyote. Na mimi kwa dhati ya moyo wangu, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, kila atakayeamua kupambana na jambo hili tuungane mkono pamoja kwani ni ajenda ya kitaifa inayotuhusu Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaoneshwa hapa ni kama vile Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli na Serikali yake hawana nia ya dhati ya jambo hili, hapana. Mheshimiwa dada yangu Mheshimiwa Halima, namheshimu, amesema hapa kitu ambacho siyo sahihi.

Waheshimiwa Wabunge, bajeti kwa ajili ya kutengeneza mamlaka hii mmeipitisha. Tumepitisha bajeti ya shilingi bilioni 2.3 kwa ajili ya kwenda kuunda mamlaka hii itakayopambana na dawa za kulevya nchini. Bajeti hiyo hatujaweka fedha ya maendeleo, kwa sababu unawapaje hawa watu fedha ya maendeleo? Unataka wakatekeleze nini… *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** ...badala ya kuwapa *OC* ya kwenda kufanya kazi…

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo bajeti, hiyo tumeitenga na tunategemea bajeti hiyo itaenda kufanya kazi…

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hunisikii au!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikuambie kwamba chini ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli tayari kanuni za sheria hizi tumeshazikamilisha na zipo tayari. Chini ya Serikali ya Dkt. John Pombe Magufuli, muundo wa mamlaka hii ya kupambana na dawa za kulevya iko tayari. Muundo umeshakamilika. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachosubiri ni uteuzi wa Kamishna ambaye ataongoza mamlaka hiyo.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unapewa taarifa huku.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jinsi…

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unapewa taarifa!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilinde muda wangu watu wana…

**MBUNGE FULANI:** Taarifa bwana, muda wako wa wapi?

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI,(SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamishna huyu…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee, naomba ukae. Tafadhali, naomba ukae.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Sasa kama…

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nieleweke, kuteua Kamishna ambaye atashughulika na jambo hili siyo jambo la lelemama. Ni lazima atafutwe mtu mwenye maadili anayeweza… *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Taarifa!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme. Narudia kusema, ni lazima atafutwe kiongozi anayeweza kuwa na maadili ya kutosha ya kupambana na tatizo hili… *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Taarifa!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jenista, naomba ukae kidogo tu.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee naomba utoe taarifa kwa haraka tena.

## T A A R I F A

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunajadili Taarifa ya Kamati, hatuzungumzii porojo anazozisema Mheshimiwa Waziri. Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI ukurasa wa saba na wa nane, naomba nirudie niseme hivi: "Hata hivyo kipindi cha mwaka 2015/2016 na 2016/2017 bajeti za Tume zilishuka hadi kufika shilingi sifuri kwa miradi ya maendeleo kwa mwaka 2016/2017." Bajeti za Tume zimefika sifuri na Tume hapa tunayoizungumza ni Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya kwa kipindi cha miaka mitano, tathimini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nimerejea taarifa ya Kamati, sasa yeye anajibu hii Taarifa ya Kamati, kama imedanganya *then* na mimi nitakuwa

nimedanganya. Sasa hizo *story* na vichagizo vingine vya hayo mambo mengine, mimi sijayazungumza, nimerejea taarifa ya Kamati. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Umeeleweka.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa asinirejee jina langu kwa kuiongezea maneno abayo mimi sijayasema. Mimi nimerejea taarifa ya Kamati. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Amekuelewa. Mheshimiwa Jenista…

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa nyingine.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jenista unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Taarifa nyingine ili azipokee kwa pamoja.

**MWENYEKITI:** Hapana, nimetoa ruhusa kwa taarifa moja tu. Naomba tafadhali sana Mheshimiwa Zitto naomba ukae.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Zinafanana.

**MWENYEKITI:** Tunachelewa, muda unakwenda kwa ajili ya taarifa ambazo hazileti faida kwa Taifa letu.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto naomba ukae. Mheshimiwa Jenista naomba uendelee.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu ulinde dakika zangu. Ninachokisema hapa sitaki kusema kwamba Mheshimiwa Halima Mdee haja-*quote* taarifa ya Kamati. Nilichokuwa nalieleza Bunge hili, sisi kama Serikali, wakati tunaelekea kuunda mamlaka mpya yenye nguvu ya kudhibiti, hatukuona haja ya kuweka fedha ya mradi wa maendeleo. Tunaipaje Tume fedha za maendeleo ambapo sisi tumeweka shilingi bilioni mbili kwa ajili ya *OC* ya kuratibu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachotaka kusema, taarifa ya Kamati hiyo anayoi-*quote* Mheshimiwa Halima, lakini mimi kama Waziri mwenye dhamana, najua Tume hii wakati inajibadilisha kwenda Mamlaka, tumeitengea shilingi bilioni 2.5 ili iweze kutengeneza Mamlaka na kufanya kazi. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti…

**MWENYEKITI:** Jamani siwezi kupokea taarifa kwa mujibu wa kanuni tunatakiwa tuendeshe kwa yale mambo muhimu na yenye msingi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri anazungumza mambo ya msingi, naomba tumsikilize. Kama hatukumsikiliza tutatoa taarifa chungu nzima. Mheshimiwa Jenista.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wabunge tuelewane. Narudia kusema, ninampongeza Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuonesha nia ya dhati… *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Lazima ujikombe kwa sababu usipojikomba unatumbuliwa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli alisema wakati anafungua Bunge hili, alionesha nia ya dhati ya kupambana na dawa za kulevya katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema ndiyo maana hii Sheria ya Namba 5 ya mwaka 2015, yale yote ambayo yanatakiwa yafanyike kwa mujibu wa sheria yameshatekelezwa yote. Bajeti kwa ajili ya mamlaka hii mpya itapangwa katika bajeti ya mwaka 2017/2018 na hiyo ndio nia ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi/Kelele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema mapambano dhidi ya dawa za kulevya ni ya Watanzania wote na sisi wote tuungane pamoja, tuhakikishe kwamba vita hii tunakwenda nayo pamoja. *(Makofi/Kelele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwenye tatizo la UKIMWI katika nchi yetu ya Tanzania. Tumejipanga. Tumegundua kwamba ufadhili wa fedha za

UKIMWI unazidi kwenda chini. Tumepitisha sheria mwaka 2016 ya kuanzisha Mfuko wa UKIMWI; na mfuko ule Serikali tumeutengengea shilingi bilioni 1.5 mpaka sasa. Naomba Waheshimiwa Wabunge mwamini Serikali ina nia ya dhati ya kuwakomboa Watanzania dhidi ya mapambano pia ya tatizo la UKIMWI katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dawa za kulevya hazikubaliki na tutaendelea kuratibu na kupambana na dawa hizi tukiongozwa na Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jenista. Tunamaliza na Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe. Karibu.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Tafdhali naomba ukae chini, miongozo baadaye. Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe…

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama mbele ya Bunge lako Tukufu kwa sauti ya huruma sana na kwa unyenyekevu mkubwa, ninategemea pia ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge mtanisikiliza vilevile kwa unyenyekevu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nazipongeza Kamati zote mbili kwa kazi nzuri. Nitachangia vitu vichache tu. Mheshimiwa Kabwe Zuberi Ruyagwa amesema kitu kizito sana leo hapa kwamba kunajengeka utamaduni mpya hapa nyumbani wa kwamba ukituhumiwa tu, wewe ujue tayari umehukumiwa. Hiyo wamesema; *once accused, you are condemned guilty*. Ni kitu kizito amekisema ambacho sikubaliani naye, lakini kwa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Susan Lyimo naye hakuwa mbali, asubuhi leo ameongelea hayo hayo akisema kuwa katika vita hii dhidi ya dawa za kulevya kuna Wakuu wa Mikoa wanataja tu majina ya watu, lakini kwa kweli alikuwa anamzungumzia Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam. Vilevile Mheshimiwa Lucy Owenya naye anaona kwa kweli kuitwa tu polisi ni kama kuhukumiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kulithibitishia Bunge lako Tukufu kuwa katika *operation* hii dhidi ya dawa za kulevya, hakuna mtu aliyekurupuka na

katika hili Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam ambaye ndio alianzisha hii *operation,* hajaenda nje kabisa ya sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ninukuu kifungu cha 10 cha *Drug Control and Enforcement Act* kinachoipa Serikali wajibu wa kuja na mikakati na hatua mbalimbali kupambana na tatizo hili la dawa za kulevya. Alichokifanya Mheshimiwa Paul Makonda - Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam ni kutekeleza tu sheria hii, naye ni sehemu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi/Kicheko/)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo kidogo hapa Bungeni, sijui tunawaonaje Wakuu wa Mikoa, pengine tunawaona hawana wajibu huo kisheria. Naomba tu jamani, sisi ndio tunaotunga sheria, tukumbushane. Ukienda kifungu cha 5 cha *Regional Administration Act,* kinatamka kwamba Mkuu wa Mkoa ndiye mwakilishi wa mhimili wa utendaji katika eneo lake *(The Regional Commissioner shall be the principal representative of the government within the area of his jurisdiction).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kulikuwepo neno moja aliliongelea Mheshimiwa Kabwe hapa, akatoa na mfano wa Kigoma kule kwamba kuna kachura kapo juu, pale chini unajua kuna mtu; hili hakuna la kuficha! Mkuu wa Mkoa anateuliwa na Rais wa nchi na hawezi kufanya vitu ambavyo havina baraka ya Rais wa nchi. Ukienda kifungu cha 6 cha *Regional Administration Act, it is clear,* inasema; *"The President may delegate any of his functions and duties under written law to any Regional Commissioner."*

*(Hapa kulikuwa na muingiliano wa sauti)*

**MHE. ZITTO Z. R. KABWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba guidance.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama tunaanza mambo ya kitoto haya ya kuzimiana *microphone,* nimepewa…

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tufanye heshima. Tuheshimiwane ndani ya Bunge, tuwe na lugha za staha, tufanye mambo kama watu wazima wa Bunge hili.

**MBUNGE FULANI:** Nani mtoto?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwakyembe, naomba tuendelee.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naeleza tu kwamba Mkuu wa Mkoa ana hayo mamlaka, lakini vile vile ukienda kifungu cha 7 kinamruhusu Mkuu wa Mkoa kuagiza mtu kutiwa ndani. Kasome tu, *Regional Administration Act,* kimepitishwa na Bunge hili hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kulikuwepo na hoja Mheshimiwa Halima Mdee; naomba nimhakikishie Mwanasheria Mdee kwamba sim-*quote out of context,* lakini aliongelea hapa kwamba vita dhidi ya dawa za kulevya inataka tuwe na pesa kwanza. Ametoa hata mfano wa Marekani, wametumia matrilioni ya pesa katika pesa hii. Angetaka leo na sisi tutumie matrilioni ya shilingi katika hii vita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu, Wamarekani wameshindwa kwa sababu walitanguliza pesa, siyo dhamira, ndiyo maana hii vita imeshindikana mpaka leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi hatujatanguliza pesa, tumetanguliza dhamira. Shida ya Bunge letu hili, tumejaa mgawanyiko kushindana shindana. Leo tungekuja na pesa, mngesema dhamira iko wapi? Tumekuja na dhamira; eeh, pesa iko wapi? Tuacheni tufanye tunavyoweza na tutafika tutakapofika. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuitwa na polisi sio kuhukumiwa. Unajua kuna tatizo hapa la *public perception* na *legal reasoning,* wanasheria mko wengi hapa, sio kwamba ukiitwa na polisi basi umefungwa, hapana, umeitwa pale kuisaidia Serikali kujua kiini cha tatizo na kuweza kujua tatizo lenyewe upana wake ukoje ili tuweze kumfikisha mtu anayehusika mahakamani.

Naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam kwa ujasiri, kwa uthubutu wa kujitoa muhanga kuonesha mfano kwamba tunaweza tukapambana na hili tatizo. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na kelele za leo ni kelele za mwanzo tu, tusubiri kesho, keshokutwa kama hii *operation* itaishia hapo mnapofikiria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nimalizie kitu kidogo kwa sababu imekuwa ni kelele kama ya shule ya msingi, naomba tu nimalizie kitu cha mwisho nisiendelee tena.

*(Hapa baadhi Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Hussein Bashe ameongea kitu kizuri sana hapa, kwamba tuna matatizo hapa mengine ya ushoga ambayo alianzisha Mheshimiwa Makonda tukamuachia mwenyewe, nataka kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge kwamba hatukumuachia na Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla ameligusia vizuri.

Naomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba suala lile tulilibeba na tumeendelea nalo kwa sababu tatizo hilo ni kubwa hatutaki kukurupuka nalo, ni kubwa na tutaliambia Taifa ndani ya mwezi huu tumechukua hatua gani. Kwa sababu tumekuja kubaini, kuna *NGOs* hapa nchini zinatumwa na nchi ambazo zinaamini kwamba mahusiano ya jinsia moja ni haki za binadamu na hizo nchi zinazoamini hivyo zinafadhili baadhi ya vyama vya siasa hapa.

Kwa hiyo, ninachosema… *(Makofi)*

*(Hapa baadhi Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tunachukua muda tuje na ushahidi wa kutosha ili tuchukue hatua. Wanasema aisifuye mvua imemnyea, unapiga kelele nini kama huusiki!

**MHE. JACQUILINE N. MSONGOZI:** Kusagana.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani, nimalizie tu kwa kusema naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Tunaendelea, sasa nawaita Wenyeviti, tunaanza na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya UKIMWI…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

**MWENYEKITI:** …ili aweze kuja kuhitimisha hoja zao.

**MBUNGE FULANI:** Kubali mwongozo!

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo!

**MWENYEKITI:** Nimeshamuita Mwenyekiti wa Kamati Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, naomba ukae chini, miongozo baadaye.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, napenda kuwashukuru sana wachangiaji wote ambao wamechangia hoja hii, walikuwa wengi sana waliochangia kwa maandishi, lakini vilevile ambao walichangia kwa kuongea. Lakini kwa nafasi ya kipekee nimshukuru sana Waziri wa Sera na Bunge, Mheshimiwa Jenista Mhagama ambaye alishiriki vikao vyetu vyote na kwa ukamilifu kuanzia asubuhi mpaka muda ambao tulikuwa tunamaliza, namshukuru sana na kumpongeza sana.

Vilevile niwapongeze Wajumbe wa Kamati mpya ya UKIMWI kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wameifanya kuhakikisha kwamba taarifa hii inakamilika ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze tu kwa kusema kwamba vita dhidi ya masuala ya UKIMWI na vita dhidi ya dawa za kulevya inahitaji dhamira ya dhati. Bila dhamira ya dhati tutakuwa tunapiga porojo na tutakuwa tunaongea lakini vita hii hatutaiweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisisitize katika maeneo machache na la kwanza nisisitize katika suala la sera. Katika Bunge la Kumi tulifanya mapitio ya Sera ya UKIMWI na Sheria ya UKIMWI lakini vilevile Sheria ya Tume ya Dawa za Kulevya ambazo zilielezea kuhusiana na muundo na mamlaka ambazo sheria hizi zimepewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nianze kwa kusema, kwa kweli Sera ya UKIMWI nayo ni ya muda mrefu, ni ya mwaka 2001 sasa hivi ni mwaka wa 16, tunahitaji tuipitie upya sera ile ili iweze kuendana na mazingira ya sasa. Vivyo hivyo, kuhusiana na Sera ya Dawa za Kulevya ni ya mwaka 2004, mbinu zimebadilika, mahitaji yamebadilika na aina ya dawa za kulevya yamebadilika, tunahitaji sera mpya ambayo itaendana na mazingira ambayo tunayo sasa. Sheria tulizozipitisha zimeelekeza kuhusu muundo mpya, tuiombe Serikali, ili

kama tuna dhamira ya dhati katika vita hii, basi miundo hii ya hizi taasisi ambazo zimeundwa upya kisheria basi ziweze kufanya kazi ikiwa ni pamoja na kupewa watumishi ambao wanahitajika kwa ajili ya kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo nataka nigusie ni suala la fedha, taasisi zote mbili. Tumeanzisha Mfuko wa Masuala ya UKIMWI, ni jambo jema, Serikali iliahidi shilingi bilioni tano imetoa shilingi bilioni 1.5, mahitaji ya masuala ya UKIMWI kwa mwaka ni takribani shilingi trilioni 1.3, hivi sasa fedha ambazo zinapatikana katika masuala ya UKIMWI ni shilingi bilioni 800, tuna *gap* ya takribani shilingi bilioni 500, tunahitaji tuongeze nguvu zaidi. Fedha za wafadhili zinapungua, ni lazima sasa tujielekeze katika vyanzo vya ndani. Niiombe Serikali na Waheshimiwa Wabunge wote kwa pamoja, ni muda muafaka sasa kuungana, tuhakikishe katika bajeti inayokuja Serikali ije, au sisi kama Wabunge tupendekeze vyanzo mahsusi, kama ilivyokuwa katika Mfuko wa Barabara, kama Mfuko wa Mawasiliano na Mfuko wa Elimu, sasa tuwe na *source* maalum kwa ajili ya kuwezesha shughuli za UKIMWI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono kauli ya Mheshimiwa Rais leo asubuhi. Katika Kamati yetu na kama mtasoma katika mapendekezo yetu, tulikuwa tunataka kauli za viongozi wa Kitaifa kukiri kwamba suala la dawa za kulevya ni janga, na leo asubuhi Mheshimiwa Rais ameitamka hiyo kauli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, na mimi niwaombe viongozi wengine, tuendelee kuibeba kauli ya Mheshimiwa Rais na sisi twende tukayasemee. Ndugu zangu, UKIMWI ulipoanza mwaka 1979 tulisema UKIMWI ni tatizo la sehemu fulani katika Tanzania yetu, hivi tuvyoongea hakuna familia ambayo haijaguswa. Na ninyi mtakuwa mashahidi, katika vijiji vyetu, vitongoji vyetu katika Wilaya zetu na Majimbo yetu, tuna wagonjwa ama tuna watu ambao wanatumia dawa za kulevya na waathirika wa dawa za kulevya. Tunapokwenda ni kubaya zaidi, tunahitaji tuweke nguvu sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yetu na sisi tungependa kusisitiza; tuna Kamati zetu katika halmashauri ambazo zinasimamia masuala ya UKIMWI na sisi kama Wabunge ni wajumbe wa zile Kamati za UKIMWI. Tunapendekeza na tungewaomba Serikali na hili mliwekee msisitizo, zile Kamati zipewe majukumu ya ziada ya kuwa ni Kamati za Halmashauri kusimamia masuala ya UKIMWI na dawa za kulevya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Kamati tunaunga mkono suala la viroba linaharibu vijana wetu, linaharibu kizazi chetu, linaharibu Taifa letu. Tanzania

tunapoelekea sasa hivi tunakuwa ni Taifa la watu walevi, na bahati mbaya sana tumezi-*package* hizi pombe kwa kiwango cha chini sana. Leo nilikuwa naongea na Mheshimiwa Mbunge mmoja anasema kule Kanda ya Magharibi pombe hizi zinauzwa shilingi 300, mpaka watoto wadogo ambao wanapewa nauli ya kwenda shuleni wana uwezo kununua ile pombe. Sasa niiombe Serikali, kwa kweli kama ni mapato yote yanapatikana kwa njia hii haramu haiwezekani, tupige vita viroba na sisi kama Wabunge tutawaunga mkono ili tuondokane na hili janga tuweze kujenga kizazi imara kwa miaka ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi wamegusia suala la tohara; ni kweli katika suala la kitaalam ni *intervention* ambayo imeonekana inaweza ikasaidia katika kupunguza ugonjwa ya UKIMWI, ni kitu ambacho kimekuwa *proven*. Lakini hatuwezi tukalazimisha mtu akafanye tohara, muhimu tuwekeze katika elimu na watu waelewe umuhimu na faida ambazo wanaweza kuzipata kutokana na jambo hili, naamini hilo tukiweza itatusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tuna changamoto kubwa sana; tumetoa elimu, na tuliwekeza sana katika elimu ya UKIMWI lakini inaonekana bado tuna changamoto kubwa. Maambukizi kwa vijana kati ya miaka 15 mpaka 19 ni makubwa sana, kwa mujibu wa takwimu ambazo zimetoka hivi karibuni za *Tanzania Demographic Health Survey* zinaonesha…

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MWENYEKITI:** Hivi utaombaje taarifa huku mtu anatoa taarifa mwenyewe jamani! Hebu naombeni tufuate kanuni, tafadhali kaeni mtulie ili Mwenyekiti aendelee.

**MBUNGE FULANI:** Anapotosha umma!

**MWENYEKITI:** Mwenyekiti, hebu naomba uendelee umalize, taarifa na miongozo baadaye.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniruhusu kuendelea. Nilikuwa nasema kwamba, katika rika la vijana wa miaka 15 mpaka 16, hususan kwa wasichana, asilimia 27 wameshapata ujauzito. Sasa tunahitaji kwa kweli tuwekeze nguvu kubwa sana katika rika hili kupunguza mimba za utotoni, lakini vilevile katika kupunguza maambukizi. Na hili suala la elimu naomba sana, tunahitaji sisi wenyewe Waheshimiwa Wabunge tujielekeze huko, lakini vilevile katika jamii nzima kuhakikisha kwamba jamii na sisi kama

wadau tunashiriki katika kuwajenga vizuri kimaadili watoto wetu, lakini vilevile kuwapa elimu jinsi ya kujikinga na maambukizi ya UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kuligusia ni hususan katika upande wa dawa za kulevya, kuna *intervention* ama mkakati ambao unasaidia kupunguza athari kwa wagonjwa ambao wanatumia dawa za kulevya. Niseme jambo moja ambalo limeongelewa hapa, watumiaji wa dawa za kulevya sio vichaa, na watumiaji wa dawa za kulevya sio wahalifu na hawapaswi kuwekwa jela, ni watu ambao wanahitaji kupata msaada wa tiba na magereza sio sehemu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuwatia moyo, tumeipiga vita na baadhi nimesikia ni maneno yapo ya kupiga vita *sober houses,* hatuhitaji kupiga vita *sober houses,* tunahitaji kuziboresha kuwasaidia na kuzisimamia na kuziratibu. Lakini vilevile Serikali iongeze nguvu kuhakikisha kwamba tuna *rehabilitation center* yetu ambayo tumekuwa tunaijenga pale Dodoma na tuliliongea hilo, Serikali iweke msukumo tuimalize ile pale. Watumiaji wa dawa za kulevya wasiwekwe Isanga ili sasa wawekwe kule wakapate tiba, wapate msaada wanaohitaji ili warudi katika jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwashauri Waheshimiwa Wabunge maana yake na mimi nasoma kwenye mitandano na magazeti, kutoka katika dawa za kulevya sio shughuli ndogo. Ni sawasawa na huyu ambaye anatumia sigara, kuna mwingine anaweza akaacha papo kwa papo, lakini kuna wengine wanaweza wakachukua hata miaka mitano; anaingia, anatoka, anaingia anatoka. Wanahitaji msaada mkubwa sana badala ya kuwanyanyapaa tuwasaidie waweze kurudi kwenye mstari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie na niokoe muda wako, nishukuru, mapendekezo yetu tumeyatoa na tumeyatoa kwa kirefu sana. Niombe sana Serikali ijaribu kuzingatia ili tutakapokutana tena katika Kamati basi itupe mrejesho wametekeleza kwa kiasi gani na wapi wamekwama na kiasi gani wamekwama ili na sisi kama Kamati ya Bunge ambayo inasimamia suala hili tuweze kutoa na kushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, nakushukuru sana kwa kunipa fursa. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo!

**MWENYEKITI:** Hitimisha hoja yako, Mwenyekiti hujahitimisha hoja yako, toa hoja yako!

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UKIMWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nitoe hoja kwamba yale mapendekezo ambayo tumetoa kupitia katika taarifa yetu yaweze kupokelewa na kufanyiwa kazi na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya UKIMWI.

Waheshimiwa Wabunge, sio utaratibu mzuri, Mwenyekiti anahitimisha hoja yake na wengine wanaanza utaratibu, tungemsubiri amalize utaratibu utakuja baadaye, kwa nini tunaingilia kwenye mambo kama haya?

Waheshimiwa Wabunge,…

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika!

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa naomba niweze kulihoji Bunge.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2016 hadi Januari 2017 ilipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Nafurahi na ninawapongeza sana Kamati ya Kudumu ya UKIMWI kwa kuwa taarifa yao, pamoja na mapendekezo yake na maoni yamepitishwa kuwa ni Maazimio ya Bunge.Tunaendelea na Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ili aweze kuja kuhitimisha hoja yake. *(Makofi)*

**MHE. PETER J. SERUKAMBA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchangia hoja yetu ya Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Wabunge waliochangia kwa kusema humu Bungeni Wabunge 32 na Wabunge waliochangia kwa maandishi ni Wabunge 20. Kwa kweli wote waliochangia, waliochangia humu ndani wamekubali mapendekezo yetu na wote ukiangalia wameeleza, walikuwa wanachangia kule ambako sisi tumeweka haya mapendekezo kama Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo ambayo ningependa kulitambulisha Bunge lako, ni muhimu sana tulifahamu mwanzo kabisa. La kwanza, Waheshimiwa Wabunge, Tanzania sensa ya mwaka 2012 ilisema kama Taifa tunakuwa kwa 2.7 *percent,* sasa maana yake tunaongeza Watanzania wenzetu karibia milioni mbili kwenye *population* yetu. Unaposema hivyo maana yake gharama za afya lazima ziongezeke, lazima gharama za *education* ziongezeke, sasa hii ndiyo changamoto tuliyonayo na changamoto yetu hii kubwa ni ya kifedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo Wabunge wengi sana wamesema na wote waliochangia humu walikuwa wanaongelea matatizo yaliyopo kwenye zahanati, kwenye vituo vya afya, kwenye hospitali za wilaya, matatizo yalipo kwenye shule za msingi, yaliyopo kwenye shule za sekondari. Moja ya mapendekezo yetu tuliyotoa kama Kamati na ninaomba Waheshimiwa Wabunge tuitafakari upya, tuangalie mfumo wetu wa *D by D. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wote waliosema, zaidi ya asilimia 80 tulikuwa tunaongea mambo ya TAMISEMI, hatukuongelea sana mambo ya Waziri wa Afya, mambo mengi ya Waziri wa Elimu. Lakini kwenye Kamati yetu wanaokuja mbele ya Kamati yetu ni Waziri wa Afya; Waziri wa Elimu na Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, lakini wanaoshughulika na utendaji wa kila siku wako TAMISEMI. Wanafunzi wakifeli sana tunasema Waziri wa Elimu hatoshi, lakini Waziri wa Elimu anaishia kwenye sera; walimu wanafundishaje, wanaajiriwaje, *whether* kuna madarasa, *whether* kuna chaki, hazipo, yeye Waziri wa Elimu hajui. Vituo vya afya vinasimamiwa na Halmashauri zetu, kukitokea leo ugonjwa mkubwa watu wakafa au madaktari, tutahangaika na Waziri wa Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, kwa nini nasema hili, nataka kama Bunge tutafakari upya mfumo wetu wa kutoa elimu na afya nchini. Ni nia ya Serikali kuhakikisha kila kituo cha afya kina daktari, kina *theatre*

ili tuweze kupunguza vifo vya akina mama na watoto. Lakini anayewaajiri hao ni nani, yuko TAMISEMI. Pendekezo letu linasema na ninaomba Waheshimiwa Wabunge mtuunge mkono kwamba umefika wakati sasa watakapokuja mbele ya Kamati, Wizara ya Afya aje na mtu wa TAMISEMI, kama ni Wizara ya Elimu aje na mtu wa TAMISEMI ili matatizo yale tuwe tuna watu wawili ambao mmoja anashughulika nayo kisera na mwingine anashughulika nayo kwenye utekelezaji. Mimi hili naliona ni tatizo ambalo lazima tulipatie majawabu na wanaoweza kutoa majawabu hayo ni sisi Waheshimiwa Wabunge, naombeni tutekeleze wajibu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hilo ambalo mimi niliona ni la kijumla zaidi, na mimi kwangu hili ndiyo tatizo ninaloliona zaidi, nilikuwa namsikiliza dada yangu Mheshimiwa Jacqueline, anaongea mambo ya Tunduru, lakini yote anaongelea kituo chake cha zahanati, anaongelea kituo chake cha afya, anaongelea hospitali yake ya Wilaya, lakini kwa kweli aliyekuwa anamwambia sio kwenye Kamati yetu, alikuwa anamwambia mtu wa TAMISEMI, na watu wengi ambao wameongea humu ndani wameongea mambo yanayotokea kwenye Wilaya zao. Kwa hiyo ni muhimu sasa tuuangalie mfumo wetu upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ya mfumo, nilitaka niongee suala la ufaulu kwenye shule za sekondari kwa sababu sisi huko tumelisema ili tuone tunaendaje kwenye suala la ufaulu. Nikisema suala la ufaulu nitaomba niunganishe na shule za binafsi na za umma, na katika mapendekezo yetu tumesema kuhusu shule za binafsi na za umma.

Waheshimiwa Wabunge, kwa wale ambao wamefuatilia matokeo ya *form four* haya yametoka juzi; Ukihesabu shule ya kwanza mpaka ya 200, shule za umma ni shule 17 tu. Ukichukua shule ya kwanza mpaka ya 100, shule za umma ni shule saba. Hili ni tatizo lazima tutafute ufumbuzi. Kwa hiyo, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge na hili linatokea na mimi ninasema ni muhimu sana sasa Wizara ya Elimu, shule hizi za binafsi pamoja na kwamba wanafanya biashara lakini wanatusaidia Watanzania.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo jukumu kama Bunge ya tuhakikishe zinatoa elimu bora. Waziri amesimama hapa anasema; shule ya Feza haina wanafunzi wengi, akailinganisha na shule ya Kibaha yenye wanafunzi wengi, ukilinganisha hivyo *yes,* lakini tumekuwa na seminari zina wanafunzi 40 zinaongoza miaka yote. Hoja yetu hapa, naombeni kama Bunge tuhakikishe tunatenga fedha nyingi ili shule za umma ziwe na fedha waweze kusimamia ili tuweze kupata ubora kwenye shule zetu za sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwahiyo niwaombe Watu wa Wizara ya Elimu kwenye moja ya pendekezo letu, tunaomba Wizara ya Elimu wajikite kwenye kuhakikisha tunapata ubora kwenye Shule zetu za umma. Na mimi hapa Waheshimiwa Wabunge mnikubalie na Kamati yangu, nimpongeze sana Rais Magufuli kwa kuamua kuleta elimu bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameleta elimu bure maana yake nikusaidia watoto wa maskini, wale wasio na uwezo. Sasa niwaombe watu wa Wizara ya Elimu tuhakikishe tunaboresha hizo sekondari zetu. Ikitokea sasa mzazi ameamua kuacha shule ya bure ameenda shule ya kulipia hilo ni tatizo lake. Haiwezekani sisi tuanze sasa kusema, shule za kulipia tuwapangie *school fees,* hapana. Sisi ndiyo maana kama Serikali nadhani mliangalia busara ya hali ya maisha ya watu mmesema shule zetu ni za bure. Hapa kuna mzazi ameamua kuacha shule ya bure ameamua kupeleka mtoto kwenye shule ya kulipia tumuache alipe anavyoweza kwasababu ni maamuzi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka niongelee suala la afya. Wizara ya Afya Wabunge wengi sana wameongelea suala la dawa. Waheshimiwa Wabunge kwanza niipongeze Serikali na sisi Kamati tumeipongeza sana. Ukiangalia bajeti ya mwaka huu iliyowekwa kwa ajili ya dawa, ndugu zangu tukubaliane kama Bunge tuwapongeze Serikali bajeti ni kubwa sana. *Challenge* ambayo nawapa watu wa Wizara ya Afya na Wizara ya Fedha, Wizara ya Fedha, fedha mnajua mtawapa na tunapeleka shilingi bilioni 20 kila mwezi kwa sababu dawa lazima kuna *process* ya kuyanunua, naiomba Serikali hasa Waziri wa Fedha, tuna mifuko yetu ya jamii tunapoanza mwaka tuiombe iipe pesa kule *MSD* wanunue dawa, lakini kila mwezi wanapoleta *disbursement* yao iende kurudisha hela kwenye Mifuko ya Jamii maana yake ni nini? Tutakuwa tumetatua tatizo la uwepo wa dawa ili ziende kwa wakati na kwa jinsi hiyo tutaonekana tumefanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hapo tunarudi kwenye dawa ni pale pale sasa TAMISEMI kuna dawa nyingine wananunua wenyewe Waziri wa Afya hajui kwahiyo yeye atakapo *report* ata-*report* hali ya dawa ambayo yeye ni *custodian* wake lakini kule TAMISEMI wanaweza wakanunua bila kumwambia Waziri wa Afya, kwa hiyo, cha msingi hii mifumo tuiunganishe ili tuweze kujua hali halisi ya dawa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifaa tiba na niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge, najua hili Serikali linakigugumizi nalo sana, lakini niwaombe sana Serikali dunia ya leo hatuwezi kununua vifaa vyote kwenye hospitali zote,

hatuwezi. Ziko taasisi kubwa duniani watakuja hapa, wataleta vifaa tiba, watafunga kwenye hospitali zote, wataviendesha lakini sisi tusimamie wasitoze bei kubwa. Teknolojia ikibadilika watabadilisha wao. Lakini sisi tukisema lazima tununue safari yetu ya kwenda kila Mkoa tutatumia miaka mingi sana kwa sababu vifaa hivi ni bei ghali sana. Niwaombe Serikali imefika wakati twende kwenye *PPP* kwa ajili ya kupata hizi mashine kubwa na ambazo *advantage* zake ni tatu; moja ni unahakika utapata *the latest technology;* pili, teknolojia ikipitwa na wakati watabadilisha na tatu, watu wetu watapata huduma bora zaidi kwa sababu watu hawa watakuja na watu wa kuviendesha vyombo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hili ni suala la Serikali naomba muende mkalisimamie ili tuone namna ambavyo tunaweza tukafanikiwa katika mambo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo tumelitolea kama Kamati ni suala la Bima ya Afya. Bima ya Afya ni jambo jema sana lakini inaumiza sisi Wabunge una kadi ya Bima ya Afya eti hapa Tanzania tu kuna hospitali hawapokei Bima ya Afya, haiwezekani.

Mimi ni matarajio yangu Serikali sasa muende mkaliangalie angalau tunapokwenda kwenye *universal coverage,* lakini hata hii iliyopo ya kwanza iwe na maana kwa maana kwamba popote nitakapoenda hawataniambia kadi hii siipokei. Kama suala ni fedha muongeze ili wanaochangia wachangie fedha nyingi, lakini waweze kupata huduma bora zaidi na muanze kufikiria suala la kwenda mpaka huko kwa Afrika ya Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo Waheshimiwa Wabunge mmelichangia kwa nguvu zote ni suala la mikopo wa elimu ya juu. Waheshimiwa Wabunge sisi Kama Kamati tumesema kuhusu namna bora ya kuangalia kuhusu suala la mikopo ya elimu ya juu. Moja ya jambo ambalo tumesema lakini hakuna Mbunge ambaye alili-*pick up,* lakini mimi naona kwetu ni muhimu sana; suala la kuanzisha *scholarship program.*

Waheshimiwa Wabunge, nchi zote wanaotuzunguka kuna *scholarship program,* ikiwezekana tuiite *Magufuli Scholarship Program* ili wale watoto ambao wamefaulu sana *form six* awe mtoto wa tajiri, awe mtoto wa maskini lakini ni mtoto ambaye ana kipaji, amefaulu sana kwenye yale maeneo ya vipaumbele watoto hawa wapewe *scholarship. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, itasaidia kuonyesha kwamba hatujawabagua. Kwa hiyo wale watoto ambao wamepata *point* tatu, mtoto amepata *point* nne kwenye *PCM* hata kama ni mtoto wa nani ni muhimu sana Serikali iangalie uwezo wa kuanzisha *scholarship program. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa suala la vigezo; naomba sana watu wa Wizara ya Elimu, vigezo vya mikopo visibadilishwe badilishwe. Maneno mengine yanaletwa kwa sababu kila mwaka kuna vigezo vyake. Ni vizuri vigezo viwe vinajulikana, vikishajulikana ni rahisi lakini ukishaanzisha na *scholarship program* itasaidia sana kwa wale watoto ambao wamefanya vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu madai ya walimu; tumesema hapa ndani, tunaomba sana Wizara ya Elimu, Wizara ya TAMISEMI na hili naomba Waziri Mkuu wewe upo hapa ikiwezekana Waziri Mkuu watu hawa wawili wakae, vyombo hivi viwili ama vitatu; Chama cha Walimu, TAMISEMI pamoja na Wizara ya Elimu tukae tulijadili suala la madai ya walimu ili tujue madai ya walimu kiukweli ni kiasi gani, yahakikiwe, tusiwe na *figure* mbili mbili na baadaye sasa Serikali kadri itakavyokuwa na uwezo iweze kuwalipa hao walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo mambo mengi ambayo Waheshimiwa Wabunge kwa suala la Wizara ya Afya na Elimu wameyasema sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengine ni suala la ugonjwa wa saratani ambalo kwa kweli wengi wamelisema, ndugu zangu tukubaliane ugonjwa huu unakuja kwa kasi sana. Tumeweka kwenye pendekezo letu, tuombe sasa Serikali ianze kuwekeza fedha nyingi kwa ajili ya kutatua tatizo hili. Ni ugonjwa mkubwa, ugonjwa unaotumia fedha nyingi lakini hatuna *choice* lazima tuhangaike kuwasaidia Watanzania hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TBC*; Waheshimiwa Wabunge wamesema kwa kweli chombo chetu cha *TBC* ndugu zangu Wabunge naomba mniunge mkono kwenye bajeti ijayo tuhakikishe wanapata fedha za kutosha ili angalau *TBC* waweze kusikika kwenye Wilaya zote Tanzania, redio yetu ya Taifa iweze kusikika kwenye Wilaya zote za Tanzania maana kupata habari ni jambo muhimu sana kama Taifa. Naombeni tuungane mkono ili tuweze kupata bajeti ili waweze kufanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo Waheshimiwa Wabunge wamelisemea ambalo ni kupongeza kuhusu Muswada wa Habari lakini kikubwa zaidi, Mheshimiwa Devotha Minja anasema suala la diploma katika uandishi wa

habari kwamba sasa kuweka kigezo cha uandishi wa habari lazima awe na elimu kwanza ya diploma Mheshimiwa Devotha anasema ni jambo kubwa hili na ni jambo jema anaamini safari yetu ya kuleta weledi kwenye uandishi wa habari Tanzania tunaanza kuelekea huko. Tunaipongeza Serikali, tunaomba tutekeleze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni suala la michezo; Mheshimiwa Kadutu anasema, ili tuweze na sisi kushangilia kwenye Michezo hatuna *shortcut* lazima tuwekeze. Tuwekeze kuanzia *kindergarten* mpaka watoto wanapopanda huku juu; na ili tuweze kupata mafanikio hayo ambayo tunayataka lazima tuwekeze na kwa kweli ndugu zangu michezo ni ajira. Tukifanikiwa kama nchi na sisi tukafika wakati ambapo tutakuwa tunatoa Watanzania wasiopungua hata wanne, watano kwenda kucheza Kimataifa maana yake tutakuwa tumesaidia sana kwa vijana wetu na fedha zile zitakuja kwenye uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni suala la mfumo wa Elimu. Waheshimiwa Wabunge wamelisema sana na sisi kwenye pendekezo letu tumesema tunaomba sasa Serikali iende ikakae, ikaungalie mfumo wetu wa elimu ili wautatue tutakapokuja kukutana baadaye watuambie wamefanya nini, kwa sababau matatizo haya tusipoyaangalia kwa upana, hatuwezi kuyatatua vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge naomba sasa niweze kutoa hoja ili Bunge lako tukufu liweze kupitisha mapendekezo yetu yote ya Kamati, naomba kutoa hoja Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono lakini kabla bado sijalihoja Bunge namkaribisha Mheshimiwa Susan Lyimo ili aweze kuleta mapendekezo yake katika hoja hiyo ya Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ni wazi kwamba suala la mfumo wa elimu ni suala tete na nashukuru kwamba Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii amelizungumza kama ambavyo linavyopatikana kwenye aya ya 3.1.6(m). Kamati ilikuwa inashauri wataalam wa elimu wafanye tathmini kuhusu mfumo wa elimu uliopo kuanzia elimu ya msingi, sekondari hadi vyuo vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeomba niboreshe pendekezo hilo kwa kusema kwamba Kamati iishauri Serikali kuunda Tume ya Kitaalam ili ipitie kwa

kina mfumo wetu wa elimu na kuja na mfumo ambao utaboresha kiwango cha elimu nchini ili kuendana na kasi ya ukuaji wa uchumi na teknolojia duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeleta pendekezo hili kwa sababu ni wazi kwamba mfumo wetu wa elimu umekuwa mbovu sana na ukiangalia nitaanzia kuanzia shule za msingi kama ambavyo wamesema Kamati, ukiangalia watoto wanamaliza darasa la saba takribani 800,000 lakini wanaoenda sekondari ni takribani nusu yake; lakini wale 400,000 hatujui walipo.

Lakini vilevile unapokuja kwenye sekondari wanaenda wanafunzi 300,000 mpaka karibu 400,000 lakini wanaomaliza *form four* unakuta wanaofaulu kwenda *form five* ni takribani 100,000, hatujui ile 300,000 inakwenda wapi. Hivyo hivyo ukienda kwenye *level* nyingine vyuo vikuu, tunatafiti zinazoonyesha kwamba asilimia 40 tu ya vijana wetu wanao-*graduate* wanaweza kuajiriwa na kubwa zaidi ni kwamba kuna tatizo kubwa sana la upungufu wa wahadhiri kiasi kwamba ni asilimia labda 35 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naamini kwamba, pamoja na kwamba Wizara ya Elimu ina Wataalam wengi sana miaka yote hata kwenye Kamati wanakuja maprofesa na madaktari kibao lakini bado hawajaweza kaungalia mfumo kwa hiyo nikadhani tukiwa na tume, tume ikaundwa ya kitaalam, inaweza ikapitia huu mfumo kuanzia msingi mpaka elimu ya juu halafu waulete tuone huo mfumo umekaaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwahiyo hiyo ndiyo ilikuwa pandekezo langu kwa sababu naona kwamba ikikaa kama ilivyo, bado hoja ya msingi ya kupata mfumo mzuri yaani tupate hiyo tume sasa ya kitaalam ambayo ita-*pick* wataalam kutoka sehemu mbalimbali waweze kuangalia, wachambue kwa kina waone tatizo liko wapi ili nchi yetu sasa wanafunzi wanapomalzia eneo lolote lile wawe na ujuzi unaostahili, lakini vilevile tuweze kuaendana sambamba na teknolojia inayokuwa sana lakini kubwa zaidi uchumi wa dunia ambapo Tanzania mimi kwa mawazo yangu na ninavyoona kiuhalisia tuko nyuma sana kwahiyo nilikuwa naomba pendekezo langu hili likubaliwe ili basi Tanzania ambayo itakuwa na elimu iliyoboreka iweze kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru sana na naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nitachukua mtu mmoja huku na mmoja huku. Mheshimiwa Amina Mollel na Mheshimiwa Gekul. Tunaanza na Mheshimiwa Mollel.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika hoja hii iliyotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa suala zima la elimu kuna changamoto nyingi katika elimu yetu na mimi tu naomba niseme kwamba nakubaliana na mapendekezo haya ili tuone ni kwa jinsi gani basi tunaweza kuboresha elimu, kwa sababu changamoto zilizopo katika elimu ni suala muhimu na vilevile hapa naangalia pia hata katika kundi zima na hasa kundi lenye mahitaji maalum changamoto ni nyingi na ndiyo maana nimelazimika kusimama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia katika mahitaji haya ya kundi hili maalum la watu wenye ulemavu changamoto ni nyingi. Tukienda katika suala zima la miundombinu na ndiyo maana hata katika vifaa tiba bado tatizo ni kubwa sana, kwa hiyo, nakubaliana na hii tuone ni kwa jinsi gani hasa tunapozungumzia hata walimu, tatizo kubwa vifaa katika mfumo mzima wa elimu hasa hawa watu hawa wenye ulemavu. Kwa hiyo nakubaliana na hoja hii ili tuangalie kwamba ni kwa jinsi gani basi elimu yetu na hasa suala zima la teknolojia tutakavyoweza kusonga mbele, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gekul. Amemuachia Mheshimiwa Mwalimu?

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Mwalimu.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Lazima tufike mahali tukubali kwamba Taifa lilipofikia upande wa elimu lime-*stuck,* hapa tumeshasimama sasa gari lilipofika ni ku-*overhaul* siyo kuweka *oil* wala kufanya nini, ni kushusha injini yote ili elimu iweze kwenda. Na hapa tulipofikia tukiendelea kufanya mchezo tutapata makubwa. Ufumbuzi wa tatizo hili ni Tume, haya mengine ni kubabaisha babaisha tu, wanafunzi wanafeli, tunadhani ufumbuzi ni kufukuza wakuu wa shule au walimu wakuu, tutafukuza wote walimu wakuu halafu tutarudi kurudisha wale wa kwanza waliowahi kufukuzwa mwanzoni baada ya kusahau kama tuliwafukuza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hoja ya Mheshimiwa Susan ndiyo inaweza ikatutoa hapa tulipo na tusiogope kuunda tume, nchi za wenzetu zimefanya haya, Marekani waliwahi kufanya waka-*come out with solution* tena *solution* inayosema kwamba *a nation at risk.* Sisi hata kabla hatujafanya, hii

Tume haijaundwa *we are at risk* upande wa elimu. Kwa hiyo, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Susan kwa nguvu zangu zote, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Upande wa Serikali. Mheshimiwa Profesa Ndalichako.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba Serikali inaunga mkono mapendekezo ya Kamati ambayo Kamati ilikuwa inashauri wataalam wa elimu wafanye tathmini ya mfumo wa elimu uliopo kuanzia elimu ya msingi hadi vyuo vikuu nakuja na mfumo ambao umeboreshwa kiwango cha elimu nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaunga mkono mapendekezo ya Kamati na kama nilivyosema katika majumuisho yangu Serikali imepokea ushauri huu na itaufanyia kazi kwa sababu lengo hapa ni kuangalia mfumo wa elimu ambao utakuwa umeboreshwa, kwa hiyo, sioni tatizo na mapendekezo ya Kamati naomba Bunge lako liliridhie mapendekezo ya Kamati yabaki kama yalivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Kamati. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA-MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja hii. Waheshimiwa Wabunge, nchi hii tumekuwa na tume nyingi sana hasa katika elimu kuna tume mpaka ya Makwetta kwa wale ambao wanakumbuka vizuri sana. Juzi tulikuwa na tume, tume zimekuwa nyingi sana, na sisi kwenye Kamati tulikaa tukajadili na Mheshimiwa Susan mwenzangu nashangaa kwa sababu hili tulilolandika tulikuwa naye. Naona mwenzangu anataka kupata kidogo siasa, hapana hili jambo tusilifanyie siasa kwa sababu naomba wote wenye hii karatasi msome haya maneno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasema, Kamati inashauri; wataalam wa elimu, kwani ninyi tume mtaleta wanasiasa? Nawauliza hiyo tume italeta wanasiasa? Sisi tumekuwa *specific* hatutaki muingize wanasiasa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema wataalam wa elimu wafanye tathmini kuhusu mfumo wa elimu uliopo kuanzia elimu ya msingi, sekondari na vyuo vikuu na kuja na mfumo ambao utaboresha kiwango chetu cha elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Kamati tumetafakari sana na tukasema twende wakakae wataalam na naomba Serikali na hili bahati nzuri Waziri umesema nendeni mkatafute wataalam wa elimu walioko popote duniani wapitie mfumo wetu wa elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilishawishi Bunge likubaliane na hoja ya Kamati yetu ili Serikali iende ikafanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wabunge mniunge mkono kwenye jambo hili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan Lyimo naomba ufunge mjadala wa hoja yako.

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa na Mheshimiwa Zitto ni Mjumbe, nilikuwa naomba ahitimishe kwa niaba yangu.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni gani ya kupigiana pasi?

**MHE. JACQUILINE N. MSONGOZI:** Hatuko uwanjani hapa.

**MWENYEKITI:** Naomba utulivu tafadhali Mheshimiwa Susan Lyimo naomba uhitimishe mjadala wa hoja yako. Mheshimiwa Susan Lyimo naomba.

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Kaa Zitto, Zitto kaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Kwanza nimemsikiliza sana Mwenyekiti Mheshimiwa Peter Serukamba akisema kwamba ni Mjumbe, ni kweli ni Mjumbe lakini vilevile naweza nikawa na *opinion* yangu na hii siyo ya kisiasa, sawa sawa?

Kwa hiyo nilitaka kusema kwamba kwenye Kamati kama ambavyo amesema ni kweli imezungumzwa iundwe Kamati. Kamati inashauri wataalam wa elimu lakini *it's too broad*, wataalamu wa elimu, Wizara ya Elimu ina wataalam wa elimu kibao lakini hawajawahi kubadili mfumo wa elimu nchi hii. Elimu yetu imeendelea kuporomoka kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, anachokisema Mwenyekiti wangu namshangaa, kwa sababu unapounda tume anazungumza habari ya wanasiasa. Tunazungumzia tume ya kitaalam maana yake kama ni tume ya kitaalam hawa wanasiasa wanakuwa na *share* gani pale? Lakini amezungumza kumekuwa na tume nyingi, *fine*. Kumekuwa na tume nyingi, je, hizo *report* za Tume zinatumika wapi? Tumeona Tume ya Makwetta *it was very nice*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali tuliyofikia katika elimu ya nchi yetu, *unless* mnataka kutuambia nchi hii tuendelee kuwa omba omba, tuendelee kushindwa kujenga hoja kwa sababu ni wazi wote hapa tunajua kwamba elimu yetu iko *ICU*. Hivi kweli tunapozungumzia tume maana yake hii tume itatuletea kitu cha maana sana kwamba elimu yetu ilikuwa vipi na sasa tunataka iende vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kurudia kusema kwamba hayo ni maoni ya Kamati, lakini mimi nimeleta hoja yangu, pendekezo langu na nilikuwa naomba *record* ziwekwe sahihi kwamba Bunge hili leo limebariki tuendelee na mtindo huo huo kwamba hatuoni kwamba elimu ya nchi hii inakufa, wataalam na wadau mbalimbali wamezungumza wanasema kwamba elimu inaporomoka na wewe Mwenyekiti unajua kabisa kwamba elimu ya nchi hii inaporomoka na *solution* pekee inekuwa tume ya wataalam ambayo ingetusaidia sana kututoa hapa tulipo ili na sisi tushiriki kama nchi nyingine katika dunia hii ya uchumi unaoendelea kwa kasi lakini teknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetoa *data,* takwimu zinaonyesha wazi *graduates* wetu asilimia 40 tu ndiyo wanaweza kuajiriwa, lakini vyuo vyetu havina wahadhiri sasa kama hilo nalo halionekani kama shule za kata zina-*perform that bad* bado hamuoni kama kuna tatizo *then its okay,* lakini nasema tume ndiyo muarobaini wa elimu yetu inakokwenda. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

**MWENYEKITI:** Hoja hii haijakubaliwa.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo.

**MWENYEKITI:** Sasa naomba…

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mwongozo

**MWENYEKITI:** Nimesimama. Waheshimiwa Wabunge naomba sasa nilihoji Bunge.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2016 hadi Januari, 2017 ilipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Unawasha *mic* Mheshimiwa haifai. Haya Waheshimiwa nawashukuru sana na nina furaha kubwa kusema kwamba…

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo.

**MWENYEKITI:** …Kamati zetu mbili hizi…subirini basi nimalize.

Waheshimiwa Wabunge, nachukua fursa hii kuzipongeza Kamati zote mbili kwa kutumia wajibu wao kikanuni, kanuni ya 117(15) kwa kuweza kuleta taarifa Bungeni na taarifa hizo mbili kupitishwa na Bunge hili kuwa ni Maazimio ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaahirisha Bunge…basi nimemaliza kwa hapo kwa vile shughuli zetu za leo...

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mwongozo.

**MWENYEKITI:** …Mungu awabariki sana. Naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo. Mwenyekiti Mwongozo.

*(Saa 1.26 usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 7 Februari, 2017, Saa Tatu Asubuhi)*